# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA TANO

## Kikao cha Nane – Tarehe 9 Novemba, 2016

*(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae, Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. FELISTER A. BURA (K.n.y. MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI):-**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* kuhusu Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Hesabu za Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2014 na tarehe 30 Juni, 2015.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* kuhusu Hesabu zilizokaguliwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2014 na tarehe 30 Juni, 2015.

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa John Peter Kadutu, Mbunge wa Ulyankulu, sasa aulize swali lake.

Na. 79

**Hitaji la Kuboresha Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi**

**MHE. JOHN P. KADUTU** aliuliza:-

Kwa miaka mingi kumekuwa na Sheria mbaya za fidia kwa wafanyakazi wapatao ajali:-

Je, ni lini Serikali italeta Muswada wa mabadiliko ya Sheria ya *Workmen's Compensation* ili kwenda na wakati kwa vile Sheria iliyopo haiwasaidii waathirika wa ajali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Peter Kadutu, Mbunge wa Ulyankulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya mwaka 2008, fidia kwa wafanyakazi zilikuwa zikilipwa kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya zamani ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura 263 na Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002 na kanuni zake za mwaka 2003. Sheria hizi za fidia kwa wafanyakazi zilitumika kulipa fidia kwa watumishi wote kutoka sekta binafsi na umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya Sheria ya *Workmen's Compensation,* Sura ya 263 yalifanyika mwaka 2008 ambapo Bunge lilitunga Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi (*Workers Compensation Act)* Na. 20 ya mwaka 2008 ili kuondoa upungufu kadhaa ulioonekana katika sheria zilizotangulia ikiwa ni pamoja na kiwango kidogo cha fidia kwa mfanyakazi aliyeumia au kupata maradhi akiwa kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii imeanzisha Mfuko wa Fidia ambao unashughulikia masuala ya fidia kwa wafanyakazi waliopo katika Sekta ya Umma na Binafsi Tanzania Bara ambao wataumia, kuugua ama kufariki kutokana na kazi wanazofanya kwa mujibu wa mikataba ya ajira zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko huo umeanza kazi rasmi tarehe 1 Julai, 2016 ambapo waajiri katika sekta binafsi wanachangia 1% na Sekta ya Umma 0.5%. Mfuko huu umeanza rasmi kulipa mafao ya fidia kwa wafanyakazi wanaoumia au kupata maradhi wakiwa kazini kuanzia tarehe 1 Julai, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupitia Mfuko huu, utaratibu wa kupata huduma za fidia umerahisishwa sambamba na mafao kuboreshwa kwa kiwango kikubwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kadutu, swali la nyongeza.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu. Swali langu la kwanza la nyongeza ni kwamba, katika ajali hizi mbalimbali zinazowapata wafanyakazi kazini, wapo wanaopoteza viungo vya mwili kwa maana wanapata ulemavu; kwa hiyo, inabidi wapate viungo bandia ili maisha yaweze kwenda. Je, Serikali sasa iko tayari kuweka sheria ili waathirika wa ajali hizi wapatiwe viungo bandia bure?

Pili, kumekuwa na usumbufu mkubwa sana katika malipo haya ya wafanyakazi wanaoumia kazini: Je, Serikali sasa iko tayari kuweka utaratibu mzuri ili wanaopata ajali kazini na kupoteza viungo na uwezo wa kazi waweze kupata malipo yao haya ambayo ni sehemu ya faraja katika maisha yao? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la msingi ameulizia kama tunaweza tukatunga sheria ambayo itawarahisishia hawa wanaopata matatizo wakiwa kazini kupata viungo bandia vya bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, kwa sasa hakuna haja ya kutunga sheria nyingine kwa sababu sheria iliyopo ndicho ambacho imekuja kuki-*address.* Sheria yetu ya sasa ya *Workers Compensation Act,* kazi yake kubwa ni pamoja na ku-*cure mischief* ambayo ilikuwa inatokana na sheria iliyopita, ambapo katika sheria ile iliyopita, fidia yoyote ambayo ilikuwa inalipwa, *maximum payment* ilikuwa ni sh. 108,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maboresho ya sheria hii sasa, inakuja kuyajibu hayo matatizo ambayo yalikuwa yakisababishwa na sheria iliyopita kiasi kwamba wafanyakazi wengi walikuwa wanaumia, lakini malipo yao yalikuwa siyo stahili na yalikuwa hayaendani na lile jeraha ambalo amelipata. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge tu kwamba, sheria

ipo na itaendelea kutekelezwa na kwa sababu ndiyo kazi imeanza hii, *WCF* ndiyo wenye jukumu la kufanya hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Mheshimiwa Mbunge, ameuliza kuhusu usumbufu wa malipo. Nimwondoe hofu pia kwamba Mfuko huu ambao umeanzishwa kwa mujibu wa sheria Na. 5 ya mwaka 2008 umeweka utaratibu mzuri wa malipo ya namna gani malipo yatafanyika ikitokea mtu amepata matatizo akiwa kazini. Kwa hiyo, kwa sababu Mfuko umeanza kazi tarehe 1 Julai, 2016 kwa maana ya kuanza kulipa fidia, nimwondoe hofu tu kwamba wenzetu wa Mfuko wamejipanga vizuri kuondoa usumbufu na kuhakikisha kila mtu ambaye amepata majeraha akiwa kazini anashughulikiwa ipasavyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi hii. Pamoja na maelezo mazuri ya Naibu Waziri juu ya *Workers Compens*ation na sheria inayohusika, kuna tatizo moja kutoka chombo kilichokuwa kinashughulikia *compensation* ambacho kimekwisha na kikachukuliwa hiki cha sasa ambacho ni *Compensation Act* ambayo imeanza Julai, 2016. Naomba anihakikishie kwamba wale wafanyakazi walioumia kwa sheria ya zamani ambayo ilikuwa inalipa viwango vidogo kama sh. 100,000/= watachukuliwa walipwe na Mfuko huu mpya kwa malipo ya Mfuko huu wa sasa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, Mfuko huu unaanza kulipa fidia kuanzia tarehe 1 Julai, 2016, hasa baada ya kuwa na kipindi cha mpito cha mwaka mmoja kuanzia mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimkumbushe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa mujibu wa taratibu za kisheria; sheria huwa haiendi *retrospectively;* kwa sababu hii sheria imeshatungwa katika mazingira haya na kuainisha wale ambao watapata madhara kuanzia kipindi hicho, basi Mfuko huu na sheria hii itahudumia wale tu ambao wanaguswa na sheria kuanzia pale ambapo ilitungwa lakini pia tarehe ya utekelezaji ambayo imetamkwa kwa maana ya kuanzia tarehe 1 Julai, 2016.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena, Mbunge wa Morogoro Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 80

**Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Mvuha**

**MHE. PROSPER J. MBENA** aliuliza:-

Wananchi wa Wilaya ya Morogoro Vijijini kwa muda mrefu wamekuwa wakikosa huduma nzuri za matibabu katika hospitali ya Wilaya kama vile *X-Ray, MRI, TSCAN* dawa za kutosha, Madaktari Bingwa na Wauguzi kwa sababu tu Wilaya na Halmashauri yake zimechelewa kuhamia Mvuha suala ambalo Ofisi ya Rais, TAMISEMI inalishughulikia:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kuanza kujenga Hospitali ya Wilaya Mvuha mahali ambapo ndipo patakapojengwa Makao Makuu ya Wilaya?

(b) Je, Serikali kwa sasa iko tayari kukiteua Kituo cha Afya cha Lukange ambacho ni bora sana kimejengwa na Kanisa Katoliki na kukikabidhi kitoe huduma kwa wananchi kama Hospitali Teule ya Wilaya ya Morogoro Kusini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena, Mbunge wa Morogoro Kusini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kusogeza huduma za afya karibu na wananchi, tayari Halmashauri imetenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya katika eneo la Mvuha yatakapohamia Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro. Halmashauri inashauriwa kuweka katika vipaumbele vyake na kutenga bajeti katika mwaka wa fedha 2017/2018 ili kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakubaliana na wazo la kukifanya Kituo cha Afya Lukange kuwa Hospitali Teule ya Wilaya kwa kipindi cha mpito. Hata hivyo, suala hili linahitaji makubaliano baina ya Serikali na mmiliki wa kituo ambaye ni Kanisa Katoliki. Hivyo, tunashauri vikao vya maamuzi vya ngazi husika vya Mkoa na Wilaya, vikiona inafaa vianze mchakato huo mapema. Vikao hivyo, vikikaa na kuridhia pendekezo hilo, Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto haitasita kuteua kituo hicho kuwa Hospitali Teule ya Wilaya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Prosper Mbena, swali la nyongeza.

**MHE. PROSPER J. MBENA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na napenda kumpa taarifa kwamba tayari vikao hivyo vimeshafanyika na tayari mkataba kati ya Kanisa Katoliki pamoja na Halmashauri ya Wilaya Morogoro umeshakamilika na nitampatia nakala ya mkataba huo. Baada ya hatua hiyo kufikiwa. Je, Mheshimiwa Waziri sasa atashughulikia lini? Itachukua muda gani kushughulikia suala la kupatikana kwa watumishi pamoja na kada nyingine zinahitajiwa kwa hospitali hiyo? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu kama mchakato huu tayari umeshaanza, basi ina maana kwamba walikuwa mbele ya tukio zaidi. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jukumu la Serikali sasa kwamba mara baada ya mchakato huo kukamilika, sasa ni kuangalia kipi kinachohitajika katika eneo lile hasa tukitoa kipaumbele katika suala zima la watumishi kama alivyozungumza. Kuhusu lini, naomba niseme ni katika kipindi kifupi kijacho. Kwa kuwa lengo letu kubwa ni kuhakikisha kwamba tunaongeza kada katika maeneo mbalimbali, basi Wilaya yake tutaipa kipaumbele hasa katika eneo hili ambapo nami nilifika kule katika Wilaya yake nikaona kwamba ni kweli, wananchi wanaotoka kule Mvuha mpaka kuja Morogoro Mjini ni kilomita nyingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuiwezesha hospitali hii. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni *commitment* ya Serikali kuwezesha kituo kile katika vifaa tiba na wataalam. Lengo kubwa ni kwamba wananchi wa eneo lile wapate huduma. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Changamoto za Morogoro Kusini zinafanana na Changamoto za Jimbo la Karagwe. Katika Hospitali ya *DDH* Nyakahanga tuna tatizo kubwa la upungufu wa madawa, vifaa tiba na Wauguzi.

Mheshimiwa Naibu Spka, swali langu ni je, Naibu Waziri, Mheshimiwa Jafo kaka yangu, anaweza kuambatana nami baada ya Bunge hili kwenda kusaidiana nami kutatua changamoto za Hospitali ya *DDH* ya Nyakahanga

pamoja na kuanza mchakato wa kujenga Hospitali ya Wilaya ukizingatia *DDH* ya Nyakahanga inahudumia Wilaya mbili; Karagwe na Kyerwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri wazi kwamba miongoni mwa Wabunge ambao walikuwa wakinisumbua sana katika Sekta ya Afya ni Mbunge huyu wa Karagwe. Ni kweli kabisa, naomba niseme kuwa, pale ana Daktari wake anaitwa Dkt. Sobo ambaye ni kijana mwenzake; naamini kwamba watashirikiana vya kutosha kuhakikisha mchakato wa Jimbo lile unakaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, *commitment* yetu ni kwamba, katika kipindi hiki nitakuwa na ziara katika Mikoa yetu mitano nikianzia Mkoa wa Tanga, Lindi, Pwani Morogoro pamoja na Mtwara, lakini nitapita Ruvuma. Vile vile Mkoa wa Kagera niliupa kipaumbele kwa zoezi maalum katika kutembelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani kwamba kabla ya Bunge lijalo, basi nitajitahidi kwa kadiri iwezekanavyo tufike eneo lile kubaini changamoto za wananchi wa eneo lile la Jimbo la Karagwe ili mwisho wa siku wananchi wa eneo lile waweze kupata huduma bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni *commitment* ya Serikali, tutajitahidi kwa kadiri iwezekanavyo, hasa nikijua nawe ni mpiganaji mkubwa katika Sekta ya Afya katika eneo lako, tutasukuma kwa kadiri iwezekanavyo wananchi pale wapate huduma bora. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Miongoni mwa matatizo ambayo tunayapata katika Wilaya ya Babati kwa Hospitali ya Mrara ni *ranking* ya hospitali hiyo ambapo mpaka sasa inaitwa Kituo cha Afya wakati hospitali hiyo imekuwa ikihudumia watu wa Kondoa na watu wa Babati Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi tumekuwa tukipendekeza kwamba hospitali hii tuipandishe *rank* iwe Hospitali Teule ya Wilaya, lakini Serikali imekuwa haitupi ushirikiano. Je, sasa wako tayari kutusaidia ili hospitali hiyo ipate dawa na vifaa tiba kuhudumia watu wote hao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Gekul kwamba Serikali lazima inatoa kipaumbele na ndiyo maana naye anakumbuka juzi juzi tulikuwa pamoja jimboni kwake tukikagua miradi mbalimbali katika Mkoa wa Manyara. Nimeweza kubaini changamoto mbalimbali kimkoa, kiujumla wake kwamba kuna mambo mengi ya kuweka kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama jambo hili lililetwa kama *request* Serikalini, lakini bado halijafanyiwa kazi, sasa ni jukumu letu kukumbushana tuone jinsi gani tutafanya ili pale ambapo pamepungua tusukume kwa sababu mwisho wa siku tunataka wananchi wapate huduma.

Kwa hiyo, ni *commitment* ya Serikali kwamba tutaangalia ni kitu gani kilichokuwa kinakwamisha mwanzo, jambo gani *(gap)* ambalo inabidi tuliweke vizuri ili tuboreshe eneo na mwisho wa siku wananchi wapate huduma ya afya, kwani ni *commitment* ya Serikali kuwahudumia wananchi wake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Ishengoma, swali fupi.

**MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Naomba kuuliza swali la nyongeza. Nashukuru sana kwa majibu ya Naibu Waziri kwa swali la msingi, lakini ningependa kuuliza kuwa kwa sababu Morogoro Vijijini hatuna mpaka sasa hivi Hospitali ya Wilaya na majibu yametolewa, naomba kuulizia je, inawezekana pia kuboresha Kituo cha Afya cha Dutumi ambacho mpaka sasa hivi na chenyewe kinatumika kwa kutupatia vitendea kazi? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ishengoma ni Mbunge wa Viti Maalum kule na nimesema kwamba katika ziara yangu nina mpango wa kuja Mkoa wetu wa Morogoro. Lengo ni kutembelea Mkoa mzima wa Morogoro na kubaini changamoto zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ishengoma najua ni mpiganaji wa siku nyingi sana katika eneo hili. Naomba nimhakikishie kwamba katika ziara yangu eneo hili tutakwenda kulitembelea na licha ya kulitembelea na kuangalia mipango ya pamoja jinsi tutakavyofanya, lakini nina maslahi mapana ya Mkoa wa Morogoro kwa sababu najua mkoa ule wananchi wanapata shida, wanatembea mbali, siyo jambo la kufichaficha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kila sababu, kipindi cha ziara yangu tufike eneo hilo, tushauriane kwa pamoja na linalotakiwa kufanywa kwa sasa

tutalifanya, lakini linalotakiwa kuwekewa mipango mbadala kwa siku za usoni, tutalijadili kwa pamoja. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Ishengoma kwamba, katika hilo tutashirikiana kwa pamoja Mheshimiwa wangu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa. Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 81

**Matatizo Yanayoikabili Hospitali ya Rufaa - Musoma**

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** aliuliza:-

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara inakabiliwa na Matatizo mbalimbali kama vile uhaba wa magari ya kubebea wagonjwa, uhaba wa vitanda hasa kwenye wodi za akinamama, uhaba wa dawa na kadhalika:-

Je, ni lini Serikali itayashughulikia matatizo hayo ili kuboresha huduma zinazotolewa hospitalini hapo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara, inayo magari mawili ya kubebea wagonjwa ambayo ni STK 8368 na STK 7079. Gari namba STK 7079 lilipata ajali, lakini limeshafanyiwa matengenezo kupitia *TEMESA* Mkoa wa Mwanza ili liendelee kutoa huduma kwa wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali hiyo ina jumla ya vitanda 240 kati ya 420 vinavyohitajika. Kwa siku inalaza wagonjwa wanaofikia 169 katika wodi tatu za wazazi zilizopo. Mkoa kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, wamepanga kujenga wodi *(Postnatal Ward)* ambayo itawezesha kuongeza idadi ya vitanda 20 kukidhi mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya dawa katika hospitali imeongezeka kutoka shilingi milioni 710 kwa mwaka wa fedha 2015/2016 hadi shilingi bilioni1.8 kwa mwaka wa 2016/2017 sawa na ongezeko la asilimia 61. Mkakati wa Serikali hivi sasa ni kuimarisha makusanyo ya mapato ya huduma kwa njia ya kielektroniki ili kuongeza uwezo wa upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika hospitali zote nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joyce Sokombi, swali la nyongeza.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Majibu ya Naibu Waziri hayajaniridhisha, ukilinganisha na kwamba vifaa tiba na madawa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa havitoshelezi. Je, ni lini atahakikisha Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara itakuwa na vifaa ambavyo vitakuwa vinatosheleza kwa asilimia mia moja? *(Makofi)*

Swali la pili; kwa kuwa gari lililopo ni moja ambalo lina uhakika wa kubeba mgonjwa mahututi kumtoa Hospitali ya Rufaa Musoma kumpeleka Mwanza na ile nyingine ni hizi gari ndogo: Je, ni lini atatuletea *ambulance* nyingine katika Hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikwambie kwamba najua, kwa sababu wakati nakwenda kufunga Mkutano wa *ALAT* kule Musoma, nilitembelea mpaka Mkoa wa Mara kuona mpango mkakati wa kujenga Hospitali hii ya Rufaa ya Mkoa wa Mara. Nimetembelea pale, nimeona na tumebadilishana mambo mengi sana na Katibu Tawala wa Mkoa ule. Kwa hiyo, najua kuna changamoto, ndiyo maana katika majibu yangu ya msingi nilisema kweli kuna changamoto katika hospitali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu ni nini? Ni kuhakikisha kwamba sasa tunasukuma jambo lile. Naomba tushirikiane na Waheshimiwa Wabunge; kama mnavyojua kwamba *commitment* za afya zina *cross cut* maeneo mbalimbali nchini. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba, tutaendelea kushirikiana. *Commitment* ya Serikali, tukiangalia sasa hivi bajeti ambayo imetoka, shilingi milioni 700 mpaka shilingi bilioni 1.8, ni ongezeko la asilimia 61. Hili ni jambo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachofanyika sasa hivi ni nini? Ni kusaidia kusukuma nguvu sasa ili fedha zipatikane na wananchi wapate huduma. Katika mchanganuo wa bajeti katika eneo hilo, ndiyo unagusa katika maeneo mbalimbali ya vifaa tiba na madawa kuiwezesha hospitali hii iweze kufanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Mheshimiwa Mbunge amezungumzia suala la *ambulance;* ni kweli. Najua kwamba *ambulance* moja inafanya kazi vizuri, lakini na hizi nyingine zina changamoto kubwa. Sasa naomba nimsisitize Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na wadau wengine mbalimbali, katika mchakato huu wa bajeti unaokuja wa 2017/2018, tuweke kipaumbele kinachojiainisha katika upatikanaji wa *ambulance*. Serikali haitasita

kulisukuma hili. Lengo ni kupata *ambulance* ya maana katika kusaidia wakati wowote *emergency* inapotokea, wananchi waweze kupata fursa za tiba. Kwa hiyo, nakubali ombi hilo, tutaenda kulifanyia kazi kwa pamoja kama Wabunge na Serikali

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tatizo lililopo kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara, linafanana kabisa na tatizo ambalo lipo kwenye Hospitali ya Mkoa wa Tabora ya Rufaa ya Kitete. Kuna tatizo kubwa sana la wagonjwa na hasa akinamama wanapoenda kujifungua, wodi ile ni ndogo na wengi wanalala chini wakiwa hata wale wachache wanakuwa wana-*share* kitanda kimoja:-

Je, Serikali inajipanga vipi kutatua hili tatizo la muda mrefu la msongamano wa akinamama wanapojifungua pale Hospitali ya Mkoa wa Tabora ya Kitete? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Hospitali ya Kitete pale Tabora ina changamoto kubwa na ndiyo maana ukifanya rejea ya majibu yangu mbalimbali niliyoyatoa hapa Bungeni, tumesema kwamba *catchment area* ya Mkoa wa Tabora, ukubwa wake na jiografia yake ilivyo ina kila sababu tuweke nguvu. Ndiyo maana katika bajeti ya mwaka huu sitaki kutaja *figure* hapa *exactly,* tuna fungu ambalo tumelitenga kwa ajili ya suala zima la ukarabati pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutaangalia ni kipi kilichotengwa katika mwaka huu. Lengo ni kwamba ile fedha ipatikane tu ikafanye kazi na *value for money* ionekane. Naamini ule ukarabati utaanza mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nikuhakikishie kwamba katika majibu yangu ambayo nayakukumbuka hapa Bungeni niliyoyatoa ni suala zima la Hospitali ya Kitete; naomba tuwasiliane kwa karibu zaidi ili tujue ni fungu kiasi gani limetengwa, lakini tuhimize sasa ile fedha ili iweze kufanya kazi vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa tatizo la Mara la vifaa tiba pamoja na gari la wagonjwa, ni kama la Rungwe. Napenda kujua *commitment* ya Serikali kwa Hospitali ya Makandana katika Wilaya ya Rungwe, ni lini watatuletea gari na kutuongezea vifaa tiba kwa ajili ya kuwasaidia wanawake wa Wilaya ya Rungwe katika Hospitali ya Makandana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri nitakuwa nakusikiliza kwa makini unavyotoa majibu ya swali hili. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikupongeze na niwashukuru sana kwa dua zenu njema. Nakumbuka siku ile nilivyotoka kule baada ya kutoa maagizo kwamba mfumo wa kielectroniki ufanye kazi pale, baada ya muda fulani nikapata ajali, watu wakasema, watu wa huko wamekushughulikia? Nikasema hapana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishukuru sana. Agizo langu nililotoa ndani ya mwezi mmoja lilitekelezeka katika hospitali ile na nilipata mrejesho kwamba makusanyo yamebadilika sana katika hospitali ile ya Makandana. Kwa hiyo, naomba niseme kwamba kweli nilitembelea pale nikakuta gari za wagonjwa hali yake sio nzuri sana. Tulibadilishana mawazo na bahati nzuri wana Mkuu wa Wilaya mzuri sana katika eneo lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nilichukue hili kwa sababu kuna vitu vingine tumeshaanza kuvizungumza kuona ni jinsi gani tutafanya kuboresha hospitali ile, tutajadili kwa pamoja ili hospitali hii iweze kupata huduma nzuri, kwa sababu kuna *network* nzuri ya Waheshimiwa Wabunge katika eneo hilo, mnaofanya kazi kwa pamoja kwa *agenda* kubwa ya hospitali yenu, basi naamini jambo hili tutalitatua kwa pamoja, kama mawazo shirikishi kuhusu tufanye nini katika mpango wa muda mfupi na mpango wa muda mrefu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, sisi ni watu tunaofuata maelekezo. Kwa hiyo, tunaamini ahadi zako utazitimiza. Mheshimiwa Felister Bura, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tatizo lililoko Mara la *ambulance* ya kuwachukua wagonjwa, ni sawasawa na tatizo lililopo Wilaya ya Kondoa ambako Kituo cha Afya cha Wilaya ya Kondoa hakina *ambulance* kwa muda mrefu sasa; iliyopo ni mbovu ya mwaka 2008 na inahitaji matengenezo makubwa sana kiasi kwamba Halmashauri haiwezi kumudu. Je, Serikali iko tayari kutuletea *ambulance* Wilaya ya Kondoa ili wagonjwa ambao wanatakiwa kupata Rufaa ya kuja Dodoma Mjini wapate usafiri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri utakuwa umetusaidia ukijibu hilo suala la *ambulance* kwa Majimbo yote, maana kila mtu ana tatizo kwenye Wilaya yake. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumelisikia suala zima la *request* katika Wilaya ya Kondoa. Niseme wazi, ukiangalia hata katika *database* ya mwaka huu, katika Halmashauri ambazo ziliomba kupata *ambulance* zilikuwa 18, katika kumbukumbu yangu ya karibuni. Hili sina hakika hapa kama tuliweza kuliainisha katika mpango wetu wa bajeti wa Halmashauri ya Kondoa kwa mwaka huu wa fedha, lakini tutaenda kuliangalia. Kama Kondoa haipo, itabidi tujipange kwa pamoja, tuone ni jinsi gani tutafanya katika mchakato wa bajeti ambao utaanza siyo muda mrefu; na mpango wake tumeujadili hapa siyo muda mrefu, tujadili kwa pamoja kwa sababu hii *needs assessment* inaanzia kutoka katika vikao vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakapolifanya hivi na kwa sababu jambo hili ni pana na ninavyojua, mgonjwa kutoka Kondoa mpaka aletwe Hospital ya *General* hapa Dodoma ambapo ni mbali sana, tuna kila sababu kuwezesha eneo hilo lipate vifaa vizuri hasa *ambulance* kuwafikisha wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Felister Bura kwamba, hili tutaliangalia kwa upana wake, tuone ni jinsi gani tutafanya ili eneo lile lipate huduma bora. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Nsimbo, sasa aulize swali lake.

Na. 82

**Hitaji la Maji kwa Wananchi wa Nsimbo**

**MHE. RICHARD P. MBOGO** aliuliza:-

Licha ya kwamba chanzo cha maji yanayotumika katika Manispaa ya Mpanda kipo katika Kijiji cha Ikolongo, Kata ya Mtapenda na Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo, lakini wananchi wa maeneo haya hawapati maji:-

(a) Je, kwa nini Serikali katika bajeti ya mwaka 2016/2017 isitenge fedha ya miradi ya maji ili wananchi wa viiji jirani vya Kata za Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo ambazo ni Kapalala, Itenka, Machimboni, Sitalike, Kanoge na Katumba wapate maji?

(b) Kwa kuwa Mto Ugalla ni chanzo kizuri cha maji: Je, Serikali itaondoa lini kero ya maji katika Kata ya Ugalla na jirani ya Litapunga?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Nsimbo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017, imetenga shilingi milioni 757.4 kwa ajili ya miradi ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo. Miradi iliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na upanuzi wa mradi wa *Nduwi Station* katika Kata ya Ntumba, kujenga mradi wa maji katika Kijiji cha Katisunga, kujenga mradi wa maji katika Kijiji cha Songambele, Kata ya Kapalala pamoja na uchimbaji wa visima virefu sita.

(b) Mheshimiwa Spika, kulingana na tathmini iliyofanywa na Mkoa kupitia Mamlaka ya Maji, Mkoa wa Katavi mwezi Desemba, 2015, chanzo cha Mto Ugalla kimeonekana kuwa siyo cha uhakika kutokana na kupungua kwa maji wakati wa kiangazi. Serikali ina mpango wa kutumia Ziwa Tanganyika ambacho ni chanzo cha uhakika kwa ajili ya kupeleka maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo na Mpanda.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Richard Mbogo, swali la nyongeza.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Serikali, napenda tu kuiambia Serikali kwamba Halmashauri ya Nsimbo ni moja ya Halmashauri katika nchi yetu ya Tanzania ambayo wananchi kwa kiwango cha chini kabisa wanapata maji safi na salama. Ni asilimia 34 tu. Sasa katika hii bajeti ya milioni 757, kuna miradi ya Kijiji cha Katesunga na Kijiji cha Nduwi ambayo itafadhiliwa na *World Bank* kama shilingi milioni 273: Je, ni lini fedha hizi zitapatikana ili miradi hii iweze kuanza?

Swali la pili, kutokana na majibu ya Serikali kwamba Mto Ugalla una maji machache kwa kipindi cha kiangazi, lakini wananchi wa pale wamekuwa wakitumia mto ule kwa ajili ya maji kipindi chote na kuna mamba ambao wanahatarisha sana maisha yao: Je, kwa nini Serikali wakati mpango wa muda mrefu; maji kutoa Ziwa Tanganyika ukiwa unafanyika, isitenge fedha ili wananchi wa Kata ya Ugalla na jirani ya Litapunga waweze kupata maji kutoka Mto Ugalla? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la kwanza kwamba lini fedha zitapatikana; mpango wa upatikanaji wa fedha ni katika mwaka huu wa fedha katika bajeti hii. Ndio maana juzi hapa katika Maswali kwa Waziri Mkuu siku ya Alhamisi, Waziri Mkuu aliongelea suala zima la mtiririko wa fedha na akalihakikishia Bunge hili kwamba kipindi siyo kirefu sana tutaanza kuziona fedha katika Halmashauri zetu; fedha za maendeleo na fedha za OC. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naomba tuwe na imani kwamba katika mchakato huu wa sasa hivi kabla muda haujapita sana, bajeti hizi zitaanza kutoka ili mradi iweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kuhusu Mto Ugalla kwamba kwa nini usitumike kwa sasa, kwa sababu mpango uliokuwepo ni wa muda mrefu? Naomba nikiri wazi kwamba Mheshimiwa Richard Mbogo ni Mbunge ambaye nilikuwa naye Jimboni kwake Nsimbo na miongoni mwa miradi tuliyoikagua ni miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri wazi kwamba nilivyotembelea Jimbo la Nsimbo, ni kweli shida ya maji imekuwa ni kubwa sana. Kwa hiyo, nadhani hili ni wazo jema. Tutalichukua lakini tutawashirikisha na wenzetu kule katika Halmashauri na katika Mkoa, kuona kama ule mradi mkubwa kutoka Ziwa Tanganyika, huenda una gharama kubwa sana, tujue ni kiasi gani, tuweze kuja na mpango mwingine mbadala kusaidia katika Kata hizi ili tusisubiri muda mrefu sana miaka miwili, mitatu au minne kwa wananchi kuendelea kupata shida ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimwambie Mheshimiwa Richard Mbogo kwamba jambo hili sasa tutalichukua, tuone ni jinsi gani tutafanya ili kama katika hizo Kata mbili kuna mradi mwingine mbadala tuweze kuufanya. Nadhani jambo hili ni jambo shirikishi sana kwetu Serikali na Halmashauri ya Wilaya. Tutashirikiana na Mheshimiwa Mbunge kwa sababu najua anafuatilia sana ili wananchi katika zile kata mbili wapate fursa ya maendeleo ya maji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Jimbo la Lushoto limezungukwa na vyanzo vingi vya maji: Je, Serikali ina mpango gani ya kuwatua ndoo kichwani akinamama hasa wa Kilole, Kwekanga, Mbwei, Makanya, Ngulwi, Ubiri, Kwemakame na maeneo mengine yaliyobaki katika Jimbo la Lushoto?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa maji kwa sasa hivi ambao Waziri wa Maji wakati wote huwa anaelezea hapa, lengo letu kubwa ni kumtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Shekilindi, kwamba, katika ratiba yangu kama tulivyoongea, tarehe 24 mwezi huu wa Novemba, nitakuwa katika Jimbo lake la Lushoto. Naomba tukiwa kule kule *site* tuweze kubadilishana mawazo. Hivyo vyanzo vilivyoko, lakini vile vile na wenzetu Wizara ya Maji ambao Mheshimiwa Waziri wa Maji yuko makini muda wote kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wanapata maji, tutaangalia na kushauri vizuri jinsi gani tutafanya kwa maeneo ya Wilaya ya Lushoto ili wananchi waweze kupata maji. Kwa hiyo, naomba tutumie vizuri ziara yetu ya tarehe 24 kuangalia vyanzo vilivyoko na mambo mengine kuwasaidia wananchi wa Lushoto.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali fupi.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa mradi wa maji unaoendelea Manispaa ya Sumbawanga umechukua muda mrefu na wananchi wa Manispaa ya Sumbawanga mpaka sasa hawajui huo mradi utaisha lini: Je, Serikali inawaambiaje wananchi wa Manispaa ya Sumbawanga ikiwepo wanawake ambao wanapata athari mpaka sasa na wengine kupata vifo kwa ajili ya kufuata maji kwenye umbali mrefu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali ina mradi mkubwa wa maji pale Manispaa ya Sumbawanga. Mradi ule ulikuwa umalizike toka Septemba, 2015, sasa yalitokea matatizo; kwanza, ilikuwa ni kuchimba visima 12; visima sita virefu upande wa kusini na visima sita upande wa kaskazini. Kwa hiyo, ikabidi baada ya kuanza kuchimba tukakosa, visima vyote havikuwa na maji. Kwa hiyo, tukatafua upande wa Kaskazini, ikabidi tuongeze sasa idadi ya visima kutoka sita mpaka 17, hii ikasababisha muda kuongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwahakikishie wananchi wa Sumbawanga, kwanza mradi kwa sehemu kubwa umeshakamilika, kilichobaki ni kujenga mtandao. Ikifika mwezi Desemba mwaka huu mradi ule utakuwa umekamilika na wananchi wa Manispaa ya Sumbawanga watakuwa wanapata maji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bawazir.

**MHE. MBARAK S. BAWAZIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nataka nimwulize Mheshimiwa Waziri, ni lini atamalizia mradi wa maji wa Kilosa, hasa akizingatia kwamba hivi sasa Kilosa kuna kipindupindu? Imebakia pesa kidogo ili wamalizie mradi huo wa maji endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwenye maji, kwa kweli maji yako mengi sana Kilosa na kuna mabwawa yanahitajika yachimbwe kama Kilimagai, Godegode na Kidete. Haya mabwawa yatasaidia hata kuleta mafuriko ndani Kilosa yangu na vile vile katika…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MBARAK S. BAWAZIR:** Duh, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri unasimama au ni Waziri wa TAMISEMI! Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirejee pia kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Hii miradi ya maji katika mwaka wa fedha 2016/2017 tumeainisha kila Wilaya ni miradi ipi ambayo ni vipaumbele inakwenda kufanywa na fedha zimetengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba sana Mheshimiwa Mbunge aseme *specifically* ni mradi upi anaoulizia? Kwa sababu ndani ya Kilosa ipo miradi mingi, ili tuweze kujua hasa ni upi na ni hatua gani ambazo tunaweza kuzichukua. Kwa hiyo, naomba tuwasiliane na Mheshimiwa Mbunge, tukae ili tuweze kubadilishana mawazo tuone ni namna gani huo mradi ambao anauulizia, nimpe majibu ambayo ni sahihi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bawaziri umekaa *row* moja na Mheshimiwa Waziri amekukaribisha hapo kwenye kiti chake.

Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa *Capt.* George Huruma Mkuchika, Mbunge wa Newala Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 83

**Serikali Kujenga Uwanja Mpya wa Ndege Newala**

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA** aliuliza:-

Mji wa Newala tangu utawala wa kikoloni ulikuwa na Uwanja wa Ndege mdogo uliowezesha kutua ndege ndogo. Uwanja huo kwa sasa umejengwa nyumba za kuishi. Kwa vile Mji wa Newala unapanuka sana na una hadhi ya Halmashauri ya Mji na Uongozi wa Wilaya umetenga eneo la kujenga uwanja mpya wa ndege:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika maandalizi ya kujenga Uwanja Mpya wa Ndege katika Halmashauri ya Mji wa Newala?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, Mbunge wa Newala Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikifunga Kiwanja cha Ndege cha Newala mwaka 1998 kutokana na uwepo wa mazingira yasiyo salama ya uendeshaji wa ndege, uliosababishwa na makazi ya watu kusonga katika maeneo yanayozunguka kiwanja hicho. Aidha, ukatizaji wa watu kiwanjani na mmomonyoko wa ardhi uliopo eneo la kiwanja ulionekana kuhatarisha usalama wa ndege na watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Halmashauri ya Mji wa Newala kutenga eneo jipya kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, ilipeleka wataalamu wake kukagua eneo hilo na ikaonekana kukidhi vigezo vya kiwanja cha ndege kulingana na viwango vya Kimataifa vinavyotolewa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga Duniani *(ICAO Standards)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kukamilika kwa ukaguzi huo, utaratibu unaofuata ni kwa Halmashauri husika kutekeleza jukumu lao muhimu ambalo ni kukamilisha upimaji na uthamini wa mali zilizomo ndani ya eneo hilo. Hadi sasa hatua hizo za kulitwaa eneo husika hazijafanyika. Hivyo, kupitia Bunge lako Tukufu, Wizara yangu inawataka Halmashauri ya Mji wa Newala kukamilisha hatua za utwaaji wa eneo hilo na kulikabidhi kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ili waweze kuanza hatua ya upembuzi na usanifu wa Kiwanja Kipya cha Ndege cha Newala.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Capt. George Mkuchika, swali la nyongeza.

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kushukuru majibu mazuri ya Serikali, lakini pia napenda nishukuru ushirikiano tulioupata kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege; kama walivyosema, walifika Newala na wameelekeza kiwanja kikaeje na wametueleza ukubwa wa eneo linalohitajika. Nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa taratibu za Kimataifa zinataka kabla hatujahamisha uwanja ule wa ndege, ule uwanja wa mwanzo ufutwe; na kwa kuwa Halmashauri imeandikiana sana na Wizara na viwanja vya ndege kutaka kufuta ule uwanja wa zamani, jambo ambalo halijafanyika mpaka sasa. Je, Serikali inaweza kutuhakikishia kwamba kazi ya kufuta ule uwanja itafanyika mara moja?

Swali la pili, kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Waziri ametupa majukumu Halmashauri ya Mji kufanya tathmini ili eneo lile liweze kutwaliwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, kazi ambayo tutakwenda kuisimamia mara baada ya kutoka hapo. Je, Halmashauri ya Mji ikishamaliza suala la tathmini na kwa kuwa viwanja vya ndege ni mali ya Serikali Kuu, siyo mali ya Halmashauri, Serikali itakuwa tayari kuwafidia wale wananchi wachache ambao walikuwa wanalima pale kwa kuzingatia kwamba gharama hazitakuwa kubwa kwa sababu pale hakuna mazao ya kudumu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu Mheshimiwa Huruma kwa jina lake ni mtu wa huruma…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, unashauriwa aidha kutumia jina la mwisho au la kwanza kwa sababu hilo huruma hawalifahamu watu, maana lipo katikati. Ni Mheshimiwa George Huruma Mkuchika.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, ana kaka yake anaitwa *Uchicheme Wala Uchimumunye; Ukimumunya Nchale Ukitema Nchale.*" *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mkuchika kwamba uwanja huu ukishakamilisha suala la *process* ya kulitwaa tutafanya kama anavyopenda na kama wenzetu wa Halmashauri ya Newala wanavyopenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba, tena naomba sana masuala ya kuvamia viwanja vya ndege, ndugu zangu, vinginevyo tutakuwa tunaipa hasara Serikali. Naombeni sana viongozi wenzetu wa Halmashauri mbalimbali watunze viwanja vyetu vya ndege ili viweze kutusaidia katika shughuli za kitalii na usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la kwanza namhakikishia kwamba tutachukua hizo hatua na pengine nichukue fursa hii kuwaagiza Bodi ya *TAA* ichukue hatua za haraka kuhakikisha kwamba uwanja huu unafutwa kwa mujibu wa taratibu tulizojiwekea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali fupi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa katika Kata ya Mnazi, Tarafa ya Umba, kuna tatizo linalofanana na huku Newala Mjini; kuna kiwanja cha ndege *(air stripe)* ambayo ni ya muda mrefu sana haitumiki na sisi tupo karibu na hifadhi ya Mkomazi: Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka sasa kukifufua kiwanja hiki ili kiweze kuchochea utalii katika hifadhi ya Mkomazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea ombi la Mheshimiwa Shangazi na nitawasiliana na Waziri wa Maliasili na Utalii ambao kiwanja hiki ilikuwa ni mali yao na ni kwa ajili ya shughuli za utalii ili tuone namna gani kiwanja hicho kitafufuliwa na kama kuna shughuli za kiuchumi zitakazowezesha kiwanja hiki kujilipa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso, swali fupi.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Sekta ya Utalii ni sekta ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa pato la Taifa na sekta hii ili iweze kuwa endelevu ni lazima pawepo na uhakika wa usafiri ikiwemo viwanja vya ndege. Kuna Kiwanja cha Ndege kilichopo Karatu kwa maana ya Kiwanja cha Ndege cha Manyara; kimetelekezwa na hakiendelezwi. Je, ni lini Serikali itahakikisha inaendeleza kiwanja hicho?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu mafupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitawasiliana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (*TAA)* na Bodi yao tuone nini kinaweza kufanyika katika kiwanja hiki na mipango yao ikoje katika kuvifufua viwanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na hiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Mussa Ntimizi, Mbunge wa Igalula.

**MHE. MUSSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa kuwa mama yetu mpendwa, Mheshimiwa Margaret Sitta yuko kwenye matatizo, amefiwa na mume wake, naomba nitoe pole nyingi sana kwa msiba uliompata. Kwa niaba ya wakazi wa Urambo, naomba swali lake Namba 84, sasa lipate majibu. Ahsante. *(Makofi)*

Na. 84

**Vikwazo Vinavyokandamiza Kilimo cha Tumbaku**

**MHE. MUSSA R. NTIMIZI (K.n.y. MHE. MARGARET S. SITTA)** aliuliza:-

Pamoja na jitihada za Serikali za kuendeleza kilimo, bado kuna vikwazo vinavyomkandamiza mkulima wa tumbaku ashindwe kujiendeleza kiuchumi:-

(a) Je, hadi sasa Serikali imechukua hatua gani ili kuongeza wanunuzi wa tumbaku ili kuleta ushindani wa bei na kuwa na masoko ya uhakika?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani kuondoa tozo na makato lukuki katika bei ya tumbaku?

(c) Je, Serikali imechukua hatua gani katika kupunguza daraja za tumbaku?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nasi kama Wizara tunatambua kwamba Mheshimiwa Margaret Sitta amekuwa mshauri mkubwa sana, lakini vile vile amesimamia suala la tumbaku nasi tunapenda kutoa pole kwa msiba mkubwa uliompata.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margaret

Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba hapa nchini yapo makampuni machache yanayojishughulisha na biashara ya tumbaku, hivi sasa Serikali kupitia Bodi ya Tumbaku inaendelea kutafuta masoko zaidi ili kuongeza uzalishaji na ushindani wa bei. Hadi sasa Kampuni ya *China Sunshine* inakamilisha taratibu za kuingiza tumbaku yetu katika soko la China. Vile vile imefanikiwa kupata Kampuni ya *Sino Cigarette* ya China ambayo inatarajia kununua tumbaku ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi imeshaisajili Kampuni hiyo na kuiruhusu kufanya maandalizi ya ununuzi wa tumbaku. Pamoja na hayo, Soko la Tumbaku Duniani lipo kwenye kampuni kubwa chache zinazofanya biashara, siyo kwa ushindani, bali ni muungano wa ukiritimba *(cartel)* katika kupanga bei na kiasi cha kununua kutoka nchi fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, pamoja na kuwa ushindani ni mojawapo ya vigezo vya kupata bei nzuri, lakini katika zao la tumbaku vipo vigezo vingine vya kuwezesha kupata bei nzuri, ambavyo ni pamoja na ubora, vigezo vya kukubalika sokoni *(compliance)* na ufanisi katika uendelezaji wa Vyama na Biashara yenyewe katika maana ya *efficiency*. Hivi sasa Serikali inaelekeza nguvu kwenye kuwezesha zao kukubalika sokoni kwa kuboresha uhifadhi wa mazingira, kuondoa ajira ya watoto na kuongeza ufanisi kwa kuimarisha Vyama vya Ushirika, mazingira ya kufanyia biashara, kuondoa tozo, kodi na gharama za uzalishaji zisizo za lazima.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara zinazohusika inafanyia mapitio tozo na kodi zilizopo katika mazao mbalimbali ikiwemo zao la tumbaku ili kuona uwezekano wa kuziondoa au kuzipunguza. Uchambuzi huo utakamilika kabla ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2017/2018 ambapo tunategemea kuwepo kwa unafuu mkubwa katika makato mbalimbali katika zao la tumbaku na mazao mengine.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi kwa kushirikiana na wadau wa tasnia ya tumbaku imepunguza madaraja 10 na hivi sasa kuna madaraja 62 badala ya 72 ambayo yatatumika msimu huu wa kilimo katika maana ya 2016/2017. Aidha, wakulima wanashauriwa kuongeza ubora wa tumbaku wanayozalisha jambo ambalo litapunguza madaraja moja kwa moja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Ntimizi, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe na pia kwa kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri; lakini katika majibu yake Serikali imekiri kwamba wanunuzi hawa wa tumbaku wana muungano wa ukiritimba katika kupanga bei na kiasi cha tumbaku cha kununua. Wanapenda kuangalia gharama za mkulima katika kuzalisha zao lake ndipo wapange bei, lakini sisi hatujui wao wanauza shilingi ngapi katika Soko la Dunia. Je, ni hatua gani Serikali inachukua katika kumsaidia mkulima huyu wa tumbaku katika kupata bei nzuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Serikali ililitangazia Bunge kwamba kupitia *WETCU* wana mpango wa kufufua Vyama 64 vya Wakulima wa Tumbaku ambapo wanachama wa vyama vile walichangishwa sh. 100,000/= kila mmoja katika kufanikisha zoezi hilo, lakini leo *WETCU* na makampuni wamewanyima wakulima hawa pembejeo, lakini vile vile wanasema kwamba soko la kununua tumbaku ile hakuna. Wakulima tayari wameshalima na utaratibu wote wameshamaliza na hawajui watauzia wapi tumbaku hiyo. Je, Serikali inawaambia nini wakulima hawa wa tumbaku ambao tayari sasa wemeshalima tumbaku yao na wanasubiri mauzo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba biashara ya tumbaku inaendeshwa kwa *cartel;* kuna makampuni machache duniani ambayo ndiyo yanaamua kila kitu, yanaamua kiasi, lakini vile vile yanaamua bei. Ni kweli vile vile kwamba mara nyingi kampuni zinazonunua tumbaku zenyewe hazina tabia ya kuonesha faida na gharama zao lakini wanataka wakulima na wazalishaji waoneshe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiendelea na majadiliano na haya makampuni na kwa sasa makampuni hayo yamekubali kutuonyesha gharama zao pamoja na faida wanazopata ili tuweze kulinganisha wakati wa kuamua bei dira. Kwa hiyo, kuanzia msimu unaokuja, Serikali vile vile sasa na wadau wengine watafahamu upande wa pili wa hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na wakulima ambao wamelima tumbaku lakini hawajawekwa kwenye utaratibu wa ununuzi, kauli ya Serikali ni kwamba tumbaku inazalishwa na inauzwa kwa kupitia Vyama vya Ushirika, ni kilimo cha mkataba. Ni vigumu sana kumhakikishia mkulima soko kama hakukuwa na makubaliano kabla ya kilimo. Kwa hiyo, tunaendelea kuwakumbusha wakulima kwamba ni vizuri wapitie utaratibu wa Vyama vya Ushirika ili kuweza kuingia mkataba na makampuni yanayonunua tumbaku kwa sababu ni zao ambalo hupati bei nje ya utaratibu wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutaendelea kuboresha mfumo ikiwa ni pamoja na kuboresha Vyama vya Ushirika kwa sababu changamoto kubwa iliyopo katika zao la tumbaku ni kwa sababu vyama vingi vya ushirika vina madeni. Mkoa wa Tabora ni Mkoa wa mfano kabisa, kwa hiyo, mara nyingi sana imetokea kwamba wakulima wengi hawataki kuuza kwenye mfumo wa Vyama vya Ushirika kwa sababu vyama vinadaiwa. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya Vyama vya Ushirika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe; muda wetu unakwenda sana na wote tunapenda kuuliza maswali. Tukiyafanya maswali marefu sana, nafasi anapata yule mwenye swali la msingi tu. Kwa hiyo, tufupishe maswali yetu ya nyongeza.

Mheshimiwa Sakaya, swali la nyongeza fupi.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali inatambua mchango wa zao la tumbaku kwenye uchumi wa Taifa hili na hivi tunavyoongea makampuni kwenye Vyama vya Ushirika hawajatoa makisio kabisa maeneo mengine na maeneo mengine wametoa makisio madogo sana, kiasi kwamba wakulima wengi mwaka huu wanashindwa kwenda kulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali iweke *commitment* hapa, itafanya utaratibu gani wa haraka kuhakikisha makampuni haya yanatoa makisio kwenye Vyama vya Msingi ili wakulima ambao wanalima miaka yote waweze kulima kwa sababu ndiyo sehemu ya maisha hayo? Nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa katika msimu unaokuja, makisio yamekuwa ni ya kiasi kidogo kuliko msimu uliopita. Makisio ya msimu unaokuja ni kilo milioni 55.9 wakati msimu uliopita ni kilo milioni 60. Kwa hiyo, maana yake ni tumbaku kidogo itanunuliwa ukilinganisha na msimu uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, shida hii imetokea kwa sababu kulikuwa na kutoelewana katika bei ya dira kati ya makampuni na Vyama Vikuu. Kwa hiyo, Serikali inachojaribu kufanya ni kuweka mikakati ili makubaliano ya bei yaweze kufanyika mapema ili katika msimu mwingine tusije tukapunguza hizi kilo, ila ziongezeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunachoweza kusema kwa sasa ni kwamba, tayari makubaliano yameshatokea, sisi tunaangalia huko mbele kuhakikisha kwamba tunaongeza kilo ambazo zitanunuliwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso, swali fupi la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali na kwa kiwango kidogo kitakachozalishwa mwaka huu:-

Je, Serikali imejipanga vipi kutatua tatizo la ukosefu wa *classifiers* ambao wanafanya msimu wa zao kuwa mrefu sana? Ni lini Serikali itakuja na bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuajiri *classifiers* ambao watasaidia kutatua tatizo la tumbaku?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Wizara na Serikali inatambua changamoto iliyopo kwa sababu kuna upungufu wa *classifiers.* Bodi ya Tumbaku iko katika hatua za kuhakikisha kwamba, changamoto hiyo inaondoka na tunaamini kwamba, kwa kiasi kikubwa tunapoelekea kwenye msimu mwingine wa tumbaku tatizo la *classifiers* halitakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wafahamu kwamba, ili kuweza kupata bei nzuri ya tumbaku na kuweza kuuza tumbaku nyingi zaidi ni lazima vile vile tumbaku yetu tufanye iweze kushindana. Kwa sasa tumbaku yetu inakabiliwa na changamoto kubwa. Imekuwa ni vigumu sana kuwapata wanunuzi kwa sababu hatutunzi mazingira na vile vile kwenye kilimo cha tumbaku tunatumia watoto kitu ambacho hakitakiwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ukiwa na tumbaku nzuri namna gani, ni lazima vilevile uangalie mazingira ambayo umezalisha. Kwa hiyo, tuhakikishe kwamba, tunapanda miti, tunafuata masharti yote, lakini vilevile watoto wasifanye kazi kwenye mashamba ya tumbaku.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, sasa aulize swali lake.

Na. 85

**Uvuvi Haramu**

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI** aliuliza:-

Kuendelea kuwepo kwa uvuvi haramu kunatokana na Serikali kutochukua hatua stahiki kwa wanaofanya vitendo hivyo, hasa watengenezaji na wauzaji wa nyavu haramu, badala yake wanabebeshwa lawama wavuvi peke yao:-

Je, Serikali itakomesha lini tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa lipo tatizo kubwa la uvuvi haramu hapa nchini. Katika kudhibiti uvuvi haramu hapa nchini, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kukabiliana na tatizo hili kwa kutoa elimu kwa wadau wanaochangia kuendelea kuwepo kwa uvuvi haramu wakiwemo wenye maduka yanayouza nyavu na zana haramu, wasuka nyavu zenye macho madogo na makokoro, wauzaji wa mabomu , ndoano na zana nyingine zinazozuiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imeendelea kufanya doria za kudhibiti uvuvi haramu na kaguzi kwenye maduka yanayouza zana za uvuvi ili kubaini uwezo wa zana haramu kupitia vituo 25 vya doria vilivyoanzishwa Kwenye maziwa makubwa, mwambao wa Bahari ya Hindi na mipaka ya nchi.

Vile vile kwa kushirikiana na Halmashauri, elimu kuhusu madhara ya uvuvi haramu imeendelea kutolewa kwa wadau mbalimbali wakiwemo wavuvi, watendaji wanaohusika na Ushuru wa Forodha mipakani ili kuwa na juhudi za pamoja za kudhibiti biashara ya zana haramu na kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi kupitia vyombo vya habari na maonesho ya Kitaifa yakiwemo Siku ya Wakulima (Nane Nane) na Siku ya Mvuvi Duniani ambayo hufanyika tarehe 21 Novemba kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ushirikishwaji wa jamii za wavuvi katika kusimamia rasilimali za uvuvi unafanyika kupitia vikundi vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi *(Beach Management Units)* 754 vilivyoanzishwa katika maeneo mbalimbali. Pia vipindi mbalimbali vya televisheni na redio

vimeandaliwa ili kuonesha madhara ya uvuvi haramu na vitaanza kurushwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hatua hizo, Serikali ikishirikiana na Idara ya Mahakama inaendesha zoezi la *Mobile Court* ili kuharakisha mashauri ya wavuvi haramu mara wanapokamatwa. Utaratibu huu umeelekezwa uanze kutumika kwenye maeneo yote yenye kukithiri katika uvuvi haramu na vyombo vyote vya dola vinapaswa kutoa ushirikiano stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako Tukufu nawaomba Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe katika Mabaraza ya Madiwani wazielekeze Halmashauri, Kata, Vijiji na Mitaa kudhibiti uvuvi haramu kwenye maeneo yao na wananchi kutoa taarifa za wavuvi haramu kwa vyombo vya dola ili hatua stahiki zichukuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Halmashauri zote nchini zielimishe jamii za wavuvi na wadau wengine kuhusu madhara ya uvuvi haramu ili kusimamia rasilimali za uvuvi na kuwa na uvuvi endelevu kwa ajili ya kuwapatia wananchi ajira, chakula, kipato na mapato kwa Taifa kwa ujumla. Ni kwa njia hii Taifa litaweza kudhibiti uvuvi haramu hapa nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chegeni, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili. Swali la kwanza, kwa kuwa hizi zana haramu, yaani nyavu pamoja na zana nyingine zinatengenezwa na viwanda vilivyoko hapa nchini na zinaagizwa kuingia hapa nchini na wafanyabiashara: Je, Serikali inachukua hatua gani kwa hao watu ambao wanaleta zana haramu hapa nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa wavuvi haramu hasa ni watu ambao wanajitafutia riziki zao, wengi wamenyang'anywa zana zao na kuchomwa moto ili kuitikia agizo la kisheria la nchi: Je, Serikali ina mpango gani kuwasaidia hao wananchi ambao maisha yao yote yanategemea uvuvi lakini kwa sasa hawawezi kufanya kwa sababu wanakiuka sheria? Wanasaidiwaje kupata mikopo angalau waweze kuendesha maisha yao, lakini pili kufundishwa namna endelevu ya kufanya uvuvi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chegeni umeuliza maswali manne katika mawili. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi chagua mawili kati ya hayo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijaishia tu katika kukamata makokoro na zana nyingine haramu zinazotumika katika uvuvi, lakini vile vile kuhakikisha kwamba, pale yanapotengenezwa na yanapotokea, vilevile wanaohusika wanakamatwa.

Waheshimiwa Wabunge, kama mtakumbuka, ni karibuni tu meli iliyoingia katika bandari ya Dar es Salam ilishikwa ikiwa imebeba zana mbalimbali za uvuvi zikiwepo zana za kutengeneza makokoro na nyavu ndogo ambazo inaaminiwa zingeweza kutengeneza mpaka nyavu 20,000. Huo ni mfano tu wa kuonesha kwamba siyo tu tunakamata wavuvi, lakini vile vile hata viwanda na hata katika kuingiza vile vile tunadhibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ifahamike tu kwamba, ugumu unaotokea ni kwamba zana za uvuvi au vifaa vinavyotumikia kutengeneza zana za uvuvi vile vile zinatumika kutengeneza vitu vingine ambavyo ni halali. Kwa mfano nyavu, siyo kwamba unakuta hasa kwamba ile bidhaa inayotoka kiwandani ni haramu; inaweza ikawa inatumika kwa ajili ya vitu vingine ambavyo vinaruhusiwa kisheria. Kwa hiyo, kidogo inaleta shida, lakini pale tunapobaini moja kwa moja kwamba ni kifaa au ni zana ambayo inaenda kutumika kufanya uvuvi haramu au kutengeneza zana za uvuvi haramu, tunachukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, ni kuhusu msaada gani Serikali inatoa kwa wavuvi wadogo? Nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kupitia Wizara hii, imeweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba wavuvi wadogo wanaweza kupata mikopo kupitia katika Benki yetu ya Kilimo, lakini vile vile kuna mikopo ambayo inapatikana kwa ajili ya pembejeo kupitia Mfuko wa Pembejeo. Tayari Benki ya Uwekezaji ambayo nayo ina fursa kwa ajili ya mikopo na Wizara pia inakopesha vikundi mbalimbali vya wavuvi. Kwa hiyo, kuna fursa mbalimbali kwa vikundi na wavuvi ambao watahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha fursa zilizopo kwa ajili ya kutoa mikopo, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri mbalimbali imeendelea kutoa elimu kuhusu uvuvi endelevu na uvuvi bora kwa kupitia vikundi mbalimbali vya *Beach Management Unit* na tayari katika maeneo mengi ya nchi yetu, elimu hii imetolewa, lakini kama nilivyosema tunatoa elimu kupitia vyombo vya habari kama *television* na tunaamini imesaidia sana kupunguza tatizo la uvuvi haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu, uvuvi haramu ni kama uhalifu mwingine. Hata watu wakiwa na elimu namna gani, bado mara nyingi kuna tabia ya wahalifu kuendelea kuwepo, lakini Serikali itaendelea na jitihada za kupambana na uvuvi haramu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante. Mheshimiwa Hamidu Bobali, swali fupi.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Mchinga wameamua kuitikia wito wa kupambana na uvuvi haramu *especially* uvuvi wa mabomu na wameanzisha *BMU* katika maeneo ya Mchinga, Mvuleni, Kijiweni na Ruvu. Je, nini kauli ya Serikali kwenye kuzisaidia na kuzijengea uwezo hizi *BMU* ili ziweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tusaidie majibu mafupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwapongeze sana wananchi wa Mkinga na ukanda huo wa Pwani kwa sababu ni kweli kwamba wameitikia ombi au mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba tunatokomeza uvuvi haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, nipo tayari kuongea naye ili tuone namna gani ya kusaidia Halmashauri yake ili waweze kutoa msaada na elimu kwa wananchi ambao wako kwenye *Beach Management Units.* Kwa hiyo, naomba kwa kuwa yuko kwenye Kamati yangu, tukitoka hapa, tuongee, tuangalie namna ya kusaidia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Majimbo yote ya Kanda ya Ziwa tunategemea uvuvi na tumekuwa tukiona kweli jitihada za Serikali katika kupambana na wavuvi haramu kuchoma nyavu na vitu vingine; lakini zile samaki zinazovuliwa na wavuvi haramu zinauzwa viwandani. Hatujawahi kuona hata siku moja *operation* inapelekwa kwenye viwanda na kwenye maduka. Je, Mheshimiwa Waziri anatuhakikishiaje Wabunge wa Kanda ya Ziwa atafanya lini ziara na kulifanya zoezi hili kuwa endelevu kwenye maduka na viwanda vinavyonunua samaki zinazovuliwa na wavuvi haramu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, vita dhidi ya uvuvi haramu kama tulivyosema ni vita kwa mtu yeyote ambaye anajihusisha na uvuvi haramu kuanzia uagizwaji wa zana ambazo zinatumika kwenye uvuvi haramu wenyewe, lakini vile vile hata kwenye samaki na biashara ambayo inatokana na uvuvi haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, hii vita haimbagui mtu yeyote, haitamwacha mtu yeyote na tayari Mheshimiwa Waziri alishatoa tamko kwamba watu wote wanaojihusisha na uvuvi haramu wamepewa fursa ya ku-*surrender* vifaa vile kwa sababu kuna

*operation* kubwa. Nimwahidi tu kwamba, hiyo *operation* itakapokuja itaenda vile vile kwenye viwanda na mtu yeyote ambaye anajihusisha na biashara ya uvuvi haramu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 86

**Uanzishwaji wa Benki ya Kilimo na Mpango wa Kuiwezesha Mtaji**

**MHE. ROSE K. SUKUM** aliuliza:-

Watanzania 89% wanategemea shughuli za kilimo na wengi wanaojihusisha na kilimo ni watu wa kipato cha chini. Serikali katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ilianzisha Benki ya Kilimo, kwa mujibu wa Mpango huo kuanzia mwaka 2011/2012 hadi 2015/2016 ilitakiwa kutoa kila mwaka shilingi bilioni 100 ili Benki hiyo iwe na mtaji wa shilingi bilioni 500; lakini hadi sasa katika kutekeleza mpango huo Serikali imepeleka shilingi bilioni 60 tu:-

(a) Je, ni lini Serikali itatekeleza matakwa ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ya kwanza katika dira ya mwaka 2025 ya shilingi bilioni 100 kila mwaka?

(b) Je, Benki hiyo ina mpango gani wa kuwafikia wakulima wadogo ambao ndio nguzo kuu nchini Tanzania katika kuondoa umasikini wa kipato?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Maendeleo ya Kilimo imezunduliwa rasmi mwezi Agosti, 2014. Serikali ina nia thabiti ya kuhakikisha benki hiyo inapata mtaji wa kutosha ili kuiwezesha kutimiza lengo lililokusudiwa la kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa wakulima wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutenga fedha hatua kwa hatua na katika bajeti ya 2016/2017, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 200 ili kuiongezea benki hiyo mtaji. Katika kumaliza tatizo la mtaji, Serikali imejizatiti kuongeza mtaji huo kupitia hati fungani ya mtaji isiyo ya fedha taslimu katika

maana ya *(Non-Cash Bond)* yenye thamani ya shilingi bilioni 800 itakayolipwa kwa kipindi cha miaka sita kuanzia mwaka ujao wa fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kupitia ujio wa Makamu wa Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)* yamekuwepo mazungumzo baina ya *AfDB* na *TADB* ili kuiongezea mtaji *TADB*. Kwa vile mkopo huo utakopwa na Serikali, majadiliano baina ya Wizara ya Fedha na Mipango na Benki hiyo yanaendelea ambapo yatakapokamilika, yatawezesha Benki ya Kilimo kuwa na mtaji mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Benki hii wa kuwafikia wakulima wadogo umejikita katika kuvijengea uwezo vikundi vya wakulima ili viweze kukopesheka na kuwa na uwezo wa kurejesha mikopo hiyo. Benki ya Kilimo imeanza kutoa huduma ya mikopo katika mikoa sita ikilenga kuwajengea uwezo wakulima wadogo kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa, Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, Mfuko wa Pembejeo na Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa mpango huo, Benki ilianza kwa kuvijengea uwezo vikundi 89 vya wakulima wadogo vyenye jumla ya wakulima 21,563 na kati ya hivyo, jumla ya vikundi nane vilitimiza masharti ya msingi ya kuweza kukopa. Vikundi hivyo vipo katika Mkoa wa Iringa na vina wakulima wadogo wapatao 800. Vikundi hivyo nane vimeshapata mikopo yenye thamani ya jumla ya sh. 1,006,822,010/=.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rose Sukum, swali la nyongeza.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ambayo kwa kweli hayatekelezeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili lilipitisha Mpango wa Miaka Mitano 2011/2012 hadi 2015/2016 na swali langu ndiko lilikoelekea, lakini kitu cha kushangaza ni kwamba, tuliamua kwamba Bunge hili shilingi bilioni 100 ziwe zinatengwa na zinatolewa kila mwaka kwa ajili ya benki hiyo kama mtaji ambapo ni shilingi bilioni 60 tu zilizotolewa katika benki hiyo kwa miaka mitano. Je, shilingi bilioni 440 ambazo hazikutolewa na Serikali hii, ziko wapi? Tunataka kujua, kama hamna huo mtaji, hiyo Benki ya Mikopo itafanyaje kazi kwa Watanzania ambao ni wakulima 98%? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; nasikitika sana kuwadanganya Watanzania. Hii benki imeundwa kwa ajili ya kuinua uchumi wa wakulima wadogo wadogo. Wako wakulima zaidi ya 98% nchini. Leo tangu benki imeanzishwa imekwenda Iringa tu na kuwapa vikundi vinane tu shilingi bilioni

moja: Je, kati ya zile shilingi bilioni 60, nyingine zilikwenda wapi kama ni shilingi bilioni moja tu zilitolewa kwa hao wakulima ambao ni wachache? Je, asilimia..

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sukumu, hilo ni la tatu, umeshauliza mawili. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na…

Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba ukae. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

*(Hapa Waziri wa Fedha na Mipango alihamia microphone nyingine baada ya kuwa yake haiwaki)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, microphone yako itawaka, nilikuwa nimezima hapa. Kwa hiyo, washa ya kwako.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kesho tunatarajia kwamba tutafanya *negotiation* na *African Development Bank* kwa ajili ya mkopo nafuu wa *UA* milioni 50 lakini pia *UA* milioni 25 ambao tunatarajia kwamba utakuwa ni mkopo nafuu ambao Serikali ita-*own land TADB* kwa ajili ya kuboresha mtaji wa benki hiyo iweze kuendelea kufanya kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya fedha zote hizo zile 50 za kwanza ni takriban shilingi bilioni 150 na hizi nyingine ni takriban shilingi bilioni 75. Kwa hiyo, Serikali inafanya jitihada ya dhati kabisa kuongeza mtaji wa *TADB.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili; niseme tu kwamba, Benki hii imetoa mikopo kwa vikundi mbalimbali zaidi ya hivyo ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri amevieleza, Mheshimiwa Rose Sukum naweza nikakupatia orodha ya vijiji ambavyo vimepatiwa jumla ya bilioni 5.9 kwa Mikoa ya Iringa, Morogoro na Tanga hadi hivi sasa na naweza nikatoa hii taarifa ya mikopo iliyotolewa hadi kufikia tarehe 31 Oktoba.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, swali la nyongeza.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Kulingana na majibu ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba, hivi karibuni tutapata mikopo kutoka Benki ya Dunia na sehemu mbalimbali kwa ajili ya kuwezesha kuwa na unafuu, niseme tu kwamba, Benki hii ya TADB kwanza iko kwenye Kanda, kwa mfano katika Kanda ya Ziwa iko Mwanza. Wakulima kwenda mpaka Mwanza kufuatilia mkopo huu kwa kweli inakuwa ni tabu na wanatumia gharama kubwa.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati iweze kuhakikisha Benki hii inafika mpaka vijijini au kwenye Makao Makuu ya Wilaya ili kuwawezesha wananchi wengi kufaidika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu niseme kwamba Serikali inaona umuhimu wa kupeleka huduma za benki hii kutoka kwenye Kanda mpaka katika ngazi za chini zaidi na ndiyo dhamira ya Serikali, lakini ni vema twende taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kwanza ambayo inafanywa na Serikali sasa hivi ni kuiongezea mtaji benki hiyo, kazi ya pili ambayo sikuisema mwanzo ni kuimarisha *Management* ya *TADB* yenyewe ili iweze kufanya kazi hiyo, yote mawili yakifanyika kwa pamoja hakika tutahakikisha kwamba benki hiyo inajitanua mpaka katika ngazi husika kuwafikia wananchi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali fupi.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Dhamira ya Benki ya Kilimo ni kuwasaidia wakulima wadogowadogo, lakini kwa muda mrefu wanaokopa katika benki hii wengi ni wakulima wakubwa ambao pia wanakopesheka katika mabenki mengine.

Swali langu kwa Mheshimiwa Waziri, ni lini sasa Serikali itahakikisha benki hii inawanufaisha wakulima wadogowadogo ambao wengi wako vijijini na si wale wakulima wakubwa ambao wanaweza kukopesheka katika mabenki mengine? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hao ambao wanasemwa ni wakubwa ambao wanakopeshwa na Benki ya Kilimo, benki hii imewakopesha wakulima wadogowadogo katika mikoa ambayo nimeitaja katika vikundi. Mpaka sasa katika hiyo mikoa niliyotaja, vimekopeshwa vikundi 89 ambavyo vina wakulima wadogowadogo 21,526 na hawa wanaokopeshwa wanakopeshwa mikopo midogomidogo kutegemea, wengine wanapata mikopo miaka miwili, wengine miwili mpaka mitano na wengine mitano mpaka 15. Kwa hiyo, si kweli kwamba benki hii imekuwa inakopesha wakulima wakubwa tu. Tunawakopesha pia vikundi vya wakulima wadogowadogo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Cosato David Chumi.

Na. 87

**Kupeleka Umeme katika Vijiji vya Jimbo la Mufindi Kaskazini**

**MHE. COSATO D. CHUMI (K.n.y. MHE. MAHMOUD H. MGIMWA)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Kata ya Ikongosi likiwemo na Gereza la Ilupilo, Kata ya Ikweha yenye Vijiji vya Ukelemi, Uyela, Ugenza, Uhambila, Makongomi, Matelefu, Utosi pamoja na Mbugi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, lililoulizwa na Mheshimiwa Chumi, Mbunge wa Mafinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya kufikisha umeme katika maeneo yote nchini ikiwa ni pamoja na maeneo ya Vijiji vya Mufindi Kaskazini. Aidha, Vijiji vya Kata ya Ikongosi likiwemo Gereza la Ilupilo, Kata ya Ikweha, Vijiji vya Ugenza, Makongomi, Matelefu, Mbugi, Uhambila, Ukelemi, Utosi na Uyela vitapatiwa umeme kupitia mradi kabambe wa *REA* Awamu ya Tatu. Ujenzi wa mradi huu utaanza mwezi Desemba, 2016 na kukamilika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kupeleka umeme kwenye vijiji hivyo pamoja na Wilaya nzima ya Mufindi itahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33, yenye urefu wa kilometa 242, ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometa 81, ufungaji wa *transformer* 24, pamoja na kuwaunganishia wateja wa awali 3,533. Kazi hizi zitagharimu shilingi bilioni 11.92.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cosato David Chumi, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kwa niaba ya Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kuna mradi wa *densification na underline*

*transformer.* Mradi huu unafikisha umeme katika maeneo ambayo *REA* Awamu ya Pili ulifikisha katika baadhi ya Kata lakini siyo vijiji vyote.

Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusiana na maeneo ambayo Kata zile zimefikiwa na umeme lakini siyo vijiji vyote na chini ya mradi huo wa *densification* na *underline transformer* inaeleza kwamba unaweza kufikisha umeme ndani ya umbali wa kilometa 10, nini kauli ya Serikali kwa wananchi wa maeneo hayo?

Swali la pili, Mji wa Mafinga ni kati ya miji michache inayokua kwa kasi hapa nchini na ndiyo kitovu cha shughuli za uchumi za Wilaya ya Mufindi, lakini maeneo mengi hayajafikiwa na umeme kama vile Machinjio Mapya, Makalala, Ihongole, Mwongozo na Lumwago. Je, Serikali iko tayari kujenga *sub-station* ili kuwezesha wananchi kufanya shughuli zao za kiuchumi kwa asilimia mia moja? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa mradi wa *REA* awamu ya tatu kimsingi una sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ni kupeleka umeme katika maeneo yote ambapo kuna miundombinu ya awamu ya pili lakini *component* ya pili na kwa niaba ya Mheshimiwa Chumi na Waheshimiwa wananchi wa kule Mufindi pamoja na Mafinga ni kwamba awamu ya tatu itahusisha sasa kupeleka umeme kwenye vitongoji na vijiji vyote kupitia mradi aliosema *densification.*

Mradi wa *densification* unapeleka umeme kutoka kwenye miundombinu mikubwa kwenda kwenye vijiji na vitongoji. Nimhakikishie Mheshimiwa Chumi kwamba, vijiji vyake vyote vya *Sao Hill* vitapata umeme kupitia mradi huu, hata pale Changarawe atapata umeme. Isalavanu, Itubiravamu na Ibongoboni vyote vitapata umeme kupitia mradi huu. Nimhakikishie hata Kijiji chake cha Mkalala pamoja na Bubirayinga vitapata umeme kupitia mradi huu wa Itubiravamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili juu ya maeneo ya Mafinga. Ni kweli kabisa maeneo ya Mafinga sasa yana kazi kubwa. Mafinga sasa inapata umeme kutoka Iringa ambako ni kilometa 70, pia kutoka Mgololo kilometa 60, sasa ipo haja kwa kweli kujenga *sub-station.* Nimhakikishie tunajenga *sub-station* mwaka wa fedha unaokuja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Juma Nkamia, swali fupi la nyongeza.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja tu dogo la nyongeza. Katika mwaka huu wa fedha kuna baadhi ya vijiji katika Wilaya ya Chemba vimeorodheshwa kwamba vitapata umeme. Nataka Mheshimiwa Waziri na Serikali nzima hii inihakikishie mradi huu utaanza kutekelezwa lini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, miradi yote niliyotaja ya *REA* awamu ya tatu inaanza kutekelezwa tarehe 15 Desemba, mwaka huu na itakamilika 2019. Kwa hiyo, eneo la Chemba Mheshimiwa Nkamia nimhakikishie vijiji vyake vyote, shule zake zote, pamoja na vituo vya maji vitapatiwa umeme kuanzia mwezi niliotaja na kuishia 2019.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, tunaendelea Waheshimiwa, Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga Mbunge wa Chilonwa, sasa aulize swali lake.

Na. 88

**Mpango wa Umeme Vijijini**

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA** aliuliza:-

Serikali ilikuja na mpango mzuri wa umeme Vijijini na kupitia mradi wa *REA* kukawa na *REA* I, *REA* II na sasa *REA* III na Serikali iliahidi kwamba miradi yote ya *REA* II ambayo haijakamilika hadi kuanzishwa kwa *REA* III itatekelezwa sambamba na *REA* III:-

(a) Je, ni lini Serikali itatekeleza miradi yote ya *REA* II Jimbo la Chilonwa katika Vijiji vinne vya Kata ya Msamalo(Myunga, Msamelo, Mnase na Mlebe) Vijiji viwili vya Kata ya Zajilwa (Zajilwa na Mayungu) na Kijiji cha Kata ya Manchali?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuviingiza vijiji ambavyo havikuwepo kwenye mpango wa *REA* II katika mpango wa *REA* III?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, Mbunge wa Chilonwa, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za kupeleka umeme katika Vijiji vya Kata za Manchali, Msamalo na Zajilwa kupitia mradi wa *REA* Awamu ya II zitakamilika mwezi Novemba mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji vyote vya Jimbo la Chilonwa ambavyo havikupata umeme kupitia REA awamu ya II vitapatiwa sasa umeme kupitia *REA* Awamu ya III. Kazi ya kupeleka umeme kwenye vijiji hivyo itahusisha ujenzi wa umeme msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 68, ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometa 301, pia ufungaji wa *transformer* 45. Mradi huu pia utapeleka umeme kwa wateja wa awali 11,276. Kazi zitaanza mwezi Desemba mwaka huu na kukamilika mwaka wa fedha 2019. Gharama ya mradi huu ni shilingi bilioni 12.09

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Makanyaga swali la nyongeza.

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante. Naishukuru Serikali kwa majibu mazuri na naamini kwamba haya yaliyozungumzwa yote yataenda kutekelezwa. Naomba kuongeza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Vijiji vingi vya Jimbo langu ni vikubwa sana na kwa kuwa, umeme huu wa *REA* umekuwa ukifikishwa kwenye maeneo ya kati ya vijiji tu. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuusogeza umeme huu sasa kwenye vitongoji vilivyo mbali na maeneo ya kati ya vijiji ili wananchi hao katika vitongoji hivyo nao waweze kunufaika na umeme huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, namshukuru sana Mheshimiwa Makanyaga kwanza kwa kuuliza swali hili.

Kwa kuwakumbusha tu, ni kweli kabisa kwa awamu ya II tumepeleka kwenye vituo, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Chilonwa kwamba awamu ya III inapeleka sasa kwenye vitongoji na kwenye vijiji vyote na kwenye mashine na kwenye taasisi za jamii ikiwemo shule. Nimhakikishie hata Kijiji chake Mheshimiwa Chilonwa cha Chalinze sasa kitapata umeme, Kijiji chake cha Kawawa kitapata umeme, Kijiji cha Malichela kitapata umeme, Kijiji cha Membe kitapata umeme, Kijiji cha Bwawani nacho kitapata umeme. Kwa hiyo, nimhakikishie kuwa vijiji vyote vitapata umeme. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.  Swali la nyongeza Mheshimiwa Latifah.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, mpango huu wa *REA* upo kwa ajili pia ya Mkoa wa Lindi hadi Lindi Vijijini, lakini mpaka sasa hivi maeneo mengi ya Mkoa wa Lindi bado hayana umeme. Je, ni vijiji vingapi katika Mkoa wa Lindi ambavyo vinatarajia kupewa umeme wa *REA* katika bajeti ya mwaka 2016/2017?

**NAIBU SPIKA:** Swali moja tu Mheshimiwa, wewe umeuliza swali la nyongeza. Halafu bajeti aliyoiuliza ni ya mwaka 2016/2017, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji vinavyotarajiwa kuunganishwa umeme katika Mkoa wa Lindi kupitia *REA* Awamu ya III ni 117. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza. Katika Mkoa wa Dar es Salaam bado kuna maeneo mbalimbali katika Kata ya Mianzini maeneo ya Mponda Wilaya ya Temeke, Chamanzi, Tuangoma, Somangila, Kimbiji, Pemba Mnazi, Vijibweni, Chanika, Majohe na Pugu, vyote hivyo bado havijapata miradi ya umeme kusambazwa katika vijiji mbalimbali.

Je, Mheshimiwa Waziri, ni lini sasa Serikali itasambaza umeme pembezoni mwa vijiji hivi vya Mkoa wa Dar es Salaam?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa maeneo ya Dar es Salaam maeneo mengi hatujapeleka umeme na hasa Kigamboni. Awamu ya kwanza tunayofanya tunapanga kujenga *sub-station* Kigamboni kwa sababu *population* ya sasa ni kubwa. Kwa hiyo, vitongoji vyote vya Kigamboni vitapelekewa umeme kupitia Awamu ya II. Pia maeneo ya Chanika, maeneo ya Gongo la Mboto, maeneo ya Kinyamwezi, maeneo ya Buyuni na yenyewe yanapelekewa kwenye mpango huu wa *REA* unaoanza mwezi Desemba. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Twahir Awesu Mohammed, Mbunge wa Mkoani, sasa aulize swali lake.

Na. 89

**Watuhumiwa wa Uhalifu Kunyanyaswa na Polisi**

**MHE. TWAHIR AWESU MOHAMMED** aliuliza:-

Kumekuwa na malalamiko ya baadhi ya watuhumiwa wa makosa mbalimbali kunyanyaswa na kupigwa na vyombo vya ulinzi na usalama hasa Jeshi la Polisi na kusababisha matatizo makubwa ya kiafya kwa watuhumiwa:-

Je, Serikali inasema nini juu ya Polisi wanaofanya vitendo hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Twahir Awesu Mohammed, Mbunge wa Mkoani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa kunawezekana kukawa na malalamiko katika vituo vyetu vya Polisi kwa mujibu wa *PGO* Na.103 (1) inaelekeza kuwa japokuwa lalamiko ni dogo kiasi gani lazima Kamanda wa eneo afungue jalada na kuchunguza ukweli wa malalamiko hayo na ikibainika Askari aliyefanya kitendo hicho atachukuliwa hatua za kinidhamu dhidi yake kama vile kukatwa mshahara ama kufukuzwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imeweka mfumo madhubuti wa kushughulikia malalamiko hayo kwa Mikoa yote ya Polisi, Makao Makuu ya Polisi na kama haitoshi Wizarani kwangu kuna dawati la kushughulikia malalamiko.

Kwa nafasi hii, nitoe rai kwa wale wote ambao hawatendewi haki wafuate utaratibu huo na hatua zitachukuliwa kikamilifu. Pia, Jeshi la Polisi limeendelea kutoa elimu kupitia mfumo wa mafunzo kazini, vilevile mafunzo ya vitendo ili kuhakikisha kuwa Askari wote wanafanya kazi zao kwa weledi na usasa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Twahir Awesu Mohammed, swali la nyongeza.

**MHE. TWAHIR AWESU MOHAMMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri, naomba nimuulize maswali madogo mawili. Je, Serikali iko tayari kwa sasa kupokea majina ya wananchi walionyanyaswa na kupigwa chini ya mikono ya Jeshi la Polisi?

Swali la pili; je, Serikali imewahi kuwatia hatiani Askari Polisi waliotajwa kuwanyanyasa raia kulingana na ukubwa wa makosa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara tuko tayari kupokea majina ya aina hiyo na tuna kitengo rasmi ambacho kinashughulikia malalamiko ya wananchi na mara wanapopokea wakijiridhisha huwa wanachukua hatua.

Kuhusu swali la pili kama Serikali ama Wizara iliwahi kuchukua hatua kwa watu ambao wamelalamikiwa kunyanyasa wananchi. Wanachukua mara kwa mara na jana tu tulisema zaidi ya Askari 154 tayari waliwahi kuchukuliwa hatua hizo na hivi tunavyoongea Waheshimiwa Wabunge hata leo kwenye magazeti mmesikia kuna Askari wamefukuzwa kazi jana tu kwa kuwanyanyasa wanafunzi kinyume na taratibu za sheria za utendaji wa kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Godfrey Mgimwa.

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa, tatizo ambalo linaonekana la kuwanyanyasa wananchi ambalo linafanywa na Polisi linafanana sana na malalamiko mbalimbali ambayo yanatoka katika Idara ya Uhamiaji kwamba Idara ya Uhamiaji nao wanafanya unyanyasaji mkubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningeomba kujua kwa sababu katika Idara hii kuna watumishi ambao hawajalipwa mishahara yao kwa kipindi kirefu sana. Serikali inasema nini au ina tamko gani kuhusu watumishi hawa wa ajira mpya ambao hawajalipwa mishahara yao ili Serikali iweze kutoa majibu yanayoeleweka, kwamba watalipwa lini mishahara yao watumishi hao wa ajira mpya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza suala la watu kunyanyaswa lina pande mbili. Sisi tumesema yale ambayo tunajiridhisha nayo tunachukua hatua, lakini suala la kutimiza wajibu ni suala la Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Askari wapya ambao hawakuwa wamelipwa mishahara yao, nimhakikishie Mbunge kwamba tatizo hilo kweli lilikuwa kubwa na niwaombe radhi wale askari wetu ambao wamefanya kazi

kwa muda bila kupata haki yao, kwa sababu mshahara na posho siyo hisani ni haki yao. Serikali imeshafanya kazi kubwa. Mwanzoni kulikuwa na idadi kubwa waliokuwa wanadai zaidi ya 297, lakini Askari 181 tayari walishapewa mishahara yao na watapewa na yale ambayo yalikuwa malimbikizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na tatizo ndani ya Wizara na nilishatoa maelekezo. Kuna watu bado wanafanya kazi kwa mazoea wakidhani labda Askari anatakiwa aishi kimsoto msoto hivi. Hakukuwa na sababu ya kutokupeleka majina yale Utumishi na kuyaingiza kwenye mfumo ili waweze kulipwa. Kuna watu kwa sababu zao wenyewe na nilielekeza wachukuliwe hatua, wamekaa na majina hayo kwa muda mrefu bila kupeleka Utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelekeza kwa wale wachache ambao walikuwa bado wanafanyiwa uhakiki waharakishe haraka, wale wanaostahili waweze kulipwa na walipwe na malimbikizo yao ili waweze kufanya kazi bila manung'uniko. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali Salim, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amesema hapa kwamba shida ni watu ambao wamewasababishia wafanyakazi hawa ambao wanafanya kazi zao kwa nia ya dhati ya kuitumikia nchi yao. Naomba Waziri atoe *commitment* ni lini wafanyakazi wote hasa wa Idara ya Uhamiaji ambao wameanza kazi zaidi ya miezi mitano sasa, hawajalipwa mshahara hata mwezi mmoja, , watalipwa malimbikizo yao ya mishahara mara moja?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba *commitment* ya Serikali. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa niunge mkono majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Sasa hivi inapotokea ajira mpya siyo kwamba hawajalipwa kwa miezi minne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyoeleza; kulikuwa na ajira mpya za Maafisa Uhamiaji 297, Maafisa wa Utumishi wa Idara ya Uhamiaji ni lazima wafanye *higher action* katika mfumo wetu wa taarifa za kiutumishi na mishahara, walikuwa hawajafanya. Kwa hiyo, ingekuwa ni vigumu wao kuweza kulipwa. Kwa mwezi huu tayari tunaendelea vizuri watakuwa wameshalipwa. Pia kuhusiana na masuala ya malimbikizo mara tu Maafisa Utumishi wa Uhamiaji

watakapokuwa wamefanya hizo *higher action* na *pending salaries arrears automatically* katika mfumo wataweza kulipwa mara moja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE C. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa, malalamiko juu ya Polisi yamekuwa mengi sana. Wamekuwa wakinyanyasa raia kila siku, kila mkoa. Hivi tu majuzi wiki iliyopita nimeshuhudia Polisi anaejulikana kwa jina la Msafiri akimpiga raia hapa Dodoma kwa amri ya bosi wake. Je, nataka kujua hivi hawa Polisi wako juu ya sheria kwa sababu wanapopiga raia wanapokwenda Polisi wenyewe ndiyo wamekuwa wakiandika kesi. Je, haki itatendeka kweli? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, maswali yameulizwa mawili hapo. Kwa hiyo chagua moja kati ya hayo ujibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, linapotokea tukio la Askari mmoja ama wawili kufanya jambo hilo si jambo la Jeshi la Polisi linakuwa la Askari mhusika, mtu mmoja na sio utaratibu wa Kiutumishi wa Kipolisi. Polisi kama Jeshi la Polisi Waheshimiwa Wabunge wote tunakubaliana kwamba wanafanya kazi nzuri kwa Taifa letu na ndiyo maana usalama upo. Kwa maana hiyo, inapotokea jambo mahsusi kama hilo tuendelee kuwasiliana na Mheshimiwa Mbunge ni mmoja wa *pioneers* wa mambo ya haki kutendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu wetu inapotokea jambo la aina hiyo tuna vitengo ambavyo vinasimamia malalamiko hayo ili haki iweze kutendeka na uzoefu unaonesha haki imekuwa ikitendeka na hata hatua zinachukuliwa katika baadhi ya maeneo na ninyi ni mashahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Catherine aendelee kusukuma hivyo utaratibu wa haki kutendeka na kwa hilo ambalo amelitaja tutalifuatilia ili haki iweze kutendeka.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, sasa ulize swali lake.

Na. 90

**Marekebisho ya Mipaka ya Hifadhi ili Kupata Ardhi ya Kilimo**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na malalamiko baina ya wakulima na Mamlaka ya Mapori ya Hifadhi ya Misitu, kwa sababu ya kuongezeka kwa watu lakini ardhi haiongezeki, hivyo kufanya ongezeko hili la watu wakose ardhi kwa shughuli zao za kilimo na mambo mengine yahusuyo ardhi:-

Je, ni lini Serikali italeta Bungeni Muswada wa Sheria husika ili kufanya marekebisho katika mipaka ya Hifadhi hizo ili kupata eneo la kilimo kwa wananchi walioongezeka ambao hawana maeneo ya kilimo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa idadi ya Watanzania inaongezeka siku hadi siku, ambapo 75% ya watu hao wanaishi vijijini na kwamba wananchi wengi wa vijijini wanategemea rasilimali za misitu na ardhi kwa ajili ya maisha yao. Pia, inaeleweka wazi kuwa kasi ya ongezeko la idadi ya watu linachangia katika kuongezeka kwa mahitaji ya mazao ya misitu na ardhi kwa ajili ya kilimo, ufugaji pamoja na makazi. Kukosekana kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji, inachochea kuongezeka kwa kasi ya uharibifu wa misitu na ukosefu wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mahitaji makubwa na umuhimu wa ardhi katika kukidhi mahitaji ya wananchi na maendeleo ya kiuchumi, Serikali inatambua misitu ni muhimu kwa maisha ya viumbe hai, katika kupunguza hewa ukaa, kulinda hewa safi, kupunguza joto la ardhi, kutunza vyanzo vya maji, upatikanaji wa nishati na shughuli mbalimbali za kibinadamu. Hivyo, kwa kutambua umuhimu wa ustawi wa maisha ya wananchi na uhifadhi wa misitu, Serikali inaendelea kuchukua hatua zinazozingatia uwiano kati ya mahitaji ya maendeleo ya wananchi na uhifadhi wa misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua changamoto zinazotokana na upungufu wa ardhi, Wizara inawashauri wananchi wote na Serikali za Vijiji vyote vinavyozunguka misitu ya hifadhi kushirikiana na sekta husika katika kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi itakayolenga kutenga maeneo kwa matumizi mbalimbali kufuatana na mahitaji katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu itaendelea kutoa ushirikiano katika kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ikiwa ni pamoja na hifadhi ya misitu. Vilevile, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge kuwahamasisha wananchi kutumia mbinu za kilimo bora chenye tija na kuibua shughuli nyingine za kiuchumi ambazo hazihitaji matumizi makubwa ya ardhi kama vile ufugaji wa samaki, ufugaji wa nyuki, uanzishaji wa viwanda vidogovidogo na shughuli nyingine ambazo ni rafiki wa mazingira.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa, wananchi wanaoingia kwenye hifadhi ya misitu siyo kwamba wanaingia kwa sababu ya ukatili ni kwa sababu ya kukosa maeneo ya kuishi na kulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano; wananchi wa Wilaya ya Kasulu wanaoingia kwenye pori ya Hifadhi ya Kagerankanda ni kwa sababu watu wameongezeka, ardhi ni ile ile, maeneo ya kilimo yamekuwa ni kidogo. Je, kwa nini, Serikali isiwaruhusu waendelee kulima wakati Serikali inaandaa utaratibu mwingine wa kupima mipaka. *(Makofi)*

Swali la pili; kwa kuwa, ongezeko la watu ni kubwa sana, kwa nini, Serikali isitenge baadhi ya maeneo ya misitu ili wananchi waruhusiwe kuishi na kuwapunguzia tatizo hili la kuhangaika kutafuta maeneo ya kulima?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba wako wananchi ambao wameingia na wamejenga ndani ya maeneo ya misitu na wanakaa humo kufanya shughuli za kibinadamu. Sheria zetu za nchi zinakataza wananchi kuingia na kujenga, kulima ndani ya hifadhi zetu. Kwa hiyo, naomba niwahamasishe wananchi hawa wafuate sheria na wafuate sheria bila shuruti. Kwa hiyo, waondoke kwenye maeneo ya hifadhi na washirikiane na Halmashauri pamoja na Serikali za vijiji vyao kuwapangia maeneo mengine ya kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la watu ni *phenomena* ambayo inatokea dunia nzima. Siyo jambo la Tanzania peke yao, kama ambavyo mmeona, nchi ambazo zinaendelea na zile ambazo zimeshaendelea, idadi ya wakulima inaendelea kupungua mpaka kufikia asilimia 20 katika nchi nyingi za Ulaya au kule Marekani, hii inatokana na watu kufanyakazi zingine, siyo lazima

wote tuwe wakulima, kufanya kazi zingine ambazo mahitaji yake ya ardhi ni madogo kama vile ufugaji wa samaki, ufugaji wa nyuki kuanzisha viwanda vidogovidogo kama nilivyoeleza kwenye swali langu la msingi ili kuhakikisha kwamba maisha yetu yanaendelea, lakini na misitu yetu inakuwepo ili maisha yetu yaendelee kwa ustaarabu ambao unatakikana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukubaliane kwamba muda wetu umekimbia sana. Kwa hiyo. turuhusu wenye maswali pekee kwa ajili ya kumalizia maswali yaliyobaki. Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa sasa aulize swali lake.

Na. 91

**Mpango wa Uchimbaji Visima katika Halmashauri**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Katika mpango wa Serikali wa kuchimba visima katika vijiji 10 vya kila Halmashauri, katika Mji Mdogo wa Makongorosi maji hayakupatikana kwenye kisima kilichochimbwa na kuwa mji huo unakua kwa kasi sana na kero ya maji ni kubwa sana:-

Je, ni lini Serikali itatatua tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Jimbo la Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji katika Mji Mdogo wa Makongorosi ni moja ya miradi ya awali iliyopewa kipaumbele kutekelezwa kwenye mpango wa vijiji 10 kwa kila Halmashauri. Baada ya maji kukosekana kwenye kisima kilichochimbwa, mradi huu haukuweza kuendelea kutekelezwa na jitihada za kutafuta chanzo kingine zinaendelea.

Mradi wa maji wa Mji Mdogo wa Makongorosi umepangwa kutekelezwa upya kwenye Awamu hii ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, ambapo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ya Chunya imepangiwa bajeti ya kiasi cha shilingi milioni 561.5 na kazi zilizopangwa kufanyika ni kutafuta chanzo kingine kufanya usanifu na ujenzi wa miundombinu ya mradi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, swali la nyongeza.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja tu la nyongeza. Katika Mji Mdogo wa Makongorosi na Mji Mkubwa wa Chunya, matatizo ya maji ni makubwa sana. Ni makubwa kiasi cha kuweza kuvunja ndoa za watu wanapofuata maji kwenye visima mbugani.

Sasa toka alipokuwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda aliona Makongorosi na Chunya, Mheshimiwa Kikwete akiwa Rais ameona matatizo ya maji Chunya na Makongorosi na Mheshimiwa Magufuli katika safari yake ya kampeni ameona matatizo ya maji katika Mji Mdogo wa Makongorosi na Mji wa Chunya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka *commitment* kutoka kwa Serikali. Ni lini Waziri pamoja na kwamba ziko milioni 500 sijui anasema zimepangwa kwa mwaka huu, lakini ikija mwisho wa mwaka watasema *Treasury* haijaleta hela. Je, ni lini Waziri au Naibu Waziri atakuja Chunya nimwoneshe hali mbaya ya maji katika Mji wa Makongorosi na Mji wa Chunya ili tukija hapa Bungeni aweze kunijibu vizuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba Mji wa Makongorosi na Chunya una matatizo makubwa ya maji lakini pia, kuna kikundi ambacho kilikuwa kinachimba madini eneo linaitwa Ujerumani, imeonekena pana maji mengi sana. Sasa hivi Wizara inafanya utafiti kama yale maji yanafaa ili yaweze kuwekewa miundombinu yasambazwe katika maeneo ya Makongorosi na Chunya.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya Mheshimiwa Mbunge kwamba ni lini Mheshimiwa Waziri atakuja, hakuna wasiwasi tutatembelea hilo eneo.

**NAIBU SPIKA:** Utatembelea lini Mheshimiwa Naibu Waziri au utajipanga? Maana ukisema tu utatembelea inawezekana ikawa mwaka kesho kutwa hivi!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tutajipanga baada ya Bunge hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

**MHE SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kabla ya swali langu, kwa masikitiko makubwa sana, kama mwanamke naomba kutoa pole nyingi sana kwa Mama Clinton kwa kushindwa uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa swali langu Namba 92 sasa lipatiwe majibu.

Na. 92

**Upungufu wa Huduma ya Tiba Shufaa Nchini**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO** aliuliza:-

Tanzania ina upungufu mkubwa wa huduma ya tiba shufaa *(Palliative Care Services)* ukilinganisha na majirani zetu wa Kenya, Uganda na Rwanda. Hali hii inapelekea wagonjwa wengi walio katika hatua za mwisho za maisha yao kuwa na maumivu na mateso makali sana:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha tiba shufaa inaboreshwa hapa nchini?

(b) Kwa kuwa, kuna upungufu mkubwa wa watoa huduma hii, Je, Serikali inatoa tamko gani au ina mkakati gani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan, wenzako tupo tunajipa moyo hapa, sasa wewe umepata wapi majibu tayari humu ndani? Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi kama Balozi wa wanawake nina masikitiko makubwa sana kwa ndugu Hillary Clinton kupoteza uchaguzi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha huduma za tiba shufaa zinapatikana hapa nchini, Hospitali takriban 35 zikiwemo Hospitali za Rufaa za Kanda za Bugando, KCMC na Mbeya, Hospitali za Mikoa na Wilaya za Mwanza, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Morogoro, Kagera, Kigoma, Mtwara, Pwani, Mara na Tanga zinatoa huduma hii. Aidha, Hospitali za dini zilizopo chini ya *ELCT* kama Hospitali ya Seliani na zingine pia zinatoa huduma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, huduma za tiba shufaa kwa majumbani zimekuwa zikitolewa sambamba kwenye maeneo yenye hospitali zinazotoa huduma hizo, hii ikimaanisha kwamba, watoa huduma za majumbani husaidia kumfikia mgonjwa nyumbani na kumpatia huduma. Kama tatizo litaonekana ni kubwa, hushauri mgonjwa apelekwe hospitali.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu uhaba wa watumishi katika Sekta ya Afya, hivyo Serikali katika Sera ya Kitaifa ya Tiba Shufaa *(National Polliative Care Policy Guideline)* iliyotolewa mwezi Juni, 2016, imeagiza mafunzo yafanyike kuwajengea uwezo watumishi waliopo katika vituo vya afya na hospitali ili watoe huduma hii ya tiba shufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road,* Chama cha Tiba Shufaa hapa nchini *(The Tanzania Palliative Care Association)* na wadau wengine wameanza kusimamia utekelezaji wa sera hii ya tiba shufaa ili kuhakikisha huduma hii inapatikana kwa wagonjwa wanaohitaji na inapatikana kwa wakati wote. Lengo kuu likiwa ni kuwepo na watumishi watano katika kila kituo cha afya wenye uwezo wa kutoa tiba shufaa wakimemo Madaktari, Wauguzi, Wafamasia na Maafisa Ustawi wa Jamii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suzan Anselm Lyimo, swali la nyongeza.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Ni wazi kwamba suala la *Palliative Care* yaani Tiba Shufaa hapa nchini halijaeleweka kabisa, naamini hata wewe labda huelewi na vilevile Wabunge wengi sana hawaelewi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri sasa yuko tayari, kutoa semina kwa Wabunge wote ili wapate uelewa wa maana ya *Palliative Care?* Vilevile, elimu hii pia itolewe kwa wananchi wote ili waweze kulielewa na waweze kuwasaidia wagonjwa wetu ambao wanakufa katika mazingira magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri anakiri kwamba tuna tatizo kubwa la wahudumu wa afya, ambao pia hawana huo uelewa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba, kuna haja kubwa sasa ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na *curriculum* ya *Palliative Care* katika *courses* za *undergraduate* kama wanavyofanya wenzetu wa Kenya

na Uganda ili sasa tuwe na wataalam wa kutosha kwa hii huduma, hasa tukizingatia sasa kwamba kuna magonjwa mengi ya kusendeka *(chronic diseases)* ambayo yako nyingi na kwa maana hiyo, wagonjwa ni wengi na hawapati huduma hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Swali la kwanza, Waziri alikuwa ananinong'oneza hapa, uzuri Waziri wangu anakaa nyuma ya kiti cha kujibia maswali, kwamba yuko tayari kuleta semina kwa Wabunge wote kwa ajili ya kutoa elimu ya Tiba Shufaa *(Palliative Care)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi *Palliative Care* ni nini? Kwenye mfumo wa afya, *Palliative Care* ni huduma ambayo inatolewa kwa wagonjwa ambao ni *terminally ill*, yaani wagonjwa ambao wanaumwa magonjwa ambayo sasa imefika wakati sayansi ya tiba haiwezi kuyatibu. Kinachofanyika sasa ni kutoa huduma ya kupunguza maumivu, lakini pia huduma ya ushauri nasaha na huduma ya kiroho *(Spiritual Services)*. Kimsingi ni kumtibu mgonjwa *holistically* kwa kumtazama kwa ujumla wake, mgonjwa kama mgonjwa kama binadamu na sio kutazama ugonjwa ambao mgonjwa anaumwa.

Mheshimiwa Niabu Spika, swali lake la pili, kuhusu *curriculum* naomba kwanza nieleze jitihada za Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tuna Sera ya Taifa, ambayo inatoa mwongozo kwenye huduma za tiba shufaa, ambayo mwezi Juni, 2016 imeanza kutumika. Sera hii inaelekeza sasa kuanzia mwaka huu vyuo vyote vinavyofundisha masomo ya Udaktari, Uuguzi, Ufamasia na Kada nyingine za afya waweke mtaala kwenye *courses* zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie jukwaa hili la kwako, kuwaagiza watu wote wanaoendesha vyuo vinavyotoa taaluma mbalimbali za kwenye sekta ya afya, kufuata mtaala ambao tayari umeandaliwa na Wizara yetu na waanze kuutumia kwenye masomo yanayoanza mwaka huu. Kwa hiyo, mtaala tunao tayari na nimeshaagiza sasa wautumie kufundishia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa swali letu la mwisho litakuwa ni la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 93

**Wanafunzi Waliofuzu kwa Kiwango cha Diploma na Digrii kwa 2010-2015**

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI** aliuliza:-

(a) Je, ni wanafunzi wangapi walifuzu kwa kiwango cha Diploma na Digrii katika Sekta za Sanaa na Ubunifu, Habari, Teknolojia na Sayansi, Elimu ya Afya kwa Mwaka 2010-2015?

(b) Je, Serikali imefanya tathmini katika maeneo ya utumishi yenye uhaba wa taaluma tajwa hapo juu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi waliofuzu kwa kiwango cha stashahada kwa kipindi cha kati ya mwaka 2010 hadi 2015 katika sekta za Sanaa na Ubunifu *(Fine and Perfoming Arts)* ni 254, Habari yaani waandishi ni 1,565, Teknolojia ya Sayansi ni 12,538 na Elimu ya Afya ni 14,177, jumla walikuwa 28,534. Aidha, kwa upande wa wanafunzi waliofuzu kwa kiwango cha shahada kwa kipindi tajwa, takwimu zinaonesha kuwa katika sekta za Sanaa na Ubunifu ni 136, Habari 2020, Teknolojia na Sayansi ni 11,953 na Elimu ya Afya ni 5,043 ambapo jumla yao walikuwa ni 17,334

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba inaeleweka kuna upungufu wa wataalam katika baadhi ya fani, kama vile Uandishi wa Habari, Afya, Ualimu wa masomo ya Sayansi, Uandishi wa Teknolojia na Gesi, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora tayari imeandaa Andiko*(Concept Note)* kwa lengo la kufanya tathmini ya kina katika sekta mbalimbali, zikiwemo zilizotajwa kwenye kipengele (a) cha swali la msingi ili kuainisha mahitaji na upungufu wa Rasilimali watu, kiidadi na kiujuzi katika Utumishi wa Umma na hatimaye kuweza kuandaa mkakati wa namna ya kushughulikia upungufu utakaoonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati utakaoandaliwa ambao unatarajiwa kukamilika mwaka wa fedha 2016/2017 utaiwezesha Serikali kuwa na matumizi mazuri ya Rasilimali iliyopo ili kufikia Malengo na Mipango ya Taifa ya Maendeleo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Immaculate Semesi, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa, kuna uhusiano chanya kati ya elimu na maendeleo katika sekta za kijamii na kiuchumi; je, ni lini Serikali au Wizara itaona umuhimu wa ku-*link* elimu na maendeleo ya Taifa letu au katika mipango ya maendeleo ya Taifa letu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kuwa, tayari Serikali imeshachelewa kutathmini; je, tuna upungufu wa aina gani au tunahitaji watu wenye elimu ya aina gani ili kuleta maendeleo katika sekta fulani? Wameji-*commit* kwamba mpaka mwisho wa mwaka huu wa fedha watakuwa tayari wamekamilisha huo mkakati.

Je, huu mkakati watau-*link* vipi na Mpango wa Maendeleo wa Taifa hili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri umeulizwa maswali matatu, chagua mawili kati ya hayo uweze kujibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kimsingi Serikali inatambua mahusiano kati ya elimu inayotolewa na ustawi wa jamii au katika kuleta maendeleo. Ndiyo maana msisitizo uliopo sasa hivi ni kuhakikisha kuwa, *course* zote zinazoanzishwa hasa katika vyuo vyetu, ni zile zinazojitahidi kujibu changamoto zilizopo katika jamii zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo basi, baada ya kukamilisha mpango huu ambao umeandaliwa, unaoangalia kwa kina sasa kwa jinsi ambavyo Mpango wetu wa Maendeleo wa Miaka Mitano lakini pia Dira yetu ya Taifa ya mwaka 2020 - 2025, kwamba tunataka kwenda wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, sasa hivi tunataka kwenda kwenye uchumi wa viwanda. Katika uchumi wa viwanda tutahitaji wataalam mbalimbali watakaoendesha viwanda vyetu, vilevile katika hao watakaoendesha viwanda tunategemea humo kutakuwa na mambo ya aina mbalimbali. Kwa mfano, afya zetu ili hao watumishi waweze kufanya kazi zao vizuri. Pia tunategemea kupunguza madhara kwa akinamama waweze kujifungua salama. Kwa hiyo, kutokana na matatizo kama hayo, ndiyo maana hata sisi sasa mitaala yetu lazima ijibu changamoto ambazo zipo katika jamii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Nitaleta kwenu matangazo yaliyotufikia.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la kwanza ni la wageni, tutaanza na wageni waliopo jukwaa la Spika. Kuna mgeni wa Mheshimiwa Spika wa Bunge Mheshimiwa Job Ndugai, ambaye ni Balozi wa Ufaransa hapa nchini, Mheshimiwa Malika Berak. Balozi huyu ameambatana na Afisa wa Ubalozi anayeshughulikia mambo ya siasa Ndugu Claude Brevin. *(Makofi)*

Sasa hawa naona inabidi waongeleshwe Kifaransa hawa. *Bien venue a* Dodoma. Watakuwa wameelewa *(Makofi/Kicheko)*

Wageni wengine waliotufikia asubuhi hii ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge na tutaanza na wageni 11 wa Mheshimiwa Nape Nnauye ambaye ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kutoka Jijini Dar es Salaam, ambao ni waendeshaji wa *project* inayoitwa Tanzania *Miss Super Model* inayojihusisha na masuala ya mitindo wakiongozwa na Ndugu Hussein Sechonge na Ndugu Jokate Mwegelo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 98 wa Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, ambao ni wanafunzi wa Kidato cha Tano kutoka Shule ya Sekondari Chamwino ya hapa Mjini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, ambao ni watoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 12 wa Mheshimiwa Elibariki Kingu ambao ni Wenyeviti wa CCM, Kata za Jimbo la Singida Magharibi wakiongozwa na Katibu wa Mbunge Jimboni, ambaye ni Ndugu Abubakar Munna. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Khamis Mtumwa Ali ambaye ni Mwalimu wa Mheshimiwa Mtumwa Ali, kutoka Idara ya Siasa na Utawala, Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)* kilichopo Mkoani Dodoma na huyu ni Dkt. Philemon Sengati. Karibu sana. Mheshimiwa Khamis Mtumwa Ali naamini unaendelea vizuri katika masomo yako, maana umesema huyo ni Mwalimu wako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni Wanne wa Mheshimiwa Susan Kiwanga ambao ni viongozi na wananchi kutoka Mlimba Mkoa wa Morogoro. Karibuni sana. Tunao pia, wageni waliokuja Bungeni kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wageni 46 kutoka Chuo Kikuu cha St. John's kilichopo Mkoani Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni waliotufikia leo lakini ninayo matangazo kadhaa hapa:

Tangazo la kwanza linatoka kwa Makamu Mwenyekiti wa *TWPG* yaani Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania na anawatangazia Wabunge Wanawake wote kuwa leo tarehe 9 Novemba, 2016, kutakuwa na semina kwa ajili ya Wabunge Wanawake wote itakayofanyika katika Ukumbi wa iliyokuwa *Dispensary* zamani, mara baada ya kuahirisha Mkutano wa Bunge, saa saba mchana. Wanawake wote mnaombwa mhudhurie.

Tangazo la pili linatoka utawala, Waheshimiwa Wabunge mnajulishwa kuwa wataalam wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA)* watakuwepo Ofisi ya Bunge kuanzia leo Jumatano, tarehe 9 - 11 Novemba, 2016, kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa chumba Na. 3 ili kugawa vitambulisho vya uraia kwa Waheshimiwa Wabunge wote, waliokamilisha taratibu zote za usajili awamu ya kwanza, pamoja na kusajili Wabunge wote ambao hawakusajiliwa, awamu ya kwanza usajili ulipofanyika.

Tangazo lingine ni kuhusu kuhudhuria uzinduzi wa Umoja wa Wabunge Vijana Tanzania, tarehe 10 Novemba, 2016; Ukumbi wa Msekwa Ofisi ya Bunge, Mjini Dodoma saa saba mchana. Tangazo linaletwa na Mwenyekiti wa Umoja huo wa Wabunge Vijana ambaye ni Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza. Anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba kesho tarehe 10 Novemba 2016, anaomba mhudhurie shughuli ya uzinduzi wa Umoja wa Wabunge Vijana utakaofanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa, Ofisi ya Bunge saa saba mchana.

Mgeni rasmi atakuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa. Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria hata wale ambao umri wa ujana umetutupa kama mimi, wote tunaombwa tuhudhurie.*(Makofi)*

Tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, ambaye ni Katibu wa Wabunge wa CCM kutoka Zanzibar, anawaarifu kuwa kuna kikao muhimu saa saba mara baada ya kuahirisha kikao cha asubuhi katika Ukumbi wa Msekwa. Kwa hiyo, mnaombwa kuhudhuria bila kukosa, Wabunge wote wa CCM kutoka Zanzibar.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo pia la misa kutoka kwa Mheshimiwa Joseph Selasini ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya, anawatangazia kwamba Jumuiya ya Mtakatifu Thomas More inawatangazia Wakristo wote kuwa kutakuwa na misa takatifu leo mara baada ya kuahirishwa kwa kikao cha Bunge saa saba mchana kwenye kanisa dogo jengo la Msekwa, mnaombwa mhudhurie ibada hiyo.

Tangazo lingine, Waheshimiwa Wabunge ni kuhusu usafiri wa kwenda Urambo siku ya Ijumaa tarehe 11 Novemba, 2016. Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kuwa pamoja na uwakilishi wa Bunge ambao utaamriwa na Uongozi wa Bunge, Ofisi ya Bunge iko tayari kuandaa usafiri wa treni ya Dilux au mabasi maalum kutoka Dodoma kwenda Urambo kutegemea na idadi ya Waheshimiwa Wabunge watakaojitokeza.

Safari hiyo, itakuwa siku ya Ijumaa tarehe 11 Novemba, 2016 jioni na kurudi Jumapili tarehe 13 Novemba, 2016 asubuhi. Waheshimiwa Wabunge wote wenye nia ya kwenda Urambo wanaombwa kujiorodhesha kwa Katibu wa Bunge. Aidha, kila Mbunge anayetarajia kusafiri, ataombwa kuchangia gharama kidogo za safari. Tangazo limeletwa na utawala.

Waheshimiwa Wabunge, jambo moja dogo kwa ajili ya kukumbushana. Tunapokuwa kwenye kipindi cha maswali wako Wabunge wanaleta ujumbe na wengine wanasimama kwa ajili ya kuuliza maswali kwa niaba ya Wabunge ambao hawapo. Kikanuni inaruhusiwa, Kanuni ya 42. Aidha, mtu atakuwa ameleta ujumbe kwamba ameachiwa majibu na yule mwenye swali lake au ataleta ujumbe kwamba ameombwa aulize swali.

Nawasihi Waheshimiwa Wabunge ili kuondoa sintofahamu inayoweza kujitokeza, usiandike ujumbe kwamba umeambiwa uulize swali kama hukuambiwa na mwenye swali. Kwa sababu, inaleta tabu kwa anayesimamia hapa akiletewa ujumbe kwamba ameombwa mtu aulize swali halafu mwingine tena analeta na yeye ameombwa, sasa inaleta tabu kwamba ni yupi kati ya hao ameombwa kuuliza swali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niwaombe tusiandike kwamba umeombwa, unaweza tu ukaomba kwamba, naomba swali la fulani niliulize mimi, akija aliyeombwa basi atapewa yule nafasi kwa sababu ndiye mwenye majibu na atakuwa amepewa maswali ya nyongeza, lakini unapokuwa umesema umeombwa wewe halafu ikatokea aliyeombwa halisi anakuja, inaleta tabu kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hilo, niseme na mimi yale ambayo alianzisha Mheshimiwa Susan Lyimo, wengi tulikuwa na matarajio fulani, lakini pengine humu ndani wapo wale ambao inabidi tukubaliane na hali, tuwape pongezi. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Donald Trump *(The Trump)* kwa kushinda uchaguzi wa Marekani, kwa sababu mpaka sasa ameshashinda, kama wanasubiri nadhani wanasubiri Jimbo moja watangaze. Mheshimiwa wetu Hillary Clinton safari hii haikuwezekana, lakini baada ya miaka minne pengine mambo yatakuwa mazuri. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, nakumbushwa hapa kwamba, nitambue juhudi zake na kwamba amejitahidi sana. Aah, nakumbushwa kwamba, tungemtuma Mheshimiwa maeneo yale angekuwa ameshinda huyu Mama! *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tuendelee. Katibu!

**NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)* pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hiyo; na Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hiyo**

**NAIBU SPIKA:** Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI *(PAC)* KWA TAARIFA YA HESABU ZILIZOKAGULIWA ZA SERIKALI KUU NA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA 30 JUNI, 2014 NA 30 JUNI, 2015**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI *(PAC)*:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* kwa Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia 30 Juni, 2014 na 30Juni, 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utangulizi; kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)*, kuhusu shughuli zilizotekelezwa kwa uchambuzi wa Hesabu zilizokaguliwa za baadhi ya Mafungu ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2014 na 30 Juni, 2015 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili inavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika kipindi cha mwaka 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* ilipokea na kujadili Taarifa ya *CAG* kuhusu ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2014 na tarehe 30 Juni, 2015. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, maelezo yanayotolewa katika Taarifa hii yanatokana na Hesabu zilizokaguliwa kama zilivyowasilishwa katika Taarifa hizo za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Kamati. Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali ilizingatia majukumu yake yaliyoainishwa katika Kifungu cha 14 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Msingi wa majukumu hayo unatokana na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 16 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2014, *CAG* alikamilisha ukaguzi wa Taasisi 176 za Serikali Kuu na 125 za Mashirika ya Umma. Kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2015, *CAG* alifanya kazi kwa jumla ya Taasisi 209 za Serikali Kuu ikijumuisha Wizara, Wakala na Idara Zinazojitegemea 150, Sekretarieti za Mikoa 25 na Balozi 34.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mashirika ya Umma, *CAG* alikaguwa na kutoa Taarifa za jumla ya Mashirika ya Umma 125 ambapo kazi hiyo aliifanya kwa kushirikisha Taasisi binafsi za Ukaguzi kama ilivyofafanuliwa katika Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwishafafanua katika utangulizi wa taarifa hii, katika ngazi ya Kamati, Kamati ilifanikiwa kuchambua na kujadili Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za jumla ya Mafungu 74 ikijumuisha Mafungu 49 ya Serikali Kuu na 25 ya Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mafungu mahususi ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma, ulibaini yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini mambo ya msingi yafuatayo ambayo ni muhimu Bunge lako likafahamishwa:-

Mheshimiwa Naibu Spika, misamaha ya kodi *(Tax exemptions)*. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2015 misamaha ya kodi ilipungua hadi kufikia jumla ya shilingi trilioni 1.6 sawa na asilimia15 ya makusanyo ya *TRA* yaliyokuwa shilingi trilioni 10.6 ukilinganisha na misamaha ya kodi ya shilingi trilioni 1.8 sawa na asilimia18.5 ya makusanyo ya *TRA* ya shilingi trilioni 9.8 kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupungua kwa misamaha ya kodi ukilinganisha na miaka ya nyuma, bado misamaha ya kodi ilikuwa zaidi ya asilimia moja ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rufaa za muda mrefu kuhusu Mashauri ya Kodi *(Long Outstanding Tax Appeals Cases);* Kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2014, Taarifa ya *CAG* ilibainisha kuwa *TRA* ilikuwa haijakusanya kodi za jumla ya shilingi trilioni 1.7 kutokana na rufaa za mashauri ya kodi zilizopo kwenye Baraza la Kodi kwa muda mrefu. Aidha, kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2015, thamani ya rufaa za mashauri hayo ya kodi ilifikia shilingi trilioni 6.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malipo ya Pensheni na Kiinua Mgongo kwa wakati mmoja *(Double Payment of Benefit Scheme)* kwa baadhi ya watumishi wa *TRA*. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2015 *TRA* iliwalipa watumishi wake 29 wa nafasi ya Menejimenti jumla ya shilingi bilioni 1.3 kama malipo ya kiinua mgongo *(Gratuity)* baada ya kumalizika kwa mikataba yao ya kazi, wakati huohuo iliendelea kuwalipia watumishi hao michango ya kati ya asilimia 10 hadi asilimia 15 katika Mifuko ya Hifadhi za Jamii kwa ajili ya michango ya pensheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Kamati na *CAG* kwa jambo hili ni kuwa, malipo hayo yanaenda kinyume na matakwa ya Sheria za Utumishi wa Umma na Sheria za Hifadhi za Jamii zinazozuia malipo ya mafao mara mbili *(Double payment of benefits)* kwa mtumishi mmoja, kama ilivyofanyika *TRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ongezeko la Nakisi ya Uwezo wa *PSPF* Kulipa Mafao ya Wastaafu *(Actuarial Deficit)*. Taarifa ya *CAG* kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2015 imebainisha kuwa uwezo wa Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma *(PSPF)* kulipa mafao yake unazidi kupungua kwa kuzingatia taarifa ya kitaalam ya tathmini ya muda mrefu ya uwezo wa Mfuko *(Actuarial Valuation Report)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Tathmini imeonyesha ongezeko la mtaji hasi *(Actuarial Deficit)* ambao umefikia kiasi cha shilingi trilioni 11.15 hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2014. Kupungua kwa mtaji huu kumesababishwa na sababu kuu zifuatazo:-

(a) Kuchelewa kwa Serikali kulipa deni la michango lililotokana na mafao yaliyolipwa kwa Wastaafu waliokuwa watumishi wa Serikali waliokuwepo kabla ya Mfuko kuanzishwa mnamo tarehe Mosi Julai, 2009.

(b) Madeni makubwa ambayo *PSPF* inadai katika Taasisi mbalimbali, shilingi bilioni 499.7 kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2015.

*(c)* *PSPF* kutekeleza miradi ya uwekezaji bila ya miradi hiyo kurudisha fedha za uwekezaji ndani ya muda muafaka.

(d) Kutozingatiwa kwa Sera ya Uwekezaji ya Shirika, ambapo *PSPF* wamewekeza asilimia 53 katika miradi maalum ya Serikali badala ya chini ya asilimia 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Kamati katika jambo hili ni kuomba Bunge lako kuitaka Serikali kutimiza wajibu wake kwa urejeshaji wa fedha zinazotakiwa na *PSPF* ili kuhakikisha Wastaafu wanalipwa stahiki zao kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matumizi Makubwa ya Fedha katika Gharama za Uendeshaji *(Staff Cost and Operating Expenses)* katika Mamlaka za Udhibiti wa Utoaji Huduma; Msingi wa hoja ya Kamati ni kufanya ulinganifu wa mapato yaliyokusanywa na Mamlaka za Udhibiti wa Huduma, Matumizi ya Mamlaka hizo na gawio wanalopeleka Serikalini. Kilichobainika kwa kiasi kikubwa ni kuwa mamlaka hizo zimekuwa na matumizi makubwa ya kiuendeshaji na utawala wakati wakipeleka gawio dogo sana Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SUMATRA* na *EWURA* wamekuwa wakipeleka Serikalini gawio la asilimia tano kinyume na masharti ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2015 ambayo ilielekeza baadhi ya mashirika ya umma kupeleka gawio Serikalini kwa kiasi cha kati ya asilimia 10 hadi asilimia 15 ya mapato yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)*; Kamati imepitia Taarifa ya *CAG* kwa Hesabu zilizokaguliwa za *NSSF*. Jambo mahsusi la msisitizo lilihusu utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Kigamboni *Satellite Village (Dege Eco Village)*. Kwa mujibu wa hoja ya *CAG*, makubaliano ya mkataba yalionesha kuwa, *NSSF* watakuwa na hisa asilimia 45 na Azimio *Housing Estates (AHEL)* hisa asilimia 55 katika mradi huo. Aidha, *AHEL* walitakiwa kutoa ardhi ya ekari 20,000 ambayo itakuwa sawa na asilimia 20 ya hisa zao na hisa asilimia 35 watachangia kwa kutoa fedha. *NSSF* wao walitakiwa kuchangia asilimia 45 ya hisa zao katika mradi kwa kutoa fedha. Hadi sasa *AHEL* wametoa ekari 300 tu kati ya ekari 20,000 zilizoingiwa katika mkataba huo. Hapa ndiyo msingi wa hoja ya *CAG* kuwa ekari 19,700 za mradi huo bado Hati zake hazijawasilishwa kwa *NSSF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya ukaguzi ya *NSSF* imebainisha kuwa Mradi wa *Dege Eco Village* umesimama kwa sasa kutokana na changamoto mbalimbali. Kamati ilikuwa na maoni kuwa jambo hili linahitaji uchambuzi na uhakiki kabla ya kuhitimishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hoja ya *CAG* kuhusu uchangiaji wa ardhi katika mradi husika kwa lengo la kuwa na wigo mpana, ili Kamati iweze kulishauri Bunge lako Tukufu kwa misingi yenye weledi na haki, Kamati imeamua kuunda Kamati Ndogo kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(18)

ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Kamati hiyo Ndogo itajikita katika kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kupata uelewa wa dhana, dhima na maudhui ya uwekezaji wa mtaji kwenye miradi ya ujenzi kwa makubaliano ya kutoa ardhi *(land for equity)* ili kubainisha vigezo vinavyokubalika *(agreed good practices)* katika utekelezaji wa miradi kwa njia hiyo.

(b) Kuthibitisha iwapo ekari 19,700 zilizotakiwa kuchangiwa katika mradi huo zipo kama taarifa ya ukaguzi ilivyokuwa imehoji.

(c) Kupitia makubaliano ya mkataba wa ugharamiaji wa mradi wa *Dege Eco Village* na mgawanyo wa hisa.

(d) Kupitia taarifa ya utekelezaji wa mradi hadi hapo ulipofikia.

(e) Kufanya ulinganifu *(review)* wa utekelezaji wa mradi wa *Dege Eco Village* na miradi mingine iliyotekelezwa na Mashirika ya Umma kwa makubaliano ya *(Land for Equity)*.

(f) Kuishauri Serikali hatua za kuchukua ili kuhakikisha mradi unakamilika na fedha za umma zilizowekezwa zinaleta tija na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine kuhusu taarifa ya ukaguzi wa *NSSF* ilikuwa utoaji wa mikopo ya *SACCOS* kwa wanachama wake. Naomba mnisikilize; dosari iliyoibuliwa na *CAG* ni kutorejeshwa kwa mikopo kwa wakati na dosari katika utaratibu mzima wa utoaji wa mikopo hiyo. Mfano wa *SACCOS* hizo ni kama *Simka General Traders, Uvikasa SACCOS, Bumbuli Development SACCOS, RUMAKO Agricultural* na nyinginezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2015, *NSSF* ilitoa jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 41.5, ambapo kwa Mwaka wa Fedha wa 2014 ilikuwa bilioni 25.58 kwa *SACCOS* mbalimbali. Miongoni mwa dosari zilizobainika ni pamoja na utoaji wa mikopo kwa *SACCOS* asilimia 50 zaidi ya thamani ya dhamana ya *SACCOS* hizo na utoaji wa mikopo bila kuchambua Taarifa za Ukaguzi wa hesabu za miaka mitatu mfululizo za *SACCOS* husika kama ilivyotakiwa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya Mwenyekiti wa Bodi ya *NSSF* kwa Kamati yalifafanua kuwa, uchunguzi wa awali umebaini kutokuwepo kwa baadhi ya *SACCOS* zilizopewa mikopo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hasara ya shilingi bilioni 6.7 katika Fungu 43 – Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, kutokana na kuharibika mahindi yaliyohifadhiwa, tani 13,583. Kamati imebaini kuwa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kupitia kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* ilipata hasara ya jumla ya shilingi bilioni 6.7 iliyotokana na kuharibika kwa tani za mahindi 13,583 zilizokuwa zimehifadhiwa na *NFRA*. Kwa kurejea majibu ya Afisa Masuuli wa Fungu 43, sababu kubwa ya kuharibika kwa mahindi hayo ni utunzaji usiofaa hali iliyosababisha mahindi kunyeshewa mvua na kuharibika kiasi ambacho hayawezi tena kutumika kwa ajili ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni ya Serikali katika Mifuko ya Hifadhi za Jamii. uchambuzi wa taarifa ya *CAG* kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2015 umebaini kuwa Serikali na Taasisi zake zinadaiwa jumla ya trilioni 1.5 na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Kamati kuhusu deni hilo ni kuwa ni wajibu wa Serikali kuwa na mpango maalum wa kulipa madeni hayo ili Mifuko hiyo iepuke athari ya kutolipa mafao kwa wastaafu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari katika mfumo wa udhibiti wa mapato ya Mamlaka ya Bandari Tanzania *(TPA)*. Kwa mwaka tunaoutolea taarifa dosari zifuatazo zilijitokeza katika udhibiti na usimamizi wa mapato katika Mamlaka ya Bandari Tanzania:-

(a) Mapungufu katika Mfumo wa *COBOL* unaotumiwa na Mamlaka ya Bandari ambao ulikuwa na changamoto za kuwasiliana na mifumo tanzu hivyo kutoa mianya ya upotevu wa mapato.

(b) Uwepo wa meli tatu ambazo taarifa za mapato yake hazikuonekana katika mfumo.

(c) Meli nne mapato yake yaliandikwa miezi 18 baada ya meli husika kuondoka.

(d) Uwepo wa meli ambazo zimesajiliwa kwa hadhi ya Kidiplomasia *(Diplomatic Status)* ambazo kwa mujibu wa Sheria hazilipi kodi, lakini katika ukaguzi ilibainika uwepo wa meli nne ambazo hazikuwa na nyaraka za uthibitisho kuwa meli hizo zina hadhi ya Kidiplomasia.

(e) Kutofanyika uhakiki wa taarifa ya meli na mizigo inayohudumiwa na Kitengo cha Kuhudumia Makontena cha *TICTS.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, katika Mamlaka ya Bandari Tanzania *(TPA)*, Kamati iliweza kubaini pia uwepo wa akaunti ya muda maalum *(fixed deposit)* ya shilingi bilioni 440 iliyokuwa imewekwa katika mabenki manne tofauti. Hata hivyo, kulijitokeza mkanganyiko wa riba iliyotumika katika ufunguzi wa akaunti hizo. Kamati imemwomba CAG kufanya ukaguzi maalum wa akaunti hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Ripoti ya CAG Kuhusiana na Ukaguzi Kwenye Manunuzi ya Umma katika Mwaka wa Fedha 2015. Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya CAG pamoja na Sehemu ya Taarifa ya *PPRA* kuhusu manunuzi ya umma umebaini yafuatayo:-

(a) Kutozingatiwa kwa mpango wa mwaka wa manunuzi *(Annual Procurement plan);*

(b) Manunuzi kufanyika bila ushindani;

(c) Manunuzi kufanyika bila kuwa na thamani halisi ya fedha, *value for money;* na

(d) Malipo yenye utata kwa huduma ambazo baadhi hazikupokelewa na zingine hazikufuata utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maelekezo ya Bunge kuhusu ufungaji wa vifaa vya *AFIS* yaliyotolewa katika Mkutano wa Tatu wa Bunge. Mnamo tarehe 23 Aprili, 2016, *PAC* iliomba kuunda Kamati Ndogo kwa mujibu wa kanuni ya 117, kifungu cha 18 kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa agizo la *PAC* katika Bunge la Kumi kwa Jeshi la Polisi, lililotolewa tarehe 23 Oktoba, 2014, kuhusu utekelezaji wa mradi wa kielektroniki wa utambuzi wa alama za vidole, *Automatic Fingerprints Identification System*.

Kazi hiyo ilitokana na mkataba uliokuwa umeingiwa kati ya Jeshi la Polisi (mnunuzi) na Kampuni ya Lugumi *Enterprises limited (*mzabuni). Agizo la Bunge, lilimtaka Afisa Masuuli wa Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba mfumo wa *AFIS* unafanya kazi katika kipindi cha miezi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Spika alielekeza kuundwa kwa Kamati ndogo ambayo ilipewa hadidu rejea moja tu kama ifuatavyo: Kamati ifanye hakiki kama vifaa vilinunuliwa na kufungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Kamati ndogo ilipokelewa na maudhui yake kuzingatiwa, kwa mujibu wa taarifa hiyo matokeo ya uhakika yalithibitisha kwamba vifaa vipo pamoja na kasoro nyingi zilizojitokeza ikiwemo kuharibika kwa vifaa kabla havijatumika na kutokuwepo vyumba bora vya

kuhifadhia vifaa husika. Hivyo basi, kwa mujibu wa kanuni ya 117(17) ya Kanuni za Bunge, taarifa ya Kamati ya *PAC* ilikabidhiwa Serikalini kwa utekelezaji.

Aidha pamoja na taarifa hiyo maagizo yafuatayo yalitolewa:-

(a) Serikali ihakikishe mfumo huu unafanya kazi ndani ya miezi mitatu kuanzia leo yaani tarehe iliyotolewa hilo agizo; na

(b) Masuala yote yaliyobainika kuwa na dosari za kiutendaji yapatiwe ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, *PAC* ilielekezwa kuhakiki utekelezaji wa maagizo hayo na kutoa taarifa ya utekelezaji wake Bungeni wakati ikiwasilisha taarifa yake ya mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 28 Oktoba, 2016 Afisa Masuuli wa Fungu 28, Jeshi la Polisi, aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa agizo la Bunge. Baada ya kupokea taarifa hiyo, Kamati ilichambua utekelezaji wa maagizo tisa yaliyotolewa kama inavyoonekana katika taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa maelekezo ya Bunge, kuhusu ufungaji wa vifaa vya *AFIS* yaliyotolewa katika Mkutano wa Tisa wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada kupokea taarifa hiyo ya utekelezaji kutoka kwa Afisa Masuhuli wa Fungu 28, Kamati ina maoni na msimamo ufuatao:-

(a) Kamati haikupata fursa ya kwenda kufanya uhakiki wa utekelezaji wa maagizo ya Bunge, kwa kuwa taarifa ya utekelezaji ya Afisa Masuuli, kuhusu agizo la Bunge, iliifikia Kamati tarehe 28 Oktoba, 2016 siku ambayo Kamati ilikuwa inakamilisha shughuli zake;

(b) Kutokana na muda mfupi wa kupokea taarifa hiyo, Kamati haitaweza kutoa maoni kuhusu usahihi wa taarifa ya utekelezaji ya Afisa Masuhuli wa Fungu 28 hadi hapo itakapotekeleza agizo lililotolewa na Bunge la kwenda kufanya uhakiki iwapo maagizo tisa yamekamilika; na

(c) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 16 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kinachobainisha kuwa msingi wa shughuli za Kamati ya *PAC* itakuwa ni taarifa ya hesabu zilizokaguliwa na *CAG*. Hivyo Kamati itafanya uhakiki wa agizo la Bunge kwa kushirikiana na *CAG* anayekagua Fungu 28 katika shughuli zijazo za Kamati zinazohusu hesabu za mwaka wa 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Changamoto za uwekezaji unaolikabili Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)*. Hoja za ukaguzi ambayo ndiyo changamoto zinazoikabili *NDC*, hivyo kukwamisha shughuli zake ni kama ifuaatavyo:-

(a) Upembuzi yakinifu wa miradi kufanywa na wabia wenza wa *NDC*, badala ya *NDC* wenyewe; na

(b) Changamoto za bajeti zinazoikabili *NDC*, na uwepo wa miradi ya muda mrefu ambao hadi sasa haijaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Usimamizi wa Mali, *(Asset Management)* katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Mifuko ya Hifadhi ya Jamii *PPF, PSPF, LAPF, NSSF* na *NHIF* kwa pamoja hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2016 walitumia jumla ya shilingi bilioni 415.4 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu cha Dodoma, kwa kuzingatia mkataba wenye masharti ya usanifu, ujenzi, miliki na kuhamisha miliki baada ya miaka 10. Hadi hivi sasa tunapowasilisha taarifa hii ya Kamati katika Bunge lako Tukufu, thamani halisi ya majengo hayo haijaingizwa katika vitabu vya hesabu za Chuo Kikuu Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malimbikizo ya Mikopo isiyorejeshwa, *(Non Performing Loans)* katika Benki ya Maendeleo ya *TIB*. Uchambuzi wa Kamati katika taarifa za ukaguzi za Benki ya Maendeleo ya *TIB* umebaini kuwa kuna changamoto kubwa za urejeshaji wa mikopo inayotolewa na benki hiyo na pia kuna dosari za uhakiki wa miradi inayogharamiwa na benki hiyo. Upungufu wa urejeshaji wa mikopo ya *TIB* ni pamoja na uwepo wa mikopo chechefu, *(Non Performing Loans*) ya kiasi cha shilingi bilioni 78.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilisikitishwa na kitendo cha Benki ya *TIB* kukataa kuwasilisha michanganuo ya madeni na wadaiwa sugu. Kamati ilimwandikia Spika, kutoa malalamiko hayo ili *TIB* walazimishwe kuleta *document* hiyo na Spika, ameweza kufanya kazi hiyo na kuielekeza *TIB* ilete kwenye Kamati michanganuo ya wadaiwa sugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokamilika kwa Mradi wa Uhamiaji Mtandao *(E- Immigration)* katika Fungu 95 - Idara ya Uhamiaji. Pamoja na kuwa Idara ya Uhamiaji imeweka mfumo wa usimamizi wa *visa* katika makao makuu ya Idara, kwenye balozi na kwenye mipaka ya nchi, taarifa ya ukaguzi imebaini kuwa mfumo uliopo katika balozi na ule wa kutoa *visa* kwa wageni wanaowasili, *(Visa on arrival)* na Makao Makuu, hauzungumzi, *not in integrated,* hivyo kutoa mwanya wa upotevu wa mapato ya Serikali yanayotakiwa kukusanywa kutokana na utoaji wa *visa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokamilika kwa muamala wa shilingi bilioni 100.5 katika kifungu 56, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Ukaguzi wa taarifa ya Fungu 56, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ilibaini kuwa muamala wa shilingi bilioni 100.5, haukukamilika kwa sababu shughuli zilizokuwa zimepangwa kugharamiwa na fedha hizo hazikufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto katika Uandaaji wa Taarifa za Hesabu kwa kuzingatia mfumo wa *IPSAS Accrual basis*. Mnamo tarehe 1 Julai, 2012, Serikali Kuu na taasisi zake, zilianza rasmi kutumia mfumo wa uandaji wa hesabu unaofahamika kama *IPSAS Accrual Basis*. Malengo yalikuwa ni kuhakikisha taarifa za Hesabu za Serikali zinatoa taswira halisi ya mali na madeni yanayohusu taasisi za Serikali. Hadi hivi sasa mfumo huo haujaweza kutekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala mengine ya msisitizo. Naomba kuhitimisha taarifa hii kwa kufafanua baadhi ya maswali ya msisitizo ambayo yanahusiana na matumizi ya fedha za umma na Kamati ingependa Serikali iyafanyie kazi, naomba yaingiye yote kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Mapendekezo ya Kamati, mapendekezo ya jumla. Kamati imetoa mapendekezo katika makundi mawili, kundi la kwanza mapendekezo ya muda mfupi ambayo utekelezaji unatakiwa kuwa ndani ya kipindi cha mwezi mmoja hadi mwaka mmoja. Kundi la pili ni mapendekezo ya muda wa kati, ambao muda wa utekelezaji wake unategemea kuwa kuanzia mwaka mmoja hadi miaka miwili, hasa yale yanayohitaji bajeti kubwa, sera na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya kamati ni kama ifuatavyo:-

(a) Kwa hiyo basi, madeni ambayo Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, inaidai Serikali, Bunge liazimie kwamba Serikali iwasilishe mpango mahususi Bungeni wa utaratibu utakaotumika kulipa mikopo na michango inayodaiwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamiii; na

(b) Serikali iwe inatoa taarifa Bungeni kila robo ya mwaka wa fedha kuhusu hali ya urejeshaji wa mikopo na michango husika;

Mheshimiwa Naibu Spika, rufaa za mashauri ya kodi zinazobishaniwa *Tax appeals and Objections* na misamaha ya kodi. Kwa hiyo basi, Bunge liazimie kwamba:-

(a) Serikali itoe fedha na bajeti ya kutosha kwa Bodi ya Rufaa za Kodi ili iweze kushughulikia mashauri ya kesi za kodi kwa haraka na kutoa uamuzi;

(b) Serikali kupitia *TRA* ishirikiane kwa ukaribu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wizara ya Fedha kwa kutumia mawakili wenye weledi na uzalendo kutafuta ufumbuzi wa kesi zilizoko mahakamani ili kuhakikisha kodi stahiki inakusanywa; na

(c) Serikali isimamie kwa ukamilifu sheria za kodi ikiwa ni pamoja na kutumia njia za kielektroniki kusimamia kwa kukamilifu na kudhibiti matumizi yasiyofaa ya misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya kifedha ya Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma *(PSPF)*, kwa hiyo basi Bunge liazimie kwamba:-

(a) Serikali itimize ahadi na malengo yake ya kibajeti kwa kuhakikisha inalipa shilingi bilioni 150 zilizotengwa mwaka huu wa fedha kulipa deni la *PSPF*,

(b) Serikali itoe hati fungati *(non cash bond)* ya shilingi trilioni 2.9 ili kuanza kulipa deni la Mfuko wa Wastaafu kabla ya tarehe 1 Julai,1999 kabla ya mwezi Februari 2017 kama ilivyokubaliwa mbele ya Kamati;

(c) Serikali isimamie kwa karibu na kuzihimiza taasisi zake zinazodaiwa na *PSPF* kiasi cha shilingi bilioni 382.9 kulipa madeni hayo mara moja;

(d) Serikali iendelee kutenga fedha kwenye bajeti ya kila mwaka ili kuongeza mtaji wa *PSPF* kwa sababu nakisi iliyopo ni kubwa, hata kama madeni yote yatalipwa; na

*(e) PSPF* isipewe maelekezo mapya ya kutekeleza miradi au kuikopesha Serikali katika kipindi hiki cha mpito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uzingatiaji wa sheria ya manunuzi ya umma na kanuni zake. Kwa hiyo basi, Bunge liazimie kwamba:-

(a) Serikali iendelee kusimamia kwa ukamilifu uzingatiaji wa sheria ya manunuzi ya umma katika taasisi zake na kuchukua hatua pale sheria inapokiukwa;

*(b) PPRA* itumie masharti ya kifungu cha 57 cha gazeti la Serikali namba 58 kuwafungia wale wote watakaothibitika kutumia rushwa katika kushawishi zabuni katika manunuzi ya umma; na

(c) Kuandaliwe utaratibu maalum wa kikanuni ili kuhakikisha taarifa ya ukaguzi inayoandaliwa na *PPRA* inawasilishwa rasmi Bungeni na kisha kushughulikiwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hasara ya shilingi bilioni 6,700,000 iliyotokana na kuharibika tani 13,583 za mahindi:-

(a) Kwa hiyo basi, Bunge liazimie kwamba Serikali itengeneze utaratibu maalum wa kuwa inafanya tathmini ya mara kwa mara ya uwezo wa nchi kuzalisha chakula, uwezo wa *NFRA* kununua na kuhifadhi chakula na mahitaji halisi ya chakula; na

(b)Serikali iongeze nguvu katika ukarabati na ujenzi wa maghala mapya na ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mfumo wa *IPSAS Accrual*. Kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza kuwa Bunge, liazimie Serikali itenge rasilimali za kutosha, fedha na wataalam ili kuhakikisha kuwa taasisi za Serikali Kuu zinatekeleza mfumo huo kabla ya muda wa kipindi cha mpito cha miaka mitano kukamilika mwezi Machi, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Maendeleo la Taifa, *NDC* kwa hiyo basi;

(a) Kwa hiyo basi, Bunge liazimie kwamba *NDC* ifanye mapitio upya, (review of *structural arrangement)* ya miradi iliyopangwa kutekelezwa kwa ubia.

*(b)* *NDC* ihakikishe inazingatia matakwa ya kanuni ya 46(2) ya kanuni za *PPA* za mwaka 2011 kwa kuhakikisha inafanya tathimini na ufuatiliaji, *(monitoring and evaluation)* ya miradi yenye ubia ili kuhakikisha maslahi ya nchi yanalindwa na faida ya uwekezaji inaonekana.

(c) Serikali iwezeshe *NDC* kifedha ili iweze kufanya kazi zake kwa ukamilifu zaidi. Kwa hiyo basi, Bunge liazimie kwamba Serikali, ianzishe Mfuko Maalum wa uwekezaji, *Special Investment Fund,* ili fedha katika Mfuko huo zitumike kama mtaji katika maeneo ambayo Serikali inataka kuwekeza.

(d) Mfuko huo wa uwekezaji uanzishwe chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kutumia mfumo wa kubakisha mapato *(retention scheme)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malipo ya *pension* na kiinua mgongo kwa wakati mmoja, *(double payment of benefits)*. Kwa hiyo basi, Bunge liazimie kuwa *TRA, EWURA* na *SUMATRA*, zisimamishe malipo hayo mara maja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mamlaka ya Udhibiti na Ssekta ya Hifadhi ya

Jamii *(SSRA)* watoe mwongozo kwa taasisi za umma kuzingatia sheria na kuepuka malipo ya *pension* na kiinua mgongo kwa wakati mmoja

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Mradi wa Uhamiaji Mtandao *(E-immigration)*. Kwa hiyo basi, Bunge liazimie kwamba Serikali itekeleze mradi wa uhamiaji mtandao *(E- Immigration)* mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo isiyorejeshwa katika Benki ya Maendeleo ya *TIB*, Kamati imebaini uwepo wa mikopo mingi isiyorejeshwa na benki ya *TIB.* Kwa hiyo basi, Bunge liazimie kwamba Serikali, iingilie kati kwa kutumia vyombo mbalimbali vya dola kuisaidia *TIB* kukusanya madeni yote ya wale *defaulters,* muamala wa shilingi billioni 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Fungu 56, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kwa hiyo basi, Bunge liazimie kuitaka Serikali kutoa maelezo ya kina kuhusiana na muamala huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Ofisi ya Ukaguzi *(National Audit Office)*. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni ofisi muhimu katika kuhakikisha kunakuwepo usimamizi unaofaa wa fedha za umma katika Serikali, lakini inakabiliwa na changamoto za kibajeti. Kwa hiyo basi, Bunge liazimie kwamba Serikali itenge na kutoa kwa wakati bajeti ya kutosha ili Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi itekeleze majukumu yake. Masuala mengine ya msisitizo yote yaingie kwenye *Hansard*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, naomba kwa namna ya pekee kabisa kukushukuru wewe binafsi, Spika na Wenyeviti wote wa Bunge. Pia napenda kumshukuru Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* Mheshimiwa Aeshi Hilary, ambaye aliiongoza Kamati tangu kuundwa kwake takribani kipindi cha miezi tisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa namna ya pekee kabisa naomba kuwashukuru Wajumbe wenzangu Kamati ya Kudumu ya Bunge ya *PAC* kwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi, wamekuwa wakishiriki mijadala ya vikao vya Kamati kwa ufanisi na kutumia vyema elimu, taaluma ya uzoefu na vipawa vyao katika kufanya uchambuzi wa kina wa taarifa za hesabu na kutoa ushauri ambao kwa namna ya pekee umefanya Kamati hii kuwa na ufanisi. Naomba majina yao yote yaingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuwashukuru Katibu wa Bunge…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA- MWENYEKITI WA KAMATI ZA HESABU ZA SERIKALI – PAC:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Waheshimiwa wote na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. JAPHET N.HASUNGA:** Mheshimwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC) KWA TAARIFA YA HESABU ZILIZOKAGULIWA ZA SERIKALI KUU NA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA JUNI 30, 2014 NA JUNI 30, 2015**

(*Inatolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016*)

**SEHEMU YA KWANZA**
**MAELEZO YA JUMLA**

**Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), kuhusu shughuli zilizotekelezwa kwa Uchambuzi wa Hesabu zilizokaguliwa za baadhi ya Mafungu ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2014 na Juni 30, 2015 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili inavyostahili.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa katika Kipindi cha mwaka 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ilipokea na kujadili Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2014 na tarehe 30 Juni, 2015, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa maelezo yanayotolewa katika Taarifa hii yanatokana na Hesabu zilizokaguliwa kama zilivyowasilishwa katika Taarifa hizo za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kipindi hicho.

## Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali zilizingatia majukumu yake yaliyoainishwa katika Kifungu cha 14 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Majukumu hayo ni: -

a) Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za Umma katika Wizara za Serikali yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

b) Kufuatilia utekelezaji wa Mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati hiyo yenye lengo la kuondoa matatizo hayo; na

c) Kutoa Mapendekezo na Ushauri kwa Wizara za Serikali kuhusu matumizi mazuri ya fedha za Umma ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa majukumu hayo unatokana na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na CAG kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 16 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Utaratibu wa kutekeleza majukumu ya Kamati kwa kipindi chote ulizingatia masharti ya Kanuni ya 117 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016. Miongoni mwa Masharti hayo ni kuzingatia Bajeti ya Kamati iliyoidhinishwa kwa mwaka na kukutana pale ilipoitishwa na Mheshimiwa Spika, Naibu Spika au Mwenyekiti wa Kamati baada ya kupata idhini ya Spika.

## Muhtasari wa Matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli za Kamati kwa mwaka 2016, zililenga kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za Umma katika Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Mashirika ya Umma kama yalivyobainishwa katika Taarifa ya CAG kwa Mwaka wa fedha unaoshia tarehe 30 Juni, 2015. Aidha, shughuli hizo zilikusudia kufuatilia utekelezaji wa Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali wakati wa kupitia na kujadili Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2013 na kipindi kilichotangulia.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2014 CAG alikamilisha ukaguzi wa Taasisi mia moja sabini na sita (176) za Serikali Kuu. Kwa upande wa Mashirika ya Umma, CAG alikamilisha ukaguzi na kutoa Taarifa za Mashirika mia moja ishirini na tano (125).

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2015 CAG alifanya ukaguzi wa jumla ya Taasisi mia mbili na tisa (209) za Serikali Kuu ikijumuisha Wizara, Wakala na Idara zinazojitegemea mia moja hamsini (150), Sekretarieti za Mikoa ishirini na tano (25) na Balozi thelathini na nne (34).

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mashirika ya Umma, CAG alikaguwa na kutoa Taarifa za jumla ya Mashirika ya Umma na Taasisi mia moja ishirini na tano (125) ambapo kazi hiyo aliifanya kwa kushirikisha Taasisi binafsi za ukaguzi kama ilivyofafanuliwa katika Sheria ya ukaguzi wa Umma namba kumi na moja (11) ya mwaka 2008.

**Mheshimiwa Spika,** Kama nilivyokwisha fafanua katika aya za Utangulizi wa Taarifa hii, Katika ngazi ya Kamati, Kamati ilifanikiwa kuchambua na kujadili Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za jumla ya Mafungu sabini na nne (74) ikijumuisha Mafungu 49 ya Serikali Kuu na 25 ya Mashirika ya Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kulijulisha Bunge hili kwa muhtasari wa Matokeo ya shughuli za Kamati wa mwaka 2016 kama ifuatavyo: -

***Maeneo yenye Matatizo ya matumizi yasiyofaa ya fedha za Umma***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kubaini maeneo yenye matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za Umma. Kutokana na shughuli hiyo Kamati ilibaini kwa ujumla baadhi ya maeneo hayo kuwa ni pamoja na haya yafuatayo: -

(a) Utekelezaji wa Miradi uliofanywa na baadhi ya Mashirika ya Umma bila kuwa na tija hivyo kuisababishia Serikali hasara;

(b) Dosari katika usimamizi wa Miradi inayotekelezwa na Wizara mbalimbali hivyo kupoteza fedha za Serikali;

(c) Kutokuwepo kwa nyaraka za Malipo kwa baadhi ya Taasisi za Wizara, Idara, Wakala na Mashirika ya Umma;

(d) Kutozingatiwa ipasavyo kwa Sheria ya Manunuzi ya Umma Namba 7 ya mwaka 2011 na Kanuni zake zilizotolewa katika GN. Namba 446 ya tarehe 20, Disemba 2013;

(e) Kutorejeshwa kwa wakati kwa Mikopo iliyochukuliwa na Serikali na Taasisi zake kutoka Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;

(f) Usimamizi wenye dosari wa Misamaha ya kodi;

(g) Kutorejeshwa kwa Mikopo iliyotolewa na Benki ya Maendeleo ya Tanzania (TIB) kwa Wateja mbalimbali;

(h) Changamoto katika kutumika kikamilifu kwa Mfumo wa utayarishaji na uandaaji wa Taarifa za Hesabu katika *"IPSAS Accrual Basis"* katika Wizara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Idara zinazojitegemea; na

(i) Matumizi makubwa ya fedha kugharimia shughuli za uendeshaji na Utawala *(Operating and administrative expenses)* katika Mashirika yanayohusika na udhibiti wa Utoaji huduma.


***Utekelezaji wa Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Hesabu za Serikali kipindi kilichopita.***

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali iliyowasilishwa Bungeni mwezi Januari, 2015 jumla ya Mapendekezo tisa (9) ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali yaliridhiwa na kuwa Maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa kipindi kilichopita Bungeni, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa za Maafisa Masuuli mbalimbali sambamba na uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2015.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya shughuli hiyo kwa ujumla yalionyesha kuwa Maazimio manne (4) kati ya Maazimio tisa (9) ambayo ni sawa 44.4% yalikuwa yametekelezwa au yalikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, Maazimio matano (5) ambayo ni sawa na 55.6% yamefafanuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuwa hayajatekelezwa hadi sasa kama inavyoonekana katika chati hapa chini: -

**Chati Namba 1. Hali ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Ripoti ya PAC**




***Chanzo: Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2015.***

**Mheshimiwa Spika**, Chati hapo juu inaonyesha hali ya utekelezaji wa Mapendekezo yanayotolewa na Kamati. Kamati inaendelea Kusisitiza, ni muhimu Serikali ikaendelea kuzingatia na kufanyia kazi Mapendekezo yanayotolewa na Kamati na Maazimio ya Bunge ambayo yanalenga kuimarisha matumizi ya fedha za Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kulipa Bunge lako mwendelezo wa majadiliano *(Coherent discussion)* naomba kuyataja Maazimio ambayo hadi sasa hayajatekelezwa kikamilifu kwa muhtasari kama ifuatavyo: -

(a) Bunge lilipendekeza kwa Serikali kuhakikisha Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA) inashughulikia kwa ukamilifu kesi mbalimbali za madai ya kodi zilizokuwa Mahakamani kwa haraka ili kuongeza mapato ya Serikali. Aidha, Bunge liliitaka TRA kuhakikisha kuwa inawatumia wataalamu wenye weledi na maadili kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) ili kuwa na malengo ya kushinda kesi hizo. Majibu ya Serikali katika hoja hii ni kuwa kesi nyingi zipo katika hatua ya usikilizwaji, hivyo utekelezaji wake utaendelea kufuatiliwa kwa karibu na Kamati ili kuhakikisha mapato ya Serikali yanapatikana kwa wakati bila kutumia mianya ya kesi kuchelewesha ukusanyaji wa kodi;

(b) Katika Azimio lingine, Bunge liliazimia kuitaka Serikali kulipa kwa haraka deni inalodaiwa na Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma (PSPF). Hadi Oktoba, 2016 Serikali ilikuwa imefidia deni hilo kwa jumla ya shilingi bilioni 243.27 kati ya deni la shilingi bilioni 429;

(c) Bunge liliazimia kuishauri Serikali kuimarisha usimamizi wa Misamaha ya kodi ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua stahiki kwa Kampuni zilizotajwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuwa zilitumia vibaya Misamaha ya kodi. Misamaha ya kodi kwa mwaka 2015 ilipungua lakini bado ipo zaidi ya 1% ya pato la Taifa;

(d) Bunge liliitaka Serikali kupitia vyombo vya Dola kama Taasisi ya kuzuia na kupambana na Rushwa (PCCB) kufanya uchunguzi wa Maafisa wa Serikali waliohusika Uingiaji na usimamizi wa Mkataba wa Ujenzi wa Jengo la Watu Mashuhuri katika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere Dar es Salaam. Pendekezo hilo la Bunge lilitokana na Taarifa ya ukaguzi maalum ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ujenzi wa Jengo hilo ambayo ilionyesha dosari kadhaa za manunuzi na usimamizi; na

(e) Mwisho, Bunge liliazimia kuzitaka Taasisi za Umma Kupunguza gharama kubwa za matangazo kwenye vyombo vya habari baada ya Bajeti za Wizara kupitishwa Bungeni kwani ilikuwa imebainika hapakuwa na uwazi wa matangazo hayo na gharama kubwa zilitumika bila kuwa na tija.

**Maoni ya Jumla kuhusu Matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla Kamati ina maoni kuwa, Serikali imekuwa ikijitihadi kuchukua hatua stahiki za kuondoa matumizi mabaya ya fedha za Umma na Kamati inatambua jitihada hizo. Hata hivyo, bado kuna changamoto kadhaa za kufanyia kazi ili kuimarisha matumizi ya rasilimali za Umma katika Wizara, Wakala, Idara za Serikali na Mashirika ya Umma. Hivyo ni muhimu Kwa hatua za kiutawala na kiuwajibikaji kuendelea kuchukuliwa ili kurekebisha dosari hizo na kuimarisha Mifumo ya uwajibikaji.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi uliofanywa katika Taarifa hii unatoa taswira halisi ya maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za Umma yanayohitaji msisitizo wa Bunge ili kuyaondoa na kupendekeza hatua stahiki za kuchukua.

## SEHEMU YA PILI

## UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI

### Maelezo ya Jumla kuhusu Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Ili kubainisha maeneo yenye matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za Umma na kwa kuzingatia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kaguzi mahsusi za Mafungu ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma, Vigezo vya msingi vilitumika kuainisha maeneo hayo ikiwa ni pamoja na: -

(a) Thamani ya pesa iliyotumika katika matumizi yaliyoripotiwa na kukaguliwa *(Value for money criteria);*

(b) Madhumuni ya Bajeti na matumizi yaliyofanyika *(Misappropriation criteria)* na iwapo Vigezo vya msingi katika matumizi ya fedha za Umma vilizingatiwa;

(c) Kiasi cha matumizi ikilinganishwa na mahitaji halisi *(Extravagance);*

(d) Matokeo ya Taarifa za Kaguzi Maalum *(Special audit)* zilizofanyika hivi karibuni;

(e) Umakini katika matumizi yaliyoripotiwa na kukaguliwa;

(f) Kujirudia mara kwa mara kwa hoja husika ya ukaguzi *(Frequency of reoccurrence)*;

(g) Uzingatiaji wa Mamlaka halali za kuidhinisha matumizi ya fedha *adherence to established controls)*;

(h) Uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na taratibu za matumizi ya fedha za Umma *(Compliance criteria)*; na

(i) Utunzaji wa Kumbukumbu na nyaraka zinazopaswa kuwepo kwa ushahidi wa matumizi ya fedha za Umma.

### Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia vigezo na mambo ya msingi niliyoyataja hapo awali, Uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mafungu mahsusi ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma ulibaini yafuatayo: -

***Ukaguzi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya Uchambuzi wa Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2014 na Juni 30, 2015. Uchambuzi wa Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA) ulilenga pamoja na mambo mengine kuangalia Taarifa za mapato na matumizi ya Mamlaka na suala zima la usimamizi wa Misamaha ya Kodi.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati ulibaini mambo ya msingi yafuatayo ambayo ni muhimu Bunge lako likafahamishwa: -

**a) Misamaha ya kodi *(Tax exemptions)***

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2015 Misamaha ya kodi ilipungua hadi kufikia Jumla ya shilingi 1,627,011,920,914 sawa na asilimia 15.1 ya Makusanyo ya TRA yaliyokuwa shilingi 10,629,231,196,907 ukilinganisha na Misamaha ya kodi ya shilingi 1,834,097,360,356 sawa na asilimia 18.5 ya Makusanyo ya TRA ya shilingi 9,889,970,048,436 kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2014.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kupungua kwa Misamaha ya kodi ukilinganisha na miaka ya nyuma, bado Misamaha ya kodi ilikuwa zaidi ya 1% ya pato la Taifa ***(Kwa mwaka wa fedha 2015, Pato la Taifa lilikadiriwa kufikia shilingi trilioni 89.0)***, hivyo kutofikiwa kwa malengo ya Serikali na Mapendekezo ya kitaalamu yanayotaka Misamaha ya kodi iwe chini ya 1% ya pato la Taifa. Kwa rejea ya ukaguzi wa CAG kuhusu Misamaha ya kodi mambo yafuatayo ni mifano ya matumizi ya Misamaha ya kodi isivyostahili: -

i. Msamaha wa kodi kwenye mafuta yenye thamani ya shilingi 22,325,178,728 uliotolewa kwa Kampuni za uchimbaji Madini za Geita na Resolute na kisha mafuta hayo yakahamishwa kwenda kutumiwa na Wakandarasi wengine;
ii. Matumizi yasiyofaa ya Msamaha wa kodi wa shilingi 392,701,565 uliofanywa na Kampuni ya Kili warrior Expeditions Ltd;

iii. Misamaha ya kodi iliyotolewa kwa Kampuni zisizostahili kiasi cha shilingi 53,399,565;

iv. Misamaha ya kodi iliyotolewa bila viambatisho vya maombi (*Tax exemptions granted to unsupported applications);*

v. Matumizi ya nyaraka za kughushi kujipatia Misamaha ya kodi;

vi. Misamaha ya kodi iliyotolewa kwa Kampuni ambazo zilikwishafunga kazi zake kiasi cha shilingi 119,194,409; na

vii. Msamaha wa kodi wa kiasi cha shilingi 2,500,103,579 uliotolewa kwa Kampuni ambazo ziliwasilisha nyaraka za leseni zilizokwisha muda wake.

Kwa muda wa Miaka mitatu iliyopita (2012 – 2015), mwenendo wa Misamaha ya kodi ukilinganisha na Makusanyo ya TRA ni kama inavyoonekana katika Jedwali lifuatalo: -

**Jedwali Namba 1.**
**Hali halisi ya Misamaha ya kodi kwa kipindi cha mwaka 2012 - 2015**


| MWAKA | MAKUSANYO HALISI (SHILINGI) | MISAMAHA YA KODI (SHILINGI) | % YA MISAMAHA UKILINGANISHA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|
| 2012/2013 | 8,117,588,095,662 | 1,515,607,377,799 | 18.67 |
| 2013/2014 | 9,889,970,048,436 | 1,834,097,360,356 | 18.55 |
| 2014/2015 | 10,629,231,196,907 | 1,627,011,920,914 | 15.31 |

***Chanzo: Taarifa ya CAG kuhusu ukaguzi Maalum wa Misamaha ya kodi.***

**Mheshimiwa Spika,** Kama inavyoonekana katika Jedwali hapo juu, Kumekuwa na kushuka kwa Misamaha ya kodi kwa mwaka 2014/2015 kutoka 18.5% (mwaka 2013/14) hadi kufikia 15.31% ya kiasi cha kodi kilichokusanywa na Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA) katika mwaka huu tunaoutolea Taarifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea Kusisitiza kuwa, jitihada ziendelee kuchukuliwa ili kupunguza Misamaha ya kodi ikiwa ni pamoja na kusimamia Misamaha inayotolewa kuhakikisha inatumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Mwenendo wa Makusanyo ya kodi ya TRA ukilinganisha na Misamaha ya kodi kati ya mwaka 2012 – 2015 ni kama inavyofafanuliwa katika grafu ifuatayo: -

**Grafu Namba 1: Mwenendo wa Makusanyo ya Kodi na Misamaha ya Kodi kuanzia mwaka wa fedha 2012/13 hadi 2014/15**




***Chanzo: Taarifa ya ukaguzi ya TRA kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2015.***

**Mheshimiwa Spika,** Grafu hapo juu inadhihirisha kuwa mwenendo wa Misamaha ya kodi ukilinganisha na Makusanyo ya kodi ya TRA inapungua mwaka hadi mwaka japokuwa bado haijashuka kiasi cha kutosha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua juhudi za Serikali kushusha Kiwango cha Misamaha ya kodi kama ilivyofafanuliwa hapo juu. Hoja ya msingi ya Kamati inayohitaji msisitizo ni kuitaka Serikali iendelee kufanya jitihada kuzuia matumizi yasiyofaa ya Misamaha ya kodi na kuipunguza kwa kadri iwezekanavyo ili kuhakikisha fedha za Serikali zinazotakiwa kukusanywa kama kodi zinakusanywa ipasavyo.

**b) Rufaa za muda mrefu kuhusu mashauri ya kodi *(Long outstanding tax appeals cases)***

Kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2014, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilibainisha kuwa TRA ilikuwa haijakusanya kodi za Jumla ya shilingi 1,716,000,000,000 kutokana na rufaa za mashauri ya kodi zilizopo kwenye Baraza la kodi kwa muda mrefu. Aidha, kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2015 thamani ya rufaa za mashauri hayo ya kodi ilifikia shilingi 6,850,000,000,000.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya Kamati katika suala hili ni kuwa, ongezeko kubwa la kodi isiyokusanywa kwa sababu ya rufaa za mashauri ya kodi ndani ya mwaka mmoja wa fedha ni kubwa. Hivyo basi, kuna umuhimu wa Serikali kupitia TRA na Wizara ya Fedha na Mipango kuwa na mikakati endelevu ya kukusanya kodi hizo kwa kumaliza mashauri hayo mapema iwezekanavyo ili kuongeza Mapato ya Serikali.

**c) Malipo ya Pensheni na Kiinua Mgongo kwa wakati mmoja *(Double payment of benefit scheme)* kwa baadhi ya Watumishi wa TRA**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2015 Mamlaka ya mapato Tanzania iliwalipa watumishi wake ishirini na tisa (29) wa nafasi ya Menejimenti Jumla ya shilingi 1,397,130,770 kama malipo ya Kiinua Mgongo *(Gratuity)* baada ya kumalizika kwa Mikataba yao ya kazi.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa wakati huo huo iliendelea kuwalipia Watumishi hao michango ya kati ya asilimia kumi (10) hadi kumi na tano (15) katika Mifuko ya Hifadhi za Jamii kwa ajili ya michango ya Pensheni.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya Kamati na CAG kwa jambo hili ni kuwa, malipo hayo yanaenda kinyume na matakwa ya Sheria za Utumishi wa Umma na Sheria za Hifadhi ya Jamii zinazozuia malipo ya mafao mara mbili *(Double payment of benefits)* kwa Mtumishi mmoja kama ilivyofanyika TRA.

***Ongezeko la nakisi ya uwezo wa PSPF kulipa mafao ya Wastaafu* (Actuarial deficit)**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2015 imebainisha kuwa uwezo wa Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma (PSPF) kulipa mafao yake unazidi kupungua kwa kuzingatia Taarifa ya kitaalam ya tathmini ya muda mrefu ya uwezo wa Mfuko[1] *(Actuarial valuation report)*.

**Mheshimiwa Spika,** Tathmini ya muda mrefu ya Mfuko hupima uwezo wa kifedha kwa kuangalia uwiano wa akiba *(Reserve)* iliyopo na akiba ya Mfuko katika kulipa mafao ya Wanachama na gharama za uendeshaji. Kipimo hiki kinaonyesha idadi ya miaka ambayo Mfuko unaweza

[1] An actuarial valuation is a mathematical analysis of the financial condition of a pension plan to cover its demographic and financial liabilities, SSRA (2015).

kulipa mafao ya Wanachama na kumudu gharama zote za uendeshaji bila kukusanya chochote.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya tathmini imeonyesha ongezeko la mtaji hasi *(Actuarial deficit)* ambao umefikia kiasi cha shilingi trilioni 11.15 hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2014.Kupungua kwa mtaji wa PSPF ambako pia kunashusha uwezo wa PSPF kulipa mafao ya Wastaafu kumesababishwa na sababu kuu zifuatazo: -

(a) Kuchelewa kwa Serikali kulipa deni la michango lililotokana na Mafao yaliyo lipwa kwa Wastaafu waliokuwa Watumishi wa Serikali waliokuwepo kabla ya Mfuko kuanzishwa mnamo tarehe 01 Julai, 2009 ambapo Serikali iliitaka PSPF kuwalipa Wastaafu hao wakati walikuwa hawachangii katika Mfuko.

(b) Madeni makubwa ambayo PSPF inadai katika Taasisi mbalimbali za Serikali na ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu yanayofikia kiasi cha shilingi bilioni 499.7, (Kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2015)

(c) PSPF kutekeleza Miradi ya Uwekezaji bila ya Miradi hiyo kurudisha fedha za Uwekezaji ndani ya muda mwafaka.

(d) Kutozingatiwa kwa Sera ya Uwekezaji ya Shirika, mathalani Sera ya Uwekezaji ya PSPF inataka Uwekezaji kwenye Mikopo na Miradi maalum ya Serikali iwe kati ya asilimia 0-10 ya Uwekezaji wote *(% of total limit of investment)*, lakini PSPF wamewekeza katika eneo hilo kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2015 kwa asilimia 53.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipitia Mkakati wa Serikali katika kurejesha deni la PSPF ambapo ilibainika kuwa kati ya mwaka 2010 hadi Oktoba 2016 Serikali imekwisha fidia kiasi cha shilingi bilioni 243.27 kati ya shilingi bilioni 429.60. Pamoja na jitihada hizo, Nakisi ya shilingi trilioni 11.15 bado haijafanyiwa kazi ipasavyo pamoja na deni ambalo PSPF inadai toka kwa Taasisi mbalimbali za Serikali linalofikia shilingi bilioni 499.7.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umedhihirisha kuwa PSPF inahitaji Mkakati wa dharula ili kutimiza majukumu yake ipasavyo. Mathalani, kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30,2015 PSPF ilikusanya michango ya shilingi bilioni 661,750,672,000 kutoka kwa Wanachama na wakati huo huo ikalipa mafao ya shilingi 663,951,130,000 kiasi ambacho ni zaidi ya shilingi 2,200,458,000 ya Makusanyo ya michango. Tafsiri ya jambo hili ni kuwa PSPF haiwezi kulipa mafao ya Wanachama wake kwa kupitia fedha za

michango pekee, inalazimika kutafuta fedha kutoka vyanzo vingine ili kulipa mafao kwa wahusika.

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto za PSPF ni za muda mrefu. Kamati ilifahamishwa kuwa Serikali imetenga [2]shilingi bilioni 150 ili kulipa deni hilo, hata hivyo fedha hizo zinategemewa kutolewa kati ya mwezi Novemba na Disemba 2016.Kwa michango ya kabla ya mwaka 1999, Serikali iliifahamisha Kamati kuwa itatolewa Hati fungani maalum *(Non cash bond)* ambayo italipwa kabla ya mwezi Februari, 2017.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya Kamati katika jambo hili ni kuwa, ni muda mwafaka sasa wa Bunge kuitaka Serikali kutimiza wajibu wake kwa kukamilisha mchakato wa urejeshaji wa fedha zinazotakiwa na PSPF ili kuhakikisha Wastaafu wanalipwa stahiki zao kwa wakati bila kuchelewa.

**Matumizi makubwa ya fedha katika gharama za uendeshaji *(Staff cost and operating expenses)* katika Mamlaka za udhibiti wa utoaji Huduma**

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi uliofanywa na Kamati katika eneo la matumizi ya gharama za Watumishi na uendeshaji *(Staff cost and operating expenses)*, katika Mashirika ya Umma yanayotekeleza shughuli za udhibiti wa utoaji wa huduma kama maji, nishati, mawasiliano na usafiri wa majini na Nchi Kavu, jambo moja kubwa la dhahiri lililobainika ni gharama kubwa zinazotumiwa na Taasisi kiuendeshaji ikilinganishwa na Taasisi nyingine za Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2015 Kamati ilichambua na kujadili Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka ya udhibiti wa nishati na maji (EWURA) na Mamlaka ya udhibiti wa usafiri wa majini na Nchi kavu (SUMATRA) ili kuweza kufafanua kwa kina hoja inayohusu matumizi makubwa katika eneo la gharama za uendeshaji katika Mamlaka hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa hoja ya Kamati ni kufanya ulinganifu wa mapato yanayokusanywa na Mamlaka za udhibiti wa Huduma, matumizi ya Mamlaka hizo na michango au gawio wanalopeleka Serikalini.Kilichobainika kwa kiasi kikubwa ni kuwa Mamlaka hizo zimekuwa na matumizi makubwa ya Kiuendeshaji na Utawala wakati wakipeleka gawio dogo Serikalini kama inavyofafanuliwa katika Jedwali lifuatalo: -

**Jedwali Namba 2.**

[2] Taarifa rasmi za Bunge (Hansard) ya tarehe 25/10/2016, Maelezo ya Naibu Katibu Mkuu wa Wizara fedha na Mipango mbele ya Kamati, Dodoma

**Mapato, Matumizi na Gawio toka EWURA na SUMATRA kwenda Serikalini kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2015**


| NA. | TAASISI | MAPATO | MATUMIZI | GAWIO LA SERIKALI |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | EWURA | 38,690,000,000 | 27,490,594,000 | 2,000,000,000 |
| **2.** | SUMATRA | 39,351,456,000 | 32,389,499,000 | 2,000,000,000 |

***Chanzo: Taarifa za ukaguzi za CAG kwa Hesabu za EWURA na SUMATRA kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2015.***

**Mheshimiwa Spika,** Kama inavyoonekana katika jedwali hapo juu, Taasisi hizo mbili (ambazo ni mfano tu wa kuwasilisha hoja hii) zinazohusika na udhibiti wa huduma kwa mwaka wa fedha 2014/ 2015 zilipeleka Serikalini gawio la wastani wa 5.1% na 5.0% ya mapato yake.

**Mheshimiwa Spika,** Utaratibu huo ni kinyume na masharti ya Sheria ya fedha ya mwaka 2015 ambayo ilielekeza baadhi ya Mashirika ya Umma kupeleka gawio Serikalini kwa kiasi cha kati ya asilimia (10) hadi kumi na tano [3](15) ya mapato yake. Mwenendo wa Makusanyo, matumizi na gawio kwenda Serikalini unaonekana katika grafu ifuatayo:-

**Grafu Namba 2: Hali ya Mapato, Matumizi na Gawio la Serikali kutoka EWURA na SUMATRA**




***Chanzo: Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za EWURA na SUMATRA kwa mwaka wa fedha 2014/15.***

[3] Masharti ya Kifungu cha 49 cha Sheria ya fedha ya mwaka 2015

**Mheshimiwa Spika,** Kama inavyoonekana katika grafu hapo juu, gawio linalokwenda Serikalini kutoka katika Mashirika hayo mawili ni dogo sana ukilinganisha na mapato yanayokusanywa pamoja na matumizi yanayofanywa na Taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya Kamati ni kuwa, ni muda mwafaka kwa Serikali kupitia kwa Msajili wa Hazina (TR) kupitia upya Sheria, Miundo, Mishahara, Posho, na Stahiki mbalimbali katika Mashirika yanayohusika na udhibiti wa huduma ili kufanyike Mabadiliko katika Sheria mbalimbali ikiwa ni pamoja na Sheria zijazo za fedha ili yaweze kuchangia ipasavyo kwa angalau asilimia ishirini (20) ya mapato yake kwenda Serikalini.

**Shirika la Taifa Hifadhi ya Jamii (NSSF)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepitia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Hesabu zilizokaguliwa za Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2015.Katika Taarifa ya ukaguzi ya NSSF, jambo mahsusi la msisitizo lilihusu utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Kigamboni Satellite Village *(Dege Eco Village)*, Kigamboni.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa hoja ya CAG, makubaliano ya Mkataba yalionyesha kuwa NSSF watakuwa na hisa 45% na Azimio Housing Estates (AHEL) hisa 55% katika Mradi huo. Aidha, AHEL walitakiwa kutoa ardhi ya ekari 20,000 ambayo itakuwa sawa na 20% ya hisa zao na hisa 35% watachangia kwa kutoa fedha. NSSF wao walitakiwa kuchangia 45% ya hisa zao katika Mradi kwa kutoa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya ukaguzi ya NSSF imebainisha kuwa Mradi wa *Dege Eco Village* umesimama kwa sasa kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo namna bora ya kugharimia Mradi huo kati ya Wabia wawili na suala la Ukubwa wa ardhi ambayo ilitakiwa katika uendelezaji wa Mradi. Pamoja na majadiliano na Wakaguzi wa Hesabu za NSSF, Bodi na Menejimenti ya NSSF na Msajili wa Hazina (TR), Kamati ilikuwa na maoni kuwa jambo hili linahitaji uchambuzi na uhakiki kabla ya kuhitimishwa.

**Mheshimiwa Spika,** [4]Maoni ya CAG *(Recommendations)* wakati anahitimisha hoja ya Mradi wa Dege Eco village hususan uchangiaji wa ardhi katika Mradi husika ni kama ifuatavyo: -

---

[4] Ukurasa wa 25 wa majibu ya hoja za ukaguzi *(Management letter)* ya NSSF kwa mwaka 2014/2015

***" …Management should ensure that the measurement of all the acres included in the Contract are the same as those indicated in the title deeds,……Management should confirm from the Ministry of land and housing development that Azimio Housing Estate owns 19,700 acres at Kigamboni free of any encumbrances to avoid NSSF entering into conflicts with villagers…"***

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na hoja ya CAG kuhusu uchangiaji wa ardhi katika Mradi husika na kwa lengo la kuwa na wigo mpana *(Scope)* ili Kamati iweze kulishauri Bunge lako Tukufu kwa misingi yenye weledi na haki, Kamati imeamua kuunda Kamati Ndogo kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (18) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.Kamati hiyo Ndogo itajikita katika kutekeleza yafuatayo: -

(a) Kupata uelewa wa dhana, dhima na maudhui ya Uwekezaji wa mtaji kwenye Miradi ya Ujenzi kwa makubaliano ya kutoa ardhi *(Land for equity)* ili kubainisha vigezo vinavyokubalika *(agreed best practices)* katika utekelezaji wa Miradi kwa njia hiyo;

(b) Kuthibitisha iwapo ekari 19,700 zilizobaki *(kwa sababu CAG amethibitisha hadi sasa zipo ekari 300)*, zilizotakiwa kuchangiwa katika Mradi huo zipo kama Taarifa ya ukaguzi ilivyokuwa imehoji;

(c) Kupitia makubaliano ya Mkataba wa ugharamiaji wa Mradi wa *Dege Eco Village* na mgawanyo wa hisa;

(d) Kupitia Taarifa ya utekelezaji wa Mradi hadi hapo ulipofikia;

(e) Kufanya ulinganifu *(Review)* wa utekelezaji wa Mradi wa Dege Eco Village na Miradi mengine iliyotekelezwa na Mashirika ya Umma kwa makubaliano ya *(Land for Equity)*; na

(f) Kuishauri Serikali hatua za kuchukua ili kuhakikisha Mradi unakamilika na fedha za Umma zilizowekezwa zinaleta tija na ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya Kamati katika jambo hili ni kuwa, kunahitajika uchambuzi wa kina na Taarifa za kutosha kuhusu utekelezaji wa Miradi ya "*Land for equity*" kama alivyoibua CAG ikizingatiwa hoja mahsusi ya ukaguzi ilihusu suala la ardhi ambayo CAG anahitaji NSSF wajiridhishe iwapo Mbia mwenza anamiliki. Ni dhahiri kuna masuala bado yanahitaji majibu kabla ya kufikia

uamuzi wa mwisho. Kamati itakuwa katika nafasi nzuri ya kulitolea Taarifa jambo hilo baada ya kukamilika kwa uchambuzi wa kitaalamu wa hoja husika ya ukaguzi utakaofanyiwa kazi na Kamati Ndogo baada ya Mkutano huu wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja nyingine kuhusu Taarifa ya ukaguzi wa NSSF ilihusu utoaji wa Mikopo ya SACCOS kwa Wanachama wake. Dosari iliyoibuliwa na CAG ni kutorejeshwa kwa Mikopo kwa wakati na dosari katika utaratibu mzima wa utoaji wa Mikopo hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30,2015 NSSF ilitoa jumla ya Mikopo yenye thamani ya Shilingi 41,580,505,000 *(kwa mwaka wa fedha 2014 ilikuwa shilingi 25,581,201,000)* kwa SACCOS mbalimbali. Miongoni mwa dosari zilizobainika wakati wa utoaji wa Mikopo hiyo ni pamoja na utoaji wa Mikopo kwa SACCOS asilimia 50 zaidi ya thamani ya dhamana ya SACCOS na utoaji wa Mikopo bila ya kuchambua Taarifa za ukaguzi wa Hesabu za miaka mitatu (3) mfululizo za SACCOS husika kama inavyotakiwa. Aidha maelezo ya [5]Mwenyekiti wa Bodi ya NSSF kwa Kamati yalifafanua kuwa uchunguzi wa awali umebaini kutokuwepo kwa baadhi ya SACCOS zilizopewa Mikopo hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Mfano wa SACCOS ambazo zilipata Mikopo zaidi ya shilingi bilioni 1 ni pamoja na Simika General traders, Uvikasa SACCOS, Bumbuli development SACCOS na RUMAKO agricultural.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na dosari hizo, mnamo tarehe 24 Oktoba, 2016 Kamati ilipokutana na Bodi na Menejimenti ya NSSF, ilifikia uamuzi wa kumuomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ukaguzi maalum wa utaratibu wa utoaji wa Mikopo hiyo. Aidha, Kamati iliazimia kuwa Kamati Ndogo ya PAC iliyoundwa kushughulikia suala la *Dege Eco Village* kutumia Taarifa ya ukaguzi maalum wa CAG kufanya uhakiki juu ya uwepo wa SACCOS husika na iwapo zilinufaika na mikopo hiyo.

**Hasara ya shilingi 6,793,310,000 katika fungu 43 Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kutokana na kuharibika mahindi yaliohifadhiwa tani 13,583**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kupitia kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya chakula (NFRA) ilipata hasara ya jumla ya shilingi 6,793,310,000 iliyotokana na kuharibika kwa tani za mahindi 13,583 zilizokuwa zimehifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya chakula. Kati

[5] Taarifa rasmi za Bunge *(Hansard)*, Maelezo ya Mwenyekiti wa Bodi ya NSSF mbele ya Kamati tarehe 24 Oktoba, 2016. Dodoma

ya tani hizo (13,583) zilizoharibika, tani 13,290 ziliharibika katika Mikoa ya Dodoma, Arusha, Rukwa na Ruvuma.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na kwa kurejea majibu ya [6]Afisa Masuuli wa fungu 43, sababu kubwa ya kuharibika kwa mahindi hayo ni utunzaji usiofaa uliotokana na Kutokuwepo kwa maghala ya kutosha ya kuhifadhia nafaka hali iliyosababisha mahindi kunyeshewa mvua na kuharibika kiasi ambacho hayawezi tena kutumika kwa ajili ya chakula.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa maelezo ya Afisa Masuuli hasara hiyo pia ilitokea kutokana na uamuzi wa Serikali kuelekeza Wakulima kutouza mahindi Nje ya Nchi na badala yake kuyapeleka katika vituo vya NFRA ili yanunuliwe na Serikali wakati uwezo wa Serikali kununua na kuhifadhi ipasavyo mahindi na nafaka zilizozalishwa na Wakulima ulikuwa mdogo.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya Kamati ni kuwa, ni muhimu Serikali ifanye tathmini ya kina na kutumia Matokeo ya tathmini hiyo kuangalia upya katazo la kuzuia Wakulima kuuza mazao ya nafaka Nje ya Nchi ikiwa ni sambamba na Ujenzi wa maghala mapya ya kuhifadhia chakula ili kuepusha hasara kwa Serikali kama ilivyotokea lakini pia kuhakikisha Wakulima Watanzania wananufaika kwa shughuli za Kilimo.

***Madeni ya Serikali katika Mifuko ya Hifadhi za Jamii***

**Mheshimiwa Spika,** Nchi yetu ina Mifuko sita (6) ya Hifadhi ya Jamii ambayo ni Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF), Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Serikali (GEPF) na Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma (PSPF). Mifuko mingine ni Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (LAPF).

**Mheshimiwa Spika,** Mifuko hiyo ya Hifadhi ya Jamii imekuwa chini ya Uangalizi wa Benki Kuu ya Tanzania (BOT) na Mamlaka ya udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) kwa kushirikiana na Wizara mama za Mifuko husika.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na utoaji wa huduma za Hifadhi ya Jamii, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imekuwa ikishiriki katika utoaji wa huduma mbalimbali za Kijamii kama Ujenzi wa Vyuo, Ujenzi wa Majengo ya Huduma za Afya, Uwekezaji kwenye Miradi mbalimbali ya Maendeleo na Uwekezaji kwenye dhamana za Serikali kama vile Hati fungani.

[6] Taarifa rasmi za Bunge *(Hansard)*, Kikao cha Kamati cha Tarehe 26/08/2016, Dodoma

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30,2015 umebaini kuwa Serikali na Taasisi zake zinadaiwa Jumla ya shilingi 1,546,650,400,000 na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

**Mheshimiwa Spika,** Mikopo hiyo yenye Jumla ya shilingi 1,546,650,400,000 inajumuisha deni halisi *(Principle)* shilingi 754,572,049,000, riba *(Interest)* shilingi 698,896,788,000 na tozo *(Penalty)* shilingi 93,181,563,000. Ukiondoa deni la Mfuko wa Pensheni la watumishi wa Serikali (GEPF) kwa Serikali, deni la Mifuko mitano ya Hifadhi ya Jamii kwa Serikali ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali lifuatalo: -

**Jedwali Namba 3.**
**Hali ya Madeni ambayo Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inadai Serikali kwa hadi tarehe 30 Juni, 2015**

| MFUKO | DENI HALISI | RIBA | ADHABU | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| **LAPF** | 47,189,300,000 | 6,445,206,000 | - | 53,634,506,000 |
| **PSPF** | 97,670,000,000 | 162,380,000,000 | 88,350,460,000 | 348,400,460,000 |
| **PPF** | 21,986,441,000 | 48,836,953,000 | - | 70,823,394,000 |
| **NHIF** | 62,334,721,000 | 9,770,449,000 | 4,831,103 | 76,936,273,000 |
| **NSSF** | 525,391,587,000 | 471,461,180,000 | - | 996,855,767,000 |
| **Jumla** | **754,572,049,000** | **698,896,788,000** | **93,181,563,000** | **1,546,650,400,000** |

***Chanzo: Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2015.***

**Mheshimiwa Spika,** Kama inavyoonekana katika jedwali hapo juu, deni la Serikali kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii limekuwa likiongezeka hasa kutokana na riba na adhabu inayotozwa kwa sababu ya kuchelewa kurejesha Mikopo husika. Kamati ilifahamishwa kuwa Serikali imekuwa katika hatua za uhakiki wa deni hilo ili lianze kulipwa. Hata hivyo, mchakato huo umechukua muda mrefu na hivyo kuendelea kuwa na athari katika utekelezaji wa Mipango ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

**Mheshimiwa Spika,** Kuchelewa kwa namna yeyote kulipa madeni haya kwa wakati kunasababisha ongezeko la riba na tozo na hivyo kuongeza deni la Serikali. Aidha, jambo hili linapunguza uwezo wa kifedha *(Liquidity)* wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kulipa Pensheni na kutekeleza majukumu yake mengine kwa mujibu wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya Kamati kuhusu deni hilo ni kuwa, pamoja na jitihada zilizochukuliwa kwa muda mrefu kuhakiki madeni hayo ya Mifuko ya Hifadhi za Jamii, ni wajibu wa Serikali kuwa na Mpango maalum wa kulipa madeni hayo ili Mifuko hiyo iepuke athari ya kuwa na uwezekano wa kutolipa Mafao kwa sababu ya kutorejeshwa Mikopo *(Credit risk)*.

### *Dosari katika Mfumo wa Udhibiti wa mapato ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua jitihada zinazofanywa na Serikali ya awamu ya tano katika kudhibiti mapato ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na kuimarisha ufanisi wa Mamlaka hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Jitihada zinazochukuliwa na Serikali zimekuja kwa muda mwafaka kwa sababu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2015 imebainisha dosari kadhaa ambazo ziliisababishia Mamlaka hiyo kupoteza Mapato yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inalazimika kuzielezea changamoto zilizosababisha Mamlaka ya Bandari kupoteza mapato ili kuunga mkono jitihada za Serikali katika kuongeza mapato ya Nchi na pia kuitaka kuendelea kuimarisha usimamizi wa Mamlaka ya Bandari ipasavyo. Kwa mwaka tunaoutolea Taarifa, dosari zifuatazo zilijitokeza katika udhibiti na usimamizi wa mapato katika Mamlaka ya Bandari Tanzania: -

(a) Mapungufu katika Mfumo wa COBOL unaotumiwa na Mamlaka ya Bandari ambao ulikuwa na changamoto za kuwasiliana na Mifumo tanzu kama vile *Harbor View Plus* (HVP), *Cargo Management System* (CMS) na *Tanzania Customs Intergrated System* (TANCIS) unaomilikiwa na Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA) hivyo kutoa mianya ya upotevu wa mapato;

(b) Taarifa ya ukaguzi ilibaini uwepo wa Meli tatu (3) ambazo Taarifa za mapato yake hazikuonekana katika Mfumo hivyo kuwepo uwezekano wa Meli hizo kuondoka bila kulipa mapato ya Mamlaka;

(c) Ilibainika kuwa mapato ya Meli nne (4) yaliandikwa katika vitabu vya Hesabu za Mamlaka miezi kumi na nane (18) baada ya Meli husika kuondoka. Tafsiri ya kawaida kwa jambo hili ni kuwa sio rahisi kuwa na uhakika iwapo mapato stahiki yalikusanywa kwa Meli hizo;

(d) Uwepo wa Meli ambazo zimesajiliwa kwa hadhi za kidiplomasia *(Diplomatic status)* ambazo kwa mujibu wa Sheria hazilipi kodi. Lakini katika ukaguzi ilibainika uwepo wa Meli nne (4) ambazo hazikuwa na Nyaraka za uthibitisho kuwa Meli hizo zina hadhi ya kidiplomasia hivyo kuna uwezekano mapato ya Serikali haya kukusanywa katika Meli hizo; na

(e) Jambo lingine ni Mamlaka ya Bandari kushindwa kupata moja kwa moja na kuhakiki Taarifa ya Meli na mizigo inayohudumiwa na Kitengo cha Kuhudumia Makontena cha TICTS hivyo kutokuwa na uhakika wa Taarifa za fedha wanazolipwa na TICTS iwapo zinaendana na uhalisia wa Meli zilizohudumiwa na Kitengo hicho.

**Mheshimiwa Spika,** Ni kutokana na hoja za ukaguzi tajwa hapo juu ilikuwa vigumu kwa Mkaguzi kuthibitisha kiasi halisi cha fedha kilichotakiwa kukusanywa na Mamlaka ya Bandari hivyo kuwepo viashiria vya upotevu wa mapato.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya Kamati katika jambo hili, ni kuongeza mapato ya Serikali kwa kuimarisha Mifumo ya udhibiti wa ndani ya Bandari na kuunga mkono jitihada za Serikali zinazoendelea kuboresha shughuli za Bandari.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwingine, katika Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Kamati iliweza kubaini pia uwepo wa Akaunti ya muda maalum *(Fixed deposit)* ya shilingi bilioni 440 iliyokuwa imewekwa katika mabenki manne tofauti. Hata hivyo, kulijitokeza mkanganyiko wa riba iliyotumika katika ufunguzi wa Akaunti hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na hali hiyo Kamati iliazimia na kumuomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalum *(Special audit)* wa miamala ya Akaunti hiyo ili kuweza kubaini riba iliyotozwa na faida iliyopatikana kutokana na Uwekezaji huo.

***Uchambuzi wa Ripoti ya CAG kuhusiana na ukaguzi kwenye manunuzi ya Umma katika mwaka wa fedha 2015***

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011, Mamlaka ya udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) hufanya ukaguzi ni kwa kiasi gani Taasisi za Umma zinakuwa zimengatia Sheria ya Manunuzi ya Umma katika utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kawaida ukaguzi unaofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), hujikita zaidi katika Taarifa za Hesabu na pia CAG katika Taarifa zake huweka aya maalum ya kuongelea masuala ya Manunuzi ya Umma kwa muhtasari.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imekuwa ikichambua Taarifa za ukaguzi za PPRA sambamba na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa sababu zote zimelenga kuibua hoja za matumizi ya fedha za Umma. Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya CAG pamoja na sehemu ya Taarifa ya PPRA kuhusu manunuzi ya Umma umebaini yafuatayo: -

a) **Kutozingatiwa kwa Mpango wa mwaka wa Manunuzi *(Annual Procurement Plan)***

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 48(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 kinamtaka Mkaguzi wa kila Wizara, Idara, Wakala au Shirika la Umma kutoa maoni iwapo Taasisi husika umezingatia Sheria ya Manunuzi katika utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ulibaini kuwa jumla ya Taasisi Saba (7) za Serikali zilikiuka Sheria ya Manunuzi ya Umma kwa kufanya manunuzi yenye thamani ya shilingi 8,462,110,917 kinyume na Mpango wa mwaka wa Manunuzi *(Annual Procurement Plan)* jambo ambalo linakiuka masharti ya Kifungu 49(2)(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011.

Taasisi hizo za Umma zilizohusika na ukiukwaji wa Sheria ya Manunuzi ya Ummana Kiwango cha fedha kilichohusika ni kama ifuatavyo katika Jedwali la uchambuzi: -

**Jedwali Namba 4.**
**Baadhi ya Taasisi ambazo zilikiuka Sheria ya Manunuzi ya Umma**

| TAASISI | MAELEZO | KIASI (TZS) |
|---|---|---|
| Idara ya Magereza | Manunuzi kufanyika Nje ya Mpango wa Manunuzi | 911,906,006 |

| TAASISI | MAELEZO | KIASI (TZS) |
|---|---|---|
| (fungu 29) | | |
| Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma (fungu 72) | Shughuli za Mkataba kutoingizwa kwenye Mpango wa manunuzi | 45,538,560 |
| Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa (fungu 73) | Gharama za Mkataba zilizoingiwa zaidi ya zilizoonyeshwa kwenye Mpango wa Manunuzi | 9,215,700 |
| Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali (fungu 23) | Manunuzi kufanyika Nje ya Mpango wa Manunuzi | 827,043,110,917 |
| Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI (fungu 56) | Manunuzi yasiyozingatia taratibu | 1,995,557,870 |
| Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa (fungu 34) | Manunuzi kufanyika kuzidi Gharama za kwenye Mpango wa Manunuzi | 4,617,947,311 |
| Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza (fungu 81) | Kuingia Mkataba bila ya kuwa na fedha za kugharimia Mkataba | 54,902,400 |
| **JUMLA** | | **8,462,110,917** |

***Chanzo: Taarifa mahsusi za ukaguzi wa Mafungu husika kwa mwaka wa fedha 2014/2015.***

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya Kamati kwa kuzingatia rejea ya jedwali hapo juu ni kuwa hali ya Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi kwa mwaka 2014/2015 ilipungua ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2013/2014. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Taasisi nne (4) ndio hazikuzingatia Mpango wa mwaka wa Manunuzi ukilinganisha na Taasisi Saba (7) katika mwaka huu wa fedha tunaoutolea Taarifa. Ongezeko hilo la Kutozingatiwa Sheria *(Non compliance)* ni kiasi cha asilimia 75 kwa mwaka mmoja wa fedha.

**b) Manunuzi kufanyika bila ushindani**

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu 163 na Kifungu 164 cha Kanuni za manunuzi ya Umma za mwaka 2013 kinaelekeza kuwa Taasisi za Ununuzi *(Procuring entity)* lazima zipate maoteo ya gharama za huduma au zabuni *(Quotation)* kutoka kwa angalau Wazabuni watatu (3) lengo likiwa ni kuangalia bei nafuu ya huduma tarajiwa bila ya kuathiri ubora wa huduma.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa jumla ya Taasisi tisa (9) za Umma zilifanya manunuzi ya Jumla ya shilingi 27,121,224,071 bila ya kuzingatia Kifungu 163 na 164 cha Kanuni za Manunuzi ya Umma. Sababu zilizotolewa na Taasisi hizo zilikuwa hazijitoshelezi ili kufunga hoja husika. Taasisi hizo ni kama inavyoonekana katika Jedwali lifuatalo: -

**Jedwali Namba 5.**
**Taasisi za Umma ambazo zilifanya Manunuzi bila ushindani**

| TAASISI | MAELEZO | KIASI (TZS) |
|---|---|---|
| Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma (fungu 82) | Manunuzi kufanyika toka kwa Mzabuni mmoja *(Single source)* bila maelezo ya kutosha ya uamuzi huo | 53,309,600 |
| Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga (fungu 86) | Ukiukwaji wa Gharama za maoteo ya Zabuni | 23,997,265 |
| Jeshi la Kujenga Taifa (fungu 39) | Mkataba wenye utata wa kutoa huduma za chakula katika Kambi ya Rwamkoma | 150,630,000 |
| Jeshi la Polisi (fungu 28) | Manunuzi kufanyika toka kwa Mzabuni mmoja *(Single source)* bila maelezo ya kutosha ya uamuzi huo | 1,517,600,000 |
| Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI (fungu 56) | Manunuzi kufanyika bila kutangaza Zabuni | 372,960,000 |
| Jeshi la Wananchi (fungu 38) | Manunuzi bila ushindani | 14,706,603,298 |
| Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi (fungu 76) | Manunuzi bila ushindani | 2,904,200 |
| Wizara ya Katiba | Uchapishaji wa Vitabu vya | 6,000,000,000 |

| TAASISI | MAELEZO | KIASI (TZS) |
|---|---|---|
| na Sheria (fungu 41) | Katiba bila kufuata Sheria | |
| **JUMLA** | | **22,834,004,363** |

***Chanzo: Taarifa mahsusi za ukaguzi wa Mafungu husika kwa mwaka wa fedha 2014/2015.***


**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya Kamati ni kuwa Kufanya manunuzi bila kushindanisha Watoa huduma na Zabuni kunaweza kuisababishia Serikali kutopata thamani halisi ya fedha *(Value for money)* zilizotumika.

**c) Manunuzi kufanyika bila kuwa na thamani halisi ya fedha *(Value for money)***

**Mheshimiwa Spika,** Vigezo vitano vilitumika ili kuchagua Miradi ya kufanyia ukaguzi ili kubaini iwapo thamani halisi ya fedha imepatikana katika Miradi hiyo. Vigezo hivyo ni pamoja na uandaaji, usanifu, uhifadhi wa nyaraka, mchakato wa manunuzi, usimamizi wa kazi za Ujenzi, ubora na ukubwa kazi zilizotekelezwa na ufungaji wa Miradi.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya uhakiki yamebaini kuwa Miradi 139 kati ya 186 ilipata alama ya kuridhisha, 32 ilipata alama za Wastani na Mikataba 15 ilipata Wastani usioridhisha (chini ya asilimia 50) ikiwa na maana kuwa malengo ya Miradi yanaweza yasifikiwe na kuna uwezekano wa kutopata thamani halisi ya fedha zilizotumika. Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi kwa Taasisi zilizokaguliwa na PPRA, umefafanuliwa katika grafu hapa chini: -

Grafu Namba 3: Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi katika Miradi iliyo kaguliwa




**Mheshimiwa Spika,** Grafu hapo juu inafafanua hali ya zingatiaji wa Sheria ya Manunuzi na Kanuni zake kwa Miradi iliyokaguliwa. Hali ya uzingatiaji inaridhisha kwa wastani hivyo kunahitajika juhudi za kuendelea kuwataka Maafisa Masuuli kuhakikisha wanazingatia Sheria husika na hatua kuchukuliwa kwa wale wanaoshindwa kuzingatia Sheria hiyo.

### d) Malipo yenye utata kwa huduma ambazo baadhi hazikupokelewa na nyingine hazikufuata utaratibu

**Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi wa manunuzi ya Umma pia ulibaini malipo ya shilingi 3,253,650,189 yenye utata yaliyofanywa na Taasisi nne (4) ambapo Watoa huduma walilipwa kwa kazi ambazo hazikufanyika *(Non existence and shoddy works)*. Taasisi hizo na kiasi cha fedha kilichohusika ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali hapa chini: -

**Jedwali Namba 6.**
**Taasisi zilizolipia huduma ambazo hazikufuata utaratibu na nyingine hazikupokelewa**

| TAASISI | MAELEZO | KIASI (TZS) |
|---|---|---|
| Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera (fungu 87) | Ununuzi wa gari ambalo halikupokelewa | 88,928,632 |
| Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha (fungu 70) | Malipo ya kusimika mtandao wa internet (LAN) ambao haukufungwa | 5,280,000 |
| Wizara ya Mifugo na Uvuvi (fungu 99) | Manunuzi ya magari na pikipiki ambazo hazikupokelwa | 302,670,681 |
| **JUMLA** | | **396,879,313** |

***Chanzo: Taarifa za ukaguzi za Mafungu husika kwa mwaka wa fedha 2014/2015.***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Mamlaka ya udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) ambayo ilitimiza wajibu wake ipasavyo kwa kuingilia kati na kuelekeza michakato ya zabuni mbalimbali kurudiwa upya baada ya kujiridhisha kuwa Serikali isingepata thamani ya fedha. Hivyo ni muhimu Taarifa za PPRA kama sehemu ya Taarifa ya CAG zikazingatiwa kwa kina na Serikali kwa kutekeleza Mapendekezo yanayokuwa yametolewa.

***Utekelezaji wa Maelekezo ya Bunge kuhusu Ufungaji wa Vifaa vya AFIS yaliyotolewa katika Mkutano wa tatu wa Bunge***

**Mheshimiwa Spika,** Mnamo tarehe 23 Aprili, 2016 Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) iliomba kuunda Kamati Ndogo kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (18) kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa Agizo la Kamati ya PAC (katika Bunge la 10) kwa Jeshi la Polisi lililotolewa tarehe 23 Oktoba, 2014 kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Kielektroniki wa Utambuzi wa Alama za Vidole *(Automated Fingerprints Identification System)*.

**Mheshimiwa Spika,** Agizo hilo lilijengwa katika Msingi wa hoja za ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika **fungu 28 - Jeshi la Polisi** kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Kilichohojiwa katika Agizo hilo ni kutokukamilika na kutofanya kazi ipasavyo kwa Mradi wa utambuzi wa alama za vidole (AFIS).

**Mheshimiwa Spika,** Kazi hiyo ilitokana na Mkataba uliokuwa umeingiwa kati ya Jeshi la Polisi (Mnunuzi) na Kampuni ya *Lugumi Enterprises Limited* (Mzabuni). Agizo la Bunge lilimtaka Afisa Masuuli wa Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba Mfumo wa AFIS unafanya kazi katika kipindi cha miezi sita kwa kusema yafuatayo: -

> **Nanukuu:**
> **"***Afisa Masuuli aliagizwa kuhakikisha kuwa mtambo wa AFIS (Automated Fingerprints Identification System) unafanya kazi ndani ya miezi sita***".** **Mwisho wa kunukuu**.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Kikao cha Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) cha tarehe 5 Aprili, 2016, kilichojadili Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za **fungu 28- Jeshi la Polisi** kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2014, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliripoti tena utekelezaji wa Agizo husika kwa Kamati. Maoni ya CAG yalionyesha kuwa, Mfumo wa AFIS unafanya kazi katika vituo 14 kati ya vituo mia moja na nane (108). Kwa maana hii, Agizo la Kamati halikuwa limetekelezwa kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na hali hiyo, Kamati ilimtaka Afisa Masuuli wa fungu 28 ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuleta kwa Kamati Taarifa ya utekelezaji wa Mradi wa AFIS. Taarifa iliwasilishwa tarehe 18 Aprili, 2016 ambapo ilibainika kuwa vifaa vya Mfumo wa AFIS vimefungwa katika vituo mia moja na hamsini na tatu (153) pamoja na Makao Makuu ya Polisi.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hiyo ilionyesha utofauti wa takwimu ikilinganishwa na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hivyo, Kamati iliazimia kumwomba Mheshimiwa Spika idhini ya kufanya Uhakiki wa Vifaa vya AFIS kama vipo katika vituo vya Polisi vilivyotajwa na Afisa Masuuli. Vilevile, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu sababu za kuchelewa kutekelezwa kwa Mradi husika.

Mheshimiwa Spika alielekeza kuundwa kwa Kamati Ndogo kwa Mujibu wa Kanuni ya 117 (18) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 ili iweze kufanya uhakiki kwa mujibu wa hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hivyo Kamati Ndogo ilipewa hadidu ya rejea moja kama ifuatavyo;

> ***"Kamati ifanye uhakiki iwapo vifaa vilinunuliwa na kufungwa"***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati Ndogo iliyoundwa ilizingatia hadidu hiyo ya rejea katika kukamilisha kazi ya uhakiki na kuwasilisha Taarifa yake PAC. Aidha, PAC iliipitia Taarifa hiyo kwa lengo la kufanikisha majukumu yake na kuikabidhi kwa Spika kama ilivyotakiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hiyo ilipokelewa na maudhui yake kuzingatiwa. Kwa mujibu wa Taarifa hiyo, Matokeo ya uhakiki yalithibitisha kwamba vifaa vipo ukiacha kasoro zilizojitokeza. Hivyo basi, Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (17) ya Kanuni za Bunge, Taarifa ya Kamati ya PAC ilikabidhiwa Serikalini kwa utekelezaji. Aidha, pamoja na Taarifa hiyo Maagizo yafuatayo yalitolewa: -

a) Serikali ihakikishe Mfumo huu unafanya kazi ndani ya miezi mitatu kuanzia [7]leo ili kuboresha uwezo wa Jeshi la Polisi kuwa na utambuzi wa haraka wa wahusika wa matukio ya kihalifu katika vituo vyote Nchini; na

b) Masuala yote yaliyobainika kuwa na dosari za kiutendaji yapatiwe ufumbuzi wa haraka.

***Aidha, PAC ilielekezwa kuhakiki utekelezaji wa Maagizo, na kutoa Taarifa ya utekelezaji wake Bungeni wakati ikiwasilisha Taarifa yake ya mwaka***.

**Mheshimiwa Spika,** Tarehe 28 Oktoba, 2016 Afisa Masuuli wa fungu 28, Jeshi la Polisi aliwasilisha Taarifa ya utekelezaji wa Agizo la Bunge. Baada ya kupokea Taarifa hiyo, Kamati ilichambua utekelezaji kwa kila Agizo lililotolewa na kubaini yafuatayo: -

**i. Agizo La Kwanza**

**Kuhakikisha Mfumo unafanya kazi ndani ya miezi mitatu**

**Mheshimiwa Spika,** Afisa Masuuli wa fungu 28 aliifahamisha Kamati kuwa, Baada ya kurekebisha kasoro zilizokuwa katika vituo mbalimbali na Kampuni ya Lugumi kukamilisha kufunga vifaa katika vituo ambavyo awali vilikuwa havijafungwa Mfumo ulianza kufanya kazi kwa vituo kuchukua, kuhifadhi na kutuma alama za vidole Makao Makuu ya Polisi. Hadi kufikia tarehe 21 Oktoba, 2016 vituo vyote 150 vina uwezo wa kuchukua na kuhifadhi alama za vidole. Kuhusu kutuma alama za vidole (kazi ya tatu) jumla ya vituo 83 kati ya vituo 150 (asilimia 55.33) vinaweza kutuma alama za vidole kama ifuatavyo: -

[7] Agizo lilitolewa mnamo tarehe 30 Juni, 2016 katika Mkutano wa tatu wa Bunge

(a) Vituo 17 vinatuma kwa kutumia Mkongo wa Taifa (TTCL).

(b) Vituo 66 vinatuma kwa kutumia modem.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Afisa Masuuli imebainisha kuwa, Vituo 67, pamoja na kwamba vina modem havijaweza kutuma kwa sababu zilizo nje ya uwezo wa Taasisi ambazo ni Ukosefu wa 3G network katika baadhi ya maeneo, kusitishwa kwa huduma za ADSL *(Asymmetric Digital Subscriber Line)* katika baadhi ya maeneo na Kumalizika kwa muda wa leseni za kuwezesha utendaji wa Mfumo wa AFIS.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa, Expert Work station (EWS) katika Ofisi za Wakuu wa Upelelezi wa Mikoa 32 hazijaanza kufanya kazi kwa sababu mafunzo ya Expert Work station Training course kwa wataalamu wa kuziendesha bado hayajatolewa.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya utekelezaji inafafanua kuwa, Wataalamu 52 waliofundishwa (Expert Work station - Coding) na *Lugumi Enterprise* hapo awali ni wale ambao wanafanya kazi ya kujenga kanzi data *(database)* Makao Makuu ya Polisi. Wanabadilisha alama za vidole kutoka kwenye makaratasi *(hard copy)* na kuzifanya kuwa katika Mfumo wa Kielektroniki *(Electronic fingerprint)*.

**ii. Agizo La Pili**

**Kufunga vifaa vya EWS katika Mikoa saba (7) na kufunga vifaa vya BWS katika vituo 28 ambavyo havijafungwa vifaa**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifahamishwa kuwa kati ya tarehe 14 Agosti hadi 19 Septemba, 2016 wataalamu wa Jeshi la Polisi na *Lugumi Enterprise Ltd* walitembelea Mikoa 32 ya kipolisi na kuhakikisha kuwa vifaa vya Expert Work Station (EWS) vimefungwa katika Ofisi zote 32 za Wakuu wa Upelelezi wa Mikoa (RCO) na vifaa vya Booking Work Station (BWS) vimefungwa katika vituo vyote 150.

**iii. Agizo La Tatu**

**iv.**

**Kufanya matengenezo ya vifaa vyote vilivyoharibika kabla ya kufanya kazi**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Afisa Masuuli wa fungu 28, imefafanua kuwa, Jeshi la Polisi na Kampuni ya Lugumi walipita kukagua na kutengeneza vifaa katika sehemu mbalimbali.

v. **Agizo La Nne**

**Kuviunganisha vituo vyote vya Polisi kwenye Mkongo wa Taifa**

**Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Polisi lina jumla ya vituo 417 hapa Nchini. Kati ya hivyo, vituo 150 ndivyo vyenye vifaa vya AFIS. Aidha, Taarifa ya utekelezaji imebainisha kuwa kuna Ofisi 32 za RCO zenye vifaa vya AFIS. Uunganishaji wa vituo na Ofisi za RCO zenye vifaa vya AFIS ni kama ifuatavyo umefanyika Ofisi ya Makao Makuu Ofisi za RCO 7 zilizokuwa zimebaki na Vituo 17 ambavyo vilikuwa havijaunganishwa na Mkongo wa Taifa na vinapata huduma ya mtandao wa internet ya uhakika.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi za RCO 7 zilizokuwa ambazo hazikuwa na huduma ya AFIS na Vituo 10 vimeunganishwa na Mkongo wa Taifa lakini havina huduma ya internet kwa sababu TTCL wanalidai Jeshi la Polisi jumla ya shilingi bilioni 2.1.

**vi. Agizo La Tano**

**Kuendesha mafunzo ya uendeshaji wa Mfumo wa AFIS kwa Askari watakaohusika na vifaa hivi katika vituo vyote vya Polisi Nchini.**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya utekelezaji katika Agizo la utoaji wa mafunzo kwa Askari imebainisha kuwa, mafunzo ya uendeshaji wa Mfumo wa AFIS yamefanyika katika Chuo cha Taaluma ya Polisi Dar es Salaam na Mikoani kati ya mwezi Julai hadi Septemba, 2016.Jumla ya Askari 388 kati ya 466 wamepatiwa Mafunzo. Askari waliobakia watapata mafunzo mwezi Disemba, 2016.

vii. **Agizo La Sita**

**Kuiingiza vifaa vya Mfumo wa AFIS katika Daftari la Mali za Jeshi la Polisi katika vituo vyote vya Polisi Wilayani.**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Afisa Masuuli kwa Kamati ilifafanua kuwa vifaa vya Mfumo wa AFIS vimeingizwa katika Daftari la Mali za Jeshi la Polisi katika vituo vyote vya Polisi Wilayani. Zoezi hilo lilikamilika tarehe 05 Septemba, 2016.

**viii. Agizo La Saba**

**Kuhakikisha kunakuwepo na Jenereta la dharula katika Makao Makuu ya Polisi ili Seva kuu ya Mfumo wa AFIS inafanya kazi zake ipasavyo.**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya utekelezaji kuhusu Mfumo wa AFIS imetanabaisha kuwa Jenereta la dharula lipo na linafanya kazi.

**ix. Agizo La Nane**

**x.**

**Kukarabati vyumba vyote vinavyotakiwa kutumika kwa ajili ya vifaa vya AFIS.**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza Agizo hili Jeshi la Polisi limeweza Kukarabati vyumba 27. Kwa vyumba ambavyo havijafanyiwa ukarabati utekelezaji wake utafanyika kwa kadri wanavyoendelea kupata mgao wa fedha toka Hazina. Kamati ilifahamishwa kuwa kunahitajika zaidi ya shilingi bilioni moja ili kukamilisha ukarabati wa vyumba husika.

**xi. Agizo La Tisa**

**Kuchukua hatua kali kwa wasimamizi na watekelezaji wa Mradi wa AFIS watakaobainika kushiriki kwa uzembe au kwa kutowajibika vilivyo hivyo kuchelewesha Mfumo wa AFIS kufanya kazi zake ilivyo.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefahamishwa kuwa, hadi hivi sasa kumekuwepo na hatua mbalimbali za kuchunguza utekelezaji wa Mradi huu wa AFIS. Uchunguzi huo ni ule uliofanywa na PPRA na ule unaoendelea kufanywa na TAKUKURU.Hatua dhidi ya wahusika zitachukuliwa baada ya uchunguzi huo kukamilika.

**Maoni ya Kamati Kuhusu utekelezaji wa maelekezo ya Bunge kuhusu ufungaji wa Vifaa vya AFIS yaliyotolewa katika Mkutano wa tatu wa Bunge.**

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kupokea Taarifa husika ya utekelezaji kutoka kwa Afisa Masuuli wa fungu 28, Kamati ina maoni na msimamo ufuatao: -

(a) Kamati haikupata fursa ya kwenda kufanya uhakiki wa utekelezaji wa Maagizo ya Bunge kwenye eneo la iwapo Vifaa vinafanya kazi kwa kuwa Taarifa ya utekelezaji ya Afisa Masuuli kuhusu Agizo la Bunge iliifikia Kamati tarehe 28 Oktoba, 2016 siku ambayo Kamati ilikuwa inakamilisha shughuli zake; na

(b) Kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 16 cha Nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 kinachobainisha kuwa msingi wa shughuli za Kamati ya PAC itakuwa ni Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hivyo, Kamati itafanya uhakiki wa Agizo la Bunge kwa kushirikiana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anayekagua fungu 28 katika shughuli zijazo za Kamati zitakazohusu Hesabu za mwaka 2015/2016 kwa kuwa hoja husika haijafungwa.

***Changamoto za uwekezaji unaolikabili Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)***

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), Kwa kuzingatia malengo ya awali ya Uanzishwaji wake linaweza kuwa injini muhimu katika kuijenga Tanzania kuwa Taifa lenye Viwanda na kuifanya kuwa Nchi yenye Uchumi wa kati hivi karibuni kwa kuishirikisha Sekta binafsi katika Miradi ya pamoja *(Private Public Partnership)*. NDC ilianzishwa mnamo mwaka 1962 ikiwa na [8]malengo makubwa ya kuchochea ukuaji wa Uchumi katika Sekta zote na majukumu hayo yamekuwa yakihuishwa mara kwa mara kuendana na mahitaji ya Nchi na Mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo Taarifa ya ukaguzi wa Hesabu za NDC kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2015 imebainisha hoja nyingi ambazo zinaifanya NDC kutotimiza wajibu wake ipasavyo hasa katika kuendeleza Uwekezaji katika Viwanda mama ambavyo vingeweza kuchochea ukuaji wa Uchumi kupitia utoaji wa ajira na kuongeza pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja za ukaguzi ambazo ndio changamoto zinazoikabili NDC hivyo kukwamisha shughuli zake ni kama ifuatavyo: -

**(a) Upembuzi yakinifu wa Miradi kufanywa na Wabia wenza wa NDC badala ya NDC wenyewe**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amebaini kuwa upembuzi yakinifu *(Techno-economic feasibility studies)* wa Miradi mikubwa minne (4) kati ya mitano (5) ambayo ilitakiwa kutekelezwa na NDC ulifanywa na Kampuni tanzu za NDC na sio NDC wenyewe hivyo NDC kutokuwa na Taarifa za kina kuhusu usahihi wa gharama za utekelezaji wa Miradi husika.

[8] An Act Of Parliament (1962) established Tanganyika Development Corporation (TDC)

Kamati imebaini kuwa inakuwa vigumu sana kwa NDC kutekeleza Miradi hiyo kwa sababu ya kutokuwa na Mfumo bora wa kusimamia na kutathmini *(Monitoring and evaluation)* usahihi wa gharama zinazokuwa zimetumiwa na Wabia wao wakati wa kufanya upembuzi yakinifu na gharama za kuendesha Mradi jambo ambalo limesababisha Miradi hiyo kutotekelezwa kwa wakati. Jambo hili ni kinyume na Kanuni ya 46(2) ya PPP za mwaka 2011 kama inavyonukuliwa hapa chini: -

***"…. The Contracting authority shall, in collaboration with the private party, prepare a monitoring and evaluation framework which shall be comprised of a Project Management Plan, Performance criteria, external audit and reporting requirements…"***

Mfano wa Miradi ambayo imekwama kutekelezwa kwa sababu ya changamoto za Upembuzi yakinifu unaofaa katika kuangalia gharama za Miradi na ugharamiaji wake ni pamoja na Mradi wa makaa ya mawe na chuma, Mchuchuma – Liganga, Mradi wa makaa ya Mawe Kusini - Ngaka, Mradi wa Makaa Maganga Matitu na Mradi wa uzalishaji wa Mawese kwa njia ya kisasa.

**(b) Changamoto za Bajeti zinazoikabili NDC**

Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kwa kipindi cha miaka minne (4) ya fedha iliyopita (2011- 2015) NDC imeendelea kukabiliwa na changamoto kubwa ya kifedha hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2015 NDC ilikuwa na limbikizo la ufinyu wa Bajeti *(Budget deficit)* uliofikia Shilingi bilioni 109.5 Hali ya kibajeti ya NDC ni kama inavyoonekana katika Jedwali lifuatalo: -

**Jedwali Namba 7.**
**Mwenendo wa Kibajeti wa NDC 2011 – 2015**

| MWAKA | BAJETI ILIYOTAKIWA | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | BAJETI ILIYOTOLEWA | UPUNGUFU WA BAJETI |
|---|---|---|---|---|
| 2011/12 | 33,758,000,000 | 7,063,835,401 | 2,900,000,000 | 30,858,000,000 |
| 2012/13 | 28,967,000,000 | 7,960,000,000 | 6,738,373,750 | 22,228,626,250 |
| 2013/14 | 49,141,800,000 | 19,900,000,000 | 13,128,180,000 | 36,013,620,000 |
| 2014/15 | 24,253,000,000 | 8,896,000,000 | 3,890,000,000 | 20,363,000,000 |
| Jumla | | | | 109,463,246,250 |

***Chanzo: Uchambuzi wa Kamati kwenye Taarifa ya CAG kuhusu ukaguzi wa NDC.***

Kama ilivyofafanuliwa katika jedwali hapo juu, Bajeti inayoidhinishwa na ile inayotolewa hazilingani. Ni kwa msingi huo wa ufinyu wa Bajeti, Kamati imebaini kuwa katika Miradi mingi iliyopangwa kutekelezwa kwa ubia, Serikali kupitia NDC anachangia mtajikupitia kutoa rasilimali zilizopo kwa ajili ya uchimbaji mathalani Makaa ya mawe na sio fedha za Uwekezaji. Ukosefu wa fedha za Uwekezaji unasababisha NDC katika maeneo mengi ya Miradi kuwa mmiliki wa hisa chache *(Minority shareholder)* jambo ambalo linaweza kuwa na athari hapo baadae katika umiliki na ugawanaji wa mapato ya Miradi husika.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya Kamati ni kuwa, NDC ikiwezeshwa ipasavyo katika Uwekezaji wa Viwanda na kuwa na Menejimenti yenye ubunifu wa kutosha itasaidia kuinua Uchumi, ni suala la muhimu kwa Serikali kuangalia upya utendaji na Uwekezaji wa NDC *(Financing investment)*.

**(c) Uwepo wa Miradi ya muda mrefu ambayo hadi sasa haijaanza kutekelezwa**

Katika uchambuzi wa Taarifa ya Hesabu za NDC, Kamati imeweza kubaini uwepo wa Miradi mingi ambayo hadi sasa haijaanza kutekelezwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na ucheleweshaji wa maamuzi toka Serikalini,

Kutelekezwa kwa mashamba ya mpira, kutokuwepo kwa mtaji na mashauriano yanayochukua muda mrefu kukamilika kati ya Shirika na Wabia wenza wa kwenye Miradi.

Kutokuanza utekelezaji wa Miradi hiyo kwa wakati kunaiingizia Serikali hasara ya kuendelea kulipa gharama za uendeshaji wa Shirika bila kuwa na Ufanisi. Mfano wa Miradi ambayo haijaanza kutekelezwa na NDC na ni ya muda mrefu ni kama ifuatavyo: -

i. Mradi wa Kiwanda cha Matairi cha General Tyre, Arusha ambao hadi sasa zimetumika shilingi 380,666,820 kwa ukarabati wa majengo na shilingi 662,936,482 kwa ajili ya vifaa vya Umeme;

ii. Mashamba ya mpira ya Kalunga, Morogoro na shamba la mpira la Kihuhwi lililopo Muheza;

iii. Mradi wa uzalishaji wa mawese *(Intergrated Oil Palm Project)*;

iv. Mradi wa utengenezaji wa Kiwanda cha kutengeneza dawa na viatilifu vya kuzuia Malaria, Kibaha;

v. Kilimanjaro Tools Company (KMTC), kwa mwaka husika wa fedha shilingi 187,544,480 zilitumika kwa ukarabati ila Kiwanda hakijaanza kupata faida;

vi. Mradi wa Mchuchuma na Liganga, Ludewa; na

vii. Mradi wa Makaa ya Mawe Ngaka, Mbinga.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya Kamati ni kuwa, ni Muhimu Miradi hiyo ikaanza kutekelezwa kwa kasi kama ilivyopendekezwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ili fedha za Umma zilizowekezwa katika NDC ziwe na thamani halisi ya matumizi yanayofaa ya fedha za Umma *(Value for money)*.

***Usimamizi wa mali* (Asset management) *katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)***

**Mheshimiwa Spika**, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (PPF, PSPF, LAPF, NSSF na NHIF) kwa pamoja hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2015 walitumia jumla ya shilingi bilioni 415.4 kwa ajili ya ujenzi wa Majengo ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), kwa kuzingatia Mkataba wenye masharti ya usanifu, ujenzi, miliki na kuhamisha miliki baada ya miaka kumi (10), *(Design, build, own and transfer)*.

**Mheshimiwa Spika,** Dosari mojawapo iliyobainika na Kamati kuhusu ujenzi wa Majengo hayo ni usimamizi usiofaa wa mali husika. Hadi hivi sasa tunapowasilisha Taarifa hii ya Kamati katika Bunge lako Tukufu, thamani halisi ya Majengo hayo haijaingizwa katika vitabu vya Hesabu za Chuo Kikuu Dodoma kinyume na Mapendekezo yaliyotolewa na CAG kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) ili yatekelezwe na Uongozi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kwa kuzingatia matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya ukaguzi wa Hesabu [9](IFRS) vinavyohitaji thamani ya Majengo hayo itambuliwe katika Vitabu vya Chuo na kuchajiwa uchakavu *(Depreciation)*.

**Mheshimiwa Spika,** Athari ya kutotambua na kutoingiza thamani halisi ya Majengo hayo ya Chuo Kikuu Dodoma katika vitabu vya Hesabu za Chuo ni pamoja na kusababisha Hesabu za Chuo kutotoa taswira halisi *(True*

[9] International Audit Standard (IAS) namba 16 inayotoa Mwongozo wa kihasibu wa Kushughulikia Mali za majengo, Mitambo na Vifaa kwa kuangalia thamani na uchakavu wake katika Hesabu kila kipindi cha Ukaguzi

*and fair view)* ya mali zake kinyume na matakwa ya Viwango vya kimataifa vya ukaguzi wa Hesabu (IFRS) na pia kuwa na athari katika Mkataba ulioingiwa kati ya Serikali na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

***Malimbikizo ya Mikopo isiyorejeshwa* (Non performing loans) *katika Benki ya Maendeleo ya TIB***

**Mheshimiwa Spika,** Benki ya Maendeleo ya TIB ilianzishwa kama Taasisi ya fedha ya Maendeleo *(Development Finance Institution)* kwa mujibu wa Sheria ya Bunge iliyopitishwa mwezi Novemba mwaka 1970.Kumekuwa kukifanyika marekebisho kadhaa ya kiutendaji na Mfumo ili Benki hiyo iweze kutimiza majukumu yake ya utoaji Mikopo kugharimia shughuli maalum za Uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa za ukaguzi za Benki ya Maendeleo ya TIB umebaini kuwa kuna changamoto kubwa za urejeshaji wa Mikopo inayotolewa na Benki hiyo na pia kuna dosari za uhakiki wa Miradi inayogharimiwa na Benki hiyo. Mapungufu ya urejeshaji wa Mikopo katika Benki ya Maendeleo ya TIB ni kama inavyofafanuliwa ifuatavyo: -

a) **Urejeshaji Usioridhisha wa mkopo wa Kilimo uliotolewa kwa Kiwanda cha SAAFI**

**Mheshimiwa Spika,** Benki ya Maendeleo ya TIB ilipewa jukumu la kuendesha shughuli za kifedha na masuala ya kiutendaji katika Kiwanda cha SAAFI ili kuwezesha Ulipaji wa Mikopo ya awali iliyotolewa na Serikali. Mkopo wa awali uliotolewa kwa SAAFI na Benki ya Standard Chartered kwa dhamana ya Serikali ulikuwa wa kiasi cha shilingi bilioni 10.097.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Benki ya TIB ilitoa Mkopo wa shilingi bilioni 2.5 kwa mara ya kwanza kwa SAAFI hata hivyo hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2014 hakuna fedha iliyolipwa. Benki iliamua kugeuza Mkopo kuwa hisa baada ya kuona utendaji wa SAAFI hauridhishi. Aidha, Serikali iliongeza Mkopo wa shilingi bilioni 4.852 kwa ajili ya kununua mitambo ya kusindikia mabaki na uzalishaji wa nyama katika Kiwanda hicho. Hivyo jumla ya mkopo uliotolewa na Serikali kwa SAAFI ni shilingi bilioni 14.95 na ule uliotolewa na Benki ya TIB ni shilingi bilioni 2.5.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya Kamati ni kuwa, Kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo kutofanyika kwa uthamini *(Valuation)* ya mali za Kiwanda ili kufahamu mtaji uliowekwa na

wamiliki wa Kiwanda, masoko hafifu ya bidhaa za Kiwanda, hadi sasa Kiwanda cha SAAFI kimeshindwa kujiendesha kibiashara kwa faida na hadi sasa Mikopo yote iliyochukuliwa haijaweza kurejeshwa jambo ambalo lina athari kwa Ufanisi wa Benki ya TIB.

**b) Mikopo iliyotolewa kupitia Mfuko wa usafirishaji Nje (ECGS)**

**Mheshimiwa Spika,** Kupitia Mfuko wa usafirishaji Nje (ECGS), TIB iliteuliwa na Serikali kupitia Wizara ya fedha na Benki Kuu kusimamia Mikopo ya shughuli za Kilimo cha maua Mkoani Arusha. Malengo ya Serikali ilikuwa ni kuongeza uzalishaji wa maua ili kuvutia Ndege za mizigo kuja Tanzania na kuongeza fedha za Kigeni kwa Taifa. Mikopo ilitolewa kwa Kampuni sita (6) kati ya mwaka 2003 na 2009 kama ifuatavyo: -

i. Kilifrola Limited shilingi bilioni 13.9;
ii. Tanzania flowers shilingi bilioni 11;
iii. Arusha blooms shilingi bilioni 10.1;
iv. Tengeru flowers shilingi bilioni 7.5;
v. Hortanzia limited shilingi bilioni 3.84; na
vi. Mount Meru flowers shilingi bilioni 4.4.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa urejeshaji wa madeni hayo kupitia Benki ya Maendeleo ya TIB sio wa kuridhisha hivyo ni maoni ya Kamati kuwa Menejimenti ya TIB inatakiwa kuimarisha usimamizi wa utaratibu wa utoaji wa Mikopo na ukusanyaji wa madeni ili kuhakikisha malengo ya Serikali ya kukuza Kilimo yanafikiwa.

**c) Madeni ya muda mrefu ya Kilimo kwanza *(Agricultural financing window)***

**Mheshimiwa Spika,** Mikopo ya Kilimo kwanza, ilitolewa na Benki katika Makundi matatu (3) ambayo ni SACCOS, Wakulima wadogo na wa kati (SMEs) na Taasisi ndogo za fedha *(Microfinance Institution)* zinazotoa Mikopo kwa Wakulima. Uchambuzi wa Kamati umebaini katika Makundi hayo matatu (3) Mikopo mingi isiyorejeshwa au Mikopo chechefu *(Non performing loans)* inatoka kundi la SACCOS.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2014 wadaiwa wa dirisha la Kilimo walikuwa wanadaiwa kiasi cha shilingi bilioni 34, kati ya hiyo, kiasi cha shilingi bilioni 11.3 kilikuwa kimepitiliza muda wa kulipa na kiasi cha shilingi bilioni 7.5 ilikuwa ni sehemu ya deni la SACCOS ambalo lilipitiliza muda wa kulipa (Kuwa na zaidi ya mwaka mmoja).

**d) Uwepo wa Mikopo chechefu *(Non performing loans)* ya kiasi cha shilingi bilioni 78**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati uliweza kubaini uwepo wa Mikopo chechefu na Mikopo isiyorejeshwa ya muda mrefu ya zaidi ya shilingi bilioni 78 katika Benki ya Maendeleo ya TIB. Mikopo hiyo ilikuwa imetolewa kwa Kampuni mbalimbali kugharimia Miradi ya Kilimo, Viwanda, Ujenzi na Usafirishaji.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya Kamati ni kuwa, kutorejeshwa kwa Mikopo hiyo ni hasara kubwa kwa Benki na kumetokana na kukiukwa kwa taratibu za Kibenki ambapo Mikopo mingi ilitolewa kwa Kampuni ambazo hazikustahili na ambazo zimekiuka taratibu za Mikopo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi yako imeiandikia barua Benki ya TIB kwa kuzingatia Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, sura ya 266 kuwasilisha orodha ya wadaiwa sugu mapema iwezekanavyo. Aidha, Kamati inashauri Bodi mpya ya Benki ya TIB ikamilishe uchunguzi unaoendelea ili kubaini dosari katika utoaji wa Mikopo hiyo na kuchukua hatua stahiki.

***Kutokamilika kwa Mradi wa uhamiaji mtandao* (E – Immigration) *katika fungu 93, Idara ya Uhamiaji***

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 15 cha Sheria ya Uhamiaji kinaweka masharti kuhusiana na utaratibu wa Wageni kuingia na kutoka hapa Nchini. Ili kutekeleza jambo hilo kwa ufanisi, Idara ya Uhamiaji imeweka Mfumo wa usimamizi wa Viza katika Makao Makuu ya Idara, kwenye Balozi na kwenye Mipaka ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na uwepo wa Mfumo huo Taarifa ya ukaguzi imebaini kuwa Mfumo uliopo katika Balozi na ule wa kutoa Viza kwa wageni wanaowasili *(Visa on arrival)* na Makao makuu havina mawasiliano *(Not Intergrated)* hivyo kutoa mwanya wa upotevu wa mapato ya Serikali yanayotakiwa kukusanywa kutokana na utoaji wa Viza. Hoja ya Kamati katika jambo hili ni kuishauri Serikali kukamilisha kwa haraka Mradi wa Uhamiaji mtandao *(E – Immigration)* ili kuhakikisha mapato ya Serikali yanakusanywa ipasavyo.

***Kutokamilika kwa muamala wa shilingi 100,525,437,562.51 katika fungu 56 Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI)***

**Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi wa Taarifa ya fungu 56 (Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI) ilibaini kuwa muamala wa shilingi 100,525,437,562.51 haukukamilika kwa sababu shughuli zilizokuwa zimepangwa kugharamiwa na fedha hizo hazikufanyika kwa sababu fedha hazikutolewa japokuwa zilikuwa zimepitishwa katika Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2014/2015.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa fedha hizo zilitakiwa kulipwa katika Makundi 8 kama ifuatavyo: -

(a) Wazabuni na Watoa huduma, shilingi 3,304,748,786.56;
(b) Kamishina wa mapato ya ndani, shilingi 75,257,155.57;
(c) PS PMORALG, shilingi 5,962,615,088;
(d) Mfuko wa barabara, shilingi 57,491,000,000,000;
(e) Hazina Dodoma, shilingi 27,406,066,930;
(f) NMB – Dodoma, shilingi 5,631,589,722;
(g) Mradi wa ULGSP, shilingi 475,065,202; na
(h) Madai ya wafanyakazi 179,094,676.25.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya Kamati katika suala hili ni kuwa, Hazina waliamua kuchukua fedha hizo bila kutoa maelezo kwa TAMISEMI hivyo kukwamisha shughuli zilizopangwa kutekelezwa. Aidha, kwa upande mwingine mwenendo mzima wa muamala huo una dosari hasa baada ya kubaini baadaye Hazina walitoa shilingi bilioni 10 kwenda TAMISEMI na kuelekeza fedha zilizobaki ziingizwe kwenye madeni ya Wizara. Hivyo ni muhimu Serikali kupitia Hazina ikatoa kwa Bunge maelezo ya kutosha kuhusiana na jambo hilo.

### *Changamoto katika uandaaji wa Taarifa za Hesabu kwa kuzingatia Mfumo wa* "IPSAS Accrual Basis"

**Mheshimiwa Spika,** Mnamo tarehe 01 Julai, 2012 Serikali Kuu na Taasisi zake zilianza rasmi kutumia Mfumo wa uandaaji wa Hesabu unaofahamika kama ***"Ipsas Accrual Basis"***. Malengo ya kutumia Mfumo huo ilikuwa ni kuhakikisha Taarifa za Hesabu za Serikali zinatoa taswira halisi ya mali, madeni na Taarifa nyinginezo muhimu ili Kuwepo na udhibiti unaofaa wa Hesabu na masuala mengine yanayohusu Taasisi za Serikali. Taarifa za Hesabu za Taasisi za Serikali Kuu zilizoandaliwa kwa kuzingatia Mfumo huo, zilitolewa kwa mara ya kwanza kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2013.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kutekeleza Mfumo huo ipasavyo, Serikali ilijiwekea kipindi cha mpito cha miaka mitano (5) kitakachomalizika mwezi Machi,

2017 ili kuhakikisha Dosari zote za uandaaji wa Hesabu zinarekebishwa na Mfumo ufanye kazi zake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo katika Taasisi nyingi za Serikali Kuu zikiwamo Sekretarieti za Mikoa ya Kagera, Pwani, Iringa, Simiyu, Dodoma na Morogoro pamoja na Wizara za Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Nishati na Madini, fungu 22 Deni la Taifa na Hesabu Jumuifu za Taifa *(Consolidated Accounts)* zote zilikuwa na changamoto ya kushindwa kutekeleza Mfumo wa IPSAS kwa Ufanisi. Dosari zilizobainika katika utekelezaji wa Mfumo huo ni kama ifuatavyo: -

(a) Baadhi ya Watumishi wa Idara na Vitengo vya Uhasibu kutopatiwa Mafunzo kuhusiana na Mfumo husika hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo;

(b) Daftari za mali za kudumu kutohuishwa ili liendane na wakati na kutoa hali halisi ya mali za Serikali kama ardhi, majengo na magari *(Update of the fixed asset register)*;

(c) Kutofanyiwa uthamini *(Valuation)* ya mali za kudumu za Serikali, changamoto kubwa ikiwa ni kwenye eneo la ardhi Kutofanyiwa uthamini na kupata Hati;

(d) Kutohifadhi Kumbukumbu sahihi za madeni na wadaiwa wa Serikali *(Poor debtors and creditors records management)*.; Kutokuwepo kwa Sera ya utunzaji wa mali za Serikali *(Lack of asset accounting policy)*, bila ya kuwepo na sera husika inasababisha kuchukua muda mrefu kuandaa Taarifa ya Hesabu Jumuifu za Taasisi zikihusisha mali; na

(e) Kutotenganisha ardhi na majengo katika Taarifa za Hesabu kinyume na matakwa ya [10]Kifungu cha 17 (74) cha IPSAS.

**Jedwali Namba 8.**

**Baadhi ya Mafungu ambayo hayakutenganisha ardhi na majengo katika Taarifa ya Hesabu kwa mwaka wa fedha 2015**

| FUNGU | JINA LA FUNGU |
|---|---|
| 14 | Jeshi la Zimamoto na Uokoaji |

[10] IPSAS 17 (74), Directs that, Land and Buildings are separable assets and are accounted for separately, even when they are acquired together.

| | |
|---|---|
| 47 | Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu |
| 51 | Wizara ya Mambo ya Ndani |
| 88 | Sekretarieti ya Mkoa wa Dar es Salaam |
| 2020 (fungu dogo) | Ubalozi wa Kudumu wa Tanzania, Geneva |
| 2033(fungu dogo) | Ubalozi wa Tanzania, Hague |
| 2014(fungu dogo) | Ubalozi wa Tanzania, China |

***Chanzo: Uchambuzi wa Kamati, 2016.***

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto zilizoainishwa hapo juu zimesababisha katika Sekretarieti nyingi za Mikoa, Wakala za Serikali na Wizara kuwa na madeni ambayo hayana maelezo ya kutosha wala uthibitisho jambo ambalo linachangia kuonekana Serikali inadaiwa wakati kiuhalisia madeni hayo yanaweza kuwa yanatengenezwa kwa makusudi ili kupoteza fedha za Umma kwa njia za udanganyifu.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya Kamati ni kuwa, Kutokana na dosari tajwa hapo juu na kwa kuzingatia kuwa kipindi cha mpito kinamalizika mapema mwezi Machi 2017, ni dhahiri Serikali inatakiwa kufanya kazi kubwa na ya ziada kuhakikisha Mfumo wa "*Ipsas Accrual Basis*" unatekelezwa kikamilifu ili kufikia malengo ya udhibiti wa fedha na mali za Serikali kwa ukamilifu.

***Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi(NAOT)***

**Mheshimiwa Spika,** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amepewa Mamlaka kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa pamoja na Kifungu cha 5(c) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 kuwa ndiye Mkaguzi wa mapato na matumizi yote ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia majukumu hayo ya Kikatiba na kisheria yaliyokabidhwa kwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, ni dhahiri Ofisi hiyo ni muhimu katika kusimamia matumizi ya fedha za Serikali na kusimika misingi ya uwajibikaji katika fedha za Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kifungu cha 16 cha Nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 msingi wa majukumu ya

shughuli za Kamati ya PAC unatokana na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Uwepo wa bajeti ya kutosha kwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi husaidia Ofisi hiyo kufanya ukaguzi kwa ufanisi, kuongeza mawanda ya kaguzi, kuandaa Taarifa za kaguzi zenye ubora na pia kuwezesha Wakaguzi kuhudhuria Vikao vya Kamati kwa muda mwafaka. Hata hivyo, kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita hali ya kibajeti kwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi haikuwa ya kuridhisha sana jambo ambalo linaweza kuathiri shughuli za ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** Mwenendo wa kibajeti wa Ofisi ya CAG unabainisha kuwa kwa mwaka 2014/2015 bajeti iliyoidhinishwa ilikuwa shilingi 55,563,651,850 na fedha iliyotolewa ilikuwa shilingi 33,599,315,000 na kwa mwaka wa fedha 2015/2016 fedha iliyoidhinishwa ilikuwa shilingi 57,942,949,000 wakati fedha iliyotolewa ilikuwa shilingi 30,712,096,383.

**Mheshimiwa Spika,** Mwenendo wa utoaji wa bajeti ya Ofisi ya Taifa ya ukaguzi (NAOT), sio wa kuridhisha. Hoja ya Kamati ni kuwa, juhudi za Serikali katika kuimarisha uwajibikaji haziwezi kufanikiwa ikiwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi haitapewa fedha za kutosha. Kupeleka fedha za Maendeleo bila kukagua matumizi yake itakuwa ni changamoto kubwa kiuwajibikaji na katika kupata Matokeo chanya.

***Masuala mengine ya Msisitizo***

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuhitimisha Taarifa hii kwa kufafanua baadhi ya masuala ya msisitizo ambayo yanahusiana na matumizi ya fedha za Umma na Kamati ingependa Serikali iyafanyie kazi: -

**(a) Ucheleweshaji wa fedha kukamilisha Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** Katika eneo hili Kamati iliweza kubaini kuwa Kumekuwa na ucheleweshaji wa fedha za kugharimia Miradi ya Maendeleo hali iliyosababisha baadhiya Miradi kutokamilika kwa wakati. Miongoni mwa Miradi ya namna hiyo na kiasi cha fedha kilichotumika ni kama ifuatavyo: -

i. Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Dodoma ambao hadi sasa haujakamilika;

ii. Ujenzi wa gati *(ramp)* Mkoani Kagera unaotekelezwa na Sekretarieti ya Mkoa (Fungu 87) ambao hadi sasa umegharimu shilingi 752,674,415. Mradi haujakamilika hadi sasa kwa kukosa fedha; na

iii. Katika fungu 87, RAS Kagera, Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ambao umegharimu shilingi 1,281,921,980.50 na Mkataba umevunjwa kwa kukosa fedha za kuendelea na Mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya Kamati kuhusu Miradi ya aina hiyo ni ongezeko la gharama kutokana na kutokamilika Miradi kwa wakati na pia kuiletea hasara Serikali hasa pale Mikataba inapovunjwa kwa kukosa fedha.

**(b) Uimarishaji wa Mifumo ya Udhibiti wa ndani na Mifumo ya ICT, katika TPA, TRA, NSSF, HESLB na PPF**

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto ya Mifumo ya udhibiti wa ndani *(Internal controls)* na Mifumo ya mawasiliano (ICT) imebainika kuwa changamoto kubwa katika udhibiti wa mapato ya Serikali katika Taasisi nyingi zinazohusika na ukusanyaji wa mapato ya Serikali kama vile TPA, TRA na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

**Mheshimiwa Spika,** Dosari katika Mifumo hiyo ndiyo imekuwa ikitumiwa na baadhi ya Watu wasiokuwa waaminifu kuwezesha upotevu wa mapato ya Serikali. Aidha, katika baadhi ya Taasisi Mifumo imekuwa ikinunuliwa kwa gharama kubwa lakini haifanyi kazi kama ilivyotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya Kamati katika jambo hili ni kuishauri Serikali kuimarisha Mifumo ya udhibiti wa ndani na kuhakikisha Mifumo ya ICT inayonunuliwa na kusimikwa kwa shughuli mbalimbali za uendeshaji wa Taasisi inakuwa na ufanisi unaotakiwa baada ya kuwa kumefanyika upembuzi yakinifu wa mahitaji.

**(c) Tume ya Taifa ya Uchaguzi**

**Mheshimiwa Spika,** Hoja kubwa ya ukaguzi kuhusu Tume ya Taifa ya Uchaguzi, fungu 61 inahusu uanzishwaji wa Mfuko maalum wa uchaguzi *(Election fund)* ili kuhakikisha shughuli mbalimbali za uchaguzi zinagharimiwa ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya Kamati imejengwa katika msingi wa kuhakikisha Serikali inatenga fedha kiasi katika kila mwaka wa fedha kuingiza katika Mfuko huo wa uchaguzi badala ya kuelekeza rasilimali nyingi kwa Tume ya uchaguzi mara moja wakati wa kipindi cha uchaguzi

## SEHEMU YA TATU
## MAONI NA MAPENDEKEZO

**Maelezo ya jumla**

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa Hesabu kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2015, Kamati inatoa maoni na Mapendekezo kama ifuatavyo: -

**Maoni (*Opinion*)**

**Mheshimiwa Spika**, Maoni ya Kamati yanazingatia azma ya Bunge kuwa na Kamati mahsusi inayohusika na usimamizi wa matumizi ya fedha za Umma. Msingi wa maoni hayo ni nia ya kuepusha matumizi mabaya ya fedha za Umma katika Serikali Kuu na Mashirika ya Umma. Kwa mantiki hiyo, Kamati ina maoni yafuatayo: -

(a) Bunge kama chombo cha juu kabisa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kwa kupitia Kamati zake ziendelee kutekeleza wajibu wake kwa weledi katika kuhakikisha matumizi yanayofaa ya fedha za Umma katika Wizara, Idara, Wakala na Mashirika ya Umma;

(b) Bunge liendelee kutenga Bajeti ya kutosha ili kuisaidia Kamati pamoja na mambo mengine kupata muda wa kutosha kufanya mahojiano na Maafisa Masuuli lakini pia kupata nafasi ya kufanya Ziara za ukaguzi wa kibunge *(Oversight visits)* katika Miradi mbalimbali ya Maendeleo ili kujiridhisha na thamani halisi ya fedha iliyotumika katika Miradi hiyo *(Value for money)*; na

(c) Mwisho, Serikali inashauriwa kuzingatia kwa umakini uchambuzi uliofanywa na Kamati kuhusu maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za Umma na kutekeleza Mapendekezo na Maazimio ya Bunge yanayotokana na Taarifa hii ili kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za Umma.

**Mapendekezo (*Recommendations*)**

**Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Kamati yameandaliwa kwa kuzingatia Matokeo ya uchambuzi wa maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi yasiyofaa ya fedha za Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatia hali halisi ya athari ya hoja husika za ukaguzi *(Risk level of the particular audit query)*. Hivyo Mapendekezo haya yamelenga katika hoja zenye athari ya juu *(High risk)* na athari ya kati *(Medium risk)* ya matumizi ya fedha za Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imetoa Mapendekezo katika Makundi mawili, kundi la kwanza ni Mapendekezo ya Muda mfupi ambayo utekelezaji wake unatakiwa kuwa ndani ya kipindi cha mwezi mmoja hadi mwaka mmoja. Kundi la pili ni Mapendekezo ya muda wa kati ambayo muda wa utekelezaji wake unategemewa kuwa kuanzia mwaka mmoja hadi miaka miwili hasa yale yanayohitaji bajeti kubwa, uundaji wa Sera na utungaji wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Kamati ni kama ifuatavyo: -

***Madeni ambayo Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inaidai Serikali***

**KWA KUWA,** Serikali na Taasisi zake kwa nyakati tofauti zimekuwa zikitekeleza shughuli mbalimbali za Maendeleo kwa kuchukua Mikopo kutoka katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;

**NA KWA KUWA,** Urejeshaji wa fedha katika Mifuko ya Hifadhi za Jamii sio wa kuridhisha hali ambayo ikiachwa hivyo itakuwa na athari kwa utendaji wa Mifuko kwa siku zijazo;

**KWA HIYO BASI,** Bunge liazimie kwamba: -

**Pendekezo la muda mfupi**

a) Serikali iwasilishe Mpango mahsusi Bungeni wa utaratibu utakaotumika kulipa Mikopo na michango inayodaiwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii; na

b) Serikali iwe inawasilisha Taarifa Bungeni kwa kila robo ya mwaka wa fedha kuhusu hali ya urejeshaji wa Mikopo na michango husika.

***Rufaa za mashauri ya kodi, kodi zinazobishaniwa* (Tax appeals and objection) *na Misamaha ya kodi***

**KWA KUWA,** Imebainika kuwa Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA) inashindwa kukusanya baadhi ya kodi stahiki kwa sababu ya rufaa za mashauri ya kodi na kodikubishaniwa katika ngazi mbalimbali *(Tax appeals and tax objection)*;

**NA KWA KUWA,** Kumekuwa na ongezeko kubwa la rufaa za kesi na kodi zinazobishaniwa ambazo zinaathiri ukusanyaji wa mapato ya Serikali;

**KWA HIYO BASI,** Bunge liazimie kwamba: -

**Pendekezo la muda mfupi**

a) Serikali itoe fedha na Bajeti ya kutosha kwa Bodi ya rufaa za kodi ili iweze kushughulikia mashauri ya kesi za kodi kwa haraka na kutoa uamuzi;

b) Serikali kupitia TRA ishirikiane kwa karibu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wizara ya fedha kwa kutumia Mawakili wenye weledi na uzalendo kutafuta ufumbuzi wa kesi zilizopo Mahakamani ili kuhakikisha kodi stahiki inakusanywa; na

c) Serikali isimamie kwa ukamilifu Sheria za kodi ikiwa ni pamoja na kutumia njia za Kielektroniki kusimamia kwa ukamilifu na kudhibiti matumizi yasiyofaa ya Misamaha ya kodi.

***Hali ya kifedha ya Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma (PSPF)***

**KWA KUWA,** Hali ya kifedha ya Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma(PSPF) sio ya kuridhisha kutokana na madeni na michango ambayo Mfuko unaidai Serikali;

**NA KWA KUWA,** Hali hiyo ya kifedha inaathiri uwezo wa Mfuko kutimiza majukumu yake ipasavyo ya kulipa Pensheni kwa Wanachama wake;

**KWA HIYO BASI,** Bunge liazimie kwamba: - **Pendekezo la muda wa kati**

(a) Serikali itimize ahadi na malengo yake ya kibajeti kwa kuhakikisha inalipa shilingi bilioni 150 zilizotengwa mwaka huu wa fedha kulipa deni la PSPF;

(b) Serikali itoe Hati fungani *(Non cash bond)* ya shilingi trilioni 2.9 ili kuanza kulipa deni la Mfuko kwa Wastaafu wa kabla ya tarehe 01 Julai, 1999 kabla ya mwezi Februari, 2017 kama iliyokubaliwa mbele ya Kamati;

(c) Serikali isimamie kwa karibu na kuzihimiza Taasisi zake zinazodaiwa na PSPF kiasi cha shilingi bilioni 382.9 kulipa madeni hayo mara moja;

(d) Serikali iendelee kutenga fedha kwenye Bajeti ya kila mwaka ili kuongeza mtaji wa PSPF kwa sababu nakisi iliyopo ni kubwa hata kama madeni yote yatalipwa; na

(e) PSPF isipewe maelekezo mapya ya kutekeleza Miradi au kuikopesha Serikali katika kipindi hiki cha mpito.

***Kuhusu Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake***

**KWA KUWA**, Taarifa ya ukaguzi wa Manunuzi ya Umma iliyotolewa na Mamlaka ya udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) kwa mwaka wa fedha 2014/15 imebainisha kuwa Taasisi za Umma ishirini na mbili (22) zilifanya manunuzi bila kukidhi Sheria ya Manunuzi ya Umma, Mikataba kumi na tano (15) haikuwa na thamani halisi ya fedha, Mikataba tisa (9) ilikuwa na viashiria vya rushwa na malipo yenye utata ya shilingi 3,253,650,189;

**NA KWA KUWA,** Mapungufu yote tajwa hapo juu yanasababisha fedha za Serikali kupotea na ni kinyume na matakwa ya Sheria ya Manunuzi ya Umma Namba 7 ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013;

**KWA HIYO BASI,** Bunge liazimie kwamba: - **Pendekezo la muda mfupi**

(a) Serikali iendelee kusimamia kwa ukamilifu Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma katika Taasisi zake na kuchukua hatua pale Sheria inapokiukwa;

(b) PPRA itumie masharti ya Kifungu cha 57 cha Gazeti la Serikali namba 58 kuzifungia *(Blacklist)*, Kampuni, Wazabuni, Watoa Huduma au Wafanyabiashara watakaothibitika kutumia rushwa katika kushawishi zabuni katika Manunuzi ya Umma; na

(c) Kuandaliwe utaratibu maalum wa Kikanuni ili kuhakikisha Taarifa ya ukaguzi inayoandaliwa na Mamlaka ya udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) iwe inafanyiwa kazi na Kamati ya PAC na kisha kuwasilishwa Bungeni.

***Hasara ya shilingi 6,793,310,000 iliyotokana na kuharibika Tani 13,583 za Mahindi***

**KWA KUWA,** Kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2015 Serikali kupitia kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya chakula (NFRA) na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ilipata hasara ya shilingi 6,793,310,000;

**NA KWA KUWA,** Hasara hiyo ilitokana na kuharibika kwa tani 13,583 za mahindi yaliyokuwa yamehifadhiwa katika maghala ya Serikali hivyo kutofaa tena kwa chakula;

**KWA HIYO BASI,** Bunge liazimie kwamba:-

(a) Serikali itengeneze utaratibu maalum wa kuwa inafanya tathmini ya mara kwa mara ya uwezo wa Nchi kuzalisha chakula, uwezo wa **Pendekezo la muda**

NFRA kununua na kuhifadhi chakula na mahitaji halisi ya chakula; na

(b) Serikali iongeze nguvu katika ukarabati na Ujenzi wa maghala mapya na ya kisasa zaidi ya kuhifadhi nafaka ikiwa ni pamoja na kuiongezea uwezo wa kifedha na nyenzo NFRA ili itekeleze majukumu yake kwa Ufanisi zaidi.

### *Utekelezaji wa Mfumo wa* "Ipsas Accrual Basis"

**KWA KUWA,** Serikali Kuu iliamua kuanza kutumia Mfumo wa *"Ipsas accrual basis"* kuanzia tarehe 01 Julai, 2012 na kutengeneza Hesabu zake za mwanzo kwa mfumo huo kwa Hesabu zilizoishia Juni 30, 2013 , lakini Taarifa hizo zimekuwa na dosari nyingi;

**NA KWA KUWA**, Dosari zilizobainika kwenye Taarifa zinasababisha Taarifa ya fedha za Wizara, Wakala,Sekretarieti za Mikoa, Idara na Balozi kuwa na mapungufu ya ongezeko au pungufu ya fedha (*Overstatement/ understatement of accounts transaction);*

**KWA HIYO BASI,** Bunge liazimie kwamba, Serikali itenge rasilimali za kutosha (Fedha na Wataalamu) ili kuhakikisha kuwa Taasisi za Serikali Kuu zinatekeleza mfumo huo kwa uhakika na ufanisi wa kutosha kabla ya muda wa kipindi cha mpito cha miaka mitano (5) kwa matumizi ya mfumo huo kukamilika mwezi Machi, 2017. **Pendekezo la muda mfupi**

### *Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)*

**KWA KUWA,** Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) ni mojawapo ya Shirika la Kimkakati *(Strategic corporation)* katika kufanikisha kuwa na Tanzania yenye Viwanda na Uchumi wa kati lakini halitimizi malengo ya kuanzishwa kwake kutokana na Mapungufu kadhaa ikiwamo, ukosefu wa fedha na kutofanyika ipasavyo kwa upembuzi yakinifu wa Miradi na gharama zake;

**NA KWAKUWA,** Mapungufu hayo yamesababisha Miradi mingi iliyoibuliwa na NDC kutotekelezwa kwa wakati na fedha za Serikali kuendelea kutumika isivyostahili;

**KWA HIYO BASI,** Bunge liazimie kwamba: -

**Pendekezo la muda wa kati**

(a) NDC ifanye mapitio upya *(Review of structural arrangement)* ya Miradi iliyopangwa kutekelezwa kwa Ubia ili kuangalia kwa kina Taarifa kuhusu gharama za Miradi husika, Mipango ya utekelezaji, Muda wa utekelezaji na ugharamiaji wa Miradi ili kuhakikisha Serikali

inafahamu kwa kina na kwa muda mwafaka gharama na mapato yatakayotokana na Miradi hiyo;

(b) NDC ihakikishe inazingatia matakwa ya Kanuni ya 46 (2) ya Kanuni za PPA za mwaka 2011 kwa kuhakikisha inafanya tathmini na ufuatiliaji *(Monitoring and evaluation)* ya Miradi yenye ubia ili kuhakikisha maslahi ya Nchi yanalindwa na faida ya Uwekezaji inaonekana; na

(c) Serikali iiwezeshe NDC kifedha ili iweze kufanya upembuzi yakinifu wa Miradi yenyewe hali ambayo itaongeza nguvu ya NDC wakati wa majadiliano na Wabia wenza kwa ajili ya Uwekezaji kwenye Miradi.

***Ukosefu wa fedha za Uwekezaji wa Umma* (Public investment)**

**KWA KUWA,** Ukaguzi uliofanywa na CAG kwa mwaka wa fedha 2014 na 2015 ulibaini kuwa rasilimali kwa ajili ya Uwekezaji wa Umma ni chache na hazitoshelezi mahitaji;

**NA KWA KUWA,** Ukosefu wa rasilimali za Uwekezaji wa Umma umesababisha hisa za Serikali kupungua kwenye Mashirika Mbalimbali kama kwenye Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) na kutotekelezwa kwa Miradi mikubwa ya Kimkakati *(Strategic development projects)*;

**KWA HIYO BASI,** Bunge liazimie kwamba: -

a) Serikali ianzishe Mfuko maalum wa Uwekezaji *(Special investment fund)* ili fedha katika Mfuko huo zitumike kama mtaji katika maeneo ambayo Serikali inataka kuwekeza au kununua hisa za ziada kwenye Taasisi / Mashirika ambayo Serikali ina hisa. **Pendekezo la muda wa kati**
b) Mfuko huo wa Uwekezaji uanzishwe chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kutumia Mfumo wa kubakisha mapato *(Retention scheme)* ambao utatumika pia kutathmini Ufanisi wa Ofisi hiyo katika kukusanya rasilimali na kuwekeza.

***Malipo ya Pensheni na Kiinua mgongo kwa wakati mmoja* (Double payment of benefits)**

**KWA KUWA,** Imebainika kuwa Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya udhibiti wa nishati na maji (EWURA) na Mamlaka ya udhibiti wa usafiri wa maji na nchi kavu (SUMATRA) zimekuwa zikiwalipa baadhi ya Watumishi wake walio katika ngazi ya Menejimenti malipo ya Pensheni na wakati huo huo kuwalipa malipo ya kiinua mgongo *(Gratutity)* baada ya kumaliza mikataba yao ya kazi;

**NA KWA KUWA,** Jambo hilo ni kinyume na matakwa na miongozo ya Sheria zinazosimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii na matumizi yasiyofaa ya fedha za Umma;

**KWA HIYO BASI,** Bunge liazimie kuwa, Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA), EWURAna SUMATRA zisimamishe malipo hayo mara moja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mamlaka ya udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) watoe mwongozo kwa Taasisi za Umma kuzingatia Sheria na kuepuka malipo ya Pensheni na kiinua mgongo kwa wakati mmoja.

**Pendekezo la muda mfupi**

***Utekelezaji wa Mradi wa Uhamiaji Mtandao* (E – Immigration)**

**KWA KUWA,** Kamati imebaini kuwa Mfumo wa usimamizi wa utoaji wa Viza katika Balozi zetu na kwenye Mipaka hauna mawasiliano ya moja kwa moja na Makao Makuu ya Idara ya Uhamiaji;

**NA KWA KUWA,** Dosari hizo zinaweza kuwa zinasababisha kuipotezea Serikali mapato yake kupitia mauzo ya Viza;

**KWA HIYO BASI,** Bunge liazimie kwamba, Serikali kwa kuzingatia Sheria zilizopo na kwa lengo la kupata ufanisi itekeleze Mradi wa Uhamiaji Mtandao *(E – Immigration)* mapema iwezekanavyo ili kuhakikisha fedha za Umma zinakusanywa ipasavyo.

**Pendekezo la muda wa kati**

***Mikopo isiyorejeshwa katika Benki ya Maendeleo ya TIB***

**KWA KUWA,** Kamati imebaini uwepo wa Mikopo mingi isiyorejeshwa katika Benki ya Maendeleo ya TIB;

**NA KWA KUWA,** Kutorejeshwa kwa Mikopo hiyo kunasababisha Benki ya Maendeleo ya TIB isitekeleze malengo ya kuanzishwa kwake hasa kuchochea Maendeleo ya Kilimo na pia inaweza kusababisha Benki hiyo kushindwa kuwa na mtaji wa kutosha;

**KWA HIYO BASI,** Bunge liazimie kwamba, Serikali iingilie kati kwa kutumia vyombo mbalimbali vya Dola kuisadia TIB kukusanya madeni yote toka kwa Wafanyabiashara na Wateja wengine ambao wamekuwa wagumu *(Defaulters)* kurejesha Mikopo yao kwa mujibu wa Mikataba husika.

**Pendekezo la muda wa kati**

***Muamala wa shilingi 100,525,437,562.51 katika fungu 56 Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI)***

**KWA KUWA,** Ukaguzi wa fungu 56, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI ulibaini dosari katika muamala *(Transaction)* ya shilingi 100,525,437,562;

**NA KWA KUWA,** Dosari hizo zilisababisha shughuli zilizopangwa TAMISEMI kutofanyika;

**KWA HIYO BASI,** Bunge liazimie kuitaka Serikali kutoa maelezo ya kina kuhusiana na muamala huo. **Pendekezo la muda mfupi**

***Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT)***

**KWA KUWA,** Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) ni Ofisi muhimu katika kuhakikisha kunakuwepo usimamizi unaofaa wa fedha za Umma katika Taasisi za Serikali lakini inakabiliwa na changamoto za kibajeti;

**NA KWA KUWA,** Ukosefu wa bajeti ya kutosha unaathiri shughuli na mawanda ya ukaguzi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge liazimie kwamba, Serikali itenge na kutoa kwa wakati bajeti ya kutosha ili Ofisi ya Taifa ya ukaguzi itekeleze majukumu yake ya Kikatiba na kisheria bila kukwama. **Pendekezo la muda mfupi**

***Masuala mengine ya Msisitizo***

**KWA KUWA,** Kamati imebaini masuala kadhaa kama vile ucheleweshaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo, kutokuwepo kwa Mfuko wa uchaguzi na Mapungufu katika Mifumo ya udhibiti wa ndani na ICT katika Taasisi mbambali za Serikali;

**NA KWA KUWA,** Changamoto hizo zinasababisha hasara kwa Serikali na muda mwingine kusababisha rasilimali nyingi kuelekezwa eneo moja hasa wakati wa uchaguzi;

**KWA HIYO BASI;** Bunge liazimie kwamba: -

**Pendekezo la muda wa kati**

(a) Serikali ijitahidi kupeleka fedha za Miradi mbalimbali ya Maendeleo kwa wakati ili kuepuka ongezeko la gharama na kuvunjwa kwa Mikataba ikiwa ni pamoja na Taasisi za Umma kuepuka kuingia Mikataba ya Miradi bila ya kuwa na fedha katika bajeti;

(b) Mashirika ya Umma yanayohusika na ukusanyaji wa mapato yahakikishe yanaimarisha Mifumo ya udhibiti wa ndani na kutumia Mifumo *(systems)* yenye ufanisi katika uendeshaji wa shughuli zake;

(c) Serikali ianzishe Mfuko maalum wa uchaguzi *(Election fund)* ili kuhakikisha bajeti ya uchaguzi inakuwepo kwa wakati badala ya kusubiri mwaka wa uchaguzi; na

(d) Ofisi ya Msajili wa Hazina (TR0) iendelee kuwezeshwa ikiwa ndiyo Ofisi ya Usimamizi wa Mashirika ya Umma na hisa za Serikali katika maeneo Serikali ilipowekeza *(Office of the public enterprises)* itekeleze wajibu wake ipasavyo kwa mujibu wa Sheria.

## SEHEMU YA NNE

## HITIMISHO

### Shukurani

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Kamati imefafanua kwa kina majukumu ya Kamati, shughuli zilizotekelezwa, Uchambuzi wa kina wa shughuli hizo, maoni ya Kamati kuhusiana na Uchambuzi wa Taarifa mbalimbali za Hesabu za Mafungu ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma na kuhitimishwa na Mapendekezo yaliyotolewa kwa Bunge ili kuyajadili na kupata Maazimio.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kwa namna ya pekee kabisa kukushukuru wewe binafsi kwa Uongozi wako imara na makini wa Bunge letu Tukufu ambao umetoa usimamizi wa kutosha kuiwezesha Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuwasilisha Taarifa yake hapa Bungeni leo. Tunashukuru kwa miongozo yako kila wakati tulipokuhitaji.

**Mheshimiwa Spika,** Tunamshukuru Mheshimiwa Naibu Spika Dr. Tulia Ackson pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge. Napenda Kumshukuru Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya PAC Mheshimiwa Aeshi Hilary Khalfan, Mb ambaye aliiongoza Kamati tangu kuundwa kwake kwa takribani kipindi cha miezi tisa (9).

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee kabisa naomba kuwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi mkubwa, wamekuwa wakishiriki mijadala ya Vikao vya Kamati kwa Ufanisi na kutumia vema, Elimu, Taaluma, Uzoefu na Vipawa vyao katika kufanya uchambuzi wa kina wa Taarifa za Hesabu na kutoa Ushauri ambao kwa namna ya pekee nikiri umeifanya Kamati kuwa na Ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwatambua Wajumbe hao wa Kamati kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Aeshi Khalfan Hilary, Mb | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Felister Aloyce Bura, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Dkt. Shukuru Kawambwa, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Hafidh Ali Tahir, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Musa Bakari Mbarouk, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Jamal Kassim Ali, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Tunza Issa Malapo, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Japhet Ngalilonga Hasunga, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Ali Salim Khamisi, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Jumaa Hamidu Aweso, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Omar Mohamed Kigua, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Khadija Nassir Ali, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Esther Lukago Midimu, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Fakharia Shomari Khamis, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Raisa Abdalla Musa, Mb | Mjumbe |
| 21 | Mhe. Yosefa Ferdinand Komba, Mb | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Munde A. Tambwe, Mb | Mjumbe |
| 23. | Mhe. Josephine Ngezabuke, Mb | Mjumbe |
| 24. | Mhe. Ezekiel Magolyo Maige, Mb | Mjumbe |
| 25. | Mhe. Allan Joseph Kiula, Mb | Mjumbe |
| 26. | Mhe. Omary Tebweta Mgumba, Mb | Mjumbe |
| 27. | Mhe. Rhoda Edward Kunchela, Mb | Mjumbe |
| 28. | Mhe. Joseph George Kakunda, Mb | Mjumbe |
| 29. | Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb | Mjumbe |
| 30. | Mhe. Abdallah Haji Ally, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah kwa Uongozi na Ushauri wake kwa Kamati wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati.Namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athumani Hussein pamoja na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Erick Maseke na Ndugu Asmini Kihemba kwa kuratibu na kutoa Ushauri wa kitaalamu kwa shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Nachukua fursa hii kuishukuru Ofisi ya Taifa ya ukaguzi NAOT) na hususan Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Profesa Mussa Assad na Maafisa wake wote kwa kuisadia Kamati kutekeleza majukumu yake kwa Ufanisi. Aidha, natoa Shukurani kwa Msajili wa Hazina Ndugu Lawrence Mafuru na Ofisi yake, Mhasibu Mkuu wa Serikali (AcGen) Ndugu Francis Mwakapalila na Ofisi yake kwa kuisaidia Kamati katika kutekeleza majukumu yake kwa weledi na Ufanisi mkubwa.

**HOJA**

**Mheshimiwa Spika,** Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC)**
09 Novemba, 2016

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tutamsikia Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI YA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* kwa mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utangulizi; kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kuwasilisha kwa Bunge lako Tukufu taarifa yenye maoni, mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, ya Hesabu za Serikali za Mitaa, kuhusu maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa kwa mwaka 2013/2014 na 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii imebeba matatizo sugu yaliyobainika katika taarifa ya CAG kwa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2013/2014, kwa kuwa kulingana na ratiba ya uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, taarifa ya Kamati ya mwaka 2013/2014 haikuwasilishwa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu ya Kamati unatokana na majukumu ya msingi yaliyoorodheshwa katika Nyongeza ya Nane, Sehemu

ya Nne, kifungu cha 15(a)(c) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, kama ifuatavyo:-

(a) Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za Serikali za Mitaa yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

(b) Kufuatilia utekelezaji wa Mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati hii ili kuondoa matatizo hayo; na

(d) Kutoa Mapendekezo na ushauri kwa Serikali za Mitaa kuhusu matumizi mazuri ya fedha ili kuhakikisha kwamba tatizo la matumizi mabaya ya fedha linapungua katika Serikali za Mitaa.

(e)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya mahojiano na Halmashauri 30 kati ya Halmashauri 163 zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* katika mwaka wa fedha 2013/2014 na katika mwaka wa fedha 2014/2015, Kamati ilifanya mahojiano na Halmashauri 36 kati ya Halmashauri 164 zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*. Hivyo taarifa hii imetokana na mahojiano ya jumla ya Halmashauri 66. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Matatizo Sugu ya Matumizi ya Fedha za Serikali za Mitaa ni mkusanyiko wa mwenendo usioridhisha unaojirudia katika matumizi ya fedha na ambao hauzingatii sheria, kanuni na taratibu bora za matumizi ya fedha za umma. Kwa mfano:- *(Makofi)*

a) Manunuzi yasiyozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011;

b) Usimamizi mbovu wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo unaopelekea kuwepo kwa miradi ya maendeleo isiyokamilika kwa muda mrefu, miradi inayokamilika lakini haitumiki kama ilivyokusudiwa na baadhi ya miradi kukamilika ikiwa katika ubora wa hali ya chini kinyume na matakwa ya mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa baadhi ya miradi hiyo ni:-

(i) Mradi wa maji katika Kijiji cha Kayenze, Jijini Mwanza, wenye thamani ya Sh. 618,704,554 ambao haukutekelezwa;

ii) Mradi wa Maji *(WSDP)* wenye thamani ya Shilingi milioni 549.8 katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma-Ujiji ambao haukukamilika kama ilivyotegemewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine yenye matatizo sugu ni pamoja na:-

(1) Kutochangia asilimia 10 ya fedha kutoka katika mapato ya ndani *(own sources revenue)* kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana; *(Makofi)*

(2) Kutotekeleza Mapendekezo ya Kamati kwa kipindi cha nyuma na kutojibu Hoja za Ukaguzi kwa wakati;

(3) Kutopeleka kikamilifu asilimia 20 ya ruzuku inayopokelewa kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya Serikali za Mitaa na Vijiji;

(4) Uzembe katika ukusanyaji wa mapato;

(5) Fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kuchelewa kutolewa na Hazina au kutotolewa kabisa;

(6) Mfumo dhaifu wa udhibiti wa ndani *(weak internal control system);*

(7) Watumishi kukaimu nafasi zao bila kuthibitishwa kwa muda mrefu; na

(8) Kubadili matumizi ya fedha kinyume na bajeti.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji, Kamati ilibaini matumizi makubwa yasiyofuata taratibu za fedha katika ujenzi wa maabara kwa shule za sekondari kufuatia agizo la Serikali lililolenga kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundisha katika masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maagizo haya ni mazuri, hata hivyo, Halmashauri hazikuwa na utaratibu maalum wa kutafuta fedha za kugharamia ujenzi huo, badala yake zilitumia fedha kutoka kasma mbalimbali, bila kufuata utaratibu wa kuhamisha fedha. Kwa mfano Halmashauri nyingi nyingi zilibainika kuhamisha fedha kutoka katika kasma ya ruzuku za kujenga uwezo wa Serikali za Mitaa *(LGCDG)* bila idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali. Kamati inashauri Halmashauri kuhakikisha kwamba maagizo kutoka ngazi za juu yanatekelezwa kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kamati ni kuwa gharama za ujenzi wa maabara katika shule za sekondari zilikuwa ni kubwa na taratibu za fedha hazikufuatwa kikamilifu. Je, Serikali imefanya ukaguzi wa kina kuhusu matumizi hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza kasi ya maendeleo katika Halmashauri zetu ipo mikataba ya miradi mbalimbali ya Halmashauri na wadau mbalimbali. Aidha, ipo baadhi ya miradi ya uwekezaji baina ya wadau na

Halmashauri katika rasilimali za Halmashauri kama vile ardhi, majengo na viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini udhaifu wa watendaji wa Halmashauri katika usimamizi wa mikataba ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini unaosababisha:-

(i) Miradi kuchelewa kukamilika;

(ii) Miradi kukamilika ikiwa na kiwango cha chini;

(iii) Fedha za miradi kutumika kwa shughuli nyingine; na

(iv) Miradi kukamilika lakini ikabaki haitumiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mifano katika mwaka wa fedha 2014/2015 ni ujenzi wa stendi ya basi Mhuze katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Mkoani Shinyanga wenye thamani ya shilingi milioni 273 ambao haukukamilika kwa wakati. Aidha, katika Halmashauri hiyo mradi wa jengo la *OPD* katika kituo cha Ng'wang'halanga ulikamilika lakini jengo halikuwa likitumika. Sababu za kutotumika kwa jengo hili zilielezwa kuwa ni kutokuwepo na choo cha nyumba ya daktari. Kamati iliona jambo hili halina mantiki wala hoja yoyote ukilinganisha gharama za mradi na gharama za ujenzi wa choo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nitumie fursa hii kutoa maelezo mafupi kuhusu mradi wa Shirika la Usafirishaji Dar es Salaam (UDA).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* ilifanya kikao cha pamoja na Msajili wa Hazina, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Menejimenti ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam tarehe 28 Oktoba, 2016 kwa lengo la kujua hatma ya mradi na shirika hilo na usalama wa hisa 7,880,303 zisizotolewa *(unallotted shares).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijulishwa kuwa Serikali ilizuia mchakato wa uuzwaji wa hisa zisizotolewa uliokuwa ukitaka kufanywa na kampuni ya *Simon Group Limited* ambayo ni mbia mwenza wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam katika Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nia ya Kamati ni kuhakikisha kuwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inaendelea kuwa mwanahisa na kwamba hisa zisizotolewa ziko chini ya Msajili wa Hazina, nyaraka zifuatazo zimeombwa kutoka kwa Msajili wa Hazina ili Kamati iweze kuzipitia na kutoa mapendekezo na ushauri kwa Serikali. Moja; *Memorandum of Association* na *Articles of*

*Association* ya UDA na cheti cha umiliki wa hisa zisizotolewa *(Certificate of owning unallotted shares)* ili kujiridhisha na usalama wa hisa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inafuatilia kwa ukaribu suala hili na italiweka katika taarifa yake katika kipindi kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilifanya mahojiano na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuhusu uwekezaji katika mradi wa machinjio ya kisasa. Mnamo mwaka 2004 Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ilianzisha Kampuni ya Nyama inayoitwa *East Africa Meat Company Limited* iliyokusudia kujenga machinjio ya kisasa katika kiwanja cha *Kiltex* – Gongo la Mboto ambacho kilinunuliwa Mwaka 1997 na iliyokuwa Tume ya Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni hiyo ya nyama ilizishirikisha Halmashauri za Manispaa za Ilala, Temeke na Kinondoni kama wabia na baadaye walikaribishwa wabia wengine ambao ni Kampuni ya *Rheinhold & Mahla* (Malaysia) na *R&M* na Kampuni ya Uwekezaji ya Taifa, *NICOL*. Kampuni ya nyama ilikuwa na hisa 7,600 ambapo jumla ya thamani ya hisa katika uwekezaji huu ilikuwa ni Jiji na Manispaa zake Dola za Marekani milioni mbili *point* tano, R&M Dola za Marekani milioni tatu *point* saba na *NICOL* Dola za Marekani milioni tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanahisa walitakiwa kulipia hisa zao ili ipatikane fedha ya kuanza ujenzi wa machinjio, lakini hadi kufikia mwezi Juni 2009 palikuwa na jumla ya Dola za Marekani 2,005,083 tu sawa na asilimia 21.8 zilizokuwa zimepatikana, huku Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ikiwa imelipa fedha zake zote wakati mbia *R&M* akiwa hajalipa kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizokusanywa hadi kufikia tarehe 18 Juni, 2010 zilikuwa ni sh. 1,771,084,595 na matumizi yakiwa ni sh. 1,771,032,781 na hivyo kuacha bakaa ya sh. 51,814 tu. Maoni ya Kamati ni kuwa matumizi hayo hayakuwa na tija kwa kuwa fedha zote zilitumika kulipa stahili za meneja, kugharamia mikutano na matumizi mengine ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Meneja alilipwa mshahara wa jumla ya sh. 532,237,414 sawa na asilimia 30 ya fedha zote zilizokusanywa, huku akilipiwa nyumba ya kuishi jumla ya shilingi milioni 40.7, vifaa vya ofisi na samani za nyumbani shilingi milioni 10.5. Aidha, palikuwa na malipo mengine makubwa kama vile gharama za upembuzi yakinifu shilingi milioni 240 na gharama za kusafiri na likizo shilingi milioni 197.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kueleza kwa masikitiko makubwa kwamba mradi huu haukutekelezwa ingawa fedha zote zilitumika. Hii ndio ilikuwa sababu ya Kamati kuhoji matumizi yake katika Taarifa yake kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013. Kwa kuwa mali pekee iliyobaki katika mradi huo wa

machinjio ya kisasa ni ardhi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inasimamia ardhi hiyo kwa manufaa ya wabia wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Kamati ni kwamba, miradi ya maendeleo inapaswa kusimamiwa kwa ukaribu ili iweze kukamilika kwa wakati na kutumika kama ilivyokusudiwa. Nini tamko la Serikali katika suala hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni kawaida sasa kwa Halmashauri kutekeleza kwa mazoea, kutekeleza kwa kuchelewa na kutotekeleza kabisa maagizo ya Kamati yako Tukufu ya *LAAC*. Hoja za ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* hazijibiwi kwa wakati na kwa ukamilifu. Kwa ujumla Halmashauri nyingi katika mwaka wa 2013/2014 na 2014/2015 zilibaki na idadi kubwa ya Maagizo yasiyotekelezeka na Hoja za Ukaguzi zisizojibiwa. Kamati imejiridhisha kuwa Halmashauri zinapuuzia kutekeleza maagizo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja ya Kamati ni kuwa, Hoja za Ukaguzi hulenga kuboresha utendaji wa Halmashauri na maagizo ya Kamati, kutokana na uchambuzi wa taarifa na mahojiano baina ya Kamati na Halmashauri kufuatia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kamati inaitaka Ofisi ya Rais, TAMISEMI kueleza sababu za kushindwa kuchukua hatua za kinidhamu kwa Halmashauri, juu ya uzembe wa kutotekeleza maagizo ya Kamati na kutojibu hoja za Ukaguzi kwa ukamilifu na kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la halmashauri kutotenga asilimia 10 ya makusanyo yake ya mapato kutoka vyanzo vya ndani *(own sources revenue)* kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana limeendelea kutopatiwa tiba ya kudumu. Baadhi ya Halmashauri hazikupeleka michango hii kwa zaidi ya miaka mitatu mfululizo bila kutoa sababu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vikao vilivyofanyika kuanzia tarehe 15 Agosti, 2016 hadi tarehe 2 Septemba, 2016 hapa Dodoma, Kamati ilitoa agizo kwa Halmashauri 20 ziandike na kuwasilisha barua ya kuthibitisha kulipa deni hili la Mfuko wa Wanawake na kuandaa mpango wa malipo na kuviwasilisha kwa Mwenyekiti wa Kamati kabla ya tarehe 30 Septemba, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo jambo la kusikitisha ni kuwa hadi kufikia siku ya leo ninapowasilisha taarifa hii Halmashauri sita hazikutekeleza agizo hilo. Halmashauri hizo ni; Halmashauri ya Wilaya Mpanda, Halmashauri ya Wilaya Kishapu, Halmashauri ya Wilaya Nsimbo, Halmashauri ya Wilaya Tunduru, Halmashauri ya Jiji la Tanga na Halmashauri ya Wilaya Ruangwa. Maoni ya Kamati ni kuwa utekelezaji wa agizo kwa Halmashauri hizo umeendelea kutopewa kipaumbele na inatia shaka iwapo deni la Mfuko huo litalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Halmashauri iliyokuwa kinara wa kutotenga asilimia kumi ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana ni Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni. Halmashauri hii hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2015 ilikuwa na jumla ya deni la Shilingi bilioni tisa la Mfuko huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upelekaji wa fedha za fidia ya vyanzo vya mapato vilivyofutwa *GPG*, asilimia 20, kwenda katika Serikali za Mitaa na Vijiji haujafanyika kama ilivyoagizwa, hali inayopelekea halmashauri kuzifanya Serikali za Mitaa na vijiji kushindwa kujiendesha. Katika Halmashauri zote zilizohojiwa hapakuwa na hata Halmashauri moja iliyotenga na kupeleka mchango huu kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika baadhi ya halmashauri, fedha zilizopelekwa katika Serikali za Mitaa na Vijiji kama ruzuku, zimeonekana kuchanganywa kimakosa na mapato ya ndani kabla ya kutenga asilimia 20. Hali hii haitoi picha halisi ya kiasi kamili kinachotakiwa kutengwa na kuwasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamekuwepo na uzembe katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vya ndani unaofanywa na Halmashauri kwa mawakala wa mapato bila hatua stahiki kuchukuliwa mapema. Hali hii husababisha:-

(i) Kiasi kikubwa cha fedha kutokusanywa kwa wakati;

(ii) Upotevu wa vitabu vya kukusanyia mapato;

(iii) Mapato kukusanywa na vitabu viwili sambamba; na

(iv) Mawakala wa Mapato kupewa mikataba bila kuweka dhamana ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri inaposuasua kukusanya mapato sio tu kwamba inaonesha kutozingatia makadirio yake, bali kuendelea kuwa tegemezi kwa ruzuku kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Rorya imeonesha udhaifu mkubwa katika kusimamia makusanyo kutoka vyanzo vya ndani. Katika mwaka wa fedha 2013/2014 Halmashauri hiyo ilikadiria kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 1.9, lakini ilikusanya kiasi cha shilingi milioni 618 sawa na asilimia 32 tu. Mwaka uliofuata, 2014/2015, Halmashauri hii ilikadiria kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 1.5, lakini ilikusanya kiasi cha shilingi milioni 594 sawa na asilimia 39

tu. Huu ni uzembe mkubwa katika kuhakikisha Halmashauri zinakusanya kiasi kikubwa cha mapato ili kupunguza utegemezi kwa Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja ya Kamati ni kwamba, Halmashauri zinapaswa kuongeza ufanisi katika kukusanya mapato kutoka vyanzo vya ndani ili kuondoa utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu katika kutekeleza majukumu yake, Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuzibana Halmashauri ili ziongeze ufanisi katika ukusanyaji wa mapato na kuongeza vyanzo vingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati baada ya kufanya mahojiano na Halmashauri ilibaini kwamba usugu katika matumizi mabaya ya fedha za umma kwa kiasi kikubwa unasababishwa na mfumo dhaifu wa udhibiti wa ndani yaani *weak internal control system. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitaka kujiridhisha na uwezo na uwajibikaji wa Kamati za Ukaguzi za halmashauri na ikama ya Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani na iligundua kwamba halmashauri nyingi zimeonekana kuwa na Kamati za Ukaguzi zisizokuwa na ufanisi na Kitengo cha ukaguzi wa ndani kutokuwa na vitendea kazi na bajeti kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utendaji wa halmashauri unategemea timu madhubuti ya wakuu wa idara na vitengo mbalimbali. Kamati imebaini kuwa moja kati ya sababu zinazofanya halmashauri kuwa na utendaji usioridhisha, ni wakuu wa idara na vitengo kukaimu nafasi zao kwa muda mrefu, kinyume na Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kukaimu ni vigumu kwa mtumishi kutoa maamuzi mazito ya kiutendaji kwa maslahi ya halmashauri yake. Hali hii hupelekea majukumu yote kuwa juu ya Afisa Masuuli na ndipo utendaji wa halmashauri nzima hushuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini baadhi ya wakuu wa idara na vitengo kwa baadhi ya halmashauri, kutokuwa na uwezo wa kutosha kutekeleza majukumu yao. Baadhi ya halmashauri zilizokuwa na wakuu wa idara walioonesha udhaifu mkubwa ni Halmashauri ya Wilaya Ngara, Halmashauri ya Wilaya Hai, Halmashauri ya Wilaya Rombo, Halmashauri ya Wilaya Mkalama na Halmashauri ya Wilaya Itilima.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kamati ni kuwa, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi za Wakuu wa Mikoa yote zihakikishe kuwa halmashauri zinakuwa na wakuu wa idara na vitengo wenye sifa. Maeneo mapya ya utawala yapangiwe wakuu wa idara na vitengo wenye weledi, sifa na uzoefu katika nafasi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini ucheleweshwaji uliokithiri wa utoaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka Hazina, Halmashauri kupelekewa fedha pungufu ya bajeti husika na katika miradi mingine fedha kutotolewa kabisa. Upungufu huu kwa kiasi kikubwa unaathiri huduma kwa wananchi na kuwaacha wakiendelea kuishi maisha magumu. Kamati haikupata maelezo ya kina ya kiini hasa cha tatizo hili hutoka Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imesikitishwa kwa kucheleshwa na kutotolewa kabisa fedha za miradi ya maendeleo. Hoja ya Kamati ni kwamba, miradi ya maendeleo inalenga kuwahudumia wananchi wa eneo husika na huwa na bajeti zake na mpango wa maendeleo katika muda maalum. Kamati inaitaka Serikali kutoa mkakati wa kuepukana na upungufu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya Kamati, baada ya kutoa maelezo ya kina kuhusu yaliyojiri katika mijadala na Halmashauri 66, nachukua fursa hii kutoa mapendekezo ya Kamati kwa ajili ya kuliomba Bunge lako Tukufu liyajadili na kuyaafiki ili yawe maazimio ya Bunge kwa ajili ya kuchochea nidhamu ya matumizi ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, Sheria ya Manunuzi ya Umma:-

KWA KUWA, imebainika kwamba Halmashauri zilizo nyingi hazifuati Sheria ya Manunuzi ya Umma katika manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali;

NA KWA KUWA, kutozingatia masharti ya Sheria ya Manunuzi kunazisababishia hasara Halmashauri nyingi nchini na kuzipunguzia uwezo wa kutoa huduma bora kwa Wananchi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kuwa Serikali:-

(i) Itoe taarifa ya hatua zilizochukuliwa kwa watumishi wa baadhi ya halmashauri kwa kushindwa kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma. *(Makofi)*

(ii) Ieleze Mpango Mkakati uliopo, unaotekelezeka, katika kuhakikisha Halmashauri zinazingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma. *(Makofi)*

(iii) Ihakikishe kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* anafanya Ukaguzi Maalum katika Halmashauri zilizokuwa na dosari katika ununuzi wa vifaa na huduma mbalimbali kwa mwaka 2014/2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili; usimamizi wa miradi ya maendeleo:-

KWA KUWA, kumekuwa na udhaifu mkubwa katika usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo unaosababisha miradi kutokamilika katika kiwango kinachotakiwa, kukamilika na kushindwa kutoa huduma kwa wananchi au kutelekezwa kabisa;

NA KWA KUWA, udhaifu huo husababisha upotevu wa fedha zilizotumika kufuatia kiwango kidogo cha utekeleaji na kuongezeka kwa gharama za miradi kutokana na kuanza upya kwa mchakato wa kuwapata wazabuni;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kuwa, Serikali itoe maelezo ya kina ya sababu ya miradi mingi kutotekelezwa kinyume na matarajio na mkakati wa kuhakikisha uchelewaji wa kupeleka fedha hautokei tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Maagizo ya Kamati na Hoja za Ukaguzi:-

KWA KUWA, baadhi ya Halmashauri nchini hazikutekeleza maagizo ya Kamati na kutokujibu hoja za ukaguzi kwa wakati, kinyume na masharti ya kifungu cha 31(1)(3) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, namba 11 ya mwaka 2008, tatizo ambalo linazidi kuota mizizi na kuendelea kuonekana katika Taarifa ya Ukaguzi mwaka hadi mwaka;

NA KWA KUWA, tatizo hilo linasababisha Halmashauri hizo kuendelea kukiuka sheria, kanuni na taratibu za fedha, hivyo kutozingatia matakwa ya utawala bora kwenye matumizi ya fedha za umma;

KWA HIYO BASI, Bunge lako Tukufu linaazimia kuwa Serikali:-

(1) Itoe sababu na kueleza mkakati wa kuondokana na mrundikano wa hoja za ukaguzi na maagizo ambayo hayajafanyiwa kazi kama ilivyobainika kwa baadhi ya halmashauri. *(Makofi)*

(2) Ieleze njia mbadala ya kuzibana Halmashauri zinazoshindwa kujibu hoja za ukaguzi na kutekeleza maagizo ya Kamati kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Mchango wa Asilimia 10:-

KWA KUWA, imebainika kuwa, Wakurugenzi wa baadhi ya Halmashauri kutochangia michango ya asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana kwa wakati au kutochangia kabisa;

NA KWA KUWA, kukosekana kwa michango ya asilimia 10 inayopelekwa na Mfuko wa Wanawake na Vijana kwa Halmashauri nchini, kunasababisha Mfuko kushindwa kujiendesha, jambo linalochangia vikundi vya wanawake na

vijana kushindwa kuendesha biashara ndogondogo na hivyo kuathiri maisha yao;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kuwa Serikali ilete Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana, kwa kuwa waraka uliopo hautekelezwi ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Fedha za Ruzuku kwa Serikali za Mitaa na Vijiji:-

KWA KUWA, uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mahojiano kati ya Kamati na Menejimenti za halmashauri 66 umeonesha kuwa, halmashauri nyingi nchini hazipeleki asilimia 20 ya ruzuku za fidia ya vyanzo vya mapato vilivyofutwa *GPG,* kwenda Vijijini au kwenye Serikali za Mitaa kama ilivyoagizwa;

NA KWA KUWA, Halmashauri hizo zinaposhindwa kupeleka fedha za ruzuku kama ilivyoagizwa zinasababisha Serikali za Mitaa na Vijiji kushindwa kujiendesha na hivyo kushindwa kutoa huduma ipasavyo kwa wananchi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kuwa Serikali:-

(a) Itathmini namna bora ya kuwasilisha asilimia ishirini ya fedha za ruzuku kwa ajili ya vijiji, ikiwa ni pamoja na kuzipeleka fedha hizo moja kwa moja Vijijini na Serikali za Mitaa kutoka Hazina. *(Makofi)*

(b) Ihakikishe kuwa, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inachangia michango hiyo, tofauti na kisingizio kwamba, haina Vijiji wala Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, Uzembe katika Usimamizi wa Mapato ya Ndani:-

KWA KUWA, Halmashauri zote zimebainika kuwa na uzembe na udhaifu katika usimamizi wa Mfumo wa Ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vya ndani;

NA KWA KUWA, uzembe huo husababisha halmashauri kukusanya makusanyo kidogo na kuendelea kuwa tegemezi kwa ruzuku kutoka Serikali Kuu;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kuwa, Serikali ieleze mkakati wake katika kuhakikisha halmashauri zinakusanya mapato kulingana na malengo yao na zinakuwa na vyanzo mbadala vya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, Udhaifu Katika Mfumo wa Udhibiti wa Ndani:-

KWA KUWA, imedhihirika kuwepo kwa udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani kunasababisha dosari nyingi katika taarifa za fedha za halmashauri, ukusanyaji hafifu wa makusanyo ya maduhuli na matumizi mabaya ya fedha;

NA KWA KUWA, udhaifu wa mfumo wa udhibiti wa ndani unachangia kukosekana kwa uhalisia katika taarifa za fedha, upotevu wa makusanyo na utekelezaji mbovu wa bajeti za miradi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kuwa Serikali iandae mkakati wa kuimarisha kitengo cha ukaguzi wa ndani kwa Halmashauri zote nchini hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, Watumishi Kukaimu Nafasi zao kwa Muda Mrefu:-

KWA KUWA, imebainika kuwa baadhi ya Wakuu wa Idara na Vitengo katika halmashauri nchini wanakaimu nafasi zao kwa kipindi kirefu;

NA KWA KUWA, katika kipindi cha kukaimu ni vigumu kwa Mkuu wa Idara kutoa maamuzi mazito ya kiutendaji kwa maslahi mapana ya halmashauri, hali inayosababisha utendaji wa Halmashauri nzima kushuka;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kuwa Serikali:-

(1) Ileze sababu ya baadhi ya Halmashauri kuwa na Wakuu wa Idara na Vitengo wanaokaimu nafasi zao kwa muda mrefu.

(2) Ieleze Mkakati uliopo katika kuhakikisha kuwa nafasi zote zinazokaimiwa zinakuwa na watumishi waliothibitishwa.

(3) Iache kupeleka Wakuu wa Idara na Vitengo wasio na uzoefu katika maeneo mapya ya utawala kwa kuwa halmashauri hizi zinakuwa na changamoto nyingi katika kipindi cha mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tisa, Fedha za Miradi ya Maendeleo:-

KWA KUWA, imebainika kuwa fedha za miradi ya maendeleo hazitolewi kwa wakati kwa mujibu wa bajeti iliyopitishwa na Bunge;

NA KWA KUWA, uchelewaji katika kutoa fedha hizo husababisha miradi kutotekelezwa kwa wakati na hivyo kuathiri moja kwa moja huduma iliyotarajiwa kutolewa kwa wananchi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kuwa, Serikali ieleze kwa kina sababu za kushindwa kupeleka fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri na iweke wazi mkakati endelevu wa kuepuka uchelewaji huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilikumbwa na changamoto kubwa za kibajeti na kushindwa kutembelea na kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo kama ilivyoelekezwa hapo awali. Kadhalika Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilikumbwa na changamoto za kibajeti zilizosababisha kushindwa kutembelea baadhi ya Halmashauri katika kuthibisha majibu ya hoja mbalimbali za ukaguzi. Kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ilirudishwa na Kamati kwa kushindwa kuweka hoja za ukaguzi katika kitabu cha *LAAC* kwa kuwa hazikuhakikiwa na *CAG*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kutenga bajeti ya kutosha kwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na Kamati za Bunge za Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma katika bajeti zinazokuja ili kuondoa changamoto hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumshukuru Mungu kwa kutupa nguvu na kuweza kutimiza majukumu yetu ya kibunge. Natoa shukurani zangu za dhati kwako kwa namna ambavyo umekuwa ukitoa miongozo mbalimbali ya kusaidia ufanisi katika utendaji wa Kamati ya *LAAC*. Nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati yangu kwa kutekeleza vyema na kwa ustadi mkubwa majukumu yao bila kuchoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashilillah na Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge ndugu Athuman Hussein kwa ufafanuzi wa mambo mbalimbali ya uendeshaji wa shughuli za Kibunge kila tulipowahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nichukue fursa hii kumshukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Watumishi wote wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa ufafanuzi wa kina waliotupa katika kipindi chote cha mahojiano na Halmashauri na pia Ofisi ya TAMISEMI na Hazina kwa ushirikiano wao mkubwa wakati wote wa vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati yangu nachukua fursa hii kuwapogeza Makatibu wa Kamati, Ndugu Dismas Muyanja na ndugu Godfrey

Kasanga na Msaidizi wao ndugu Waziri Kizingiti pamoja na watumishi wote katika Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kwa ushirikiano wao wakati wote wa vikao, Kamati yangu ilipowahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ya Kudumu ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* imeundwa na Wajumbe 24, ambao kutokana na muda naomba nisitaje majina yao, badala yake yaingie kwenye *Hansard* kama yalivyoorodheshwa kwenye taarifa zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, Kamati yangu imebainisha matatizo sugu katika matumizi ya fedha za umma katika Halmashauri zetu katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2013/2014 na mwendelezo wake katika mwaka 2014/2015. Aidha, Kamati imetoa Mapendekezo dhidi ya matatizo hayo kama suluhisho. Kwa maana hiyo sasa, ni wajibu wa Serikali katika kujipanga vema kutekeleza ushauri huo bila kutegemea usimamizi wa Kibunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngombale, ahsante. *(Makofi)*

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC) KWA MWAKA 2016- KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

(*Inatolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016*)

## SEHEMU YA KWANZA

## MAELEZO YA JUMLA

### Utangulizi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha katika Bunge lako Tukufu, Taarifa yenye Maoni na Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, kuhusu maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya Fedha za Umma katika Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2013/14 na 2014/15.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii imebeba matatizo sugu yaliyobainika katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG),

kwa hesabu za serikali za mitaa, kwa mwaka wa fedha 2013/14 kwa kuwa kulingana na ratiba ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 taarifa ya Kamati ya mwaka 2013/14 haikuwasilishwa katika Bunge lako tukufu.

Sehemu hii ya kwanza ya Taarifa ya Mwaka ya Kamati inaelezea Muundo na Majukumu ya Kamati, mifano ya matatizo sugu katika matumizi ya Fedha za Umma katika serikali za mitaa, kama yalivyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), na taswira ya namna Kamati ilivyotekeleza Majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa katika kipindi cha mwaka 2016 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) ilipokea na kujadili Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kuhusu Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2014, na tarehe 30 Juni, 2015; naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, maelezo yanayotolewa katika Taarifa hii yanatokana na hesabu zilizokaguliwa, na kama zilivyowasilishwa katika Taarifa hizo za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kipindi hicho.

**Majukumu ya Kamati.**

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa kazi za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa unatokana na taarifa ya hesabu, zilizokaguliwa, na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ambapo Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati unatokana na Majukumu ya Msingi yaliyo orodheshwa katika Nyongeza ya 8 sehemu ya 4 kifungu cha 15 (a)-(c) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, ambayo kwa Kamati hii ni Hadidu za Rejea. Majukumu hayo ni kama ifuatavyo;

a) **Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya Fedha za Serikali za Mitaa yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;**

b) **Kufuatilia utekelezaji wa Mapendekezo yaliyokwisha tolewa na Kamati ili kuondoa matatizo hayo; na**

c) **Kutoa Mapendekezo na ushauri kwa Serikali za Mitaa kuhusu matumizi mazuri ya fedha ili kuhakikisha kwamba tatizo la matumizi mabaya ya fedha linapungua katika Serikali za Mitaa.**

**Mheshimiwa Spika,** Zipo namna kuu tatu za kutekeleza Majukumu hayo ambazo ni;

1. Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambapo kusudio ni kubaini maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma,

2. Kufanya mahojiano ya Mezani baina ya Kamati na Menejimenti za Halmashauri ili kupata ufafanuzi wa hoja mbalimbali na kutoa mapendekezo ya maboresho, na

3. Kamati kuzuru na kufanya Ukaguzi wa Matumizi ya fedha katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika baadhi ya Halmashauri ili kujiridhisha na thamani ya fedha katika miradi hiyo (value for money).

Katika kujiridhisha na mwenendo wa matumizi ya fedha za serikali za mitaa kwa mwaka 2013/14 na 2014/15, Kamati ilifanya mahojiano ya mezani, yaani ana kwa ana, kwa kuziita menejimenti za Halmashauri mkoani Dar es salaam na Dodoma. Kutokana na ukosefu wa fedha Kamati ilishindwa kutembelea Halmashauri kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa thamani ya fedha (value for money) katika miradi mbalimbali ya maendeleo iliyotekelezwa kwa kipindi hicho hata kama kulikuwa na umuhimu wa kufanya hivyo.

Katika kuziita Halmashauri kwa mahojiano, Kamati ilizingatia mambo yafuatayo;

1. Idadi ya Hamashauri zilizopewa Hati isiyoridhisha na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,

2. Halmashauri zilizoporomoka kutoka kwenye Hati inayoridhisha hadi Hati yenye shaka,

3. Halmashauri zilizofanyiwa Ukaguzi Maalumu mwaka 2012,

4. Halmashauri zenye dosari kubwa katika taarifa zake za fedha, na

5. Halmashauri mpya zilizoanzishwa ambazo taarifa zake zina dosari kubwa na hazijawahi kuitwa mbele ya Kamati kwa mahojiano.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya mahojiano na Halmashauri 30 kati ya Halmashauri 163 zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika mwaka wa fedha 2013/14 na katika mwaka wa fedha 2014/15 Kamati ilifanya mahojiano na Halmashauri 36 kati ya Halmashauri 164 zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu

za Serikali (CAG) . Hivyo taarifa hii imetokana na mahojiano ya jumla ya Halmashauri 66.

**Muhtasari wa Matokeo ya Mahojiano baina ya Halmashauri na Kamati.**

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli za Kamati kwa mwaka 2016 zililenga kushughulikia;

1. Maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma,

2. Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo na ushauri yaliyotolewa na Kamati,

3. Kufuatilia hoja za ukaguzi zilizotolewa na CAG, na

4. Kutoa maoni na mapendekezo katika uboreshaji wa matumizi ya fedha katika serikali za mitaa.

**Mheshimiwa Spika,** Awali naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwa muhtasari matokeo ya shughuli za Kamati wa mwaka 2016 kama ifuatavyo:-

***Maeneo yenye Matatizo Sugu ya Matumizi yasiyofaa ya Fedha za Umma;***

**Mheshimiwa Spika,** Matatizo Sugu ya Matumizi ya Fedha za Serikali za Mitaa ni mkusanyiko wa mwenendo usioridhisha unaojirudia katika matumizi ya fedha na ambao hauzingatii Sheria, Kanuni na Taratibu Bora za Matumizi ya Fedha za Umma na ambao kimsingi hauna tija.

Ifuatayo ni mifano ya maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi ya fedha za serikali za mitaa yaliyobainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2013/14 na mwaka 2014/15:

a) Manunuzi yasiyozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011,

b) Usimamizi mbovu wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo unaopelekea kuwepo kwa Miradi ya Maendeleo isiyo kamilika kwa muda mrefu, miradi inayokamilika lakini haitumiki kama ilivyokusudiwa, na baadhi ya miradi kukamilika ikiwa katika ubora wa hali ya chini kinyume na matakwa ya mkataba. Mfano wa baadhi ya miradi hiyo ni:

i. Mradi wa maji katika kijiji cha Kayenze, Jijini Mwanza, wenye thamani ya Shilingi. 618,704,554 ambao haukutekelezwa,

ii. Mradi wa Maendeleo wa Shule za Sekondari (SEDP) katika ujenzi wa Bweni wenye thamani ya Shilingi Milioni 94.2 katika kijiji cha Ndongosi, na Shilingi Milioni 100.13 katika kijiji cha Ruanda Hamlashauri ya Wilaya ya Mbinga ambao haukukamilika,

iii. Mradi wa Maji (WSDP) wenye thamani ya Shilingi Milioni 549.8 katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji ambao haukukamilika kama ilivyotegemewa,

iv. Katika mfuko wa LGCDG, Katika Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, miradi yenye thamani ya Shilingi Milioni 182.5 ilikamilika lakini haikuwa ikitumika,

v. Mradi wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida ulitumia kiasi cha Shilingi Milioni 133 nje ya shughuli za mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Maeneo mengine yenye matatizo sugu ni pamoja na:-

a) Baadhi ya Halmashauri kutochangia kabisa na nyingine kutochangia kikamilifu na kwa wakati asilimia kumi (10%) ya fedha kutoka katika mapato ya vyanzo vya ndani (own sources revenue) kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana,

b) Kutotekeleza Mapendekezo ya Kamati kwa kipindi cha nyuma na kutojibu Hoja za Ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa wakati,

c) Baadhi ya Halmashauri kutokupeleka kabisa na nyingine kutopeleka kikamilifu asilimia ishirini (20%) ya ruzuku inayopokelewa kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya Mamlaka za Chini (Vijiji na Serikali za Mitaa);

d) Uzembe katika ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri na upotevu usio na maelezo ya kuridhisha wa Vitabu vya Wazi vya kukusanyia mapato;

e) Fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kuchelewa kutolewa na Hazina au kutotolewa kabisa;

f) Mfumo dhaifu wa udhibiti wa ndani (weak internal control system);

g) Watumishi kukaimu Nafasi zao bila kuthibitishwa kwa muda mrefu; na

h) Kubadili matumizi ya fedha kinyume na bajeti kwa kutumia kivuli cha maagizo kutoka ngazi za juu.

### *Utekelezaji wa Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa katika kipindi kilichopita.*

**Mheshimiwa Spika**, Ili kujiridhisha na utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kipindi kilichopita, Kamati ilipitia taarifa ya ukaguzi ya CAG ili kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati, kufuatilia hoja za ukaguzi zilizotolewa na CAG, na kutoa maoni na mapendekezo katika uboreshaji wa matumizi ya fedha katika Serikali za Mitaa.

Matokeo ya shughuli hiyo kwa ujumla yalionesha kuwa pamekuwa na udhaifu mkubwa katika kujibu hoja za ukaguzi na kutekeleza mapendekezo ya Kamati. Maoni ya Kamati hulenga kufanya maboresho katika matumizi ya fedha za umma, hata hivyo ni Halmashauri chache tu zilitekeleza maoni hayo kwa zaidi ya asilimia 50.

### Maoni ya Jumla kuhusu Matokeo ya Mahojiano baina ya Halmashauri na Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na matokeo hayo, kwa ujumla Kamati imebaini kuwa Halmashauri hazitoi kipaumbele katika utekelezaji wa maoni yanayotolewa kwa kuwa:

- Kamati hukutana na Halmashauri moja baada ya kipindi kirefu,
- Kamati kukosa nguvu ya kushtaki pale inapobaini ubadhirifu katika matumizi ya fedha za umma, na
- Kamati kufungwa katika kutoa mapendekezo na maoni tu.

## SEHEMU YA PILI

## UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI

### Maelezo ya Jumla kuhusu Uchambuzi;

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2013/14 jumla ya Halmashauri 163 zilikaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kupatiwa Hati ya Ukaguzi (Audit Opinion) aidha katika mwaka wa fedha 2014/15 jumla ya Halmashauri 164 zilikaguliwa na kupatiwa Hati ya Ukaguzi (Audit Opinion) kulingana matokeo ya ukaguzi huo.

Taarifa ya CAG kwa mwaka wa fedha 2014/15 imeonesha kuwa Hati Zinazo ridhisha zimepungua kutoka 150 katika mwaka 2013/14 hadi kufikia hati 47 katika mwaka 2014/15. Idadi hiyo imepungua kwa asilimia 68. Hiki ni kiwango kikubwa cha upungufu. Kamati imebaini kwamba upungufu huo umesababishwa na Halmashauri kutothaminisha mali za kudumu kama vile ardhi, majengo na mitambo kwa mujibu wa Kanuni za Kimataifa za Uhasibu kwa Sekta za Umma (IPSAS 17).

**Mheshimwa Spika,** Hati zenye Shaka zimeongezeka kutoka 13 katika mwaka 2013/14 hadi kufikia hati 113 katika mwaka wa fedha 2014/15. Ongezeko hilo ni sawa asilimia 88.5 kutokana Halmashauri kutozingatia ushauri na mapendekezo yanayotolewa na CAG wakati wa ukaguzi na Halmashauri kutothaminisha mali za kudumu kama vile ardhi, majengo na mitambo kwa mujibu wa Kanuni za Kimataifa za Uhasibu kwa Sekta za Umma (IPSAS 17).
Hali hiyo ya kupungua kwa hati zinazoridhisha na kuongezeka kwa hati zenye shaka, kwa miaka minne, inaonekana katika kielelezo namba 1.

**Kielelezo Namba 1:**
*Idadi na aina ya hati zilizotolewa na CAG kwa miaka minne*

| Mwaka | Hati Zinazoridhisha | Hati Zenye Shaka | Hati Zisizoridhisha | Hati Mbaya |
|---|---|---|---|---|
| 2014/2015 | 47 | 113 | 3 | 1 |
| 2013/2014 | 150 | 13 | 0 | 0 |


| Mwaka | Hati Zinazoridhisha | Hati Zenye Shaka | Hati Zisizoridhisha | Hati Mbaya |
|---|---|---|---|---|
| 2012/2013 | 112 | 27 | 1 | 0 |
| 2011/2012 | 104 | 29 | 1 | 1 |

**Chanzo**:

*Ripoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Taarifa ya Fedha ya Serikali za Mitaa kwa Mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2015.*

**Mheshimiwa Spika,** Ili kulinganisha mwenendo wa idadi ya Hati Zinazo ridhisha na Hati zenye Shaka kuanzia mwaka 2011/12 hadi mwaka 2014/15 takwimu hizo zinaonekana katika kielelezo namba 2.

**Kielelezo Namba 2: Mwenendo wa aina ya hati za ukaguzi zilizotolewa kuanzia mwaka 2011/12 hadi 2014/15**




**Chanzo**: *Kielelezo Namba 1.*

**Mheshimiwa Spika,** Katika mahojiano na Halmashauri 30 kwa mwaka wa fedha 2013/14 Halmashauri 8 zilikuwa na mapungufu makubwa na dosari nyingi za hesabu katika taarifa zake na hivyo zilirudishwa ili ziandae upya taarifa zake za utekelezaji. Halmashauri hizo zilitakiwa kurekebisha taarifa katika masuala yafuatayo:

i. Miradi ya Maendeleo,
ii. Maagizo ya Kamati kwa kipindi kilichopita, na
iii. Majibu ya hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Halmashauri hizo ni: **H/W Gairo, H/M Kigoma/Ujiji, H/W Kasulu, H/W Mbulu**, **H/W Kiteto, H/W Kalambo, H/W Longido** na **H/W Kwimba.**

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Halmashauri hizi katika mahojiano yaliyofanyika mwezi Agosti, 2016 zilitekeleza maagizo ya Kamati na hivyo Kamati kuridhika na hatua zilizochukuliwa.

Katika mwaka wa fedha 2014/15 Kamati ilifanya mahojiano na Halmashauri 36 ambapo Halmashauri 7 zilirudishwa kufuatia kubainika kwa matatizo mbalimbali katika taarifa zake.

**Mheshimiwa Spika,** Kielelezo namba 3 kinaonesha Halmashauri hizo pamoja na sababu za Kamati kuzirudisha.

**Kielelezo Namba 3:**
*Baadhi ya Halmashauri zilizorudishwa*

| Na | Halmashauri | Sababu zilizopelekea Halmashauri kurudishwa |
|---|---|---|
| 1 | H/W Itilima | Ubadhirifu uliokithiri wa fedha za umma na kutokujibu hoja nyingi za ukaguzi - Halmashauri hii ilikuwa na hoja 69 za ukaguzi kwa mwaka 2014/15 lakini ilijibu hoja 18 tu sawa na asilimia 26 na kuacha hoja 51 sawa na asilimia 74 bila majibu. |
| 2 | H/W Nyasa | Kitabu cha LAAC kilichowasilishwa mbele ya Kamati kwa mahojiano kilikuwa ni tofauti na kile kilichowasilishwa awali kwa CAG kwa mapitio. |
| 3 | H/W Hanang' | Hoja nyingi za ukaguzi hazikuoneshwa katika kitabu cha LAAC hivyo Kamati kushindwa kujua undani wa hoja hizo na kudhibitiwa mawanda ya kuhoji (limited scope). |
| 4 | H/W Korogwe | Hoja za ukaguzi zilizojibiwa hazikuwa zimehakikiwa na CAG na hivyo Kamati kutokuwa na uwezo wa kuhoji kwa mujibu wa Kanuni ya 15 na 16 ya sehemu ya 4 ya nyongeza ya 8 ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016. Kati ya hoja 78 za ukaguzi kwa mwaka 2014/15 ni hoja 4 tu ndizo zilijibiwa na kuhakikiwa na hivyo kuwa sehemu ya taarifa ya Halmashauri). |
| 5 | H/W Ngara | Hoja nyingi za CAG hazikuwa na majibu. |
| 6 | H/W Hai | Hoja nyingi za CAG hazikuwa na majibu. |
| 7 | H/W Rombo | Hoja nyingi za CAG hazikuwa na majibu. |

**Chanzo**: *Matokeo ya uchambuzi wa taarifa za Halmashauri husika zilizowasilishwa kwenye Kamati.*

**Uchambuzi.**

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia vigezo na mambo ya msingi niliyoyataja hapo awali, Uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ulibainisha mambo yafuatayo:-

***Manunuzi yasiyozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011.***


**Mheshimiwa Spika,** Katika baadhi ya Halmashauri ilibainika kwamba baadhi ya manunuzi ya bidhaa na huduma yamefanyika nje ya bajeti ya mwaka husika. Katika Halmashauri nyingine hapakuwa na kamati za ukaguzi wa manunuzi hivyo kutothibitisha kwa ubora na idadi kulingana na thamani ya fedha (value for money). Mfano Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua Mkoani Tabora, katika ujenzi wa Ofisi ya Mkurugenzi na Kituo cha Afya.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini matumizi makubwa na yasiyofuata taratibu za fedha katika ujenzi wa Maabara kwa Shule za Sekondari kufuatia agizo la serikali lililolenga kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundisha katika masomo ya Sayansi.

Maagizo haya ni mazuri, hata hivyo Halmashauri hazikuwa na utaratibu maalum wa kutafuta fedha za kugharamia ujenzi huo, badala yake zilitumika fedha kutoka kasma mbalimbali, bila kufuata utaratibu wa kuhamisha fedha ili kutekeleza agizo hilo, na hivyo kuathiri moja kwa moja shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika Mpango wa Bajeti. Kwa mfano, Halmashauri nyingi zilibainika kuhamisha fedha kutoka katika kasma ya ruzuku za kujenga uwezo wa serikali za mitaa (LGCDG) bila idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali. Kamati inashauri Halmashauri kuhakikisha kwamba Maagizo kutoka ngazi za juu yanatekelezwa kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za Fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Kielelezo Namba 4 kinaonesha jinsi fedha zilivyohamishwa kutoka katika akaunti ya ruzuku za kujenga uwezo wa serikali za mitaa (LGCDG) kwa baadhi ya Halmashauri na kuelekezwa katika ujenzi wa maabara kwa shule za sekondari.

**Kielelezo Namba 4: Mifano ya Halmashauri zilizohamisha fedha kutoka katika akaunti ya LGCDG na kupeleka katika ujenzi wa maabara kwa mwaka wa fedha 2014/15**




**Chanzo**: *Matokeo ya uchambuzi wa taarifa za Halmashauri husika zilizowasilishwa kwenye Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** Kutoka katika kielelezo namba 4 hapo juu, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inaonekana kuhamisha kiasi kikubwa cha fedha ukilinganisha na Halmashauri ya Wilaya ya Hai. Kamati inatoa rai kwamba ukubwa wa Halmashauri (kuwepo na idadi kubwa ya shule za sekondari) au udogo wake (kuwepo na idadi ndogo ya shule za sekondari) hauwezi kutoa fursa ya uhamishaji wa fedha bila idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Halmashauri nyingine palibainika:

i. Kufanyika manunuzi kwa fedha taslimu kinyume na Sheria ya Manunuzi ya Umma, **H/W Nsimbo,**

ii. Manunuzi kufanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni, **H/W Kaliua,**

iii. Fedha kulipwa kwa manunuzi ambayo hayakufanyika (manunuzi hewa) mfano **H/Jiji Mwanza**,

iv. Manunuzi kufanyika bila stakabadhi za kielektroniki (matumizi ya EFD). **H/W Mufindi,**

v. Manunuzi kufanyika kwa kutumia Wazabuni wasio idhinishwa na Halmashauri. **H/W Nachingwea,**

vi. Utekelezaji wa shughuli za Miradi ambayo haipo kwenye Mpango wa Manunuzi wa Mwaka. **H/W Tunduru,**

vii. Hazina kutoa fedha zaidi ya bajeti kwa Halmashauri. **H/W Mpanda**.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2014/15 utekelezaji wa miradi mbalimbali katika Mfuko wa Barabara (Road Fund) katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, malipo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 1.1, yalifanyika kwa Wakandarasi bila kuwa na Hati ya Madai (Tax Invoice). Malipo haya yalifanyika kwa kutumia Cheti cha Madai (Claim Certificate) kutoka kwa Wakandarasi hao. Kimsingi malipo hayo hayakufuata taratibu za fedha.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba, Kamati ya Tathmini iliwaondoa wazabuni waliokuwa na bei ya chini (lowest evaluated bidder) na kusababisha gharama ya ziada ya Shilingi Milioni 106.4 ambayo ingeweza kuepukika. Hii ni kinyume na Kanuni ya 85(1) C ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, za Mwaka 2013.

**Maoni ya Kamati ni kuwa gharama za ujenzi wa maabara katika shule za sekondari zilikuwa ni kubwa na taratibu za fedha hazikufuatwa kikamilifu. Je, Serikali imefanya ukaguzi wa kina kuhusu matumizi hayo?**

Mfano mwingine wa manunuzi yasiyozingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Fedha ni katika mwaka wa fedha 2013/14 ambapo Halmashauri ya Jiji la Mwanza ilifanya manunuzi ya Nyasi Bandia zenye thamani ya Shilingi Milioni 192.3, kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Duniani (FIFA), kwa ajili ya ukarabati wa Uwanja wa Mpira wa Nyamagana lakini hapakuwa na nyaraka za uthibitisho wa manunuzi hayo na nyasi hizo hazikupokelewa.

**Hoja ya Kamati ni Kwamba manunuzi haya ni mlolongo wa ufujaji wa fedha za Serikali za Mitaa na hayana tija kwa kuwa hayakufuata taratibu na sheria zilizopo. Kwa kuwa manunuzi haya yalifanyika kwa kutumia fedha za umma na hakuna uthibitisho wa manunuzi hayo, Je fedha hizo zimekwenda wapi? Nini tamko la Serikali katika suala hili?**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaitaka serikali kuhakikisha kuwa ukaguzi maalum wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) anafanya ukaguzi maalum katika Halmashauri zifuatazo baada ya kubainika kukiuka kwa kiasi kikubwa sheria, kanuni na taratibu za fedha katika kufanya manunuzi ya vifaa na huduma na kuwa na dosari nyingi katika taarifa zake:

**Halmashauri ya Mji Tunduma.**

Katika Halmashauri hii palibainika:

i. Mfumo dhaifu wa udhibiti wa ndani (weak internal control system) uliosababisha matumizi mengi kutofuata Sheria, Kanuni na Taratibu za matumizi ya fedha,

ii. Hapakuwa na taarifa ya Matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo kuanzia mwaka wa fedha 2010/11 hadi 2014/2015, na

iii. Fedha za posho ya vikao zililipwa juu ya kiwango (excessive payment) kiasi cha Shilingi. 288,092,300.00 kwa mwaka wa fedha 2014/15.

**Halmashauri ya Manispaa ya Iringa.**

Katika Halmashauri hii palibainika:

i. Fedha za malipo madogo madogo (petty cash) kiasi cha Shilingi. 203,561,738 zilitumika juu ya kiwango (beyond petty cash limit) kwa mwaka wa fedha 2014/15, na

ii. Fedha zilizotumika katika ujenzi wa machinjio ya Ngelewala na fedha zilizotumika katika kumalizia ujenzi wa machinjio hayo zilizotolewa na mbia katika mradi huo kiasi cha Shilingi Bilioni 1.2, na taratibu zilizotumika kumpata mbia huyo hazikuwa wazi.

**Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema.**

Katika Halmashauri hii palibainika:

i. Mfumo dhaifu wa ukusanyaji wa mapato ya ndani (internal revenue collection system), na kutofuata taratibu za fedha katika kutunza makusanyo ikiwa ni pamoja na kupeleka makusanyo benki kwa wakati. Makusanyo kiasi cha Shilingi Milioni 103.7 hayakupelekwa benki kinyume na sheria, kanuni na taratibu za fedha,

ii. Hundi yenye thamani ya Shilingi Milioni 12.1 ilipokelewa na haikupelekwa benki kwa muda mrefu,

iii. Maduhuli yenye thamani ya Shilingi 74.9 hayakukusanywa kutoka kwa mawakala wa mapato hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2016,

iv. Fedha za madai ya walimu Shilingi Milioni 15.8 hazikulipwa kwa walimu badala yake zilitumika katika matumizi mengine, na

v. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2016 Mradi wa ujenzi wa mabomba ya maji wenye thamani ya Shilingi Bilioni 1.8 haukukamilika.

**Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.**

Katika Halmashauri hii palibainika:

Taratibu zilizotumika katika kumpata Mkandarasi Saram Company Ltd katika zabuni za ujenzi wa ofisi ya Mkurugenzi Shilingi Milioni 868 na kituo cha Afya Shilingi Milioni 349 na utekelezaji wa miradi hazikuwa wazi na hapakuwa na tathmini ya hasara iliyopatikana baada ya kuvunja mkataba.

Kadhalika, Halmashauri za Majiji yafuatayo zifanyiwe ukaguzi maalum kama ifuatavyo:

**Halmashauri ya Jiji la Mbeya.**

Kamati inasisitiza agizo la ukaguzi maalum lililotolewa na Waziri Mkuu katika ujenzi wa soko la Mwanjelwa, Mkoani Mbeya litekelezwe.

**Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam.**

Kusisitiza Ukaguzi maalum ufanyike katika gharama zilizotumika katika mradi wa kiwanda cha nyama (EAMEATCO LTD) kama Ofisi ya Rais TAMISEMI ilivyoagiza tarehe 2 Februari, 2015.

***Udhaifu katika usimamizi wa mikataba na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.***

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuongeza kasi ya maendeleo katika Halmashauri zetu ipo mikataba ya miradi mbalimbali kati ya Halmashauri na Wadau mbalimbali inayohusu ujenzi wa maabara, ujenzi wa barabara, ujenzi wa madarasa, ujenzi wa madaraja, miradi ya maji, na ujenzi wa nyumba za

wafanyakazi. Aidha, ipo baadhi ya miradi ya uwekezaji baina ya Wadau na Halmashauri katika rasilimali za Halmashauri kama vile ardhi, majengo na viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini udhaifu wa watendaji wa baadhi ya Halmashauri nchini unaosababisha:

- Miradi kuchelewa kukamilika,
- Miradi kukamilika ikiwa na kiwango cha chini,
- Fedha za miradi kutumika kwa shughuli nyingine,
- Miradi kukamilika lakini ikabaki haitumiki, na
- Halmashauri kufunga mwaka wa fedha zikiwa na bakaa kubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Baadhi ya mifano katika mwaka 2014/15 ni ujenzi wa Stendi ya Basi Mhuze katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu Mkoani Shinyanga wenye thamani ya Shilingi Milioni 273 ambao haukukamilika kwa wakati. Kadhalika, katika Halmashauri hiyo mradi wa Jengo la OPD Ng'wang'halanga ulikamilika lakini jengo halikuwa likitumika. Sababu za kutotumika kwa jengo hilo zilielezwa kuwa ni kutokuwepo na Choo cha Nyumba ya Daktari. Kamati iliona jambo hili halina mantiki wala hoja yeyote ukilinganisha gharama za mradi, na gharama za ujenzi wa Choo. Kadhalika, ujenzi wa Maabara katika Shule za Sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu wenye thamani ya Shilingi Bilioni 1.43 ulishindwa kukamilika hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2015.

**Mheshimiwa Spika,** Kumekuwepo na kiasi kikubwa kinachobaki kama bakaa ambacho hakitumiki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo hadi kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha husika. Kawaida, utekelezaji wa miradi ya maendeleo huenda sambamba na muda na mtiririko wa fedha kwa kila hatua. Kutokamilika kwa utekelezaji wa miradi kunatoa picha ya uzembe wa Halmashauri katika usimamizi. Kwa mfano; Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2015 Halmashauri ya Jiji la Mbeya, ilikuwa na bakaa ya Shilingi Bilioni 1.1, ambayo haikuwa imetumika katika kasma ya ruzuku ya kujenga uwezo wa serikali za mitaa (LGCDG). Vilevile katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kiasi cha Shilingi Milioni 380 kilichopelekwa katika serikali za mitaa hazikutumika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba sasa nitumie fursa hii kutoa maelezo mafupi kuhusu mradi wa Shirika la Usafirishaji Dar es salaam (UDA).

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) ilifanya kikao cha pamoja na Msajili wa Hazina, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Menejimenti ya

Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam tarehe 28 Oktoba, 2016 kwa lengo la kujua hatma ya mradi na Shirika hilo na usalama wa hisa 7,880,303 zisizotolewa (unallotted shares).

Kamati ilijulishwa kuwa Serikali ilizuia mchakato wa uuzwaji wa hisa zisizotolewa (unalloted shares) uliokuwa ukitaka kufanywa na kampuni ya Simon Group Ltd ambayo ni mbia mwenza wa Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam katika Shirika la Usafiri Dar es salaam (UDA).

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa nia ya Kamati ni kuhakikisha kuwa Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam inaendelea kuwa mwanahisa, na kwamba hisa zisizotolewa ziko chini ya Msajili wa Hazina, Nyaraka zifuatazo zimeombwa kutoka kwa Msajili wa Hazina ili Kamati iweze kuzipitia na kutoa mapendekezo na ushauri kwa Serikali:


1. Memorandum of Association na Articles of Association ya UDA, na
2. Cheti cha Umiliki wa Hisa zisizotolewa (Certificate of owning unallotted shares) ili kujiridhisha na usalama wa hisa hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inafuatilia kwa karibu suala hili na italiweka katika taarifa yake katika kipindi kijacho.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilifanya mahojiano na Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam kuhusu uwekezaji katika Mradi wa Machinjio ya kisasa. Mnamo mwaka 2004 Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam ilianzisha kampuni ya nyama (East Africa Meat Company Limited – EAMEATCO LTD) iliyokusudia kujenga machinjio ya kisasa katika kiwanja cha Kiltex – Gongo la Mboto chenye ekari 63; kiwanja ambacho kilinunuliwa Mwaka 1997 na iliyokuwa Tume ya Jiji la Dar es salaam.

**Mheshimiwa Spika,** Kampuni hiyo ya nyama (EAMEATCO LTD) ilizishirikisha Halmashauri za Manispaa za Ilala, Temeke na Kinondoni kama Wabia, na baadaye walikaribishwa Wabia wengine ambao ni Kampuni ya Rheinhold & Mahla (Malaysia) Sdn Bhd au kwa kifupi R&M na Kampuni ya Uwekezaji ya Taifa, NICOL. Kampuni ya nyama ilikuwa na hisa 7,600 ambapo jumla ya thamani ya hisa katika uwekezaji huu ilikuwa ni Jiji na Manispaa zake Dola za Marekani Milioni 2.5, R&M Dola za Marekani Milioni 3.7 na NICOL Dola za Marekani Milioni 3. Mgawanyo wa hisa ni kama inavyoonekana katika kielelezo namba 5.

**Kielelezo Namba 5:**
**Mgawanyo wa hisa katika mradi wa machinjio ya kisasa.**




**Chanzo**: *Matokeo ya uchambuzi wa taarifa za Halmashauri husika zilizowasilishwa kwenye Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** Mnamo mwaka 2005, Ndg. Benjamini T. Chipazi aliteuliwa na kupewa mkataba wa miaka miwili (2) kuwa meneja wa mradi akiwa Mtaalam kutoka Tume ya Nyama nchini Botswana.

Wanahisa walitakiwa kulipia hisa zao ili ipatikane fedha ya kuanza ujenzi wa machinjio, lakini hadi kufikia mwezi Juni 2009 palikuwa na jumla ya Dola za Marekani 2,005,083 tu sawa na asilimia 21.8 zilizokuwa zimepatikana, huku Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam ikiwa imelipa fedha zake zote wakati mbia R&M akiwa hajalipa kitu.

**Mheshimiwa Spika,** Fedha zilizokusanywa hadi kufikia tarehe 18 Juni, 2010 zilikuwa ni Shilingi 1,771,084,595 na matumizi yakiwa ni Shilingi 1,771,032,781 na hivyo kuacha bakaa ya Shilingi 51,814. Maoni ya Kamati ni kuwa matumizi hayo hayakuwa na tija kwa kuwa fedha zote zilitumika kulipa stahili za Meneja, kugharamia mikutano na matumizi mengine ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika,** Meneja alilipwa mshahara wa jumla ya Shilingi. 532,237,414 sawa na asilimia 30 ya fedha zote zilizokusanywa, huku akilipiwa nyumba ya kuishi jumla ya Shilingi Milioni 40.7, vifaa vya ofisi na samani za nyumbani Shilingi Milioni 10.5 na kibali cha Meneja cha kufanya kazi nchini Shilingi Milioni 2.3. Aidha, palikuwa na malipo mengine

makubwa kama vile gharama za upembuzi yakinifu Shilingi Milioni 240 na gharama za kusafiri na likizo Shilingi Milioni 197.9.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kueleza kwa masikitiko makubwa kwamba mradi huu haukutekelezwa ingawa fedha zote zilitumika. Hii ndio ilikuwa sababu ya Kamati kuhoji matumizi yake katika Taarifa yake kwa Mwaka wa Fedha 2012/13.
Kwa kuwa mali pekee iliyobaki katika mradi huo wa machinjio ya kisasa ni ardhi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inasimamia ardhi hiyo kwa manufaa ya wabia wote.

**Hoja ya Kamati ni kwamba, miradi ya maendeleo inapaswa kusimamiwa kwa ukaribu ili iweze kukamilika kwa wakati na kutumika kama ilivyokusudiwa. Nini tamko la Serikali katika suala hili?**

***Kutotekeleza Maagizo ya Kamati na kutojibu Hoja za Ukaguzi.***

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonyesha kuwa, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2014 Kamati ilikuwa imetoa maagizo 1,146 kwa Halmashauri zilizofika mbele yake, lakini ni maagizo 536 tu, sawa na asilimia 47%, ndiyo yaliyokuwa yametekelezwa kikamilifu. Kadhalika, jumla ya hoja za Ukaguzi zilizotolewa zilikuwa 7,474 lakini zilizojibiwa kwa ukamilifu ni hoja 3,217 tu sawa na asilimia 43%.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2014/15 Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, ilikuwa na Hoja 49 za Ukaguzi ambapo ilijibu Hoja 14 tu (sawa na asilimia 28) na kubakiza Hoja 35 (sawa na asilimia 72) ambazo hazikuwa na majibu. Aidha Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa ilikuwa na Hoja 63 ambapo ilijibu Hoja 17 (sawa na asilimia 27) tu na kubakiza Hoja 46 (sawa na asilimia 54) ambazo hazikuwa na majibu, Halmashauri ya Manispaa Shinyanga ilikuwa na Hoja 58 ambapo ilijibu Hoja 11 tu (sawa na asilimia 19) na kubakiza Hoja 47 (sawa na asilimia 81) ambazo hazikuwa na majibu, na Halmashauri ya Jiji Mbeya ilikuwa na Hoja za Ukaguzi 78 lakini ilijibu Hoja 20 tu (sawa na asilimia 22) na kubakiza Hoja 72 (sawa na asilimia 78) ambazo hazikuwa na majibu.

**Mheshimiwa Spika,** Imekuwa ni kawaida sasa kwa Halmashauri kutekeleza kwa mazoea, kutekeleza kwa kuchelewa, na kutotekeleza kabisa maagizo ya Kamati yako tukufu ya LAAC. Hoja za Ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) hazijibiwi kwa wakati na kwa ukamilifu. Kwa ujumla Halmashauri nyingi katika mwaka 2013/14 na 2014/15 zilibaki na idadi kubwa ya Maagizo yasiyotekelezeka

na Hoja za Ukaguzi zisizojibiwa. Kamati imejiridhisha kuwa Halmashauri zinapuuzia kutekeleza maagizo hayo. Maoni ya Kamati ni kuwa kwa miaka yote miwili ya fedha 2013/14 na 2014/15 hali ya kujibu hoja za ukaguzi na kutotekeleza maagizo ya Kamati, imeendelea kuzorota kwa sababu ya uzembe wa watendaji, kutokuwepo na uwajibikaji wa Menejimenti za Halmashauri au kufanya kazi kwa mazoea.

**Hoja ya Kamati ni kuwa, Hoja za Ukaguzi hulenga kuboresha utendaji wa Halmashauri na Maagizo ya Kamati, hutokana na uchambuzi wa Taarifa na mahojiano baina ya Kamati na Halmashauri kufuatia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kamati inaitaka Ofisi ya Rais – TAMISEMI kueleza sababu za kushindwa kuchukua hatua za kinidhamu kwa Halmashauri, juu ya uzembe wa kutotekeleza maagizo ya Kamati na kutojibu hoja za Ukaguzi kwa ukamilifu na kwa wakati.**

***Halmashauri kutokutenga Mchango wa Asilimia Kumi (10%) ya Mapato kutoka vyanzo vya ndani kwa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana.***

**Mheshimiwa Spika,** Tatizo la Halmashauri kutotenga asilimia kumi (10%) ya makusanyo yake ya mapato kutoka Vyanzo vya Ndani (own sources revenue) kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana limeendelea kutopatiwa tiba ya kudumu. Baadhi ya Halmashauri hazikupeleka michango hii kwa zaidi ya miaka mitatu (3) mfululizo bila kutoa sababu za msingi, nyingine kupeleka kiasi kidogo na baadhi ya Halmashauri hazikufuata utaratibu sahihi wa kukokotoa michango hii.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mchango wa asilimia 10 ya fedha za makusanyo kutoka vyanzo vya ndani, baadhi ya Halmashauri zilibainika kukopesha mtu mmoja mmoja ndani ya kikundi tofauti na utaratibu unaoitaka Halmashauri kutoa fedha kwa kikundi ili kutekeleza shughuli mahsusi ambayo kimsingi huwa katika mpango wa biashara (yaani business plan).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba; Mwaka 1993 Serikali ilianzisha Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana kwa Azimio la Bunge kwa mujibu wa "Exchequer and Audit Ordinance" ya mwaka 1961 kwa kuzingatia kwamba Wanawake na Vijana hawapati mikopo kutoka katika mabenki na mashirika ya fedha kwa sababu mbalimbali, mojawapo ikiwa ni kukosa dhamana ya mkopo na kuwa na mikopo midogo ya kuendesha biashara ndogondogo. Katika mwongozo wa uendeshaji wa mfuko huo

Halmashauri zinatakiwa kuchangia asilimia 10 ya mapato yake ya ndani ili kutunisha mfuko huu na kutoa mikopo kwa vikundi vingi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa na maelezo na sababu zisizoridhisha juu ya Halmashauri kushindwa kutenga fedha za mapato yake ya ndani kwa ajili ya mfuko huu na badala yake kufanya matumizi ambayo yako nje na matakwa ya mfuko. Maoni ya Kamati ni kuwa, kutopeleka michango katika Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana kunapunguza tija ya mfuko huo kwa kuwa unajiendesha kwa mkopo unaojizungusha (loan revolving fund).

Katika jumla ya Halmashauri 164 zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2014/15 Halmashauri 112 hazikuwasilisha mchango wa asilimia kumi (10%) kwa ukamilifu na hivyo kufanya deni kwa mwaka huo wa fedha kwa Halmashauri hizo kufikia Shilingi Bilioni 17.7. Hii inatoa picha kuwa kiasi cha Shilingi Bilioni. 17.7 hakikuelekezwa katika vikundi vya Wanawake na Vijana ili kuboresha na kupanua biashara ndogondogo. Mfano wa Halmashauri hizo ni; **H/W Nkasi, H/M Songea, H/M Mtwara, H/W Singida, H/W Lushoto, H/M Dodoma, H/W Bukoba, H/W Geita, H/W Same, H/W Mbozi na H/W Namtumbo.**

**Mheshimiwa Spika,** Katika vikao vilivyofanyika kuanzia tarehe 15 Agosti, 2016 hadi tarehe 2 Septemba, 2016 hapa Dodoma, Kamati ilitoa agizo kwa Halmashauri 20 ziandike na kuwasilisha barua ya kuthibitisha kulipa deni la Mfuko wa Wanawake na Vijana (commitment letter) na kuandaa mpango wa malipo na kuviwasilisha kwa Mwenyekiti wa Kamati kabla ya tarehe 30 Septemba, 2016. Hata hivyo jambo la kusikitisha ni kuwa hadi kufikia siku ya leo ninapowasilisha taarifa hii Halmashauri 6 hazikutekeleza agizo hilo. Halmashauri hizo ni; **H/W Mpanda, H/W Kishapu, H/W Nsimbo, H/W Tunduru, H/Jiji la Tanga na H/W Ruangwa.** Maoni ya Kamati ni kuwa utekelezaji wa agizo kwa Halmashauri hizo umeendelea kutopewa kipaumbele na inatia shaka iwapo deni la mfuko huo litalipwa.

**Hoja ya Kamati ni kwamba, uwepo wa michango hii unaboresha na kuongeza shughuli za maendeleo kwa Wananchi katika Mamlaka za Chini, Je Serikali haioni sasa kuwa ni wakati muafaka kutunga Sheria na Kanuni zitakazosimamia michango na uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana ili kuongeza uwajibikaji?**

**Mheshimiwa Spika,** Kadhalika kwa mwaka 2014/15 Halmashauri ziliendelea kutochangia mchango wa asilimia kumi (10%) kutoka katika makusanyo ya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana. Kamati ilipotaka kujua sababu za kushindwa kutenga mchango huo hapakuwa na sababu na maelezo ya msingi zaidi ya

kwamba Halmashauri zina upungufu mkubwa wa fedha na kwamba makusanyo hayatoshi kugharamia uendeshaji wa shughuli.

Katika mwaka wa fedha 2014/15 Halmashauri iliyokuwa kinara wa kutotenga asilimia kumi (10%) ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana ni Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni. Halmashauri hii hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2015 ilikuwa na jumla ya deni la Shilingi Bilioni 9 la mfuko huo.

**Kielelezo Namba 6:**
*Baadhi ya Halmashauri ambazo hazikuchangia kabisa mchango wa asilimia kumi (10%) ya mapato yake ya ndani kama ilivyoripotiwa katika taarifa ya CAG kwa mwaka 2014/15 kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana.*

| Na. | Halmashauri | Mapato ya Ndani | Kiasi kilichotakiwa kulipwa mwaka 2014/15 | Kiasi kilicholi-pwa | Jumla ya deni hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2015 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Kalambo | 822,334,649 | 82,233,465 | 0 | 155,214,365 |
| 2 | H/W Tunduru | 1,014,816,055 | 101,481,605 | 0 | 460,462,017 |
| 3 | H/W Mpanda | 2,094,797,488 | 209,479,749 | 0 | 838,453,760 |
| 4 | H/Mji Tunduma | 1,283,765,911 | 128,376,591 | 0 | 203,152,257.00 |
| 5 | H/W Ludewa | 1,496,569,818 | 149,656,981 | 0 | 351,031,468 |
| 6 | H/W Sengerema | 1,451,093,246 | 145,109,324 | 0 | 262,681,300 |
| 7 | H/Jiji Dar es salaam | 571,258,979 | 571,258,979 | 0 | 1,876,480,479.00 |

**Chanzo**: *Matokeo ya uchambuzi wa taarifa za Halmashauri husika zilizowasilishwa kwenye Kamati.*

***Kutokutenga na Kupeleka ruzuku ya asilimia ishirini (20%) kwa ajili ya Serikali za Mitaa na Vijiji.***

**Mheshimiwa Spika,** Upelekaji wa fedha za fidia ya vyanzo vya mapato vilivyofutwa GPG (General Purpose Grant), asilimia ishirini (20%), kwenda katika Serikali za Mitaa na Vijiji haufanyiki kama ilivyoagizwa, hali inayopelekea Halmashauri kuzifanya serikali za mitaa na vijiji kushindwa kujiendesha. Katika Halmashauri 30 zilizohojiwa kwa mwaka 2013/14 na

Halmashauri 36 zilizohojiwa kwa mwaka wa fedha 2014/15 hapakuwa na Halmashauri hata moja iliyotenga na kupeleka mchango huu kwa ukamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** Kielelezo namba 7 kinaonyesha baadhi ya Halmashauri ambazo hazikupeleka fedha ya ruzuku kutoka serikali kuu kwa ajili ya Mamlaka za Chini kuanzia mwaka wa fedha 2012/13 hadi mwaka 2014/15.

**Kielelezo Namba 7:**
*Baadhi ya Halmashauri ambazo hazikupeleka ruzuku kwa ajili ya vijiji na mitaa kwa miaka mitatu mfululizo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2015.*

| Na | Halmashauri | Kiasi kilichotakiwa kupelekwa mwaka 2012/13 | Kiasi kilichotakiwa kupelekwa mwaka 2013/14 | Kiasi kilichotakiwa kupelekwa mwaka 2014/15 | Jumla ya Kiasi ambacho hakikupelekwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2015 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Kilwa | 17,376,224 | 53,530,079 | 13,766200 | 84,672,503 |
| 2 | H/W Ngara | 33,660,933 | 23,091,000 | 2,167,000 | 58,918,933 |
| 3 | H/W Hai | 21,420,908 | 27,681,533 | 11,933,800 | 61,036,241.00 |
| 4 | H/W Rombo | 12,098,216 | 24,137,650 | 9,719,000 | 45,954,866.00 |
| 5 | H/Jiji Dar es salaam | Katika miaka hii hapakuonyeshwa kiasi kilichotakiwa kupelekwa. Taarifa ya CAG kwa mwaka 2014/15 imetoa jumla ya fedha zilizotakiwa kupelekwa kuanzia 2012/13 hadi 2014/15. Sababu iliyotolewa na Halmashauri katika mahojiano ni kuwa Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam haina Vijiji wala Seriksli za Mitaa. | | | 405,019,500.00 |

**Chanzo**: *Matokeo ya uchambuzi wa taarifa za Halmashauri husika zilizowasilishwa kwenye Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** Katika baadhi ya Halmashauri, fedha zilizopelekwa katika Serikali za Mitaa na Vijiji kama ruzuku, zimeonekana kuchanganywa kimakosa na mapato ya ndani kabla ya kutenga asilimia ishirini (20%). Hali hii haitoi picha halisi ya kiasi kamili kinachotakiwa kutengwa na kuwasilishwa. Kwa mfano katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2012/13 hadi 2014/15 **Halmashauri ya Wilaya ya Longido,** ilipaswa

kutenga kiasi cha Shilingi. 93,060,446 lakini ilitenga na kulipa kiasi cha Shilingi. 95,568,961 sawa na asilimia 102.6. Hii ni sawa na kusema kuwa Halmashauri hii ilipeleka fedha zaidi ya kiwango ilichotakiwa kupeleka. Vilevile, **Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara/Mikindani** ilitakiwa kutenga kiasi cha Shilingi 94,356,263.80 kuanzia mwaka wa fedha 2012/13 hadi 2014/15 lakini ilitenga na kulipa Shilingi 109,677,359 sawa na asilimia 116.2 na **Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga** ilitakiwa kutenga kiasi cha Shilingi 16,257,000.00 katika mwaka wa fedha 2014/15 lakini ilitenga na kulipa kiasi cha Shilingi 92,479,163.00 sawa na asilimia 568.8. Halmashauri hizi zinaonekana kupeleka kiwango cha fedha zaidi ya kile kilichotakiwa ingawa hakuna ukweli kwa kuwa mapato ya ndani yamechanganywa na ruzuku kutoka Serikali Kuu.

**Hoja ya Kamati ni kwamba, asilimia ishirini (20%) ya fedha za ruzuku kutoka Serikali Kuu kwenda Vijijini na Serikali za Mitaa ililenga kuvipatia fedha Vijiji na Serikali za Mitaa kufuatia kufutwa kwa vyanzo vya mapato vilivyokuwa na kero. Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka kuwasilisha fedha hizi moja kwa moja kutoka Hazina kwenda Mamlaka za Chini bila kutegemea Halmashauri?**

***Uzembe Katika Ukusanyaji wa Mapato kutoka vyanzo vya ndani.***

**Mheshimiwa Spika,** Pamekuwepo na uzembe katika usimamizi wa ukusanyaji wa Mapato kutoka Vyanzo vya Ndani unaofanywa na Halmashauri kwa Mawakala wa Mapato bila hatua stahiki kuchukuliwa mapema. Hali hii imepelekea;

1. Kiasi kikubwa cha fedha kutokusanywa kwa wakati,
2. Upotevu wa vitabu vya kukusanyia mapato,
3. Mapato kukusanywa na vitabu viwili sambamba,
4. Halmashauri kushindwa kukusanya kabisa mapato yake, na
5. Mawakala wa Mapato kupewa mikataba bila kuweka dhamana (fedha).

Katika mwaka 2013/14 Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto Mkoani Tanga ilishindwa kumchukulia hatua za kinidhamu Afisa Mapato – Ndg. Edwin Kigoda, aliyehamia Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, kwa kushindwa kutoa maelezo ya kutorejeshwa kwa mapato ya Halmashauri kiasi cha Shilingi 36,520,880. Kadhalika mtumishi huyo alishindwa kuwasilisha makusanyo ya Shilingi 65,120,275 ambazo alizikusanya kwa kutumia vitabu viwili kwa wakati mmoja (dublicate books).

**Mheshimiwa Spika,** Halmashauri inaposuasua kukusanya mapato sio tu kwamba inaonyesha kutozingatia makadirio yake, bali kuendelea kuwa tegemezi kwa ruzuku kutoka Serikali Kuu.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2014/15 jumla ya vitabu 814 vya kukusanyia mapato ya ndani kutoka katika Halmashauri 45 havikuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa ajili ya ukaguzi na hivyo CAG kushindwa kujua jumla ya makusanyo hayo. Kadhalika, katika Halmashauri 76, kiasi cha Shilingi Bilioni 5.3 hakikukusanywa kutoka kwa Mawakala wa kukusanya mapato na hivyo kushindwa kutumika katika uendeshaji wa Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini udhaifu katika mfumo wa ukusanyaji wa mapato, na Halmashauri kutegemea chanzo kikuu kimoja tu (kama vile ushuru wa mazao kama korosho, kahawa, tumbaku n.k ambao ni wa msimu); kwa mfano Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba na Nanyumbu mkoa wa Mtwara kutegemea mapato yake kutoka kwenye ushuru wa korosho, na Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama hutegemea mapato yake kutoka kwenye ushuru wa zao la tumbaku peke yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini Halmashauri nyingi kutofanya tathmini ya kina ya vyanzo vya mapato vilivyopo ili kufahamu makusanyo yanayofanywa na Mawakala wa Makusanyo na kuishia kutegemea taarifa kutoka kwa Mawakala. Aidha kwa kutofanya tathmini ya makusanyo na kubuni vyanzo vipya ili kutanua wigo wa mapato, Halmashauri nyingi zimeshindwa kuelewa uwezo wa vyanzo vyake vya mapato ya ndani. Vilevile hakuna utaratibu maalum unaotumika wakati wa kufanya makadirio.

**Mheshimiwa Spika,** Halmashauri ya Wilaya ya Rorya imeonyesha udhaifu mkubwa katika kusimamia makusanyo kutoka vyanzo vya ndani. Katika mwaka wa fedha 2013/14 Halmashauri hiyo ilikadiria kukusanya kiasi cha Shilingi Bilioni 1.9 lakini ilikusanya kiasi cha Shilingi Milioni 618 sawa na asilimia 32 tu. Mwaka uliofuata, 2014/15 Halmashauri hii ilikadiria kukusanya kiasi cha Shilingi Bilioni 1.5 lakini ilikusanya kiasi cha Shilingi Milioni 594 sawa na asilimia 39 tu. Huu ni uzembe mkubwa katika kuhakikisha Halmashauri zinakusanya kiasi kikubwa cha mapato ili kupunguza utegemezi kwa Serikali Kuu.

Kielelezo namba 8 kinaonesha mwenendo wa baadhi ya Halmashauri zilivyokadiria makusanyo kwa mwaka wa fedha 2014/15 na makusanyo halisi kwa mwaka huo huo.

**Hoja ya Kamati ni kwamba, Halmashauri zinapaswa kuongeza ufanisi katika kukusanya mapato kutoka vyanzo vya ndani ili kuondoa utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu katika kutekeleza majukumu yake, Je Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuzibana Halmashauri ili ziongeze ufanisi katika ukusanyaji wa mapato na kuongeza vyanzo vingine?**


**Kielelezo Namba 8:**
*Mwenendo wa baadhi ya Halmashauri zilivyokadiria makusanyo kwa mwaka 2014/15 na makusanyo halisi kwa mwaka huo huo.*

| Na | Halmashauri | Makadirio kwa mwaka 2014/15 | Makusanyo halisi kwa mwaka 2014/15 | Asilimia ya makusanyo kulinganisha na makadirio |
|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Kwimba | 1,945,102,000.00 | 805,117,098.00 | 41% |
| 2 | H/W Itilima | 1,598,071,000.00 | 789,225,139.00 | 49% |
| 3 | H/ Jiji Mbeya | 11,720,472,000.00 | 6,273,510,000.00 | 52.9% |
| 4 | H/Wilaya Mbarali | 3,136,831,968.00 | 2,226,542,834.00 | 70% |
| 5 | H/W Ngara | 845,000,000.00 | 242,168,292.00 | 71% |
| 6 | H/W Rorya | 1,509,500,000.00 | 594,306,844.00 | 39% |

**Chanzo**: *Matokeo ya uchambuzi wa taarifa za Halmashauri husika zilizowasilishwa kwenye Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** Kielelezo namba 9 kinaonesha jinsi Halmashauri 8 zilivyokusanya mapato kutoka vyanzo vya ndani kwa kulinganisha na makadirio kwa mwaka wa fedha 2014/15.

**Kielelezo Namba 9: Mwenendo wa makadirio na makusanyo halisi ya mapato kutoka vyanzo vya ndani kwa Halmashauri 8 katika mwaka wa fedha 2014/15.**




***Chanzo:*** Kielelezo Namba 8.

**Mheshimiwa Spika,** Kielelezo Namba 9 kinaonyesha mwenendo wa makadirio na makusanyo ya mapato ya ndani kwa Halmashauri 8 kwa mwaka wa fedha 2014/15. Halmashauri ya Jiji la Mbeya inaonekana kuwa na makadirio makubwa lakini mapato yake kuwa madogo, wakati huo huo Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa inaonekana kuwa na makadirio madogo na mapato yanayokaribia makadirio. Maoni ya Kamati ni kuwa Halmashauri zinapotegemea mapato yake kutoka chanzo kimoja, ziko katika hatari ya kutofikia malengo kwa kuwa nyingi hutegemea ushuru wa mazao. Kadhalika, usimamizi wa makusanyo na udhibiti dhaifu hupelekea Halmashauri nyingi kuwa na makadirio makubwa na makusanyo halisi kidogo.

***Mfumo dhaifu wa udhibiti wa ndani (weak internal control system).***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati baada ya kufanya mahojiano na Halmashauri ilibaini kwamba usugu katika matumizi mabaya ya fedha za umma kwa kiasi kikubwa unasababishwa na mfumo dhaifu wa udhibiti wa ndani (weak internal control system). Halmashauri inaposhindwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za matumizi ya fedha za umma, kukosekana kwa sera za kudhibiti vihatarishi (risk management policy) na daftari la vihatarishi (risk register), husababisha mapungufu na dosari nyingi katika matumizi na taarifa zake za fedha. Vilevile, baadhi ya Halmashauri zilibainika kutounganishwa katika Mfumo wa Udhibiti wa Fedha, wa EPICOR, au

kuunganishwa lakini kushindwa kufanya kazi kama inavyokusudiwa, hali inayoongeza hatari ya matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Mfumo wa EPICOR umeonekana kuwa na mapungufu katika kutoa baadhi ya taarifa muhimu, na hivyo kulazimisha Halmashauri kuandaa taarifa nje ya mfumo. Maoni ya Kamati ni kuwa mfumo huo umepitwa na wakati kwa kuwa unashindwa kuungana na mifumo mingine muhimu na kutoa taarifa muhimu kama vile; taarifa ya mali (assets report), taarifa ya ulinganifu wa kibenki (bank reconciliation statement), na taarifa ya umri wa madeni (debtors and creditors aging analysis). Kamati imeshindwa kuelewa sababu ya Wizara ya Fedha (Hazina) kushindwa kufanya usimamizi (monitoring) wa mfumo huo na kuruhusu upindishwaji wa taratibu na usalama (system security).

**Mheshimiwa Spika,** Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua haijaunganishwa katika mfumo wa udhibiti fedha wa EPICOR na hivyo hulazimika kwenda Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ili kuandaa taarifa zake. Hata hivyo mfumo huo wa EPICOR katika Halmashauri ya Wilaya ya Urambo haufanyi kazi vizuri na hufikia wakati mfumo huo Wilayani Urambo hushindwa kupatikana kwa siku nzima.

**Kielelezo Namba 10:**
*Baadhi ya Halmashauri zilizokuwa na mfumo wa udhibiti wa fedha wa EPICOR usiofanya kazi vizuri hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2015.*

| Na | Halmashauri | Kuunganishwa/Kuto kuunganishwa | Hali ya Mfumo wa EPICOR |
|---|---|---|---|
| 1 | H/W Kilwa | Imeunganishwa | Haufanyi kazi kama inavyotakiwa; baadhi ya taarifa hazitolewi na EPICOR |
| 2 | H/W Ulanga | Imeunganishwa | Haufanyi kazi kama inavyotakiwa; baadhi ya taarifa hazitolewi na EPICOR |
| 3 | H/W Mbarali | Imeunganishwa | Hautumiki, Halmashauri ina andaa taarifa zake nje ya mfumo. |
| 4 | H/W Mlele | Imeunganishwa | Hautumiki, Halmashauri ina andaa taarifa zake nje ya mfumo. |
| 5 | H/W Kaliua | Haijaungwa | Halmashauri inaandaa taarifa zake nje ya mfumo |

| Na | Halmashauri | Kuunganishwa/Kuto kuunganishwa | Hali ya Mfumo wa EPICOR |
|---|---|---|---|
| 6 | H/W Urambo | Imeunganishwa | Haufanyi kazi ipasavyo. EPICOR haiungani na mfumo wa PLAN-REP |
| 7 | H/W Rorya | Imeunganishwa | Haufanyi kazi ipasavyo. EPICOR haiungani na mfumo wa PLAN-REP na LAWSON. |
| 8 | H/Jiji Arusha | Imeunganishwa | Haufanyi kazi ipasavyo. Baadhi ya taarifa bado zinatolewa nje ya mfumo. |

**Chanzo**: *Matokeo ya uchambuzi wa taarifa za Halmashauri husika zilizowasilishwa kwenye Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaka kujiridhisha na uwezo na uwajibikaji wa Kamati za Ukaguzi za Halmashauri na ikama ya Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, na iligundua kwamba:

1. Halmashauri nyingi zimeonekana kuwa na Kamati za Ukaguzi zisizokuwa na ufanisi, na
2. Kitengo cha ukaguzi wa ndani kutokuwa na vitendea kazi na bajeti kutosha.

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia mfumo dhaifu wa udhibiti wa ndani, uhamishaji wa fedha, bila kufuata utaratibu, kutoka kifungu kimoja kwenda kifungu kingine katika Halmashauri nyingi, imekuwa ni suala la kawaida kabisa, na linaloathiri utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo. Kwa mfano, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2015 Halmashauri ya Wilaya ya Mlele, ilikuwa imehamisha fedha kutoka katika akaunti ya mandeleo kiasi cha Shilingi Milioni 725.9 na kugharamia shughuli ambazo hazikuwa kwenye bajeti ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2014/15, bila idhini Mlipaji Mkuu wa Serikali (Paymaster General).

**Hoja ya Kamati ni kuwa, Mfumo wa Udhibiti wa Ndani unalenga kubaini na kudhibiti kasoro mbalimbali katika matumizi ya fedha za umma na kuhakikisha kuwa Sheria, Kanuni na Taratibu za Fedha zinafuatwa kikamilifu. Serikali ina mpango gani kufuatia Halmashauri nyingi kubainika kuwa na mfumo dhaifu wa udhibiti wa ndani na uhamishaji fedha wa ndani usiozingatia sheria, kanuni na taratibu za fedha?**

***Wakuu wa Idara na Vitengo kukaimu nafasi zao bila kuthibitishwa kwa muda mrefu na baadhi ya wakuu wa idara kutokuwa na uwezo.***

**Mheshimiwa Spika,** Utendaji wa Halmashauri unategemea timu madhubuti ya Wakuu wa Idara na Vitengo mbalimbali. Kamati imebaini kuwa moja kati ya sababu zinazofanya Halmashauri kuwa na utendaji usioridhisha, ni Wakuu wa Idara na Vitengo kukaimu nafasi zao kwa muda mrefu, kinyume na Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma namba 8, ya mwaka 2002.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha kumaimu ni vigumu kwa mtumishi kutoa maamuzi mazito ya kiutendaji kwa maslahi ya Halmashauri yake. Hali hii hupelekea majukumu yote kuwa juu ya Afisa Masuuli na ndipo utendaji wa Halmashauri nzima hushuka, mfano Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam imekuwa na Kaimu Mkuu wa kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kwa zaidi ya miaka 7.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaelewa wazi kuwa mlolongo wa uthibitisho wa wakuu wa idara na vitengo ni mrefu kwa sababu huhusisha zoezi la upekuzi (vetting), hata hivyo mamlaka husika zinapaswa kuharakisha mchakato wa uthibitisho ili kuepuka ucheleweshaji usio wa lazima.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini baadhi ya wakuu wa idara na vitengo kwa baadhi ya Halmashauri, kutokuwa na uwezo wa kutosha kutekeleza majukumu yao. Kamati imeshuhudia wakuu wengi wa idara na vitengo wakishindwa kutoa majibu sahihi na kamilifu mbele ya Kamati na kushindwa na kushindwa kuelewa shughuli zinazofanyika ndani ya idara zao. Kimsingi, Kamati hufanya mahojiano na Halmashauri baada ya kupitia taarifa ya hesabu ya Halmashauri husika ambapo Kamati huamini watendaji wa Halmashauri wanao ufahamu mkubwa juu ya utendaji wa Halmashauri na hoja mbali mbali zilizomo katika taarifa zao. Baadhi ya Halmashauri zilizokuwa na wakuu wa idara walioonyesha udhaifu mkubwa ni **H/W Ngara, H/W Hai, H/W Rombo, H/W Mkalama na H/W Itilima.**

**Maoni ya Kamati ni kuwa, Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi za Wakuu wa Mikoa yote zihakikishe kuwa Halmashauri zinakuwa na wakuu wa idara na vitengo wenye sifa. Maeneo mapya ya utawala wapangiwe wakuu wa idara na vitengo wenye weledi, sifa na uzoefu katika nafasi zao.**

**Kielelezo Namba 11:**
*Idadi ya Watumishi wanaokaimu nafasi zao katika baadhi ya Halmashauri kwa mwaka 2013/14 na 2014/15*

| Na | Halmashauri | Idadi ya Wakuu wa Idara na Vitengo waliokuwa wakikaimu nafasi kwa mwaka 2013/14 | Idadi ya Wakuu wa Idara na Vitengo waliokuwa wakikaimu nafasi kwa mwaka 2014/15 |
|---|---|---|---|
| 1 | H/W Busokelo | 10 | 9 |
| 2 | H/W Msalala | 14 | 12 |
| 3 | H/W Ulanga | 6 | 8 |
| 4 | H/Mji Mpanda | 5 | 5 |
| 5 | H/W Kongwa | 7 | 7 |
| 6 | H/W Urambo | 4 | 3 |

**Chanzo**: *Matokeo ya uchambuzi wa taarifa za Halmashauri husika zilizowasilishwa kwenye Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** Kutoka katika kielelezo namba 11 Halmashauri ya Wilaya ya Msalala imeonekana kuwa na makaimu Wakuu wa Idara na Vitengo wengi kwa miaka yote miwili na kuathiri kwa kiasi kikubwa utendaji wa Halmashauri hiyo. Muundo wa sasa wa Halmashauri nchini una jumla ya Idara na Vitengo kumi na tano (15).

***Fedha za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kuchelewa kutolewa au kutotolewa kabisa na Hazina.***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini ucheleweshwaji uliokithiri wa utoaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka Hazina, Halmashauri kupelekewa fedha pungufu ya bajeti husika, na katika miradi mingine fedha kutotolewa kabisa. Mapungufu haya kwa kiasi kikubwa yanaathiri huduma kwa Wananchi na kuwaacha wakiendelea kuishi maisha magumu. Kamati haikupata maelezo ya kina ya kiini hasa cha tatizo hili hutoka Hazina.

**Kielelezo Namba 12:**

*Mifano ya Baadhi ya Halmashauri ambazo ambazo hazikupelekewa fedha za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2016.*

| Na | Halmashauri | Mradi | Kiasi |
|---|---|---|---|
| 1 | H/W Ludewa | Ruzuku kwa ajili ya kujenga uwezo wa serikali za mitaa (LGCDG) | 514,981,600 |
| 2 | H/W Mbarali | Ruzuku kwa ajili ya kujenga uwezo wa serikali za mitaa (LGCDG) | 1,834,401,600 |
| 3 | H/W Mkalama | Ruzuku kwa Shule za Msingi (Capitation Grant) | 127,594,384 |
| 4 | H/W Tunduru | Mfuko wa Barabara (Road Fund) | 945,935,673 |
| 5 | H/W Itilima | Mfuko wa Barabara (Road Fund) | 435,313,795 |
| 5 | H/W Mpanda | Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP) | 209,641,000 |
| 6 | H/W Ulanga | Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP) | 250,706,104 |

**Chanzo**: *Matokeo ya uchambuzi wa taarifa za Halmashauri husika zilizowasilishwa kwenye Kamati.*

**Kamati imesikitishwa kwa kucheleshwa na kutotolewa kabisa fedha za miradi ya maendeleo. Hoja ya Kamati ni kwamba, miradi ya maendeleo inalenga kuwahudumia Wanachi wa eneo husika na huwa na bajeti zake na mpango wa utekelezaji katika muda maalum. Kamati inataka maelezo ya kina ya Serikali juu ya suala hili na Kamati inasisitiza Serikali kupeleka fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati kama zilivyopitishwa na Bunge katika bajeti kwa mwaka husika.**

## SEHEMU YA TATU

## MAPENDEKEZO YA KAMATI

### Maelezo ya jumla.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kutoa maelezo ya kina kuhusu yaliyojiri katika mijadala na Halmashauri 66, Halmashauri 30 kwa mwaka 2013/14 na Halmashauri 36 kwa mwaka 2014/15, zilizoitwa mbele ya Kamati, sehemu hii ya tatu na ya mwisho ya Taarifa itatoa Maoni na Mapendekezo Nane (8) kwa ajili ya kuliomba Bunge lako Tukufu liyajadili na kuyaafiki ili yawe Maazimio ya Bunge kwa ajili ya kuchochea nidhamu ya matumizi ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa.

Mapendekezo haya yanatolewa kwa kuzingatia maeneo yenye Matatizo Sugu ya matumizi mabaya ya Fedha za Umma katika Serikali za Mitaa.

**Mapendekezo.**

**Mheshimiwa Spika,** Naomba sasa nitoe mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

***Manunuzi yasiyozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma.***

***Kwa kuwa,*** imebainika kwamba Halmashauri zilizonyingi hazifuati Sheria ya Manunuzi ya Umma katika manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali,

***Na kwa kuwa,*** kutozingatia masharti ya Sheria ya Manunuzi kunazisababishia hasara Halmashauri nyingi nchini na kuzipunguzia uwezo wa kutoa huduma bora kwa Wananchi,

***Kwa hiyo basi,*** Bunge linaazimia kuwa Serikali:

a) Itoe taarifa ya hatua zilizochukuliwa kwa watumishi wa baadhi ya Halmashauri kwa kushindwa kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma.

b) Ieleze Mpango Mkakati uliopo, unaotekelezeka, katika kuhakikisha Halmashauri zinazingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma.

c) Ihakikishe kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) anafanya Ukaguzi Maalum katika Halmashauri zilizokuwa na dosari katika ununuzi wa vifaa na huduma mbalimbali kwa mwaka 2014/15.

***Udhaifu katika usimamizi wa mikataba na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.***

***Kwa kuwa,*** kumekuwa na udhaifu mkubwa katika usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo unaosababisha miradi kutokamilika katika kiwango kinachotakiwa, kukamilika na kushindwa kutoa huduma kwa Wananchi, au kutelekezwa kabisa;

***Na kwa kuwa,*** udhaifu huo husababisha upotevu wa fedha zilizotumika kufuatia kiwango kidogo cha utekeleaji na kuongezeka kwa gharama za miradi kutokana na kuanza upya kwa mchakato wa kuwapata wazabuni,

***Kwa hiyo basi,*** Bunge linaazimia kuwa Serikali itoe maelezo ya kina na sababu za miradi mingi kutekelezwa kinyume na matarajio na mkakati wa kuhakikisha uchelewaji wa kupeleka fedha hautokei tena.

***Kutotekeleza Maagizo ya Kamati na kutojibu Hoja za Ukaguzi.***

***Kwa kuwa,*** baadhi ya Halmashauri nchini hazikutekeleza maagizo ya Kamati na kutokujibu hoja za ukaguzi kwa wakati, kinyume na masharti ya kifungu 31 (1) – (3) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma namba 11 ya mwaka 2008, tatizo ambalo linazidi kuota mizizi na kuendelea kuonekana katika Taarifa ya Ukaguzi mwaka hadi mwaka,

***Na kwa kuwa,*** tatizo hilo linasababisha Halmashauri hizo kuendelea kukiuka sheria, kanuni na taratibu za fedha, hivyo kutozingatia matakwa ya utawala bora kwenye matumizi ya fedha za umma,

***Kwa hiyo basi,*** bunge lako Tukufu linaazimia kuwa Serikali:

a) Itoe sababu na kueleza Mkakati wa kuondokana na mrundikano wa hoja za ukaguzi na maagizo ambayo hayajafanyiwa kazi kama ilivyobainika kwa baadhi ya Halmashauri.

b) Ieleze njia mbadala ya kuzibana Halmashauri zinazoshindwa kujibu Hoja za Ukaguzi, na kutekeleza maagizo ya Kamati kwa wakati.

***Halmashauri kutokutenga Mchango wa Asilimia Kumi (10%) ya Mapato kutoka vyanzo vya ndani kwa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana.***

***Kwa kuwa,*** imebainika kuwa Wakurugenzi wa baadhi ya Halmashauri kutochangia michango ya asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani kwa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana kwa wakati au kutochangia kabisa; na kuwa upelekaji wa fedha za ruzuku kutoka serikali kuu (asilimia 20) kwa Vijiji na Mitaa haufanyiki ipasavyo,

***Na kwa kuwa,*** kukosekana kwa michango ya asilimia kumi inayotakiwa kupokelewa na mfuko wa wanawake na vijana kwenye halmashauri nchini, kunasababisha mfuko kushindwa kujiendesha, jambo linalochangia vikundi vya wanawake na vijana kushindwa kuendesha biashara ndogondogo na hivyo kuathiri maisha yao,

***Kwa hiyo basi,*** Bunge linaazimia kuwa Serikali ilete Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana, kwa kuwa waraka uliopo hautekelezwi ipasavyo.

***Kutokutenga na Kupeleka ruzuku ya asilimia ishirini (20%) kwa ajili ya Serikali za Mitaa na Vijiji.***

***Kwa kuwa,*** uchambuzi wa Tarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mahojiano kati ya Kamati na Menejimenti za Halmashauri 66 umeonesha kuwa Halmashauri nyingi nchini hazipeleki asilimia ishirini (20%) ya ruzuku za fidia ya vyanzo vya mapato vilivyofutwa GPG (General Purpose Grant), kwenda Vijijini au kwenye serikali za mitaa kama ilivyoagizwa,

**Na kwa kuwa,** Halmashauri hizo zinaposhindwa kupeleka fedha za ruzuku kama ilivyoagizwa zinasababisha serikali za mitaa na vijiji kushindwa kujiendesha, na hivyo kushindwa kutoa huduma ipasavyo kwa Wananchi,

***Kwa hiyo basi,*** Bunge linaazimia kuwa Serikali:

a) Itathmini namna bora ya kuwasilisha asilimia ishirini ya fedha za ruzuku kwa ajili ya Vijiji, ikiwa ni pamoja na kuzipeleka fedha hizo moja kwa moja Vijijini na Serikali za Mitaa kutoka Hazina;

b) Ihakikishe kuwa Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam inachangia michango hiyo, tofauti na kisingizio kwamba haina Vijiji wala Mitaa.

***Uzembe katika kusimamia mfumo wa makusanyo ya ndani.***

***Kwa kuwa,*** Halmashauri zote zimebainika kuwa na uzembe na udhaifu katika kusimamia Mfumo wa Ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vya ndani;

***Na kwa kuwa,*** uzembe huo husababisha Halmashauri kukusanya makusanyo kidogo na kuendelea kuwa tegemezi kwa ruzuku kutoka Serikali kuu;

***Kwa hiyo basi***, Bunge linaazimia kuwa Serikali ieleze mkakati wake katika kuhakikisha Halmashauri zinakusanya mapato kulingana na malengo yao na zinakuwa na vyanzo mbadala vya mapato.

***Mfumo dhaifu wa udhibiti wa ndani (weak internal control system).***

***Kwa kuwa,*** imedhihirika kuwepo kwa udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani kunasababisha dosari nyingi katika taarifa za fedha za Halmashauri, ukusanyaji hafifu wa makusanyo ya maduhuli na matumizi mabaya ya fedha,

***Na kwa kuwa,*** udhaifu wa mfumo wa udhibiti wa ndani unachangia kukosekana kwa uhalisia katika taarifa za fedha, upotevu wa makusanyo na utekelezaji mbovu wa bajeti za miradi,

***Kwa hiyo basi,*** Bunge linaazimia kuwa Serikali iandae mkakati wa kuimarisha kitengo cha ukaguzi wa ndani kwenye halmashauri zote nchini hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2017/18.

***Wakuu wa Idara na Vitengo kukaimu Nafasi zao kwa muda mrefu bila kuthibitishwa.***

***Kwa kuwa,*** imebainika kuwa baadhi ya Wakuu wa Idara na Vitengo katika Halmashauri nchini wanakaimu nafasi zao kwa kipindi kirefu,

***Na kwa kuwa,*** katika kipindi cha kumaimu ni vigumu kwa Mkuu wa Idara/Kitengo kutoa maamuzi mazito ya kiutendaji kwa maslahi mapana ya Halmashauri, hali inayosababisha utendaji wa Halmashauri nzima kushuka,

***Kwa hiyo basi,*** Bunge linaazimia kuwa Serikali:

a) Ileze sababu ya baadhi ya Halmashauri kuwa na Wakuu wa Idara na Vitengo wanaokaimu nafasi zao kwa muda mrefu;

b) Ieleze Mkakati uliopo katika kuhakikisha kuwa nafasi zote zinazo kaimiwa zinakuwa na watumishi waliothibitishwa,

c) Iache kupeleka Wakuu wa Idara na Vitengo wasio na uzoefu katika maeneo mapya ya utawala kwa kuwa Halmashauri hizi zinakuwa na changamoto nyingi katika kipindi cha mwazo.

***Fedha za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kuchelewa kutolewa au kutotolewa kabisa na Hazina.***

***Kwa kuwa,*** imebainika kuwa fedha za miradi ya maendeleo hazitolewi kwa wakati kwa mujibu wa bajeti iliyopitishwa na Bunge,

***Na kwa kuwa*** uchelewaji katika kutoa fedha hizo husababisha miradi kutotekelezwa kwa wakati na hivyo kuathiri moja kwa moja huduma iliyotarajiwa kutolewa kwa Wananchi,

***Kwa hiyo basi,*** Bunge linaazimia kuwa Serikali ieleze kwa kina sababu za kushindwa kupeleka fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri na iweke wazi mkakati endelevu wa kuepuka uchelewaji huo.

## SEHEMU YA NNE

## HITIMISHO

### Shukurani.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 15 ya Nyongeza ya 8 sehemu ya 4, ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati inatekeleza majukumu yake kutokana na taarifa ya ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka husika. Katika kutekeleza majukumu yake kufuatia taarifa ya CAG kwa mwaka wa fedha 2013/14 na 2014/15 Kamati ilikumbwa na changamoto kubwa ya kibajeti na kulazimika kufanya mahojiano ya mezani, ya ana kwa ana tu, badala ya kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo na kufanya mahojiano ya mezani.

Kadhalika, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilikumbwa na changamoto za kibajeti iliyosababisha kushindwa kutembelea baadhi Halmashauri katika kuthibitisha majibu ya hoja mbalimbali za ukaguzi, kwa mfano Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ilirudishwa na Kamati kwa kushindwa kuweka hoja za ukaguzi katika kitabu cha LAAC kwa kuwa hazikuhakikiwa na CAG. Pia Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kutokana na ufinyu wa bajeti ilikumbana na changamoto katika kujiandaa kwa vikao vya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Nichukue fursa hii kumshukuru Mungu kwa kutupa nguvu na kuweza kutimiza majukumu yetu ya kibunge. Natoa shukrani zangu za dhati kwako kwa namna ambavyo umekuwa ukitoa Miongozo mbalimbali ya kusaidia ufanisi katika utendaji wa Kamati ya LAAC. Nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati yangu kwa kutekeleza vyema na kwa ustadi mkubwa, Majukumu yao bila kuchoka. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ushirikiano mkubwa waliouonyesha katika kipindi cha Majadiliano baina ya Kamati na Halmashauri, kwa hesabu za mwaka wa fedha 2013/14 na 2014/15.

**Mheshimiwa Spika,** Namshukuru sana Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah na Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athumani Hussein kwa ufafanuzi wa mambo mbalimbali ya uendeshaji wa shughuli za Kibunge kila tulipowahitaji. Aidha, nichukue fursa hii kumshukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Watumishi wote wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Taarifa ya Ukaguzi na ufafanuzi wa kina tulioupata katika kipindi chote cha Mahojiano na Halmashauri, na pia Ofisi ya Rais TAMISEMI na Hazina, kwa ushirikiano wao mkubwa wakati wote wa vikao vya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa niaba ya Kamati yangu, nachukua fursa hii kuwapongeza Makatibu wa Kamati hii Ndg. Dismas Muyanja na Ndg. Godfrey Kassanga, na Msaidizi wao Ndg. Waziri Kizingiti, pamoja na Watumishi wote kutoka Idara ya Taarifa rasmi za Bunge (Hansard) kwa ushirikiano wao wakati wote wa vikao Kamati yangu ilipowahitaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) inaundwa na Wajumbe 24, kama yalivyoorodheshwa kwenye taarifa yetu:

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Vedasto Edgar Ngombale | **Mwenyekiti** |
| 2. Mhe. Abdallah Dadi Chikota, Mb | **Makamu Mwenyekiti** |
| 3. Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mb | Mjumbe |
| 4. Mhe. Rose Kamili Sukum, Mb | Mjumbe |
| 5. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| 6. Mhe. Amina Nassoro Makilagi, Mb | Mjumbe |
| 7. Mhe. Lucy Mayenga, Mb | Mjumbe |
| 8. Mhe. Godfrey William Mgimwa, Mb | Mjumbe |
| 9. Mhe. Nimrod Mkono, Mb | Mjumbe |
| 10. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb | Mjumbe |
| 11. Mhe. Ignas Aloyce Malocha, Mb | Mjumbe |
| 12. Mhe. Aysharose Ndogholi Matembe, Mb | Mjumbe |
| 13. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb | Mjumbe |
| 14. Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza, Mb | Mjumbe |
| 15. Mhe. Mangungu Ali Issa, Mb | Mumbe |
| 16. Mhe. Martin Mtonda Msuha, Mb | Mjumbe |
| 17. Mhe. Edward Franz Mwalongo, Mb | Mjumbe |
| 18. Mhe. Alex Raphael Gashaza, Mb | Mjumbe |
| 19. Mhe. Joseph Raman Selasini, Mb | Mjumbe |
| 20. Mhe. Jackline Ngonyani Msongozi, Mb | Mjumbe |
| 21. Mhe. Mgeni Jadi Kadika, Mb | Mjumbe |
| 22. Mhe. Richard Phillip Mbogo, Mb | Mjumbe |
| 23. Mhe. John Peter Kadutu, Mb | Mjumbe |
| 24. Mhe. Azza Hamad Hillal, Mb | Mjumbe |

Aidha, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Mhe. George Simbachawene, Mb., na Naibu Waziri katika Wizara hiyo Mhe. Suleiman Jafo, Mb., hushiriki katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati kama Mawaziri wenye dhamana katika eneo husika kwa nyakati tofauti.

**HOJA**

**Mheshimiwa Spika,** Nimalizie kwa kusema kwamba, Kamati yangu imebainisha Matatizo Sugu katika Matumizi ya Fedha za Umma katika Halmashauri zetu katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2013/14 na muendelezo wake katika mwaka 2014/15. Aidha, Kamati imetoa Mapendekezo dhidi ya matatizo hayo kama suluhisho. Kwa maana hiyo sasa, ni Wajibu wa Serikali katika kujipanga vema kutekeleza ushauri huo bila kutegemea usimamizi wa karibu wa Kibunge. Baada ya kufanya uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Ukaguzi, ni rai ya Kamati kwa Halmashauri kujitathmini na kutambua nafasi zao katika ujenzi wa Uchumi na Maendeleo ya Taifa letu kwa ujuml. Ni imani ya Kamati kuwa Halmashauri zetu zitatimiza wajibu wao ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kusema hayo, NAOMBA KUTOA HOJA

…………………………………………

Mhe. Vedasto Edgar Ngombale Mwiru ,Mb.

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YAHESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC)**

9 Novemba, 2016

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kamati zetu mbili zimemaliza mawasilisho. Kwa hiyo, tutaendelea sasa na uchangiaji, lakini kwa muda tuliobaki nao, tutakuwa na wachangiaji wawili na baadaye jioni tutakapokutana nitataja majina kabla hatujaahirisha Bunge ili tujue nani wanafuata. Kwa wakati huu nitaanza na Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, atafuatiwa na Mheshimiwa George Lubeleje.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu wa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya mwanzo kuchangia hoja hii. Kwanza niseme kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC* na kwa sababu hiyo mengi nitakayozungumza yatahusu maoni na mapendekezo ya Kamati yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema tu kwamba, matatizo mengi ambayo tumeyaona katika ukaguzi yanafanana kwa halmashauri zote. Nipende kuzungumza zaidi maeneo yanayohusu fedha za Serikali ambazo zinapelekwa katika Halmashauri zetu. Karibu halmashauri zote nchini, zinakabiliwa na tatizo la kutopata fedha za maendeleo kutoka Hazina kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili ni kubwa kiasi kwamba, karibu katika halmashauri zote, kuna miradi ya maendeleo au haijakamilika au iko nusunusu na kwa kweli karibu halmashauri zote zina madeni yanayotokana na wakandarasi kutolipwa fedha zao kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kucheleweshwa kwa fedha hizi kwenda kwenye halmashauri, hakuna sababu yoyote ambayo katika ukaguzi tumeambiwa, ambayo Hazina wanazieleza halmashauri na ndiyo maana tungependa kusikia kama Bunge, Waziri wa Fedha atuambie tatizo linaloikumba Hazina kutopeleka fedha kwa wakati kwenye halmashauri ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Halmashauri kuna matatizo makubwa sana ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Tatizo la maji ambalo Wabunge wote tunalizungumza, kiini chake ni kwamba, baadhi ya miradi inayosimamiwa na Halmashauri haitekelezeki kwa sababu ya madeni. Siyo hilo tu, tatizo ambalo tunalipata la ukarabati wa miundombinu ya elimu, ukarabati wa barabara na kadhalika linatokana na shida hii hii ya Hazina kutopeleka fedha kwa wakati. Kwa hiyo ili kuzisaidia halmashauri zetu, ni lazima utaratibu uangaliwe wa kusaidia hizi halmashauri ziweze kutekeleza bajeti zake kwa Hazina kupeleka fedha kwa wakati katika halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ambalo ni kubwa na linakabili halmashauri zote ni Maafisa Masuuli kuhamisha fedha za miradi ya halmashauri bila kufuata taratibu za fedha. Tatizo hili ni kubwa zaidi, kw sababu maagizo ya Viongozi Wakuu na Viongozi wa Mikoa na Wilaya yanakwenda kwa Wakurugenzi wakati kukiwa hakuna fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili naomba nilieleze, halmashauri nyingi zimekuja mbele yetu, zimekumbana na tatizo hili, lakini ukiwauliza watakwambia tulikuwa tunatekeleza agizo la Rais kutengeneza madawati. Tumehamisha, tulikuwa tunatekeleza agizo la Rais, kujenga maabara. Maagizo haya yamesababisha uchochoro mkubwa sana wa wizi wa fedha za umma. Kwa sababu sasa fedha zinahamishwa bila utaratibu, bila kibali, bila maombi maalum, lakini ikuliza unaambiwa tulikuwa tunatekeleza maagizo ya kiongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maagizo ya Mheshimiwa Rais, inavyoelekea na Marais wengine huko Mikoani, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na wenyewe wameingia katika utaratibu huu huu wa kutoa maagizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo linalokumbwa zaidi na uchotaji wa fedha hizi ni asilimia 10, fedha zinazopaswa zitengwe kutokana na *own source* ya Halmashauri kwa vijana na akinamama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, agizo hili la kutenga asilimia 10 kwa ajili ya akinamama na vijana ni agizo zuri na lengo lake lilikuwa ni kuwasaidia akinamama na vijana kuweza kujiajiri. Vijana wengi wanaotoka vijijini kuja mijini wanakuja kwa sababu katika vijiji hawana kitu cha kufanya, wanajua kwamba, kule mijni ndiyo kuna kila kitu. Sasa kila Afisa Masuuli anayeulizwa ni kwamba, fedha za Mfuko huu wa Vijana na Akinamama zimekwenda kujenga maabara, zimekwenda kutengeneza madawati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kushangaza ziko Halmashauri ambazo zimetekeleza agizo hili bila kutumia fedha hizi. Kuna Halmashauri ambazo Wakurugenzi wake wamewahamasisha wananchi wamechanga kuku, mazao, wametekeleza agizo hili. Zile halmashauri ambazo Wakuu wake wamekaa hawatafakari, hawafanyi utaratibu wa ubunifu wa namna ya kutekeleza agizo hili ndiyo kwa kiasi kikubwa akinamama na vijana wa maeneo hayo, fedha zao zimechukuliwa kwa ajili ya kutekeleza haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kuna halmashauri nyingi ni maskini kwa maana zile fedha zenyewe haziwatoshi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi yao ya maendeleo na kwa sababu fedha kutoka Hazina haziji wanaingia kwenye ushawishi wa kutumia hizi fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana tukasema lazima tuangalie utaratibu mwingine wa namna ambavyo fedha hizi vitawafikia akinamama na vijana kwa sababu lengo la kuwafikia akinamama na vijana bado lipo na litaendelea kuwepo na tunasema lazima miradi hii iboreshwe ili vijana wapate namna ambavyo wanaweza kujiajiri. Kwa sababu tunavyoona ni kwamba, uwezo wa Serikali hata na wa sekta binafsi kuwaajiri vijana wote na akinamama wote ni mgumu. Kwa hiyo, kama Serikali itaimarisha huu Mfuko kwa ajili ya kuwawezesha hawa vijana ni jambo jema, tena ni jema kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo fedha zinatumika vibaya ni ile asilimia 20, ambayo inatokana na kufutwa kwa vile vyanzo vya mapato ambavyo halmashauri zote zilikuwa zinatumia. Fedha hizi zinatoka Hazina moja kwa moja zinakwenda halmashauri ili halmashauri izitumie kwa ajili ya kupeleka kwenye kata na kwenye vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri nyingi fedha hizi haziendi vijijini na wote tunafahamu jinsi ambavyo Viongozi wetu wa Vijiji, Viongozi wetu wa Kata wanavyofanya kazi katika mazingira magumu. Sasa hata hizi fedha ambazo Serikali kwa makusudi mazima iliamua ili kuwasaidia hawa ili kuweza kufanya kazi vizuri hazifiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hii asilimia 20 hakuna utetezi, vitabu vyote tulivyokagua, Hazina wanapeleka hizi fedha, lakini hizi fedha zikifika kwa Wakurugenzi wanazitumia jinsi ambavyo wao wanaona inafaa. Ndiyo maana kama umesikia hotuba yetu tumependekeza kwamba, Serikali itafute njia nyingine ya kupeleka hizi fedha zisipitie kwa Wakurugenzi ikiwezekana ziende moja kwa moja kwenye kata au ziende moja kwa moja kwenye vijiji, kama vile fedha kwa ajili ya elimu zinavyokwenda kwenye shule zinazohusika moja kwa moja.Vinginevyo, hili tatizo litaendelea kusumbua na wananchi hawatapata faida na hizi fedha hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la mwisho, ambalo ningependa kulizungumza, ni kuhusu Sheria ya Manunuzi. Hili tumelipigia kelele katika Bunge lililopita na hata katika Bunge hili tumeendelea kulizungumza, ni vizuri Sheria ya Manunuzi ikaletwa kufanyiwa mapitio. Kwa sababu mpaka dakika hii kuna vifaa ambavyo vinaweza vikanunuliwa kwa bei ya soko lakini kwa sababu tu kwamba mkandarasi ametafutwa, bei ya vile vifaa inabadilika inakuwa mara mbili au mara tatu ya bei ya vifaa ambavyo viko sokoni, kwa hiyo, eneo hili linaziumiza halmashauri. Fedha ambazo zingeweza zikafanya kazi kiwango cha kuridhisha zinapunguzwa kutokana na matumizi mabaya ya Sheria ya Manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni ushauri wa Kamati kwamba, kwa sababu eneo hili litaendelea kusumbua, ni vizuri Sheria ya Manunuzi ikaangaliwa ili vile vifaa ambavyo vinaweza vikanunuliwa kwa bei ya soko, sheria ielekeze ili kupunguza mianya ya wizi inayotokana na matumizi mabaya ya hii sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ni pendekezo; tumeongea na Wakurugenzi wetu na tulichogundua ni kwamba Wakurugenzi wengi sasa hivi ambao tunaongea nao, hawa wapya, maana huu ukaguzi ni ukaguzi uliotokana na hesabu za 2012/2013 – 2013/2014, sasa tutakwenda kwenye ukaguzi wa mwaka 2014/2015 na 2015/2016, ni vyema TAMISEMI ikaangalia uwezekano wa kukaa na hawa Wakurugenzi kuwapa kama semina hivi. Hili tumelisema sana, naomba lisibezwe, Wakurugenzi wengi tuliokaa nao uwezo wao ni mdogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashauri kwa nia nzuri, uteuzi umeshafanyika, sisi hatuna mamlaka ya kuwaondoa lakini tunawashauri, hawahawa mliowateua kama mnaona wanafaa vizuri, lakini tafuteni namna ya kuwapa semina, namna ya kuwaongoza ili waweze kujua namna ya kutenda kazi, kwa sababu Wakurugenzi wengine hata taratibu za namna ya kuendesha Serikali hawajui, kwa hiyo ni kwa nia nzuri tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vinginevyo, ukaguzi unaokuja tunakwenda kuona hoja nyingi zaidi za ukaguzi kwa sababu ndogo tu kwamba, Wakurugenzi hawana uwezo wa kusimamia halmashauri a, wengine wako *rigid* hawataki kusikiliza ushauri kutoka kwa wakuu wa idara waliowakuta pale, wengine wanafikiri wanajua zaidi kuliko wale waliowakuta, wengine walikuwa wanaendesha *NGOs* zao huko sasa wamekuja kwenye utumishi wa Serikali wanafikiri uendeshaji wa halmashauri ni sawasawa na uendeshaji wa *NGOs* zao kumbe ni vitu viwili tofauti. Kwa hiyo, sisi tunawashauri kwa nia njema kabisa ni vizuri TAMISEMI wafanye semina ya hawa Wakurugenzi waweze kuongezewa uwezo wa kufanya kazi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja zilizotolewa na Kamati zetu za Fedha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Selasini. Mheshimiwa George Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hizi Kamati mbili. Niwapongeze Wenyeviti wa Kamati na Wajumbe kwa kazi nzuri. Naomba nianze na hili, kwamba Bunge ni mhimili unaojitegemea na sisi Wabunge kazi yetu ni kuisimamia Serikali, lakini hatuwezi kuisimamia Serikali kwa kupata taarifa tu kutoka kwenye taasisi mbalimbali bila kutembelea miradi ya maendeleo, huko sio kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, safari hii tumeshindwa kabisa kwa sababu Bunge halina fedha. Sasa nauliza, tulikuwa na Mfuko wa Bunge, huo Mfuko wa Bunge tulikuwa na fedha, je, Mfuko wa Bunge aliyeuondoa nani? Kwa sababu Mahakama wana Mfuko wao, Serikali na Bunge lilikuwa na Mfuko wake. Kwa hiyo, Bunge lazima liwe na fedha za kutosha kuwawezesha Wabunge, Kamati kutembelea miradi, huku ndiko kuisimamia Serikali. Hatuwezi kuisimamia Serikali kila siku tunakaa Dodoma kwenye Kamati, eti tunasubiri wataalam waje watoe taarifa, hapana, lazima tuisimamie Serikali kwa kutembelea miradi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, mwezi wa Sita tumepitisha bajeti ya Serikali, lakini cha kushangaza sasa hivi wilayani hakuna fedha ambazo zimepelekwa kule, hakuna kabisa. Hakuna barabara inayotengenezwa, hakuna kisima kinachochimbwa, kwa mfano kwangu pale Wilaya ya Mpwapwa, kuna vituo vya afya viwili, Kituo cha Afya cha Mima pamoja na Kituo cha Afya cha Mbori, ni muda mrefu, miaka 10 havijakamilika vituo vile, ni kwa sababu fedha hazipo. Sasa mwaka huu vile vituo vimetengewa, kwa mfano Mima imetengewa milioni 25, lakini hizo fedha sijui kama zimeshapelekwa au hazijapelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kituo cha Afya Mbori kimetengewa milioni 20, sijui kama pesa zimeshapelekwa au hazijapelekwa, ni miaka 10 havijakamilika. Akinamama wajawazito wanapoteza maisha kwa sababu ya usafiri kutoka Mima kwenda Mpwapwa. Kwa hiyo, naiomba Serikali, pamoja na matatizo, haya mazingira magumu ya ufinyu wa bajeti lakini fedha zipelekwe kwenye halmashauri zetu ili miradi hii iweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, kuhusu utendaji wa halmashauri, halmashauri zinafanya kazi katika mazingira magumu. Halmashauri zilikuwa zinapata fedha toka TAMISEMI kwa ajili ya fidia, kwa sababu halmashauri zilikuwa zinakusanya kodi, kwa mfano kodi ya mafuta, kodi ya hoteli, Serikali kuu ilikuwa ndiyo inayokusanya na sasa kodi ya majengo inakusanya *TRA*. Kwa hiyo, tunaomba kama *TRA* watakusanya hiyo kodi, basi wapeleke hizi fedha haraka, wasikae nazo mpaka halmashauri tuanze kudai tena, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine asilimia 20; vijiji vina miradi mbalimbali, sasa vijiji vimekwama kutekeleza miradi yao kwa sababu hawana fedha na wanategemea hii asilimia 20, lakini asilimia 20 haiwezi kupelekwa vijijini kwa sababu halmashauri hazina fedha. Halmashauri nyingi hazikusanyi vizuri mapato ya ndani, usipokusanya mapato ya ndani huwezi kupeleka hii asilimia 20 kwenye Serikali za Vijiji. Nataka nijue, kwa sababu Waziri na Naibu Waziri wapo; hivi ni kweli ile fidia waliyokuwa wanapeleka halmashauri ya kufidia hii kodi ya maendeleo ambayo ilifutwa na ushuru mbalimbali wa halmashauri, wamesitisha au bado wanapeleka?

Mheshimiwa Naibu Spika, hii asilimia 10 ya akinamama na vijana, hii ni *revolving fund* wala siyo zawadi. Nakubaliana na Kamati, kwamba halmashauri zitenge asilimia 10 kwa ajili ya kuwapatia akinamama na vijana, lakini warejeshe hii mikopo, bila kurejesha hii mikopo vikundi vingine haviwezi kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu manunuzi, pamoja na kwamba tumerekebisha Sheria ya Manunuzi hapa, lakini halmashauri nyingi bado karibu asilimia 75, fedha zinapotea kwenye manunuzi kwa sababu hawafuati

utaratibu. Kwa hiyo, lazima halmashauri zisimamamiwe ili kufuata Sheria hii ya Manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utengenezaji wa magari, hivi najiuliza, halmashauri za wilaya hazina gereji au kila halmashauri inatengeneza magari inapotaka? Ndiyo maana gharama zinakuwa kubwa na halmashauri zinakosa pesa

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukaimu, ni halmashauri nyingi. Nimekuwa Mjumbe wa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, nimetembelea halmashauri nyingi sana, watumishi wengi wanakaimu. Sasa kama anakaimu, Mheshimiwa Waziri, kama mtumishi huyo ana sifa kwa nini asithibitishwe kazini apate kile cheo. Ukaimu una mwisho wake, miezi sita, lakini mtumishi anakaimu zaidi ya miaka miwili, miaka mitatu, huo ni ukaimu wa namna gani, lazima wathibitishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwangu yalikuwa hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa hiyo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja za Kamati zote mbili, Kamati ya *LAAC* pamoja na Kamati ya *PAC*. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu uliobaki ni dakika kumi na kidogo hivi, lakini kwa kuwa wachangiaji wana dakika 15, nikiita mchangiaji sasa maana yake nitakuwa nimempunja dakika zake.

Nitumie fursa hii kuwasoma majina wachangiaji tutakaoanza nao leo mchana, halafu wengine tutawasoma hiyo jioni wakati tukiendelea. Mheshimiwa Martin Msuha, Mheshimiwa John Kadutu, Mheshimiwa Leah Komanya, Mheshimiwa Richard Mbogo, Mheshimiwa Aysharose Matembe, Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mheshimiwa Issa Mangungu, Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim; hao ndio tutakaoanza nao mchana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasoma majina haya, nasitisha shughuli za Bunge mpaka leo saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.53 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Tukae. Katibu.

**NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Hoja za Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)* pamoja na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)***

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na michango kuhusu hoja zilizoletwa na Kamati ya Hesabu za Serikali na Hesabu za Serikali za Mitaa. Kabla hatujasitisha shughuli za Bunge nilisoma majina kadhaa kwa hivyo nitaendelea nao hao. Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim atafutiawa na Mheshimiwa Rose Kamil Sukum.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, *Subhana Wataala* kwa kunijalia uzima na afya na kuniwezesha kuchangia taarifa hizi mbili muhimu, ile ya *LAAC* ambayo imetolewa na Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale Mwiru, mtoto wa Kingunge, hongera sana kwa kazi nzuri na Mheshimiwa Kaboyoka, taarifa zao ni za kina kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za *CAG* ndizo ambazo wenzetu hawa wanazifanyia kazi. Taarifa zote hizi mbili ni nzuri, lakini tatizo la kutopatikana kwa fedha kwa viongozi wa Kamati hizi mbili kwenda katika maeneo mbalimbali kujionea uhalisia wa miradi ya maendeleo, kuangalia *value for money*, jinsi gani fedha zilivyotumika, limekuwa ni kubwa kweli. Kazi ambayo wameifanya Wenyeviti hawa wawili ni kubwa lakini kama hawapewi fedha za kwenda katika maeneo mbalimbali kuangilia uhalisia na kile kitu kinachoitwa *value for money* ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi nimpongeze Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, naye vilevile nimwonee huruma kidogo baada ya kumpongeza, kama alihitaji shilingi bilioni 62, Serikali imekwenda kumpa shilingi bilioni 18 atafanya kazi vipi? Huu ni upungufu mkubwa sana! Kila mtu aliyepewa dhamana na Serikali atengewe fedha ya kutosha ili atakapotoa mapendekezo yake basi yawe ni kweli. Kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaomba shilingi bilioni 62 anaenda kupewa shilingi bilioni 18 kuna jambo, tatizo kubwa. Kwa mara nyingine naishauri Serikali iandae mpango madhubuti, mpango makakati, ulio mzuri na mahsusi wa kuweza kutoa fedha hizi kwa wahusika hawa. Hiyo ili kuwa ni chombeza ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, wachangiaji wenzetu waliopita walisema kwamba moja ya tatizo kubwa hapa ni Hazina kuchelewesha kutoa fedha za maendeleo katika Halmashauri au kutopeleka kabisa. Utekelezaji wa miradi ambayo tumepanga sisi Waheshimiwa Wabunge na ikumbukwe kwamba asilimia 70 ya fedha za maendeleo zinakwenda kwenye Halmashauri, kama Serikali haitaki kutoa fedha kwa wakati, inachelewesha au haitoi kabisa ina maana sisi Wabunge ni kama danganya toto tu. Tatizo ni nini kwa Serikali? Ni lazima Serikali ikumbuke kwamba sisi Wabunge tunapopiga kelele na kuandaa mazingira mazuri basi hizi fedha waweze kuzitoa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya upungufu mkubwa unaonekana ni suala zima la Wakurugenzi wengi katika Halmashuri kutokuwa na sifa na ndiyo maana miradi mingi ya maendeleo huwa inakwama. Wenyeviti wetu na Kamati kwa ujumla waliwaita baadhi ya Wakurugenzi kuja kutoa taarifa, unaona jinsi wanavyojikanyaga kanyaga, hawana sifa. Wakurugenzi hawa wanachukuliwa kwenye *NGOs,* ni vyema Wakurugenzi hawa watoke katika utumishi na wajulikane wana sifa fulani lakini wapi, tatizo nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mikakati ya kuziboresha hizi Halmashauri zetu ni kwamba yale makusanyo ya ardhi ambapo fedha hizi zinakwenda moja kwa moja Serikalini inatakiwa asilimia 30 zirudi kwenye Halmashauri lakini hawapewi. Kwa hiyo, Halmashuri zinadhulumiwa, zinanyanyaswa, zimekuwa maskini na Serikali imekaa tu, tutafika kweli? Sijui. Niiombe sana Serikali iandae mpango mkakati na mzuri kabisa ili Halmashauri iweze kupata hizi asilimia 30 kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende sasa katika lile la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambaye katika taarifa hizi ni jicho la kuona. Nitaanza na taarifa moja moja na naomba niende kwenye ukurasa wa 141 ambapo kuna ubadhirifu wa fedha ambao umefanywa. Kwa mujibu wa ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2005 kuna suala zima la Kivuko cha Kigamboni ambacho kinatoka Kigamboni kwenda Dar es Salaam. Kivuko hicho kilifanyiwa majaribio ni kibovu na kwa mujibu wa ripoti kilinunuliwa kwa dola za Kimarekani 4,980,000 karibu shilingi bilioni 10 lakini hakikufanya kazi, ni tatizo kweli, ina maana hapa Serikali imeingia hasara wakati tuliambiwa kivuko hiki ni kizuri, ni bora lakini hapa pametokea matumizi mabaya ya fedha za umma.

Niishauri Serikali kwa kuwa aliyekuwa Waziri katika Wizara hii sasa ni Mtukufu mwenyewe wa heshima, kiongozi wetu, ni vema ashauriwe kwamba watu wote waliompelekea Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuingia katika mkataba huu mbovu wa shilingi karibu bilioni 10 kununua kivuko kibovu ambacho ni cha kutoka Bagamoyo kuja Dar es Salaam na hakifanyi kazi, watu hawa Mheshimiwa Rais awatumbue. Yeye mwenyewe anawajua,

yeye mwenyewe Mheshimiwa Rais awatumbue watu hawa ambao walituingiza katika mkataba mbovu na Ujerumani kwa dola za Kimarekani 4,980,000 karibu shilingi bilioni 10 na kivuko hiki kikawa hakina sifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ikasema kwamba hati ya makabidhiano haikutolewa. Kivuko kilikabidhiwa bila hati ya makabidhiano jambo ambalo ni baya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa kuliko yote sifa ya kiwango cha kutembea ni tatizo. Ukiangalia kivuko cha Bakhresa kinatoka Dar es Salaam kwenda Zanzibar ambacho kimenunuliwa shilingi bilioni nne, kinatumia saa moja na nusu lakini kutoka Bagamoyo kuja Dar es Salaam saa tatu. Ni vema kwa kuwa kiongozi mkuu yeye mwenyewe alikuwa ndiyo wakati huo ana dhamana mumshauri wale wote waliotuingiza katika mkataba huu awatumbue alfajiri mapema ili wananchi wapate imani nao, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala zima la wastaafu. Mara nyingi kumekuwa na malalamiko, ripoti nyingi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zimekuwa zikizungumzia jinsi gani wastaafu wanavyoonewa, wanavyopunjwa na wanavyodhulumiwa. Ukiangalia ripoti zote za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, nianze na inayoishia mwaka 2015, kati ya majalada 4,683 ya wastaafu yaliyokaguliwa majalada 200 yalipunjwa jumla ya shilingi milioni tatu themanini na tano laki tatu na mia nne themani na moja. Utetezi wa Serikali na kinachoonekana tatizo ni kukokotoa, mnakokotoa jambo gani jamani? Majalada 200 wastaafu wamepunjwa, wamedhulumiwa na ndiyo maana wakawa maskini. Wastaafu hawa wakishakufa risala nzuri na mnatoa machozi, machozi ya nini wakati mliwaonea alfajiri mapema? Roho mbaya kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inakuwaje leo ripoti inayoishia 2014, majalada 4,764 ya wastaafu yaliyokaguliwa majalada 283 yamepunjwa shilingi 481,456,311, jamani! Kila siku wakati wa kustaafu hawataki kuwatendea haki wastaafu. Wastaafu hawa na wao walikuwa ni wafanyakazi wetu, wameshastaafu jambo gani kubwa la msingi mnashindwa kukokotoa mkawapa haki zao. Kila siku ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaonya kwamba wakati wa kukokotoa basi Serikali iwe makini au hakuna wataalam? Jamani, aibu si aibu, ni shida kweli. Kila mmoja ni mstaafu mtarajiwa kuna Wabunge wastaafu na watu wengine mbalimbali, lakini wastaafu hawa ni vema kwa vyovyote iwavyo waangaliwe kwa jicho la huruma ni jinsi gani wanavyodhulimiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye jambo lingine, nikuombe habari zifike kunakohusika, kwa sababu Serikali hapa ipo, inakuwaje sisi kila siku tunaingia kwenye mikataba mibovu? Tumeingia mkataba na Shirika la Ndege kipindi kile la *South Africa* na Shirika letu la Ndege la Tanzania *(ATCL)* tukakodi ndege (*Airbus 320)* na baadaye ndege hiyo ilikuwa ni mbovu, ikapelekwa Ufaransa kwa matengenezo, ikasuasua, ikaondolewa ikapelekwa Guinea, ikapakwa rangi, tumepata hasara ya shilingi bilioni 91 nani katumbuliwa? Mnatumbua maskini za Mungu waliokuwa hawana kitu, tumbueni hawa, hawa ndiyo wa kutumbuliwa. Wameiingizia hasara Serikali ya shilingi bilioni 91 mbona hawa hawatumbuliwi? Muwatumbue na hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anapotoa maelezo yake kwamba kuna wizi, ubadhirifu na ufisadi mkubwa kama huu, Serikali lazima mtilie maanani, muone kwamba hili jambo ni la msingi sana vinginevyo ni shida kweli! Hata ukichangia kiasi gani, Serikali inasema ni sikivu, inasikia kilio chetu lakini usikivu uko wapi? Sisi wengine tunapata shida kweli Serikali ukiishauri haikubali. Kazi ya Bunge ni kuishauri na kuisimamia Serikali lakini Serikali haikubali kusimamiwa ni shida na inavyoonekana Serikali haitaki kusimamiwa, wanataka watusimamie sisi tutakubali wapi, hatukubali. Tutachombeza hivi hivi kidogo kidogo kuna siku mambo yatawaingia vizuri muweze kutufanyia yale ya haki na hasa kwa wananchi. Haiwezekani shilingi bilioni 91 ziende, ndege mbovu, muiondoshe Ufaransa muipeleke Guinea muipake rangi, lakini hakuna aliyekamatwa, ni shida kweli, tutafika sisi kweli? Sijui, kwa sababu ameingia Trump inawezekana akatusaidia pengine anasikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, mimi sitaki nichombeze chombeze sana, naomba jicho hili la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mumpatie fedha aende katika maeneo mbalimbali. Haiwezekani anaomba shilingi bilioni 62 anapewa shilingi bilioni 18. Mheshimiwa Kaboyoka na Mheshimiwa Ngombale nao hawakupewa fedha za kutembelea maeneo mbalimbali kujionea wenyewe, *value for money* iko wapi, hamna kitu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbe wao ripoti walitumiwa moja kwa moja kwenda *site* hakuna. Bunge ndiyo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsanteni sana nashukuru na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Masoud. Mheshimiwa Rose Kamil Sukum atafuatiwa na Mheshimiwa Martin Msuha na Mheshimiwa John Kadutu ajiandae.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana nami kupata fursa hii ili niweze kuchangia taarifa ya Kamati kuhusu Hesabu Serikali za Mitaa pamoja na *PAC*. Kwanza kabisa niombe Wabunge wote tukubali kupokea maoni au mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ili kuweza kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya hii ya *LAAC* ina kazi ngumu sana. Wote tutambue kabisa kwamba Halmashauri zetu zote zinatakiwa zikaguliwe na Kamati ya *LAAC*. Kila Mbunge hapa ana Halmashauri yake, nadhani haya maoni yanamgusa kila mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuzungumzia suala la ugumu na usugu wa matatizo ambayo yako kwenye Halmashauri na yote yanatokana na kwamba sasa hivi Serikali yetu ambayo haitaki kusikia imesema ina ufinyu wa bajeti. Kama kuna ufinyu wa bajeti, umebana hizo fedha ili uweze kufanya jambo, kama hawakaguliwi si ndiyo wizi unaongezeka? Kama unaongezeka, nani anaweza kuwabana kama Kamati ya *LAAC* au *PAC* haitapewa mafungu ya fedha ili kwenda kutembelea miradi yote ambayo inafanyiwa kazi na Halmashauri zetu au na Wizara mbalimbali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ucheleweshaji wa fedha katika Halmashauri zetu umesababisha baadhi ya miradi kutokamilika. Miradi hiyo haikamiliki kwa sababu fedha zinapochelewa kwa kuwa baadhi ya Maafisa Masuuli na Wakuu wa Idara waliopo kwa tamaa waliyonayo basi hutumia fedha zile halafu wanasubiri za mwaka unaofuata. Kwa hiyo, hili ni tatizo kubwa ambalo lipo la Serikali kuchelewesha hizo fedha za maendeleo nao wanachangia hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ifikie sasa mahali Serikali ikubali kwamba fedha zikitolewa zitolewe kwa wakati ili maendeleo ya watu yaweze kufanyika. Ndicho tulichokiona kwenye Kamati ya *LAAC* tulipokuwa tunaendelea kukagua kwamba ucheleweshaji ule unasababisha Maafisa Masuuli kula hizo fedha bila kutumia utaratibu unaofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine maagizo kutoka ngazi ya juu yamesababisha ubadhirifu wa fedha au kutumia fedha ambazo haziko kwenye bajeti katika Halmashauri zetu. Utakuta Mkuu wa Mkoa anawaagiza wakatumie fedha kwenye mafungu ambayo yeye hausiki kupitisha hiyo bajeti, *DC* naye

anaagiza, *DAS* anaagiza, *RAS* anaagiza na kuchukua fedha. Kwenye ukaguzi huo tumeona kwamba kuna *RC* alikuwa anaagiza fedha zitumike kwenye sehemu ambayo haipaswi kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, huo ndiyo ubadhirifu mmojawapo ambao tumeugundua kwenye Kamati ya *LAAC*. Tunaomba haya maagizo yanayotoka juu basi wawe na mafungu yao ya fedha, mnataka kutengeneza madawati mtuambie fedha iko wapi ili wakatengeneze madawati. Siyo unaagiza watengeneze madawati halafu hakuna fedha kwenye bajeti, ni ngumu sana kufanya hiyo kazi kwenye Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, sisi Kamati ya *LAAC* mmepata taarifa kwamba tumekagua Halmashauri 66. Sababu ya kukagua Halmashauri 66 ni ukosefu wa fedha tumeshindwa kwenda kukagua hata miradi ya maendeleo. Kati ya Halmashauri 164, ni Halmashauri 66 tu ndiyo zimekaguliwa, je, ubadhirifu unaoendelea kufanyika kwenye zile Halmashauri zilizobaki ni kiasi gani? *CAG* pia amekosa hizo fedha, je, kama *CAG* hajaenda kukagua ile miradi ya maendeleo ubadhirifu unafanyika kwa kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke suala *value money,* wanasema fedha zimekwenda kuchimba kisima, visima ni hewa, zimeenda kujenga sekondari, sekondari ni hewa, zimeenda kutengeneza barabara, barabara ni hewa na hakuna anayekwenda kukagua. Waziri wa TAMISEMI unafahamu kabisa wewe peke yako hutoshi kwenda kukagua hizo Halmashauri zote, lazima tusaidiane. Leo mnabana hizo fedha, je, tunafanyaje sasa na fedha zimetumika vibaya na hakuna miradi ya maendeleo iliyofanyika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, udhaifu na udhibiti wa Mkaguzi wa Ndani. Mkaguzi wa Ndani yuko chini ya *Internal Auditor General,* lakini huyu Mkaguzi wa Ndani kwa masuala ya kiutawala yuko chini ya *DED,* hebu niambieni atawapeni taarifa iliyo sahihi kweli kama yuko chini ya *DED?* Matokeo yake yule Mkaguzi wa Ndani anashikwa anaambiwa ukitaka usafiri, ukitaka hela usitoe taarifa inabidi asizitoe. Je, tunafanya nini kuhusu huyu Mkaguzi wa Ndani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri katika Halmashauri zetu Mkaguzi wa Ndani asiwe chini ya Mkurugenzi au Afisa Masuuli kwa sababu taarifa hazitolewi mpaka wagombane, wakishagombana na Mkurugenzi ndiyo unapewa taarifa kwamba kuna fedha imeliwa au kuna kitu fulani kimefanyika. Nashauri kwamba Mkaguzi wa Ndani awe chini ya *Internal Auditor General* na taarifa zake ziende pale na utaratibu wa shughuli zake zote utoke kule au awe chini ya *CAG* kuliko kuwa chini ya Mkurugenzi wa Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kulizingumzia, kazi ya ufuatiliaji na usimamizi ni ngumu sana na kubana matumizi pia inahitajika lakini Kamati zote kutotembelea miradi hatufanikiwa. Kamati ya *PAC* na *LAAC* kama hazitatembelea miradi hatutaweza kufanikiwa kwa jambo lolote. Tumeona wote tuliokuwepo kwenye hizo Kamati kwamba kama hatukwenda kutembelea tunaangalia taarifa ya kwenye makaratasi hatutafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Afisa Masuuli anaweza kuwa mjanja, suala la risiti zinaweza kuandikwa zikaletwa hapo na akawa na hati safi, lakini kumbe kule kwenye kazi hakuna kilichofanyika. Kwa hiyo, nadhani sasa suala la ufuatiliaji kama lipo tunatakiwa sisi kama Kamati ya *LAAC,* kama Kamati ya *PAC* au Wabunge wote kwa ujumla kutembelea miradi ili kuhakikisha kwamba miradi inafanywa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho kimeonekana zaidi ni kwamba wakati Bunge linaendelea na Halmashauri zinaendelea na vikao vyao. Hiyo imesababisha sehemu kubwa sana ya Wabunge kutokujua mapato na matumizi yanayofanyika kule. Hata Mfuko wa Jimbo imeonekana wazi kabisa Mbunge hajui fedha zake zimetumikaje na hata akiuliza anaambiwa hela zimeshatumika zimefanya kazi zingine. Kama Mfuko wa Jimbo unaweza kutumika, Wabunge mna kazi gani kama hamuwezi kudhibiti mapato na matumizi ya Halmashauri zetu au ya Serikali kwa ujumla? Kwa hiyo, tunatakiwa kupata hiyo fursa ili kuweza kufanya kazi ya usimamizi wa Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichokigundua zaidi kwenye Halmashauri zetu pamoja na kwamba tuna manunuzi yasiyozingatia sheria lakini pia kuna watu ambao wanatumia nafasi zao kuingiza mikono yao pale. Mkuu wa Mkoa anakwambia umtumie mkandarasi huyu, mimi ndiyo nawaagiza na mkandarasi hajatimiza wajibu wake. Je, hamuoni kwamba tunatumia fedha za umma vibaya? Tunawalalamikia sana Maafisa Masuuli kutofanya kazi yao vizuri lakini sehemu kubwa ni maagizo yale yanayotoka kwa sababu ni mkubwa anamuagiza Mkurugenzi, haya yametokea maeneo mengi kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi suala la Wakurugenzi ambao hawaelewi utaratibu wa Halmashauri imekuwa ni tatizo kubwa. Uteuzi wa juzi tu umefanyika Julai lakini kilichotokea kwenye Halmashauri ya Hanang mfano kuna watumishi wamekula fedha shilingi bilioni 1.2 na uchunguzi umefanywa na Mkuu wa Mkoa na imebainika fedha hiyo kuliwa, lakini kwa kuwa Mkurugenzi haelewi, maskini ya Mungu ametoka *TFDA* hajui masuala ya Halmashauri akapewa ushauri na wale waliotumia ile fedha kwamba hawa watumishi waliokuwa hiyo fedha tunashauri warudi kazini wateremshwe vyeo siyo wachukuliwe hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiona suala kama hilo ujue kwamba hawa Wakurugenzi wapya wanahitajika aidha wakapewe semina au waende shule ambayo itawasaidia kujua ni namna gani watakavyoweza kuendesha hizo Halmashauri. Kwa sababu kama unashauriwa na mtumishi wa chini yako uliyemkuta pale ambaye na yeye amehusika kwenye kutumia hizo fedha halafu na wewe unaishauri *council* kwamba hawa watumishi adhabu yao ni kuteremshwa cheo, wamekula shilingi bilioni 1.2. Hebu niambie kwa nini wale wa Kagera wameshtakiwa kwa Rais wakati yule wa Hanang aliyekula shilingi bilioni 1.2 anaambiwa aendelee na kazi? Kwa hiyo, kuna mambo ya kufanya ili kuweza kuisaidia Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sukum. Tunaendelea na Mheshimiwa Martin Msuha atafuatiwa na Mheshimiwa John Kadutu na Mheshimiwa Leah Komanya ajiandae.

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia taarifa zilizoko mezani kwako. Mimi nitachangia upande wa taarifa ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge la Bajeti la 2016/2017 asilimia 40 zinapelekwa kwenye kutekekeleza miradi ya maendeleo, lakini miradi hiyo mingi inatekelezwa katika ngazi za Halmashauri. Pia katika mabadiliko ya sheria za fedha yaliyofanyika mwaka huu yamepandisha kiwango cha kuiwezesha Halmashauri kusaini mikataba kutoka kwenye shilingi milioni 50 mpaka shilingi bilioni moja. Hii ina maana kwamba Halmashauri hizi zinapewa uhuru zaidi wa kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa upande mwingine tunazo *oversight committees*, tunayo Ofisi ya CAG na tunazo hizi Kamati. Kwa bahati mbaya sana tunakwenda *contrary* kwa maana kwamba hizo *oversight committees* zimenyimwa uwezo wa kifedha kwenda kufanya ukaguzi wa miradi. Kwa hiyo, tunachotegemea kuona baada ya mwaka huu wa fedha ni kwamba pengine miradi hii haijatekelezeka kwa kiasi ambacho kinaridhisha kwa sababu ya hizo *oversight committees* kunyimwa uwezo wa kifedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya maeneo ambayo Halmashauri zote zilionekana kuwa na matatizo makubwa ni kwenye usimamizi wa mikataba na miradi ya maendeleo. Kati ya Halmashauri zote 66 ambazo tulizihoji mbele ya Kamati, zaidi ya asilimia 75 zilionekana kuwa na upungufu katika usimamizi wa mikataba. Mikataba mingi haikuweza kufikia mwisho kwa maana kwamba mingi ilivunjwa njiani na hivyo kuzisababishia Halmashauri kuingia gharama zaidi.

Kutokana na kuvunjika kwa mikataba hiyo ilisababisha pia miradi mingi kutokamilika kwa wakati na chini ya kiwango ambacho kilikusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya sana miradi ambayo iliathirika zaidi ni ya maji. Maeneo mengi miradi mingi ya maji ambayo ilikamilika pia haikuweza kutoa maji, lakini mingine pia imekwama kwa kipindi cha muda mrefu.  Kwa mfano, mradi wa maji Wilayani Tunduru wa Nalasi na Nandembo ilionekana kuwa imekamilika lakini haitoi maji na mkandarasi ameshasaini. Huu ni udhaifu katika usimamizi wa miradi ya maendeleo lakini pia mikataba husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ipo miradi mingine kama mradi wa ujenzi wa madarasa katika Kata ya Namswea Ndongosi. Shule ya sekondari ilishakamilika siku nyingi, lakini haikuweza kutumika kwa sababu fedha hazijatolewa na Serikali Kuu kwa ajili ya kukamilisha hii shule ili iweze kutoa huduma ambayo imekusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo liliathirika sana kwenye hizi Halmashauri zetu ni matumizi nje ya bajeti. Halmashauri nyingi zimeonekana zimetumia fedha nyingi sana nje ya bajeti ambayo imepitishwa lakini Halmashauri hizi zilikuwa zinatumia kivuli cha maagizo kutoka kwa viongozi wa juu. Tulipowahoji kwamba hao viongozi waliwaambia wavunje Sheria za Matumizi ya Fedha za Umma wakasema hapana.  Hiyo nayo ilipelekea kuathiri miradi mingi sana ya maendeleo kwa sababu fedha zote ambazo zilionekana kama ziko *idle* zilichukuliwa na kupelekwa kwa mfano kwenye ujenzi wa maabara kwenye shule zetu za sekondari. Bahati mbaya zaidi hizi maabara nyingi pia hazijakamilika japokuwa fedha nyingi sana zilichukuliwa kutoka maeneo mengine kwenda kutekeleza mradi huu wa ujenzi wa maabara.

Kwa hiyo, Kamati ilikuwa inashauri TAMISEMI wafanye juhudi pengine kwenda kutathmini ni kiasi gani fedha zilichukuliwa kutoka maeneo mengine zikatekeleza mradi wa maabara, lakini kuna tija kiasi gani imepatikana upande huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya miradi ambayo tulifanikiwa pia kuipitia ni mradi wa uuzwaji wa Shirika la Usafirishaji Dar es Salaam (UDA). UDA ni shirika la umma ambalo lilikuwa chini ya Hazina. Shirika hili lilikuwa na jumla ya mtaji wa hisa milioni 15 lakini Serikali iliamua ku-*issue* hisa milioni 7.1 na ikabakiza hisa milioni 7.8 ambazo hazikuwa *allotted*. Kati ya zile hisa ambazo Serikali ili-*issue,* zile milioni 7.1 iliamua kutoa hisa zake asilimia 51 kuipa Jiji la Dar es Salaam, lakini baadaye Jiji la Dar es Salaam waliamua kuuza hisa zao zile asilimia 51 kwa Kampuni moja binafsi ambayo inaitwa *Simon Group*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baadaye pia Bodi ya UDA iliamua nayo kufanya mchakato wa kuuza zile *unissued and unallotted shares* za milioni 7.8. Hisa za Jiji zililipwa na *Simon Group* na fedha hizo zikawekwa kwenye akaunti ya Amana Benki Kuu na fedha hizo bado zipo kwenye Akaunti hiyo, Jiji halijaweza kuzitumia. Fedha ambazo zilipatikana kutokana na uuzaji wa hisa hizo ni kiasi cha shilingi bilioni 5.875. Baadaye Serikali iliona kwamba uuzwaji wa zile hisa ambazo hazikuwa *issued* na kuwa *allotted* za milioni 7.8 ilikuwa ni kinyume na sheria na taratibu. Kwa hiyo, Serikali iliamua kuzuia mauzo hayo na *Simon Group* aliamua ku-*surrender* hisa hizo kwa hiyo zikabaki chini ya Msajili wa Hazina mpaka hivi tunavyoongea. Pia zile fedha ambazo zilipatikana kutokana na uuzwaji wa zile hisa za Jiji zile bilioni 5.8 hazijaweza kutumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo ndani ya Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kusubiri baadhi ya nyaraka kutoka kwa Msajili wa Hazina ili jambo hili liweze kufika mwisho, Kamati ilikuwa inapendekeza mambo mawili; la kwanza, Halmashauri za Manispaa za Dar es Salaam ziweze kushirikishwa katika umiliki wa UDA ili ziweze kuwa wabia wa uendeshaji wa kampuni hiyo kwani ndiyo kampuni ambayo inategemewa kusafirisha abiria ndani ya Jiji la Dar es Salaam kwa kuwauzia baadhi ya hiza zile ambazo hazikuwa *allotted* za milioni 7.8.

Lakini pia tulikuwa tunapendekeza kwa vile hizi fedha shilingi bilioni 5.8 ambazo zimebaki BOT bila kutumika, Serikali ingetengeneza utaratibu wa kuangalia ni namna gani fedha hizo zinaweza zikaruhusiwa zitumike kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ndani ya Manispaa zinazounda Jiji la Dar es Salaam badala ya kuzibakiza ziwe *idle* katika Akaunti ya Amana Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo liligusa karibu Halmashauri nyingi ni upotevu wa nyaraka za matumizi. Utakuta mkaguzi anakagua unakuta nyaraka za thamani kubwa tu hazionekani lakini baada ya wakaguzi kuwa wamemaliza kazi yao wametoka Afisa Masuuli anakuja na majibu kwamba nyaraka hizo sasa zimeshapatikana na ziko tayari kwa ukaguzi.

Kamati inauliza kama kweli nyaraka hizo zilikuwa ni halisi kwa nini zisipatikane wakati zoezi la ukaguzi linafanyika na siyo baada ya zoezi kumalizika na pengine baada ya miezi mingi sana ndiyo nyaraka hizo ziweze kupatikana? Hilo limeonekana ni eneo ambalo lina udhaifu mkubwa katika utunzaji wa hizi nyaraka kinyume na taratibu na sheria za fedha zinavyohitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine lililoonekana kuwa na matatizo makubwa hasa kwenye Halmashauri mpya ni ufanyaji kazi wa Mfumo wa Uandaaji wa Taarifa za Fedha unaoutwa *EPICOR*. Halmashauri nyingi mpya hazijaunganisha kwenye mtandao huu kwa hiyo taarifa zao nyingi aidha wanatengeneza nje ya mfumo au wanasafiri kwenda kutengenezea kwenye

Halmashauri ya jirani. Pia ilionekana kwamba taarifa nyingi haziwezi kutolewa na mfumo huu. Kwa hiyo, Serikali iangalie ni namna gani ya kuboresha mfumo huu ili uweze kukidhi mahitaji ya utengenezaji wa taarifa za fedha katika Halmashauri hizi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ilionekana wahasibu wengi hawaufahamu vizuri mfumo huu. Wahasibu walio wengi hulazimika kutengeneza baadhi ya taarifa kwenye mfumo huu lakini taarifa nyingine kutengeneza nje ya mfumo na hivyo kukosa uwiano wa taarifa zinazotoka katika hiyo mifumo miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliona maeneo mengi yenye changamoto lakini kwa vile kuna wachangiaji wengi, naomba niunge mkono hoja na niwaachie wenzangu wagusie maeneo mengine. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Msuha. Mheshimiwa John Kadutu, atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Komanya na Mheshimiwa Richard Mbogo ajiandae.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia taarifa hizi za Kamati mbili kutokana na ukaguzi wa CAG.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niiambie Serikali kwamba eneo hili ni muhimu kuliangalia na kusikiliza kwa makini lakini tupate matokeo mazuri. Kwenye ripoti hizi hakuna siasa, hili ni jicho la tatu la kuona utendaji wa Serikali yetu kupitia Halmashauri na Serikali kwa ujumla na kwa sababu nia yetu ni kutengeneza na siyo kuharibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la uteuzi wa Wakurugenzi. Kwa upande wangu sina tatizo na mamlaka ya uteuzi kwani inafanya kazi yake vizuri, lakini sisi kama Kamati ya *LAAC* tumeona upungufu mwingi siyo kidogo ya utendaji ya Wakurugenzi wetu. Wapo Wakurugenzi ambao hawajawahi kufanya kazi kabisa kwenye mfumo wa Serikali hata kwenye mashirika ya Serikali kiasi kwamba hata hawajui uendeshaji wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Serikali kwa nia njema tu, tusibane sana matumizi, tuwafanyie mafunzo kidogo. Kuna Wakurugenzi walikuja mbele ya Kamati hawajui hata itifaki ya vikao. Sasa ukiwa na Mkurugenzi wa aina hiyo, unajua maneno wanayotumia wengi wanasema mimi nimeteuliwa na Rais, wanadhani uteuzi wa Rais unaweza kumfanya akaendelea kudumu pale, mimi sikubaliani nao. Bahati nzuri mimi nimetokea kwenye Halmashauri, kwa hiyo najua vizuri mno shughuli za Halmashauri, lakini kwa uelewa wangu mdogo wa hesabu Wakurugenzi wengi kwa kweli hawana uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hilo tu, wapo ma-*DT* kwa maana ya Watunza Hazina wetu pamoja na kuwa na vyeti hawana uwezo wa kazi. Wapo ma-*DT* ambao wana *CPA,* lakini uwezo wao wa kufanya kazi ni mdogo sana. Kwa hiyo, niiombe Serikali tutupie macho utendaji wa watu hawa hasa Wakurugenzi na Watunza Hazina. Kule kwenye uteuzi kama nilivyosema hatuna mamlaka nako, lakini basi wapewe mafunzo kuwapa uwezo wa kufanya kazi na kuzielewa kazi. Wenzangu wamesema kuna watu wametoka kwenye *NGOs*, mashirika, *VETA* na sehemu mbalimbali, kwa idadi kubwa wachache sana waliotoka kwenye *Local Government*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie kidogo suala hili la UDA. Tumepata taarifa Kamati mbalimbali zimekuwa zinashughulika na jambo hili la UDA. Niiombe Serikali ifike mahali tumalizane na UDA. UDA kila siku inatajwa Bungeni, kila siku haina mwenyewe, tumehoji nani mmiliki wa UDA mpaka tunamaliza vikao hatujapata majibu nani wamiliki wa UDA. Ifike mahali sasa tupate majibu nani wanamiliki na ilikuwaje alipatikana *Simon Group.*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Simon Group* kwenye ripoti mbalimbali ameibuka tu kwamba huyu kapatikana anauziwa hisa, sasa amepatikana vipi hapaonyeshi mchakato ulioendeshwa kumpata *Simon Group*. Hili ni jambo la hatari kama kampuni inakuja tu ghafla, Serikali inakubali inaipa kazi. Tumempa umiliki mtu ambaye hajashindanishwa, hili ni jambo la hatari sana. Sasa tunataka tumjue mmiliki kwa sababu kumekuwa na shida ya kujua nani na nani anamiliki UDA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema mwenzangu pale Mheshimiwa Msuha zipo hisa zilipouzwa ilikubalika ziende kwenye shughuli za maendeleo, kwa muda wote hizi pesa zimetunzwa pale *BOT*. Kwa nini sasa muda usifike uamuzi upite zile fedha ziende kwenye shughuli za maendeleo. Ni fedha ndefu hizi, barabara, huduma za hospitali na shughuli mbalimbali za maendeleo zinahitajika kwa nini pesa ikae tu *BOT* ambapo yenyewe inatunza pesa tu ambazo kumbe zingekwenda kwenye shughuli za maendeleo. Zile hisa nyingine zilizobaki zigawanywe kwenye Manispaa nyingine ili Manispaa zote ziweze kumiliki UDA kwa pamoja. Hata hivyo, kama Serikali inaamua iachane nayo basi tujue imefika mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipendekeze sasa labda Kamati ya *PAC*, *LAAC* zikutane kwa pamoja kulimaliza jambo hili. Kwa sababu kila Kamati ina uamuzi wake, ina uchunguzi wake, ina mapendekezo yake ambayo hayaishi. Kwa nini sasa sisi kama Bunge tusiungane pamoja tukamaliza jambo hili. Sasa UDA tunaona imeingia kwenye kazi nyingine mradi unazidi kuwa mkubwa halafu tunamuacha mwekezaji huyu ambaye hatujui wenzake ni akina nani na kazi gani anafanya, lakini baadaye hata huu mradi wa *DART* utatuingiza kwenye shida. Nina imani Serikali ni sikivu na Mawaziri wapo wanasikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni uhai wa Halmashauri. Kwa wale ambao hamfahamu hizi Halmashauri zilikuwepo zikafa kama ushirika lazima tuangalie nini kiliua Halmashauri zetu. Sasa hivi toka tulipokwenda kwenye uchaguzi mwezi Juni, 2015 pesa ya maendeleo haijaenda na hii *quarter* ndiyo kabisa pesa ya maendeleo haijaenda, kule kwenye Halmashauri zimelala hakuna kazi inayoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie Serikali pamoja na Waheshimiwa Wabunge tutaua hizi Halmashauri kwa mara nyingine tena kama hatukuwa makini. Tuliua Halmashauri hizi zamani, tukaua ushirika baadaye tumevirudisha vyama vya ushirika pamoja na Halmashauri, kutozipelekea pesa kunaua kila kitu. Athari zake ni nini? Toka tumemaliza uchaguzi wananchi wanadhani Serikali ipo likizo kwa sababu hakuna kazi inayoendelea kwenye Halamshauri zetu, Halmashauri zimelala, ofisi za Serikali za Vijiji hazichangamki. Siku zote kukiwa na pesa vijijini wanachangamka na utaratibu wetu ule wa kupeleka watu sita kwenda kusaini hata kama shilingi 200,000 hakuna sasa. Kwa hiyo, lazima tuhakikishe Serikali lazima ipeleke pesa kule. Pesa haziendi, tunasema madawati, tunasema hiki, sasa hivi kuna maboma mengi, litakuja agizo maboma yaishe, wanatoa wapi pesa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zipo Halmashauri zinaishi kwa ubuyu. Samahani watani zangu Wagogo, zipo Halmashauri zipo hoi bin taabani lazima tuziwezeshe. Zipo Halmashauri mpya ambazo zinahitaji kuongezewa nguvu ili ziweze kusogea. Halmashauri hizi nyingine hazina mapato. Kulishawahi kutoka tishio hapa kwamba Halmashauri kama haikusanyi itajifuta, sasa mbona Serikali yenyewe haipeleki pesa na yenyewe itajifuta? Jambo hili haliwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwasihi sana Serikali tupeleke pesa za maendeleo ili maendeleo yaonekane. Pia ni namna gani tunatimiza ahadi au Ilani ya Chama cha Mapinduzi ni lazima pesa ziende kama haziendi tutakuwa tunarudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la madeni. Halmashauri hizi pamoja na mambo mengine kuna Halmashauri zinadaiwa mpaka shilingi bilioni 16 na wadau mbalimbali, watoa huduma, *tender,* Halmashauri zitalipa lini. Kama Serikali tunalipa madeni ya nje sasa wakati muafaka umefika tulipe madeni ya ndani ili huduma ziendelee. Shule na vyuo wataanza kufunga kwa sababu hakuna mtu ataendelea kutoa huduma wakati halipwi. Kwa hiyo, Serikali tupelekeni pesa tulipe madeni ya ndani ili Halmashauri zetu zifanye kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo mengi sana yametokea huko lakini kikubwa kingine tumeshindwa kuelewa Wakurugenzi wanatoa wapi kiburi cha kutokujibu hoja za *CAG*. Siyo hoja tu za *CAG* hata maagizo ya Kamati yaliyopita, Wakurugenzi wanakuwa na kiburi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri Mheshimiwa Waziri ajaribu kuliona hili kama *CAG* anadharauliwa, kama Kamati ya Bunge inatoa maagizo hayajibiwi maana yake ni dharau. Hebu tulirekebishe hili ili Bunge kama Bunge maana yake Kamati ni Bunge lichukue nafasi yake tukiwa tunatoa maelekezo na maagizo yajibiwe. *CAG* anatoa maelezo yake yajibiwe, kama yanakaliwa kwa kweli tunakuwa hatuitendei haki ripoti ya *CAG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, *CAG* hapiwi pesa za kutosha na kuna tishio mwaka huu *CAG* anaweza asikague Halmashauri hata kumi. Kwa hiyo, kama pesa haziendi kwa *CAG* ambaye ndiyo jicho letu sisi hatuna uwezo wa kwenda kwenye Halmashauri kugundua tunaletewa kitu kilichofanyiwa kazi. Niiombe Serikali pamoja na mwaka huu tulipiga kelele wakati wa bajeti hebu mchakato wa bajeti unaokuja tumuangalie kwa karibu sana *CAG* ili apewe pesa za kutosha kufanya kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo vizuri kupigiwa kengele la pili na mimi ni Chifu nisingependa kupewa adhabu, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Leah Komanya atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Mbogo na Mheshimiwa Aisharose Matembe ajiandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya ili na mimi niweze kuchangia taarifa hizi za Kamati mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Naomba nianze kuchangia moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Sehemu ya Nne fasili ya (16) inasema Kamati yetu ya *LAAC* itafanya kazi kwa kutumia taarifa zilizokaguliwa na Mkaguzi wa Nje. Kamati ilikumbana na changamoto nyingi wakati wa utekelezaji wa majukumu haya ikiwemo Ofisi ya *CAG* kukosa fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tukichangia bajeti ya mwaka 2016/2017 tuliongelea sana suala hili. Pamoja na bajeti iliyopitishwa upelekaji wa fedha umekuwa ni wa shida. Tunafahamu kwamba kazi za *CAG* zinafanyika kwa msimu kwa hiyo, kufikia ile Julai, 2016, *CAG* alikuwa hajapelekewa fedha za

kutosha kumuwezesha kutekeleza majukumu yake ili Kamati iweze kutumia taarifa zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hiyo ilipelekea Halmashauri ya Korogwe ambayo walikuwa wametumia fedha kwa ajili ya kujiandaa kuja kukaguliwa na Kamati mfano usafiri, posho za kujikimu, *stationery* tuliwarudisha kwa sababu hoja zao zilikuwa hazijafanyiwa *verification*. Hivyo, nashauri Wizara ya Fedha ipeleke fedha kulingana na *plan of action* ya Ofisi ya *CAG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kipengele cha mishahara isiyolipwa. Serikali ilianza utaratibu wa kulipa mishahara ya watumishi wa Halmashauri moja kwa moja kupitia akaunti zao. Changamoto iliyopo, Mkurugenzi wa Halmashauri anatoa zuio la mishahara kulipwa kwa Meneja wa Benki. Mishahara inapozuiliwa Meneja wa Benki anairudisha moja kwa moja Hazina Kuu, Hazina Kuu inakiri kupokea fedha hizo kutoka kwa Meneja wa Benki. Changamoto inayotokea ni kwamba kunakuwa na *gap* kati ya Meneja wa Benki na Mkurugenzi na Mkurugenzi na Wizara ya Fedha. Meneja wa Benki hana *document* ya kuweza kumrudishia Mkurugenzi kuonyesha mishahara iliyozuiliwa kwa sababu hawezi kuirudisha kwenye akaunti ya Halmashauri. Hazina hawawezi kutoa risiti tena kwa Mkurugenzi itakuwa ni *double accounting* ya *revenue*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lililopo Wizara ya Fedha haijatoa maelekezo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri ni nini wafanye ili kuweza ku-*reconcile* mishahara ambayo haijalipwa. Wasipofanya hivyo kutatokea *loophole* kwa watumishi wa benki wasio waaminifu, wakiona hakuna ufuatiliaji wa karibu mishahara mingine inaweza ikalipwa tu kwa watumishi wasiostahili.

Naishauri Wizara ya Fedha ifanye mawasiliano na Wakurugenzi Watendaji. Kwa mfano, Jiji la Tanga lilikuwa lina hoja ya mishahara isiyolipwa ya shilingi milioni 168. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MBUNGE FULANI:** Naibu Spika.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Huyo huyo. *(Kicheko)*

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MBUNGE FULANI:** Naibu Spika. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika,…

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo. *(Makofi)*

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie katika kipengele cha mfumo wa kihasibu wa *EPICOR*. Halmashauri nyingi zilikuwa zina hoja…

Mheshimiwa Mwenyekiti,…

**MBUNGE FULANI:** Eeeh!

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Ninyi mbona mnanichanganya bwana.

**WABUNGE FULANI:** Endelea.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Haya sawa. Mheshimiwa Naibu Spika,…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumuache Mheshimiwa Leah Komanya achangie kwa sababu mkiwa mnaongea sasa, unajua miluzi mingi inampoteza mbwa njia. *(Kicheko)*

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunilinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri nyingi zilikuwa zina hoja ya matumizi mabaya ya mfumo wa *EPICOR*. Tunavyofahamu Serikali ilitumia fedha nyingi kwa ajili ya kupeleka mfumo huu kwa lengo la kudhibiti matumizi mabaya na kudhibiti mapato. Changamoto iliyopo kuna baadhi ya *package* bado hazijaingizwa katika mfumo wa *EPICOR,* kwa mfano *asset management*. Hii inapelekea Halmashauri nyingi kutoa taarifa au kukamilisha kazi zao nje ya mfumo kwa sababu mfumo haupo wakati Serikali ilitumia fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la mfumo huu pia ilikuwa ni ku-*control* matumizi mabaya ya vifungu. Tukiangalia kuna hoja nyingi za *wrong accounting coding.* Hii inapelekea hata taarifa zinazotolewa kwenye Halmashauri katika vikao mbalimbali kuwa siyo zenyewe kwa sababu zinafanywa nje ya mfumo. Nashauri Serikali ifanye ufuatiliaji kuhusu matatizo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu matumizi ya fedha nje ya bajeti katika fedha za miradi. Kwanza, napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa maagizo anayotoa kwa ajili ya Halmashauri. Mheshimiwa Rais ana lengo zuri lakini changamoto inakuja maagizo yanapotolewa zipo Halmashauri nyingine zina uwezo wa kutumia wadau waliopo katika Manispaa

au Majiji kazi hiyo ikafanyika. Halmashauri nyingine hazina uwezo wa kupata wadau hao inawalazimu watumie fedha kwa kutozingatia bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunapitia taarifa Halmashauri nyingi zilionekana miradi mingi haijatekelezwa kwa mfano miradi ya maji, miradi ya …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya naomba umalizie sentensi muda wako umekwisha.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati fedha hizo zimetumika katika maabara. Je, Serikali inafahamu ni miradi kiasi gani iliyoathirika na ina mkakati gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Komanya. Mheshimiwa Richard Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Aisharose Matembe na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis ajiandae.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza nimshukuru Mungu kwa namna pekee ametujalia mpaka muda huu tuna afya njema. Naomba tu niseme mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na naanza kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza naomba Serikali iiangalie Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kwanza kwa masuala ya bajeti. Tulisema na wenzangu wamesema basi ni wakati muafaka sasa kushughulikia suala hili. Waziri wa Fedha aliahidi mwezi Disemba ataangalia utekelezaji na ataongeza fedha kulingana na kazi zinavyoenda. Tunaomba ahadi hiyo ikifika Disemba wakati wa kupitia bajeti aliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Ofisi ya *CAG* kwa kazi nzuri ambayo imekuwa ikifanya, tumeona matunda yake kwani wameibua hoja nyingi, kwa hiyo tunawapongeza sana. Pamoja na pongezi hizi tunahitaji Ofisi ya *CAG* iboreshwe zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa vikao vya *briefing* vya kupitia hoja zao ambazo wamezikagua na wamezileta kwenye Kamati tuliweza kugundua upungufu mdogo mdogo aidha ni wa wafanyakazi au mfumo, hili tutaomba aliangalie. Kwa mfano, kuna wakati tuliwahi kuwauliza maofisa wanaotoka *CAG*, kwenye *auditing* kuna kitu kinaitwa *analytical review*, una-*check movement,* una-*analyze* kati ya mwaka wa fedha huu na mwaka wa fedha

hata miwili, mitatu iliyopita. Hiyo ndiyo *auditing* ambayo inafanyika tukaona kwamba hii Ofisi ya *CAG* ni kama vile inafanya kazi kama *internal auditor* badala ya *external auditor.* Kwa sababu uki-*check movement* ya *accounts* mbalimbali hiyo ndiyo *audit* japokuwa utaenda kwenye *item* na ukapata zile *schedule* na utaangalia utajiridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunahitaji wa-*improve* maeneo mbalimbali kwenye *audit procedures, audit technique* na *audit plan* ili waweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika utendaji wa Ofisi ya *CAG* tunajua wanaangalia muhtasari wa vikao vya Kamati za Fedha za Halmashauri zetu, lakini inabidi waongeze juhudi kwa sababu kwenye Kamati hizi za Fedha na Mipango ndipo mahali ambapo maoni mengi yanatolewa kuhusiana na matumizi mbalimbali ya fedha za Halmashauri. Kwa hiyo, tunaomba waongeze sana juhudi kwenye kuangalia muhtasari wa vikao vya Kamati vya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tukizihoji Halmashauri mbalimbali tuligundua kuna upungufu kwenye mfumo wa kihasibu kwa kutumia *computer (EPICOR).* Maoni yangu ni kwamba Serikali iangalie mfumo huu wa *EPICOR* tangu tumekuwa nao kwa miaka yote hii umetusaidia nini? Kama hauna msaada wowote ambao umeutoa kwa nini tusipate mfumo mwingine wa kihasibu kwa kutumia *computer?* Kwa sababu kumekuwa na upungufu mbalimbali, *modules* nyingi zimekuwa hazifanyi kazi na maeneo mengine kweli Halmashauri wanakuwa hawajawekewa mfumo huu, lakini ile *link* pamoja na *platform* zingine za kiuhasibu na za *report* zimekuwa hazifanyi kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ifanye upembuzi yakinifu kuangalia upungufu ulioko kwenye *EPICOR.* Dunia ya sasa hivi ina mifumo mingi ya *accounting package* ambayo inakuwa ni *strong* hata *internal control* yake inakuwa ni *strong,* huwezi uka-*temper data.* Kwa hiyo, tuhame kutoka kwenye *EPICOR* twende kwenye *software* zingine ambazo zitakuwa na msaada kwenye Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona maeneo mengi pia kama TAMISEMI haijaweza kukamilisha ufungaji wa *EPICOR* na wakati huo huo kwenye Halmashauri zetu kumekuwa na tatizo la mtu mmoja ndiyo anakuwa mtu wa *EPICOR* tu watu wengine wanakuwa hawajifunzi pale pale ndani. Kwa hiyo, hilo nalo Waziri wa TAMISEMI aangalie, kwenye Halmashauri isiwe anategemewa mtu mmoja kama atahama au atakufa au atakuwa anaumwa mambo mengine yatakuwa yamelala.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni upande wa Hazina, miradi mingi haijatekelezwa kwa sababu fedha zimekuwa hazipelekwi kwa wakati au zimepelekwa kiasi. Kwa hiyo, tumuombe Waziri wa Fedha akaangalie *commitment* ambazo zimefanywa na Halmashauri zetu, wengi walishatoa *GPN* wapelekewe fedha ili miradi ya maendeleo iweze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni upande wa Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa. Wakati wa vikao vyetu Katibu Tawala wa Mkoa wameji-*commit* kwenda kuhakikisha kwamba Halmashauri zinafanya kazi ipasavyo.

Kwa hiyo, tumuombe Waziri wa TAMISEMI akahakikishe kwamba anawakumbusha, maana Wakurugenzi wengi wameahidi kushughulikia ule upungufu ulioonekana na wengi wameahidi kwa maandishi. Tuombe Ofisi ya Katibu Tawala ya Mkoa kuhakikisha kwamba anazisimamia hizi Halmashauri ipasavyo ili hata masuala mengine *CAG* anakuwa anapunguziwa kazi kwa sababu wao wapo kila siku na wana watumishi katika ngazi ya Mkoa wenye fani mbalimbali na wanaweza kusimamia hizi Halmashauri ndani ya Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni deni la 10% ambapo Halmashauri zinatakiwa zitenge fedha kwa ajili ya kukopesha vijana na akina mama ili waweze kupata mikopo ambayo riba yake ni nafuu sana. Tatizo ambalo tumeligundua fedha hizi hazina akaunti maalum benki, kwa hiyo, zinakuwa kwenye *pool* moja na Halmashauri zetu pale *OC* zinapochelewa wanatumia fedha hizi. Kwa hiyo, niombe Waziri wa TAMISEMI alichukue hili, apeleke mwongozo waidhinishe Halmashauri ili ziweze kufungua *account bank* ziwe maalum kwa ajili ya kuweka hizi fedha za 10% baada ya kuwa wamezikusanya ili kuongeza udhibiti wa kutokutumia kwenye matumizi mengine. *(Makofi)*

Jambo lingine ni suala zima la Kamati za Bunge kuwa na ufinyu wa bajeti. Tunaelewa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 63, wajibu wa Bunge ni kutunga sheria na kuisimamia Serikali na kupitia hizi Kamati tunakuwa tunaisimamia Serikali lakini fedha zimetengwa kwa kiasi kidogo na hatukamilishi kazi. Kwa hiyo, tutakuwa tuna-*save* kumi lakini kwa usimamizi ambao hatuufanyi tunapoteza mia. Kwa hiyo, niiombe Serikali kwenye mapendekezo ya mpango tulichangia hivyo na Waziri wa Fedha ahakikishe kwamba bajeti ya Bunge isiwe chini ya 20% ya bajeti ya mwaka wa fedha wa 2015/2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kuchangia ni kuhusu operesheni za Halmashauri zetu. Makusanyo ya ndani yana mgawanyo kwa mujibu wa kanuni na sheria, kuna 60% iende kwenye miradi ya maendeleo,

20% maeneo mengine na 10% kwa vijana na akina mama. Niombe Ofisi ya *CAG* ikasimamie sana mgawanyo wa hizi fedha wanazokusanya wenyewe *(own source)* kulingana na sheria ili tuhakikishe kwamba miradi ya maendeleo kwenye Halmashauri zetu na kwa wananchi wetu hasa maeneo ya afya, elimu na maji inafanyika kwa fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kwa kuunga mkono ripoti ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na niombe Serikali ikatekeleze mapendekezo yote ambayo yameonyeshwa mule ndani na sisi kama Kamati ihakikishe kwamba tunapata mrejesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mbogo. Tunaendelea na Mheshimiwa Aisharose Matembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis na Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali ajiandae.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia mjadala ulioko mbele yako sasa. Awali ya yote namshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, mwingi wa neema kwa kunijalia uzima na afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutoa pole kwa Watanzania wote, familia, ndugu, jamaa na marafiki kwa msiba uliotufika wa kuondokewa na Spika Mstaafu, Marehemu Mzee Samuel Sitta. Enzi za uhai wake aliweza kutoa mchango mkubwa wa maendeleo katika Taifa hili hivyo basi hatuna budi kumuunga mkono na kumuenzi kwa vitendo vyake vizuri. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi, Amina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na umuhimu wa Halmashauri katika kuleta maendeleo ya Taifa hili bado kuna ubadhirifu mkubwa wa watendaji wa Halmashauri katika usimamizi na utekelezaji wa miradi na hii husababisha miradi kutokukamilika kwa wakati na mingine kuvunjika kinyume cha mikataba. Ukitazama kitabu hiki cha taarifa yetu, ukurasa wa 8 utaweza kuona baadhi ya mifano ya miradi ambayo haijakamilika au kutekelezeka. Mfano, mradi wa maji katika Kijiji cha Kayenze Jijini Mwanza wenye thamani ya shilingi milioni 618.7, mradi huu haukutekelezwa. Mradi wa maendeleo wa shule ya sekondari wa ujenzi wa bweni wenye thamani ya shilingi milioni 94.2 katika Kijiji cha Ndogosi na shilingi milioni 100.13 katika Kijiji cha Ruanda katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ambao haujakamilika na mifano mingine inajionesha hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe katika Kamati ya *LAAC*. Katika utekelezaji wa majukumu yetu, tumebaini mambo mengi hayako sawa katika Halmashauri zetu kwani kuna ubadhirifu mkubwa wa rasilimali za umma pamoja na matumizi mabaya ya fedha ambayo yanakinzana na sheria na kanuni za fedha za Serikali za Mitaa. Hapa naishauri Serikali kuweka sheria kali na kuzisimamia kwa uwazi ili watendaji ambao wanakwenda kinyume na matarajio ya Watanzania na kinyume na dhamira safi ya Mheshimiwa Rais wetu ambaye anataka kuona nidhamu katika rasilimali za umma washughulikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara kwa mara tunakaa hapa tukiwajadili watendaji wabadhirifu wa mali za umma wakati sheria zipo kwani hawa watendaji wana pembe? Kwa nini wasishughulikiwe kikamilifu? Nini *commitment* ya Serikali juu ya jambo hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakati mwingine Serikali inahusika kwenye udhaifu huu kwa kuwaacha watendaji wa Halmashauri kwenye kituo kimoja kwa muda mrefu. Hii humfanya mtendaji kujisahau au kufanya kazi kwa mazoea na wakati mwingine watendaji wengine kukaimu nafasi zao kwa muda mrefu. Kama wana uwezo kwa nini wasithibitishwe? Kama hawana uwezo kwa nini wasiondolewe katika nafasi hizo ili tuweze kuwabana vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumebaini Halmashauri nyingi hazizingatii Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011, aidha, kwa makusudi au kwa matakwa yao binafsi. Tulibaini baadhi ya Halmashauri zinafanya manunuzi ya bidhaa na huduma nje ya bajeti husika wakati kanuni zinazitaka kufanya manunuzi kulingana na bajeti zilizoidhinishwa. Katika Halmashauri nyingine hakukuwa na kamati za manunuzi hivyo kutokudhibiti ubora na idadi ya bidhaa kulingana na thamani ya pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tulibaini baadhi ya watendaji hutoa zabuni kwa wazabuni ambao hawana sifa wala vigezo vya kupewa zabuni hizo na kusababisha mikataba mingi kuvunjika kabla ya utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali iendelee kuwabana watendaji ambao hawazingatii kikamilifu Sheria ya Manunuzi ya Umma ambao mara nyingi wamekuwa wakiitia hasara Serikali na kusababisha upotevu wa fedha za umma. Kwa upande mwingine naiomba Serikali kupeleka pesa za miradi ya maendeleo kwa wakati kwani kwa kufanya hivyo wataweza kuondoa mianya ya kupanda gharama za miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto nilizozitaja hapa juu naongea kwa masikitiko makubwa juu ya jambo hili, Halmashauri zetu nyingi zimekuwa hazipeleki 10% kwenye Mfuko wa Wanawake na Vijana na hii

imesababisha vijana kutokupata fursa za kujiajiri au kufanya miradi ya maendeleo. Fedha hizi zingekuwa zinapelekwa kwa wakati zingeweza kusaidia vijana kujiajiri au kujikwamua kiuchumi. Mbali na watendaji kushindwa kupeleka 10% kwa vijana na wanawake lakini pia wameshindwa kupeleka 20% za fedha zinazotoka Serikali Kuu kwa vijiji kana kwamba pesa hizo ni za hisani na siyo lazima. Kwa hiyo, naiomba Serikali, kwa kuwa hakuna sheria za kuwabana watendaji kupeleka kwa wakati 10% kwa vijana na wanawake na 20% kwa vijiji itunge sheria ili kuhakikisha agizo hili linatekelezwa kwa wakati na kwa mtiririko unaofaa. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamezungumzia mengi, kwa haya machache naomba niishie hapa. Ahsante kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Matembe. Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis atafuatiwa na Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali na Mheshimiwa Japhary Michael ajiandae.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nashukuru kwa kupata nafasi hii adhimu katika Bunge lako Tukufu ya kuweza kuchangia hoja ya *PAC* na *LAAC* kama hivi nitakavyoelezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Kamati na *CAG* wote fedha za kufanyia kazi zilikuwa ndogo, lakini tumshukuru Mwenyezi Mungu kila mmoja ilibidi atekeleze wajibu wake ili suala hili liweze kufanikiwa. Ukweli ni kwamba kulikuwa na uhaba wa fedha za kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (*NSSF)*. Kulikuwa na hoja hapa ilizungumzwa kuhusu ujenzi wa Kigamboni ambapo *NSSF* waliingia mkataba na *Azimio Housing Estate*. *Azimio House Estate* ilikuwa watoe ekari 20,000 za ujenzi huo kulingana na makubaliano ya mkataba. Kiukweli ekari walizotoa ni 300. Makubaliano yao ilikuwa kama wangetoa ekari 20,000 ilikuwa na sawasawa na 20% ya hisa na 35% ya hisa ilikuwa ni kuchangia fedha, lakini hayo hayakuweza kutendeka na ndiyo maana ujenzi wa Kigamboni ukasuasua na kusimama kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya Kamati aliyoeleza Mwenyekiti nakubaliana nayo kwamba kuundwe Kamati Ndogo iweze kusimamia na kufuatilia nini kilichokwamisha, nini ilikuwa tatizo hata makubaliano hayo hayakufikiwa na mradi huo ukawa haukuendelea. Taarifa hiyo baadaye iletwe Serikalini kuangaliwa na kujadiliwa hadi suala hilo liweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kuongelea Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Umma. Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma una matatizo, baadhi ya wastaafu wetu wanahangaika, hawalipwi na kutokana na upungufu uliojitokeza katika tathmini ya kitaalam kwa muda mrefu mfuko huo umekuwa unasuasua haufanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona mfuko huu unakwamishwa na Serikali, inatakiwa Serikali ikikopa kwenye mifuko hii iweze kulipa. Serikali imechukua fedha za mfuko huu na tumefanya kazi zetu, lakini hatulipi tutegemee hawa wastaafu wetu watapata fedha wapi na wanategemea walipwe na mfuko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa tathmini iliyofanyika inaonesha kuanzia mwaka 1999 hadi leo wazee wetu wanahangaika. Wengine hawana watoto, wengine hawajiwezi, tunategemea hawa watapata wapi matumizi yao? Ingawa wamezungumzia kwamba wanategemea Februari watamaliza tathmini yao na waweze kuwalipa, hivi kweli mtu ataweza kukaa bila kutumia, bila kula mpaka ifike Februari? Naiomba na Serikali iweze kulipa madeni ya mashirika yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala lingine la Bandari. Udhibiti wa mapato ya bandari kidogo uko hafifu, na kwanini nasema hivyo? Kuna meli nne zilikuja bandarini lakini hakuna mapato yaliyokusanywa kutokana na meli hizo kuwepo pale. Meli ziliondoka na baada ya kuondoka, baada ya muda wa miezi 18; *CAG* katika kuangalia taarifa kwenye vitabu vya hesabu za bandari ile anakuta kwamba meli nne zimeingia na zimetoka, makusanyo hayakupatikana kiusahihi na meli zimeshaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie ni meli ngapi zimeingia. Hizi nne *CAG* ameziona, je, hizo za nyuma ambapo siku nyingine hata kwenye vitabu hazikuingizwa? Inamaana wao wenyewe Bandari wanajikosesha mapato yao kutokana na kutokuwa udhibiti katika makusanyo yake.

Mimi ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kufanya ziara bandarini, kaujua udhaifu wa bandari yetu na ndiyo maana Mheshimiwa Rais ikabidi aende akaangalie hali halisi na sote tulisikia kwenye vyombo vya habari nini Mheshimiwa Rais alichogundua na matokeo yake yalikuwa nini. Ushauri wangu, naiomba bandari iweze kudhibiti mapato yao maana tunaitegemea kimapato. Wakiweza kudhibiti mapato yao ndipo Serikali yetu itakapoweza kufanyakazi na wananchi tutafaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba kuzungumzia Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*. Taarifa ya *CAG* inayoishia Juni 30, 2015 ilionesha kwamba misamaha ya kodi imepungua kufikia jumla ya bilioni 1.6, sawa na asilimia 15.1

kwenye makusanyo ya *TRA*. Ingawa tunasema misamaha ya kodi imepungua lakini Serikali bado inapoteza mapato yake kutokana na misamaha hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninao mfano naweza kutoa. Kuna misamaha ya kodi iliyotolewa kwenye mafuta yenye thamani ya shilingi bilioni 22.3 ya Kampuni ya Uchimbaji Madini ya Geita na *Resolute*. Mafuta hayo badala ya kutumiwa na Kampuni ya Uchimbaji Madini ya Geita na *Resolute* wao wakawapelekea wakandarasi wengine kuyatumia. Sasa msamaha umepewa wewe kisha wewe unampelekea mwenzio, hilo si tatizo? Tena tatizo sugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningeiomba Serikali, masuala kama haya *CAG* akishayaona lazima tuwe tunayafuatilia. Lakini wakati mwingine ufuatiliaji unashindikana kwa sababu fedha ambayo ndiyo nyenzo hakuna.

Kamati imetaka kufuatilia ili ipate uhakika, inashindwa kwenda kutokana na nyenzo ziko hafifu. Sasa nafikiri kwa haya machache niliyoyazungumza na yote ambayo yanakwamishwa na nyenzo za kifedha naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Fakharia Khamis. Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali atafuatiwa na Mheshimiwa Japhary Michael, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza ajiandae.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii adhimu na mimi niweze kuchangia taarifa hizi mbili za *oversight committee* ya *PAC* na *LAAC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaingia ndani kwenye kuona madudu makubwa ambayo yameainishwa na Mdhibiti pamoja na viongozi wa hizi Kamati, niungane na wenzangu na mimi kuzungumzia juu ya weledi mdogo walionao Wakurugenzi na Wakuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ambao uko dhahiri kwamba kama kuna jambo ambalo Halmashauri zetu zitakwama ni kuwa na watendaji dhaifu, ni kuwa na Wakurugenzi ambao hawajui walifanyalo. Na jana hapa wakati Mheshimiwa Waziri wa Habari anajibu baadhi ya hoja nilistaajabu sana aliposema kwamba walioteuliwa ndio watakaokuwa watekelezaji wazuri wa Ilani ya CCM. Kama CCM imekaa ikiwategemea Wakurugenzi wa aina ile ninawathibitishia mnakwenda kushindwa. Kama aina ya Wakurugenzi tulionao ndio mnaowategemea kufanikisha Ilani ya Chama cha Mapinduzi wanakwenda kushindwa muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, aina ya Wakurugenzi tulionao hawajui walitendalo na Mheshimiwa Waziri mimi nakuambia tuna Wakurugenzi ambao wanafanya mambo ya ajabu kweli kweli kwenye Halmashauri. Baraza la Madiwani linakaa likapitisha maamuzi yake, Mkurugenzi anabeba *document* anampelekea Mkuu wa Wilaya anakwenda kumwambia hebu pitia haya sahihi kweli haya? Yaani Mkuu wa Wilaya sasa ndiye anayefanya maamuzi kwa niaba ya Halmashauri. Kwa hiyo, tumekuwa na Wakurugenzi ambao hawajui walifanyalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nawaomba katika namna ya kuwasaidia na kuzisaidia Halmashauri zetu, Serikali ihakikishe inatoa mafunzo kwa Wakurugenzi hawa mliowateua *from nowhere*. Mfumo wa utendaji wa kazi Serikalini unajulikana na unatambulika, huwezi kumtoa mtu kutoka huko kwenye *NGO* ukampeleka kwenye taasisi kubwa kama Halmashauri, ni shida. Mmetengeneza matatizo makubwa kwenye Halmashauri zetu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa wapi inatoka?

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**T A A R I F A**

**NAIBU SPIKA:** Aaah Mheshimiwa Costantine Kanyasu, Mheshimiwa Bobali naomba ukae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru, nilikuwa naomba sana kwa sababu nimeona *attacking* ya Wakurugenzi inafanana, lakini hawafanani. Mimi Mkurugenzi wangu ni mpya, lakini uwezo wake ni mkubwa sana. Sasa hii kesi ingekuwa *specific*. *Information* zinatoka kama vile watu wote tunakaa kwenye Jimbo moja halafu si kweli hatuko Jimbo moja. Kama mmoja hafai ni huyo hafai. Azungumzie *specific case* siyo wote, kuna wengine uwezo ni mkubwa na wanauelewa mkubwa, hawakutoka kwenye *NGOs* na wanauwezo mkubwa. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bobali unaikubali taraifa hiyo kwamba Wakurugenzi wanatofautiana uwezo wao?

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hajanipa taarifa alikuwa anachangia, kwa hiyo *obvious* siwezi kuikubali na mimi ninachokichangia ninachangia kwa mujibu wa taarifa hii iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya *LAAC,* kwamba asilimia 60 ya Wakurugenzi waliokutana nao wameonyesha udhaifu kwamba hawajui walitendalo, ndiyo

taarifa inavyosema. Hatuchangii kwa mujibu wa mtu, hapa ninachozungumza tunachangia Taarifa za Kamati. Kwa hiyo, ukisema ukitoa taarifa maana yake unampa taarifa Mwenyekiti wa Kamati aliyewasilisha hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika kwa hiyo niendelee kusisitiza kuna haja ya kuwapa mafunzo, kuna haja ya kuwapa semina ili watende vile mtakavyo, ili watende kwa mujibu wa sheria na ili tupate manufaa na mafanikio kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *TIB (Tanzania Investment Bank),* ukisoma Taarifa ya Mkaguzi ukasoma na Taarifa ya Kamati ya *PAC* inaonesha kwamba *Tanzania Investment Bank* imetoa mikopo zaidi ya shilingi bilioni 64 kwa watu ambao hata kuwataja hawataki. Taarifa ya Kamati inaeleza kwamba hata Mwenyekiti wa Bodi alivyoitwa kwenye Kamati aje aeleze kwamba hizi shilingi bilioni 64 imewakopesha akina nani ameshindwa kuwataja na katika masikitiko yangu makubwa Mwenyekiti wa Bodi juzi alikuja hapa kutueleza mambo ya *EPA,* namheshimu sana Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi, akaonesha kwamba ni mzalendo sana. Kama ana kiwango hicho cha uzalendo kinachomshinda kutaja hawa waliokopeshwa bilioni 64 ni nini? Na taarifa inaonesha kwamba wao wamefungua kesi 21 kuwashtaki watu, akina nani? Wanapata ukakasi gani kuwataja hawa waliowakopesha shilingi bilioni 64? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii tuombe, kama Mwenyekiti wa Bodi anashindwa kutaja au kama Mtendaji Mkuu wa hii Benki anashindwa kuwataja, rungu lako la Bunge lifanye kazi ili hawa waliokopeshwa shilingi bilioni 64 ambao hawatajiki waje waelezwe ndani ya Bunge humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie juu ya suala la misamaha ya kodi kwenye uingizaji wa mafuta. Mheshimiwa Waziri wa Fedha anatafuta sana pesa kwenye kodi. Taarifa ya Mkaguzi inaeleza kwamba mwaka 2012/2013 *Geita Gold Mines* na *Resolute Tanzania Limited* walipatiwa msamaha wa kodi ya mafuta, lakini wao ule msamaha wakautumia nje ya mizania, nje kabisa ya utaratibu wakahamisha yale mafuta kwenda kupeleka kwenye kampuni nyingine. Zaidi ya bilioni 22 zinaoneshwa hapa kwamba watu wa *Geita Gold Mines* walihamisha kodi ile ya mafuta kwenda kuipa kampuni nyingine yale mafuta, jambo ambalo ni kinyume kabisa na Tamko la Serikali Namba 480 la mwaka 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji hizi bilioni 22 ambazo zilitolewa, ambazo zilikuwa ni kodi ya msamaha kwa *Geita Gold Mines pamoja* na *Resolute Tanzania Limited,* fedha hizi zipatikane, Waziri wa Fedha ulisikie hili, ulifanyie kazi ili kodi iweze kurudi kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naomba nichangie juu ya ucheleweshaji wa fedha kutoka Hazina kwenda Halmashauri na kwenda Wizarani. Kumekuwa na tabia iliyozoeleka kwamba Hazina inasubiri robo ya mwisho ya mwaka wa fedha ndipo hupeleka fedha nyingi kwenye Halmashauri, ama inasubiri robo ya mwisho wa mwaka kupeleka fedha nyingi Wizarani, matokeo yake nini kitatokea? Miradi ya maendeleo iliyokuwa inatekelezwa inaongezeka riba na Serikali inapata hasara kubwa kwa kuwa imechelewesha malipo ya wakandarasi. Lakini jambo la pili, fedha nyingi zinapelekwa katika Halmashauri katika kipindi ambacho muda wa utekelezaji unakuwa unakaribia kwisha kabla ya mwaka wa fedha kuisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma *report* inaonesha wazi kwamba katika mwaka wa fedha 2012/2013 zaidi ya shilingi trilioni 1.8, fedha ya maendeleo haikupelekwa, zaidi ya asilimia 38. Lakini pia ripoti inaonyesha kwamba zaidi ya Shilingi bilioni 19 zilipelekwa katika kipindi cha mwisho kabisa cha robo ya mwaka, fedha za *OC* na fedha zile hazikutumika. Katika mazingira kama haya tunatengeneza mwanya wa watendaji wetu wa Halmashauri wafanye vitendo ambavyo siwezi kusema kama ni wizi, isipokuwa si vizuri kwa mujibu wa sheria za fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine Serikali imepunguza sana uwekezaji wake kwenye baadhi ya taasisi. Ukisoma ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeonesha kwamba uwekezaji wa Serikali katika Shirika la *TAZARA* hisa zake zimepungua sana. Serikali imepunguza hisa nyingi katika Benki ya *NBC,* lakini pia hata katika mashirika mengine ambayo hapo awali yalikuwa na hisa nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kupungua kwa hisa za Serikali katika *TAZARA* ina-*reflect* nini? Serikali imekuwa na uwekezaji mdogo katika hili shirika la reli ambalo tuna-*share* na watu wa Zambia. Kama Serikali ya Tanzania haipeleki fedha za kutosha *TAZARA which means* kama wenzetu wa Zambia kama wataendelea kuwekeza katika hili shirika mwisho wa siku hawa watu wa Zambia watakuwa wanamiliki hisa nyingi *TAZARA* kuliko vile ambavyo sisi Watanzania tunamiliki hisa maeneo hayo. Ni jambo la aibu sana shirika la reli ambalo tunalimiki kwa pamoja, tumelianzisha kwa pamoja sisi Watanzai kuwa nyuma katika kupeleka fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni la msingi sana lazima tulizungumzie ni suala la Halmashauri na fedha za vyanzo vilivyofutwa. Halmashauri zetu zinajulikana kwamba kuna vyanzo Serikali imevifuta katika kumpunguzia mzigo mlipa kodi kule ndani ya Halmashauri, hili jambo lilikuwa jema sana na sisi tulidhani kwamba ili Halmashauri ziweze kujiendesha kwa ufanisi Serikali mngekuwa mnapeleka pesa kwa wakati. Lakini leo hii tuhojiane humu ni Halmashauri gani imepata pesa kutoka Serikalini au kutoka Hazina

katika vyanzo vilivyofutwa na Serikali? Inatoa *justification* kwamba Serikali mnahatarisha uhai wa Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Halmashauri huko ni mbaya na ubaya huu umechochewa kwa kiwango kikubwa kabisa na kufuta baadhi ya vyanzo ambavyo vilikuwa vinatusaidia kwenye Halmashauri kuendesha Halmashauri zetu. Mmevifuta, kufanya *compensation* mpaka sasa hamfanyi, pesa hampeleki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwahiyo ni jambo ambalo Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa TAMISEMI wanatakiwa kutazama, kwa sababu Halmashauri zinakufa na Halmashauri zikifa ita-*justify* kwamba *performance* yako siyo nzuri Mheshimiwa Waziri wa Fedha, haitakuwa jambo jema kwako Halmashauri kufa kwa kikwazo tu kwamba Waziri wa Fedha hapeleki fedha kwenye Halmashauri kutokana na vyanzo vilivyokufa.

Kwa hiyo mimi niombe sana, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI wewe unajua, unazunguka kwenye Halmashauri unajua kwamba Halmashauri zote zina vilio vya juu ya fedha za vyanzo vilivyofutwa, kwa hiyo ni jambo la msingi wewe kumbana Waziri wa Fedha aweze kupeleka hizo fedha katika Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho la kumalizia, naona muda umekaribia sana, kwamba Mkaguzi na Taarifa za Kamati zinaonesha wazi, Mkaguzi fungu la pesa alilotengewa ni dogo kiasi kwamba halimuwezeshi kufanyakazi yake ipasavyo, na cha ajabu ni kwamba kwa mujibu wa bajeti inaonesha kwamba mtapeleka fedha shilingi milioni sijui 50 katika kila kijiji, ingawa kwenye bajeti hazionekani lakini wenyewe mnasema bado maana yake hayo maneno mnayarudia kwamba mtapeleka hizo fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama mnapeleka fedha vijijini maana yake kwamba mnapanua wigo wa kazi za Mkaguzi kutoka kwenye *central government* kwenda mpaka kwenye *local government* mpaka kwenye *village level,* kwa sababu popote zilipo fedha za Serikali Mkaguzi ana wajibu wa kwenda kuzikagua. Ikiwa hamjamtengea fungu la kutosha huyu Mkaguzi hizi kazi ataifanyaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi napata wasiwasi kwamba tunakuwa na Serikali ya aina gani ambayo inaogopa kivuli chake yenyewe, Serikali inayoogopa kukaguliwa, Serikali inayopambana na rushwa kwamba mnajionesha, mnaji-*brand* kwamba nyie mnapambana na rushwa lakini kumuwezesha Mkaguzi kwenda kukagua hamtaki, tutajuaje weledi wenu wa kupambana na rushwa? Mimi napata wasiwasi kwamba inawezekana

mnatumia kumminya huyu Mkaguzi asiende kuwakagua ili udhaifu wenu na aina ya ufisadi mwingine mnaotengeneza huko sisi tusije tukaujua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninaomba sana, ninaomba sana, ikiwa Serikali inampango wa kumfunga kama ni midomo au kama ni miguu huyu Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali asiende kukagua fedha za Serikali mnajikaanga kwa mafuta yenu ninyi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Bobali, Mheshimiwa Japhary Michael atafuatiwa na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Issa Mangungu ajiandae.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, hii na namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na kuweza kuchangia katika hoja hizi za Kamati hizi mbili za *PAC* na *LAAC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitajikita kwenye Kamati ya Serikali za Mitaa na ninaunga mkono hoja zote ambazo zimeibuliwa na Kamati ya *LAAC* kwamba ni hoja za msingi zinazoonyesha baadhi ya matatizo ambayo yapo kwenye utendaji wa Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilikuwa naomba pia *mindset* za Wabunge zibadilike kidogo. *The way* tunavyokwenda tunataka kuipeleka Serikali inapotaka kwa mtazamo wangu. Lengo la Serikali ni kuua Serikali za Mitaa, ndilo lengo la Serikali. Tunapojaribu kwenda tunataka kuwathibitishia kwamba Halmashari hazina uwezo wa kutimiza wajibu wake jambo ambalo si la kweli kabisa. Halmashauri zetu zina uwezo wa kutimiza wajibu wake. Kama tutarudi nyuma, *reform* iliyofanyika mwaka 1998 mpaka 2008 ilikuwa ina lengo la kuzifanya Halmashauri ziwe na uwezo wa kujitegemea zaidi jambo ambalo Serikali ya Awamu ya Tano hailitaki kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja za Kamati zinasema Halmashauri hazina uwezo wa kukusanya fedha vizuri, zinakusanya kutoka wapi? Vyanzo muhimu vya mapato vimechukuliwa na Serikali Kuu. Sasa Halmashauri zinakusanya kutoka wapi? Mimi naamini bado Serikali ya Awamu ya Tano haina dhamira ya dhati ya kuzisaidia Halmashauri, ina dhamira ya kupora madaraka ya wananchi kuyarudisha kwenye *central government*. Mimi ndiyo ninachokiona katika mawazo yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi naomba, la kwanza kubwa kuliko lote Wabunge wailazimishe Serikali itambue wajibu wa Serikali za Mitaa na dhamira ya kuanzishwa kwa Serikali za mitaa za kupeleka madaraka kwa wananchi.

Tukifanikiwa kuifahamu hiyo dhana vizuri, na nimuombe Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI awaite Wenyeviti wa Halmashauri na Mameya wakae na Wabunge, kila mmoja azungumze matatizo ya Halmashauri ili Wabunge watambue vizuri matatizo ya Halmashuri ili wakijadili hapa ndani waelewe vizuri kwamba Halmashuri zina matatizo gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu inawezekana hata sisi baadhi ya Wabunge hatufahamu vizuri matatizo ya Halmashauri ndiyo maana tunapelekea kuzilaumu Halmashauri kama vile wao ni wakosaji kuliko Serikali Kuu. Kwa hili la kwanza nilikuwa naomba kama Waziri mwenye dhamana anaona inafaa na itampendeza basi afanye hivyo kwa manufaa na malengo mazima ya kusaidia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunazungumzia habari ya Wakurugenzi. Ukizungumzia Wizara nyingi kama Wizara ya Ujenzi utasikia wanakuambia tunataka tupate ma-*CEO* wazuri watakaoimarisha shirika la ndege, watakaoimarisha bandari, wengine mpaka tumewatoa nje. Lakini ni maajabu kwamba Wakurugenzi tunawachukua kutokana na itikadi zao za kisiasa tunawapeleka kwenye Halmashauri, kitu ambacho ni *contrary* kabisa na dhana ya uboreshwaji wa Serikali za mitaa tuliofanya 1998 mpaka 2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la uboreshwaji ni kwamba Wakurugenzi watafutwe watu wenye uwezo na ndiyo maana wakatakwa wasiusike na mambo ya kisiasa. Lakini leo Mheshimiwa Waziri wa Habari anatuambia kwamba Serikali imepeleka watu wa kutekeleza ajenda, watu wa kutekeleza ajenda ni Wakuu wa Wilaya. Watu wa kutekeleza ajenda ni Wakuu wa Mikoa, watu wa kutekeleza ajenda si Wakurugenzi wala Makatibu Tawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unapopeleka hawa watu wa kutekeleza ajenda Wakurugenzi ni nani atakayesaidia Halmashauri zifanye kazi? Unapopeleka mtu kwa sababu unamfahamu kwa uzuri, haiba yake kwa namna anavyovyaa au kwa sababu ni rafiki yako, utafanyaje hizo Halmashauri zifanye kazi? Kila siku Taarifa za Kamati zitakuwa na madudu yasiyoisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mmeona mwaka 2013/2014 kulikuwa na taarifa za hati safi za Halmashauri zaidi ya 133, 2014/2015 zaidi ya asilimia 68 ya Halmashauri zina hati chafu, ni kwa sababu gani, kwa sababu mmepeleka watu gani wenye uwezo wa kusimamia hizo Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo rai yangu kwa Serikali kama tunataka kuisaidia nchi hii lazima tuzisaidie Serikali za Mitaa. Kama tunataka kuua nchi hii tubaki na kauli na maneno yasiyoisha ya kisiasa tuue Serikali za Mitaa, ndio mtazamo wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tufike mahali ambapo tunawachagua Wakurugenzi kwa vigezo. Kama ni lazima sana tubadilishe Sheria Namba 7 na Namba 8 hapa ili tupeleke Wakurugenzi ambao wamechaguliwa kwa vigezo, si Wakurugenzi wanaopelekwa kwa sababu ya kujuana. Ukiangalia wakurugenzi waliopelekwa katika Halmashauri leo kuna watu wanaowatetea hapa. Kuna Wakuu wa Idara wenye uwezo kabisa lakini hawakuchaguliwa kuwa Wakurugenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua ni mamlaka ya Rais na mimi sitaki kubishana na mamlaka ya Rais lakini Rais ashauriwe vizuri. Anachagua akina nani wa kwenda kwenye Halmashauri? Leo mnazungumzia habari ya ubovu wa mwaka 2014/2015 sasa mtaona madudu mwaka wa 2016/2017, ndio mtakaoona madudu kwa watu mliowapeleka Halmashauri. Naomba hilo suala lichukuliwe katika uzito wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna suala la Halmashuri, kama nilivyosema kwamba mnasema halikusanyi vyanzo vya mapato. Tumekuja kwenye Bunge la Bajeti hapa mmechukua chanzo muhimu sana cha Halmashauri cha kodi ya majengo na mmetudanganya hapa ndani ya Bunge kwamba chanzo kile mmeshakikusanya mtakuwa mnakusanya kama vile mnavyokusanya asilimia 30 ya *land rent* na mtarejesha. Tunapozungumza leo hakuna shilingi moja imerejeshwa, Halmsahauri zinafanyaje kazi? Mtakuja kuzilaumu kila siku kwenye Taarifa za *LAAC* na *LAAC* yenyewe ndiyo hiyo hata fedha hamuipi, hamumpi Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Mahesabu ya Serikali fedha kwa sababu hamtaki Halmashauri zifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba vyanzo ambavyo ni vya lazima, kwa sasa hivi kuna mpango kwa mujibu wa sheria tuliyopitisha, inawezekana hata mkachukua *service levy* katika Halmashauri, Halmashauri zitajiendesha na nini? Kwa hiyo naomba vyanzo vya Halmashauri viachwe, halafu tuwapime Wakurugenzi na Watendaji wa Halmashauri kwa uwezo wao. Tuwaongezee *manpower,* tuwaongezee namna ya kukusanya vizuri, *TRA* hawana uwezo wa kukusanya mapato yote katika nchi hii kama mnavyotaka kuwapa hiyo *burden* ambayo hawaiwezi. Mapato ya bandari hawawezi kukusanya, mapato ya utalii hawawezi kukusanya, mnataka kuwaongezea mapato ya Halmashauri ya sababu gani? Nilikuwa naomba Serikali iliangalie hilo kwa makini sana kama mnataka kuzilaumu Halmashauri kwamba hazina uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za miradi ya maendeleo haziendi, hazipo. Angalau kule nyuma tulikuwa tunapata asilimia nane, asilimia tano, leo hazipo mpaka tunavyozungumza karibu nusu ya kwanza inakwisha, hakuna fedha za mradi wa maendeleo. Leo kuna hoja yetu ya Kamati inasema miradi mingine inachukua muda kukamilika, itakamilikaje kwa muda kama fedha haziendi? Miradi inakamilikaje kwa muda wakati fedha hampeleki? Miradi

mingine mingi inategemea fedha za Serikali kuu, haziendi! Itakamilikaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna hoja ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwamba hati nyingi chafu zimesababishwa na Halmashauri kutokuwa na taarifa sahihi ya mali zake iliyonazo.

Sasa mimi nashauri Serikali na nakushauri Mheshimiwa Waziri, zisukume Halmashauri zote zitengeneze *database,* zifahamu wapi zinakusanya mapato, zifahamu mali zake iliyonazo *(inventory)* zake ili hiyo hoja ya ukaguzi isijirudie tena. Na ili zifanye hivyo ni lazima zitenge fedha ya kutosha kwenye bajeti katika kitengo cha takwimu. Bila ya kutenga fedha za kutosha katika kitengo hawatafanikiwa, hizi hoja za ukaguzi zitaendelea na bado Halmashauri zitapata hati chafu, zenye mashaka ambazo sio za lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la kukaimu, kwamba ni mojawapo ya sababu ambazo zinazifanya Halmashauri zisifanye vizuri. Kamati imeonesha kwamba Serikali inachelewa kupeleka *permanent employer's* katika Halmashauri, hilo ni tatizo la kwanza ambalo Serikali inatakiwa ikabiliane nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, Wakurugenzi wetu tunaowachagua hawakai maofisini kufanya kazi zao, wanakaimisha nafasi zao kila siku. Mkurugenzi anakaimisha nafasi yake kikao cha Kamati ya Fedha hayupo, yupo kwenye Kamati ya Siasa ya CCM anakuwa anapeleka taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya CCM, sasa utafanyaje kazi? Mkurugenzi hakai. Leo ameitwa na Mkuu wa Mkoa asubuhi, Mkurugenzi anaripoti kwa Mkuu wa Mkoa asubuhi, kwa Mkuu wa Wilaya jioni. Halafu hawezi kukaa kwenye Halmashauri, atafanyaje kazi zake?

Sasa matokeo yake sio tu kwamba kukaimisha kwa maana hiyo ya kwamba Serikali haijapeleka hao waajiriwa wa kudumu lakini hata Wakurugenzi wenyewe hawakai kwenye Halmashauri zao kufanya wajibu wao. Matokeo yake Mkurugenzi muda wote anapata taarifa zake za utekelezaji kupitia kwa watu wa kukaimu tu, kwa hiyo hapati taarifa ambazo ni sahihi, hapati namna ya kupambana na madiwani wake ili ajue namna ambavyo anaweka madiwani wake sawasawa ili wapeleke Halmashauri mbele. *(Makofi)*

Kwa hiyo ni lazima utoe agizo, Wakurugenzi wasimamie vikao vyote wanavyovisimamia katika Halmashauri *unless* kuwe na *strong reason.* Lakini kila Mkurugenzi kikao cha Baraza anakuwa yeye, kikao cha Kamati ya Fedha anakuwa yeye, kikao cha Afya na Uchumi anakuwa yeye, kikao cha Mipango Miji anakuwa yeye ili apate taarifa halisi kama Katibu halisi wa Baraza. *Otherwise* kila siku watakuwa wanaletewa taarifa za uongo na hata kujibu kwenye Kamati hawawezi kujibu wanapoitwa kwenye vikao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka nizungumzie suala la *internal auditors* ambalo limezungumzwa kama tatizo pia kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, *internal auditors* tulionao ni kweli kwamba wanafanya kazi chini ya Mkurugenzi, na kwa misingi hiyo wataripoti *according* kwa matakwa ya Mkurugenzi kwa sababu hawana fedha wakipewa fedha kidogo wataripoti kadri Mkurugenzi anavyotaka. Sasa usipopeleka Mkurugenzi ambaye ni mahiri ukapeleka Mkurugenzi mla rushwa, Mkurugenzi asiye na mtazamo, asiyefahamu kwamba Halmashauri ni sehemu yake kwa vyovyote vile *internal auditors* hawezi kumsaidia Mkurugenzi na Halmashauri lazima ifanye vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakati mwingine *internal auditors* wanaweza wakawa wanasaidiana kuharibu Halmashauri kwa sababu wakati mwingine wanaweza wakatumiwa vibaya na hata madiwani ambao hamtaki kuwapa mafunzo. Mmeamua sasa hivi kwamba Madiwani hawapati mafunzo, Diwani hawezi kwenda hata kwenye Halmashauri nyingine kujifunza mpaka Mkuu wa Mkoa atake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hizi Halmashauri mnapozibana namna hii, zinapokuwa na *intervention* ya Mkoa namna hii, Wakuu wa Mikoa wanaingilia Halmashauri, Wakuu wa Wilaya wanaingilia Halmashauri, kila mmoja na kauli yake, mnapelekaje Halmashauri? Halmashauri kwa mujibu wa Katiba yetu ni Serikali ambayo ni ndani ya Serikali Kuu, na zina utaratibu wake. Wajibu wa Mkoa ni kutoa ushauri, wajibu wa Wilaya ni kutoa ushauri, si kuziingilia Halmashauri. Leo Wakuu wa Mikoa, Wilaya wanaziingilia Halmashauri kama ni vyombo vyao vya pale ofisini, kama ni Idara katika ofisi zao. Zinawezaje zikafanya kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunalalamika hapa bure tu kuhusu Halmashauri. Wanaoua Halmashauri hapa ni Serikali Kuu, anayeua ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Kwa hiyo kama tunataka kuzisaidia Halmashauri, Waziri mwenye dhamana ya Serikali za mitaa asaidiwe, aelimishwe, zifanyeni Halmashauri zilizo na *creativity,* watu wawe wabunifu, watu wawe na uwezo wa kujituma, watu waweze na kubuni mikakati yao halafu wasaidieni. Saidieni Halmashauri katika dhana ya *PPP* zifanye kazi vizuri na hizi hoja za ukaguzi yatapungua sana. Lakini bila kuzisaidia hizi hoja za ukaguzi yatakuja kila siku mpaka mtachanganyikiwa hapa Bungeni tu. Wabunge mtawalaumu Madiwani Bure, mtawalaumu Wakurugenzi bure lakini tatizo liko kwenye *central government,* ndio mtazamo wangu na mimi nashauri Serikali ilichukue katika uzito wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama muda wangu haujaisha nilikuwa naomba sana tuyatilie uzito mawazo ya wenzetu kwamba *CAG* apewe fedha ya kutosha, Kamati ya *LAAC* ipewe fedha ya kutosha, iende kwenye Halmashauri ifanye ukaguzi wa kutosha, itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya *PAC* ipewe pia fedha za kutosha. Tuzisaidieni hizi Kamati kama *overside committees* zetu ziweze kutusaidia kujua Halmashauri zilivyo na kujua na sisi tulivyo ili tusaidiane katika kuhakikisha kwamba nchi hii inakwenda mbele. Bila kusaidiana sisi Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, mtakaa mkitoa maagizo; ni kweli kabisa kwa mujibu wa taarifa ya Kamati Halmashauri nyingi zimekuwa zikibadilisha matumizi yake kutokana na maelekezo ya Serikali Kuu, kutokana na maelekezo ya Mkuu wa Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wana mpango wao wanaambiwa kuanzia leo mnajenga maabara, fedha zinatoka wapi? Hawaambiwi. Lazima Mkurugenzi afanye hivyo maana ni muoga atafanye? Asipofanya vizuri atatumbuliwa. Madawati yameagizwa anafanya nini? Asipofanya hivyo anatumbuliwa, hata akifanya akija kwenye hoja ya ukaguzi inampiga, anatumbuliwa. Wakurugenzi hawana hata mahali pa kupumulia wakati mwingine kwasababu mnawaumiza. Wakuu wa Idara hawana mahali pa kupumulia, ni waoga kwa sababu wanakwenda pale wakitishwa na mambo ya itikadi. Tuacheni mambo ya itikadi tuamueni kupeleka hili Taifa mbele ili tuweze kufanikiwa katika mambo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena kuipongeza Kamati, imefanya kazi yake vizuri na nadhani tuna umuhimu wa kuchukulia uzito matatizo waliyoyaona lakini Serikali itimize wajibu wake ili twende mbele. Ahsante sana kwa kunisikiliza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Japhary ahsante sana. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Mangungu. Mheshimiwa Godfrey Mgimwa ajiandae.

**MHE. CONCESTTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuongea machache kutoa maoni yangu juu ya taarifa za Kamati ambazo zimetolewa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC* kwa hiyo nianze kwa kuunga mkono maamuzi na mapendekezo ambayo yametolewa na Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maneno mengi yameshasemwa lakini ni muhimu na sisi tuendelee kuyasema, tuyawekee uzito wake lakini na kuwekea msisitizo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge lako nilirudishe nyuma wakati Serikali imefuta Serikali za Mitaa mwaka 1972 na kuweka mfumo wa madaraka Mikoani. Serikali ilifanya hii *decentralization* lakini baadae Serikali iligundua kwamba ilishindwa kutoa huduma kwa wananchi. Kwasababu Serikali za Mitaa ni vyombo ambavyo viko pale kutoa huduma kwa watu wa ngazi ya chini, lakini pia vinatekeleza Sera ambazo zinaelekezwa na Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kama wenzangu walivyosema, kama Halmashauri zitakwenda katika mwenendo huu tunakwenda kuziua na kuzifuta kama ilivyokuwa mwaka 1972. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mfumo wa ukaguzi katika Halmashauri. Wakaguzi wa Ndani hawana kasma, Wakaguzi wa Ndani wako chini ya Mkurugenzi. Katika ukaguzi wetu tumegundua Mkaguzi wa Ndani mmoja ambaye alijitokeza kujibu hoja za uhasibu wa Halmashauri. Sasa tukajiuliza, huyu ni *auditor* wa ndani lakini yeye amejitokeza kujibu hoja za mhasibu ambazo tumemuuliza, je, huyu anaweza kusimamia kweli ukaguzi katika Halmashauri yake?

Kwa hiyo tunachoishauri Serikali, ihakikishe inaimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ili Halmashauri hizi na Wakurugenzi waweze kukaguliwa na hata wenyewe hawa ma-*auditors* wa ndani waweze kushauri Halmashauri zao katika mambo ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee Mfuko wa Wanawake na Vijana wa asilimia 10. Mfuko huu uko *very sensitive,* kila Mbunge anauhitaji, anahitaji kuona Halmashauri inatoa mchango wa asilimia tano kwa vijana  na aslimia tano kwa wanawake ili waweze kuwa na shughuli za kufanya. Tuwaweke vijana wawe *busy,* wasiingie kwenye panya *road,* tuwaweke akina mama waweze kupata kazi za kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu katika ukaguzi wetu na kuhoji Halmashauri, kila Halmashauri ina deni kubwa la mifuko hii, lakini madeni hayo yamesababishwa na maagizo yanayotoka juu ambayo yanawapa *deadline* yaani yanawapa *ultimatums* ku-*raise* tengeneza madawati Halmashauri, katika miezi miwili tunaomba madawati yako tayari. Wananchi? Hawana pesa za kuchangia. Halmashauri ifanye nini? Kwa hiyo, wanachukua mafungu kutoka *own sources,* wanachukua mafungu kutoka katika *development* wanatengeneza madawati na kwa kweli kama walivyosema wenzangu imekuwa ni mwanya wa kuiba hela za Serikali. Ukiwauliza wote wanakuambia kwamba sisi tumechukua hizi pesa kwa sababu tuliambiwa tutengeneze madawati katika miezi miwili, tumetengeneza maabara katika miezi miwili, kwa hiyo,  matokeo yake pesa zinapotea bure. *(Makofi)*

Mheshimwa Naibu Spika, sasa wasiwasi wangu, hii mifuko, Halmashauri zote zinadaiwa mamilioni ya pesa, je, wana uwezo wa kulipa madeni haya? Kwa sababu kama walivyochangia wenzangu Halmashauri hizi zimekatwa mikono, haziwezi kuwa na pesa, Serikali Kuu imechukua vyanzo vyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Katika bajeti ya mwaka jana kama mnakumbuka katika kitabu cha Waziri wa Ardhi, alionesha kwamba walikusanya shilingi bilioni 54 lakini walipeleka bilioni nne tu katika Halmashauri karibu 138. Mkoa wangu wa Kagera tulipewa shilingi milioni 138, Halmashauri ya Ngara ilipewa milioni nne kitu kama hicho. Sasa unaweza kuona kama wameweza kukusanya pesa zikaenda kule juu hazirudi, hizi kwa mfano za kodi ya majengo zitarudi? Nina wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana katika kitabu chetu tumependekeza kwamba iundwe sheria ya mfuko huu. Hakuna sheria ni agizo sawa, lakini hata sheria yenyewe itazame ni jinsi gani mfumo huu unaweza kuwekwa na unaweeza kutumika. Kwa mfano, tumegundua kwamba hata makundi mengine yanayopewa mikopo ni hewa na yanayopewa hayarejeshi, kwa hiyo hiyo, mifuko haiwezi *kurotate,* hairudishi pesa tena. Kwa hiyo, mimi nashauri kwamba Serikali iziangalie hizi Halmashauri upya ziweze kupata makusanyo na ziweze kukata 5% kwa ajili ya vijana na 5% kwa ajili ya wanawake vinginevyo, itabaki katika hoja za ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Na namwomba Waziri mwende nalo hili kwamba, tuangalie upya namna ya kuweka mfuko huu, ili tuweze ku-*materialize* yaani uweze kuona kama unaweza kuleta *impact* kwa wanawake vinginevyo Halmashauri zitashindwa, mtazituhumu hapa na zitashindwa kabisa kukusanya hizi fedha na hawatakuwa na uwezo wa kuwasaidia wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye hoja ya Serikali kutokupeleka fedha. Serikali haipeleki fedha, lakini ziko Halmashauri nyingine zinapelekewa fedha nyingi nje ya bajeti. Kwa mfano katika kukagua tuligundua katika Halmashauri ya Mpanda katika mwaka wa fedha 2014/2015 walikuwa wametenga bajeti ya shilingi milioni 432 lakini wakapewa fedha shilingi milioni 303.8 ya ziada. Kwa hiyo, wakawa na fedha karibu milioni mia saba na kitu. Ukiuliza Hazina kwa nini mmewapa fedha ya ziada ambayo haipo kwenye bajeti? Hawana majibu, ukiuliza Mkurugenzi, hana majibu, tuonyeshe mmetumiaje hawana majibu. Sasa wasiwasi wangu ni kwamba, inawezekana kuna *chain* ya wizi kuanzia Hazina, TAMISEMI mpaka kwa Mkurugenzi. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ilijue hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kama fedha zinaweza kutolewa za ziada basi *CAG* apewe maelezo na hata Kamati ipewe maelezo. Kwa hiyo, kuna mambo kama hayo ambayo yanafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uteuzi wa wakurugenzi, watu wamesema sana. Si wote ni baadhi, lakini naomba niseme hapa kuna Chuo cha Hombolo. Serikali za Mitaa zina chuo cha kuweza kufundisha watu wake, sasa imekuwaje chuo hiki hakiwezi kutumika kufundisha watu? Kiko pale *purposely* kwa ajili ya kufundisha namna ya kuendesha Serikali za Mitaa, ni kwa nini watu hawapewi mafunzo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mafunzo pia yatolewe kwa Madiwani. Madiwani wetu wanakuja hata sisi hapa Wabunge, kuna wapya, kuna wa zamani, mnatuweka kwenye semina tunajifunza. Hata Madiwani wafundishwe ili waweze kukabiliana na *executive*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakukaribisha siku moja uje kwenye kamati yetu huko ya *LAAC*, yako ma-*book* pale, yanakuja wale wataalamu wanakuandikia, *book* linalingana hivi, yaani unalinganisha biblia tatu, nne, tano unalitazama mpaka unaanza kujiuliza nianzie wapi? Na watu hawa wanafanya *purposely* ili ukienda pale utazametazame macho tu uwe kama buibui usielewe hata cha kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mtindo huo ndio ulio ndani ya Halmashauri mimi nimekuwa diwani tangu mwaka 2000, najua, wanaleta ma-*book* yaani madiwani wanaanza kuyatazama *up side-down*, na wale wanakuwa *ile executive* ina hawasomi. Unakuta Mkurugenzi ana *degree,* Bwana Mipango ana ma-*degree,* wengine wana *CPA*, wengine wana nini; halafu Madiwani wanaweka pale wanachanganya changanya. Madiwani wapewe mafunzo. Halafu wanakuta wameandika kwa kimombo bwana. Sasa wewe unaleta taarifa hii kwa madiwani unaandika kimombo wakati hata sheria ya uchaguzi inasema mtu ujue kusoma na kuandika. *How*? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninachoshauri Serikali isitazame haya mambo ya kubana matumizi haya, mnabanabana kitu gani? Na mnabana nini, hamjapata chochote, kwa sababu sisi *LAAC* tunafanya *paper work*. Huwezi kufanya *paper work* kwa hizi Kamati, wakati una watu huku wanajua *kuchodoa,* yaani ninyi hamuwajui watu wa Halmashauri. Huwezi kufanya *paper work,* wanakuja wameandika vitabu vizuri kabisa, wanapewa hata zile ripoti za *CAG* zile za ukaguzi, hati safi. Hati safi unakuta mtu amelamba shilingi milioni 300, shilingi milioni 500, utawauliza hata *CAG*, mnawapaje hati safi hawa watu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza kuona kinachotokea. Kwa hiyo, tunaomba na wale madiwani wapewe mafunzo. Serikali isiseme kubana matumizi. Watanzania wana tabia moja, wana tabia ya kufanya mambo kimya kimya. Wanaweza kukubali kutii, bila kuwa na utii. Kwa hiyo Serikali hii itaendelea kuibiwa, haki ya Mungu mpaka mtakoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu gani? Kwa sababu huku chini sisi tunafaya *pepar work*. Tunashinda mle ndani ya kamati, kuanzia saa moja mpaka saa tatu usiku hatuna hata chakula, Naibu Spika, tupe na chai basi, maji moja, tunakagua vitabu vile mpaka tunachanganyikiwa lakini uko wizi mkubwa, na sisi tunawaambia haya kwa heri mwende, hatuendi kukagua, *what do you expect?* Mnachotegemea ni nini? Mtaibiwa yaani hata huku kutumbuana hakutakuwa na faida yoyote. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi Halmashauri naomba msiziue. Kama mkiendelea na mtindo huu wa kuwanyima fedha, mtindo huu wa kuhakikisha kwamba makusanyo yote mmewanyanganya, halafu ninyi mnawaambia kwamba jamani hamkusanyi mapato, wanakusanya wapi? Hakuna mapato ndani ya Halmashauri. Hakuna 5% za wananwake, hakuna 5% za vijana. Sana sana mtakuwa mnafukuza wakurugenzi mnatumbua na anayekuja mnatumbua wote mtawatumbua kwa sababu hawatakuwa na uwezo wa kuchangia hii 5%. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni kengele ya ngapi?

**MBUNGE FULANI:** Ya kwanza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Aah ni ya kwanza Mheshimiwa?

**NAIBU SPIKA:** Hapana ni ya mwisho. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, lakini naona umeleta na maombi hapo ambayo Mheshimiwa Spika alishayatolea maamuzi, kwa Kamati zile zinazochukua muda mrefu zaidi ya zingine Makatibu Kamati wameagizwa kuiarifu Ofisi ya Bunge ili wapelekewe chai mara mbili. Lakini pia maji hayatakuwa na kikomo. Mtu atakunywa kwa kadri aonavyo yeye inafaa. *(Makofi)*

Mimi nilijua mtashangilia basi maji mnaletewa katoni zote. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Issa Mangungu atafuatiwa na Mheshimiwa Godfrey Mgimwa, Mheshimiwa Abdallah Chikota ajiandae.

**MHE. ISSA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kupata nafasi ya kuchangia taarifa hizi za Kamati mbili. Lakini, maji na chai peke yake havitoshi Wajumbe wa Kamati hii tunataka *oversight* ili tukaikague Serikali vizuri hasa Serikali za Mitaa. Lakini maji peke yake na hivi vitabu mama yangu Rwamlaza amesema pale vinatuzidi umri…

**NAIBU SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Mangungu si mnakuwa mmeshalipwa tayari hela za siku hiyo na ninyi ndio wakaguzi wa mahesabu. Sasa hizo hesabu zitakaaje tena tukilipa mara mbili?

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Waambie, waambie waelewe.

**MHE. ISSA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, hilo nitalifafanua mbele, lakini ningependa nianze kwa kushukuru kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia. Na mimi moja kwa moja wenzangu wengi wamezungumza mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Wenzangu wengi wamezungumza kwa masikitiko makubwa jinsi gani Serikali yetu inavyoweza kuchangia kuzorotesha maendeleo katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hayo kwa sababu wengi wamezungumza, Serikali imekuwa ikichelewa sana kupeleka fedha za maendeleo katika Halmashauri hizi, lakini tunapouliza maofisa kutoka Hazina wanakuwa hawana maelezo na sababu za msingi. Kwa hiyo, ningeomba Waziri wa Fedha atujibu na atueleze tatizo ni la kibajeti au kuna uzembe na hao wazembe wanachukuliwa hatua gani kwa sababu watendaji wetu huko chini wanaumia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Halmashauri hasa za pembezoni, mfano Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo kwa kipindi kirefu haikupelekewa fedha kabisa za maendeleo. Lakini kama walivyosema watangulizi wangu waliozungumza hapa, maagizo yanatoka, tujenge maabara, tufanye shughuli mbalimbali, mwenge na mambo mengine; kwa hiyo, Afisa Masuuli inabidi achambuechambue vifungu kuweza kukamilisha yale ambayo yameagizwa. Kama hizi fedha haziwezi kwenda kwa wakati ni kweli kabisa na usahihi tunaziua hizi Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini lengo la Serikali ni jema, inawezekana katikati hapa kuna vitu ambavyo vinasababisha hizi fedha zisiende. Kwa hiyo, Serikali iwe makini kupeleka hizi fedha za maendeleo kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile suala la hizi Kamati, tumeomba muda mrefu kwenda *oversight* ili tuweze kukagua, kwa sababu tunachoandikiwa kwenye vitabu sicho kile ambacho kiko katika *site*. Kwa hiyo, tumeambiwa kibali hakijatoka fungu halijaingia. Lakini kama mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge

wenzangu, Mheshimiwa Rais alisema tumsaidie kazi ili aweze kupambana na ufisadi katika nchi hii. Leo tunawekwa katika chumba kimoja tupewe maji au chai tunamsaidiaje kazi tukiwa ndani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba Serikali ione haja ya kuziongezea bajeti hizi kamati ili twende kufanya *oversight* kukagua miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nirudi moja kwa moja kwa Mkoa wangu wa Dar es Salaam, haswa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Kwa sisi watu wa Dar es Salaam Halmashauri ya Jiji kwetu ni tatizo. Na ningeomba Waziri uangalie muundo wa Jiji kama ikiwezekana basi tuvunje lile jiji kwa sababu sasa hivi tuna Halmashauri tano za Manispaa za Jiji la Dar es Salaam. Kwa sababu katika kitabu hiki cha *LAAC* ukurasa wa 28…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Yaani Jiji mharibu wenyewe umetumwa eeh! Tena ukome usituzungumzie sisi.

**MHE. ISSA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wachangiaji wawili au ndio tunaonyesha na ubabe humu wa kuongea.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Ukome…

**MHE. ISSA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, na sisi tunajua kuongea na tunayajua matusi isipokuwa tunaheshimiana kutokana na rika…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Ukome, mharibu Jiji halafu unaleta…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa naomba tupeane nafasi za kuzungumza anayekuwa ameitwa ndiye anayeruhusiwa kuchangia na mwingine utapewa nafasi wakati wako. Mheshimiwa Mangungu.

**MHE. ISSA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba kwanza afute kauli yake au na mimi niruhusu nimjibu lile tusi alilolitoa.

**MBUNGE FULANI:** Wewe changia achana naye.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mangungu sikumsikia alichosema, naomba tuendelee wewe endelea kuchangia lakini Mheshimiwa Halima tafadhali usiwashe *mic*.

**MHE. ISSA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilichokuwa naeleza *East Africa Meat Company Limited,* imezungumzwa hapa tatizo lake. Tumegawanya rasilimali katika hizi Halmashauri, lakini hili deni au hizi fedha

ambazo Halmashauri zote hizi zilichangia kwenda Jiji hatujagawana wala hatujaambiwa na Serikali kwamba hizi fedha ziko wapi? Halmashauri ya Temeke, Ilala, Kinondoni zilitoa fedha kuchangia katika mradi huu, na ni pesa nyingi sana *billions of money*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mpaka leo Jiji halijaelezwa kwamba hizi fedha ziko wapi, Halmashauri hizi zitafaidika na nini. Leo kwa Jiji kazi iliyobaki kwake ni sera, lakini sera iliyokuwepo pale kwa wengi wa Dar es Salaam tunaona ni kuongeza *parking* wasizozianda. Jiji pale kazi yao kubwa ni kukamata bodaboda kuwapa majembe na kampuni zingine hakuna kazi zinazofanywa na Jiji, zinaingilia mpaka maeneo ya Halmashauri zetu, ndio maana tunasema Jiji sasa hivi halina kazi. Lazima tuseme ukweli, tusifichane, jiji bora livunjwe ili Halmashauri ili zipate uwezo na Serikali ipunguze mzigo mkubwa wa kulilea Jiji ili Halmashauri mpya na zilizokuwepo za zamani. Huo ndio ushauri wangu kwa Serikali na ninaamini mtazingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie hii *East African Meat* kuna ardhi pale ambayo ipo. Ardhi ile sasa hivi imegeuka kichaka, haijaendelezwa bora Halmashauri ya Ilala ipewe lile eneo waweze kuendeleza au kujenga shule na shughuli zingine za maendeleo kuliko vile lilivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile nizungumzie suala la watumishi katika maeneo ya pembezoni. Hivi leo kuna haja gani eneo kama la Kariakoo kuwa na Afisa Kilimo au Afisa Mifugo, au Upanga? Mfano kwenye Halmashauri yangu ya Temeke pale Afisa Kilimo hakuwa na bajeti amekaa mwaka mzima analipwa mshahara wa Serikali. Lakini Kalambo kule tuliona Afisa Mipango Miji ndio ana kaimu kuwa Afisa Kilimo, watu wako Dar es Salaam kule hawafanyi kazi, wanalipwa mishahara, maeneo ya pembezoni watu wa kufanya kazi hizi hawapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasikia Wabunge wenzetu wa pembezoni wanalalamika kuwa Maafisa Ugani hawapo, lakini Dar es Salaam wapo. Sio hilo tu, Wabunge wengi hapa wamezungumzia na wamelalamika suala la kukaimu watu ukuu wa idara. Lakini katika Halmashauri zetu za Dar es Salaam unaweza ukakuta idara moja ina maofisa zaidi ya sita, hawana shughuli ya kufanya zaidi ya kusubiri semina. Kwa nini wanakaa Dar es Salaam kule, waende maeneo mengine wakalitumikie hili Taifa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo wa rasilimaliwatu lazima uzingatiwe. Wataalam waende kwenye maeneo yenye mahitaji ili waweze kutusaidia kusukuma gurudumu la maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba sana suala la mradi wa mabasi yaendayo kasi ambayo unasimamiwa na *DART,* mara nyingi nikipita pale *TAZARA* huwa nashangaa kidogo, ule mchoro unavyoonesha kwa sababu *DART Phase II,* utagusa eneo la Gongo la Mboto kupita *TAZARA* mpaka Kariakoo. Lakini ule mchoro wa *interchange* pale hauoneshi kama zimetengwa tayari, eneo la barabara za mwendo kasi. Kwa hiyo tunategemea mwakakni tukianza kutekeleza huu mradi, tuvunje tena. Kwa hiyo, naomba Serikali itupe majibu je, pale wana mpango gani au huu mradi tena umeshakufa umeishia pale ulipo?.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa eneo la Mbagala, Mheshimiwa Mwijage anasema kila siku hapa tunataka kuimarisha viwanda, tunataka kufufua viwanda. Eneo ambalo *DART* wameamua ku-*plan* kwa ajili ya kulipa fidia zaidi ya bilioni 186 ni eneo la viwanda ambavyo vingine vinazalisha. Lakini ukitoka kilometa sita kutoka pale Mbagala Rangi Tatu kwenda mpaka Kongowe kuna msitu mkubwa umejaa pale hauna kazi yeyote, kwa nini wasi-*extend* mpaka kufikisha pale vikindu ule msitu, hauna kazi yoyote zaidi ya kuwa maficho ya majambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Mheshimiwa Waziri Maghembe ametoa heka pale ambazo zile zingesaidia ile *DART* wangei-*extend* ili Serikali isipoteze fedha nyingi ya fidia ikiwa eneo lipo. Ningeomba sana Mheshimiwa Simbachawene watu wa *DART* walitizame hili kuliko kupoteza fedha pasipokuwa na sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wengi wamezungumza kuhusu *CAG,* ni kweli *CAG* anafanya kazi katika mazingiara magumu sana. Naomba Serikali hii ya Awamu ya Tano yenye nia njema ya kumkomboa Mtanzania wamuwezeshe *CAG* aweze kufanya kazi. Bila kufanya kazi *CAG* Kamati hizi zinakuwa hazina macho kabisa na zinakuwa hazina uwezo wa kutekeleza majukumu yake. Lakini nimuombe Waziri wa Fedha, nina taarifa Halmashauri zetu Dar es Salaam bado hazijapata gawio la *property tax*. Na hata hao *TRA* wenyewe wanasema ndiyo kwanza wanaanza kujipanga na kutoa semina ili waanze kukusanya mapato. Ndugu zetu mmetuchukulia chanzo hiki kikubwa kwa Halmashauri za Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Serikali inashindwa kuleta hizi fedha mnategemea tutekeleze vipi miradi ya maendeleo, mnategemea tujiendeshe vipi? Kama jukumu hili mmelishindwa naomba mrudi nyuma, mjisahihishe mtuachie Halmashauri tukusanye *property tax* ili tuweze kutekeleza miradi yeti ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimwa Naibu Spika, Sheria ya Manunuzi ya Umma *(Public Procurement Act)* ni tatizo katika Halmashauri zetu, zinachukua muda mrefu *procedure* hizi mpaka kuweza kutangaza mzabuni. Lakini huyo mzabuni

anayepatikana, anapatikana kwa gharama kubwa, naomba sana Serikali ifanye marekebisho ya sheria ili sheria hii iweze kutusaidia, isiwe kikwazo katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna kero kubwa ya uhakiki wa madeni ya walimu, hasa waliosahihisha mitihani ya darasa la saba na darasa la nne. Walimu hawa hawajalipwa muda mrefu, wamekuwa wakilalamika na kila wakija Wakurugenzi wanasema fedha hazijatoka kutoka Hazina hazijaletwa kutoka Serikali Kuu. Naomba Serikali iangalie kwa jicho la huruma walimu hawa ambao wanatusaidia kuboresha elimu ya watoto wetu na wao ni watumishi wanastahili kupewa haki, kwa wakati ili waweze kuwa na moyo na morali wa kuweza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini eneo lingine ningependa kulizungumzia na nitatolea mfano Halmashauri ya Jiji au Mji wa Iringa. Walikuwa na mpango na mwekezaji wa kuwekeza katika eneo la machinjio na kituo cha mabasi, lakini wamepeleka Wizarani karibu miaka minne sasa hivi hawajapata majibu na sisi Temeke pia tumepeleka Wizarani *project* zetu, lakini mpaka leo hatujapa kibali cha Waziri husika na ushauri wa *CAG*. Kwa hiyo, ile miradi baadaye inakuja ina-*collapse* Halmashauri zinashindwa kuwekeza.

Kwa hiyo mimi ningeomba sana Serikali ibadilishe utaratibu, ili Halmashauri hizi zikiwa na *plan* ya kuwekeza basi uwekezaji ule ufanyike kwa haraka na wapate ridhaa ya Waziri na wahusika kwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile suala la Mifuko ya Hifadhi za Jamii. Jamani wastaafu wetu wanateseka sana, hawapewi mafao yao kwa wakati, tangazo la nyongeza ya Serikali mpaka sasa hivi hakuna na majibu yanakuwa hakuna na hawa watu ni wastaafu, wanachotegemea ndicho hicho hicho kilichokuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapa nimesoma ripoti ya *PAC* Serikali inadaiwa pesa nyingi sana na Mifuko ya Hifhadhi za Jamii. Lazima tuseme ukweli kama hili ni tatizo basi Serikali ijipange, Mifuko ya Hifadhi za Jamii iwe inalipwa *at least* nusu ya madeni yao ili waweze kujiendesha na waweze kulipa madeni yao mbalimbali ikiwemo pamoja na kuwalipa wastaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wastaafu wanahangaika sana, wastaafu wanapata shida sana. Mimi ningeshauri sana Serikali iwaangalie wastaafu kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile limezungumzwa hapa kwa upana sana suala la UDA. Ni kweli UDA ina kigugumizi na hatujapata majibu yake, lakini sisi tuombe Halmashauri zetu nazo zinatakiwa zipate zile *unallotted share* basi na sisi

tuelekezwe jinsi gani ya kuzipata ili tuweze kumiliki. Lakini sio hilo tu kuna suala la pesa ambazo ziko mpaka sasa hivi benki, kama ni ndogo kaeni fanyeni *negotiation* na mwekezaji, ziongezeke au kama mwekezaji hatakiwi tupewe taarifa hizi ili zile pesa kama inawezekana basi zitumike kwenye miradi ya manendeleo katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio hilo tu kuna suala la pesa ambazo ziko mpaka sasahivi benki. Kama ni ndogo kaeni fanyeni *negotiation* na mwekezaji ziongezeke au kama mwekezaji hatakiwi, tupewe taarifa ili zile pesa kama inawezekana basi zitumike kwenye miradi ya maendeleo katika Halmashauri zetu na Manispaa zetu, lakini kero hii naomba iishe na hili neno liwe lilefutika kwa sababu, linawezekana na kama kukiwa na nia njema na ukweli na uwazi katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeomba sana, wengi wamezungumza na ni kweli sasahivi kuna mkanganyiko maana sasahivi Mbunge ukishirikiana na wananchi unaambiwa mchochezi. Mkuu wa Wilaya anataka wewe uende pale umpigie *salute.* Ni vizuri mkawapa semina Wakuu wetu wa Wilaya, mkawapa semina viongozi wetu ili wajue mipaka ya majukumu yao, wajue heshima ya Mbunge ni ipi, heshima yake yeye ni ipi na vilevile mgawanyo wa madaraka yake na majukumu yake ni upi.

Mheshimiwa Naibu Spika, isifike mahali Mbunge unaalikwa uende kwenye mahafali na Mkuu wa Wilaya mnapishana na yeye anataka kwenda kwenye mahafali. Kila mtu ana majukumu yake na katika maeneo yake. Naomba sana semina elekezi kwa viongozi wetu zitolewe ili kusiwe na mgongano. *(Makofi)*

Lakini lingine kumekuwa sasa hivi, hasa kwa Madiwani, nilipata taarifa kwamba kuna baadhi ya Madiwani wamekamatwa, wamewekwa ndani kisa wanaambiwa ni wachochezi. Haya mambo yanaweza yakazungumzika katika maeneo yale na yakaweza kusawazishika. Si kila jambo lazima itumike nguvu, kuna mambo ambayo tunaweza tukawaelewesha, watu wakaelewa na wakatekeleza wajibu wao na nchi yetu ikabaki kuwa salama na tukawa wamoja kwa amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme pale ambapo kuna maelewano, pale ambapo kuna maridhiano maendeleo yatapatikana. Pale ambapo kuna migongano maendeleo hayawezi kupatikana, tutumie busara katika…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ISSA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwanza au ya pili?

**NAIBU SPIKA:** Ya pili! Ukishagongewa hivyo maana yake malizia sentensi.

**MHE. ISSA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Godfrey Mgimwa atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Chikota, tutaangalia kama muda bado upo.

**MHE. DKT. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia jioni ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengi yameshazungumzwa kuhusu suala hili, lakini lazima tuwe wazi tunavyozungumza Halmashauri na tunavyozizungumzia Halmashauri ninaomba tuweze kujiuliza maswali kadhaa. Tatizo tunalolipata katika Halmashauri zetu ni tatizo la kutopelekwa kwa fedha kwa wakati au kutopelekwa fedha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tukawasema Wakurugenzi, tunaweza tukasema Halmashauri hazifanyi kazi, lakini tatizo tunalolipata ni kwamba Wizara haipeleki pesa katika Halmashauri kwa muda. Sasa tatizo kama hili linapotokea kule kwenye Halmashauri kunakuwa hakuna namna nyingine ya kuweza kufanya kazi katika utaratibu ambao Serikali ilikuwa inataka na ndiyo maana tunakuta kwamba miradi mbalimbali haikamiliki. Kwa mfano, miradi ya maji inashindwa kukamilika, miradi ya barabara inashindwa kukamilika, lawama zinaenda kwa Wakurugenzi, lakini tatizo hili lazima tujiulize je, Wizara ya Fedha inasema nini kuhusu suala hili? Halmashauri ngapi ambazo tayari zimepata zaidi ya asilimia 70 ya bajeti? Ni nani ambaye anaweza akasimama na kusema Halmashauri yake imepata pesa za kutisha za miradi katika mwaka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tatizo hili kubwa tunalolipata lazima Wizara ya Fedha iweze kusimama na kusema pesa zinakwenda wapi au pesa zinapelekwa namna gani katika Halmashauri mbalimbali. Tunavyosema makusanyo yanaongezeka lazima tuangalie upande wa pili, unavyokusanya basi tujue tunavyopeleka katika Halmashauri twende kwa uwiano, hatuwezi kusema tunakusanya kiasi hiki, lakini kwenye Halmashauri hatupeleki pesa zozote. Kuna Halmashauri zimepata asilimia 30 ya bajeti, kuna Halmashauri zimepata asilimia 20, asilimia 30, asilimia 40; lakini kuna miradi mbalimbali na Halmashauri nyingi zina madeni makubwa. Wengine wameshazungumza hapa na wamesema kwa undani zaidi, kuna Halmashauri zinadaiwa mabilioni ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi lazima niwe wazi na niseme kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC,* nimeona mambo mengi na tumejadili na tumeziita Halmashauri mbalimbali kwenye Kamati. Tatizo tunalolipata si tatizo la Wakurugenzi peke yake. Ndiyo kuna Wakurugenzi wapya, ndiyo kuna watumishi wapya, lakini tunachokisema tunaomba sasa Wizara husika iweze kuchukua

nafasi ya kuweza kuwaelimisha hawa Wakurugenzi wapya na watumishi wapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchangiaji aliyepita alizungumza akasema tuna chuo pale Hombolo, sasa kwa nini tunashinwa kukitumia chuo hiki ili watu hawa waweze kufanya kazi katika hali ambayo tunadhani itaweza kuleta tija katika Halmashauri zetu? Kuna mambo mengi ambayo wanashindwa kuyafahamu, wanakuja kwenye Kamati wanashindwa kujieleza. Ile *competitiveness* haipo! Unashindwa kujua kwamba huyu mtu ame-*qualify* katika sekta gani, katika eneo gani? Unapomuuliza kwa nini uli-*realocate* fedha hizi anashindwa kueleza. Kwa hiyo, lazima tuweze kujua Wizara inayohusika imefanya kazi gani kuhakikisha kwamba watu hawa wanaweza wakatumika inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo kadhaa ambayo tumeweza kuyatizama, lakini jambo la msingi kuna asilimia 10 na kuna asilimia 20; asilimia 10 za vijana na akinamama na asilimia 20 zinazotakiwa kupelekwa kwenye vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni masikitiko makubwa kuona Halmashauri zote tulizozihoji katika Kamati yetu hakuna Halmashauri ambayo ilifanikiwa kupeleka asilimia 10 kwa uzito wake au kwa ujumla wake. Sasa tunafanye ili kuhakikisha kwamba Halmashauri hizi zinawaangalia vijana? Halmashauri hizi zinawaangalia akinamama? Halmashauri hizi zinaangalia wananchi kule vijijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunavyoshindwa kupeleka hizi asilimia tano kwa vijana, na mimi kama kijana lazima niwe na masikitiko makubwa. Vijana wenzangu kule wanataka kuendesha miradi yao, lazima waone hizi hela zinakwenda. Sasa ni maajabu ambapo utaweza kusimama hapa na kutetea kwamba Halmashauri zinapeleka asilimia 20 jambo ambalo sio sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba kwamba Wizara iweze kuangalia kwa undani zaidi halmashauri zinafanyaje kazi, hizi asilimia 10 za vijana na akinamama ni fedha ambazo zinatoka kwenye mapato ya ndani ya Halmashauri, lakini kwa bahati mbaya ukiangalia hata hizi Halmashauri zetu ukusanyaji wa mapato ya ndani bado unasuasua. Hatuna makusanyo ya kutosha, vyanzo vya mapato hatuna vya kutosha kwenye Halmashauri kuweza kuhakikisha kwamba, hizi asilimia 10 zinakwenda kwa wahusika na walengwa. Sasa tutakaa na tutajiuliza muda wote namna gani tunavyoweza kusonga mbele, lakini tatizo linabaki palepale kwamba kama Wizara haipeleki fedha kwenye Halmashauri na tunazituma Halmashauri ziweze kufanya makusanyo ya ndani kupitia miradi yake mbalimbali, tutaweza kupata matatizo makubwa huko mbele kwa sababu tunashindwa kuzihudumia hizi Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine baya zaidi, afadhali useme kijana, lakini unavyomnyanyasa mwanamke kwa kumnyima ile asilimia yake tano ni kitu kibaya kuliko vyote. Unakuta Mkurugenzi yuko pale kwenye Kamati anashindwa kujieleza kwa nini kashindwa kupeleka zile asilimia tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilikuwa nikiangalia katika chombo kimoja cha habari watu wanalalamika sehemu fulani wanasema akinamama na ndoa zao zinaenda kuvunjika kwa sababu ya kwenda mbali kutafuta maji, wanatumia masaa matatu, manne, matano. Sasa fedha hizi ambazo tunazisema ndizo ambazo tunataka watu wa kutoka halmashauri waweze kuhakikisha kwamba zinaenda kwa akinamama. Na akirudi nyumbani anapata kichapo vilevile kutoka kwa mume wake. Sasa hili sio jambo la kuweza kulifumbia macho, ni jambo la msingi sana kwa sababu, misingi ya jamii yetu nayo itaenda kuporomoka kwa sababu ya kukosa mambo ya namna hii ambayo tunayazungumza, na ni mambo ambayo yanajirudia mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyozungumza kuhusu upelekwaji wa miradi mbalimbali katika maeneo yetu na tukiangalia hasa sisi tunaotoka katika maeneo ya vijijini kule tunajua changamoto ya maji, kwamba unavyoshindwa kuwa na maji hilo ni tatizo kubwa. Lakini vilevile tunavyoshindwa kuwaeleza wananchi wetu kwamba kuna asilimia tano, kwa sababu haya ni mambo ambayo aidha Wakurugenzi au wanasiasa tunashindwa kuwaeleza wananchi wetu kwamba kuna asilimia tano na mambo yanakuwa kimya kimya watu wanapiga ile pesa na ndiyo maana watu wanatumia maneno wanasema wanapiga-*deal* kwa sababu wamekula fedha ambazo zilitakiwa ziende kwa wahusika, sasa sijajua tunaweza kuwachukulia hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ukiangalia katika miaka mitatu, mine, mitano ambayo tumekuwa tukikagua hizi Halmashauri, hakuna Halmashauri ambayo imetekeleza hilo, lakini bado tunakuta hakuna namna ambavyo hawa watu wa Halmashauri wanachukuliwa hatua za kisheria. Kwa hiyo, mimi ningependa kushauri kwamba, sheria iweze kuchukua mkondo wake wakati mwingine kwamba, tunavyoshindwa kuwapelekea hawa vijana, akinamama na hizi fedha za asilimia 20 kule vijijini basi tuweze kujua namna gani tunaweza kuwaadabisha hawa, nitumie hilo neno.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ningependa kuzungumza kwamba kuna matatizo ya watumishi ambao wamekaimishwa kwa muda mrefu, hili kwa sasa ni tatizo kubwa. Mtu amekaimishwa miaka mitatu, mtu amekaimishwa miezi zaidi ya sita, lakini unashindwa kujua kwa nini Serikali au TAMISEMI inashindwa kufanya huyu mtu sasa apewe nafasi yake kwa sababu kama anaweza kufanya kazi basi mpeni nafasi, lakini kama anashindwa basi mmuondoe. Unamkaimisha mtu kwa zaidi ya miezi sita, zaidi ya mwaka mmoja,

zaidi ya miaka miwili, halafu unategemea kutakuwa kuna utendaji pale katika Halmashauri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni mambo ambayo yapo, si mambo ambayo tunayatoa kwenye hadithi ni mambo ambayo yapo kwenye Halmashauri zetu, na ndiyo maana hata utekelezaji wa baadhi ya majukumu katika Halmashauri yetu watu wanakuwa wanshindwa kuwa na uhakika, je, kesho watakuwepo au hawatakuwepo. Kwa hiyo, mimi nilikuwa napenda kushauri kwamba sasa umefika wakati kwa wale wanaokaimishwa waweze kupata nafasi zao au waweze kuondolewa katika nafasi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mbalimbali tumeyaona. Kuna mikataba mibovu imeingiwa katika maeneo mbalimbali, mikataba ambayo huwezi hata ukaamini kwamba hivi kwa nini mwanasheria aliweza kusaini mkataba kama huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni masuala hayo hayo kwamba watu wamekaimishwa kwa muda mrefu, wanashindwa kupata majibu ya ajira zao, wanaona tu wasaini mikataba wapate vijisentisenti wakimbie. Na kuna maeneo ambayo tumeyaangalia kwa undani tukajua kabisa hapa kuna tatizo la kimkataba. Kwa hiyo, mimi ningependa kuangalia hili kwa undani na kuiomba Serikali iweze kutizama kwa umakini masuala ya watumishi ili kwamba TAMISEMI sasa ichukue jukumu hili kuweza kuwapa nafasi hawa watu ambao wanakaimishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *CAG*. Ni kweli kwamba wengine wengi wamezungumza wamesema *CAG* anashindwa kuwezeshwa. Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ilikuja kwenye Kamati ikarudishwa kwa sababu kulikuwa hakuna tathmini iliyofanywa na *CAG*. Sasa hii ni aibu kubwa kwamba unavyoirudisha Halmashauri je, hizi fedha ambazo wamekujanazo kwenye Kamati, kama ilikuwa Dar es Salaam au Dodoma? Lakini kumbe tatizo linakuwa ni *CAG* ameshindwa kuwezeshwa. Kwa hiyo, mimi ningependa kuishauri Serikali kwamba sasa kama tunasema *CAG* ndio jicho letu basi tumuwezeshe *CAG,* tatizo liko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakuwa tunalalamika kila siku kwamba, hatuna fedha huku hatuna fedha kule, lakini ninachokisema ni kwamba lazima tuwe tuna mikakati. Tuweke mikakati yetu sawa ili kwamba kama *CAG* tutamtumia na tunaendelea kumtumia basi tumuwezeshe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yetu sisi tunashindwa kwenda kukagua miradi mbalimbali katika maeneo mbalimbali, tunakaa tunawaita Wakurugenzi waje na mavitabu makubwa namna hii. Mtu ukiliangalia lile likitabu unashindwa

hata kuanza useme nianzie wapi. Lakini kumbe ile miradi ambayo ipo kule majimboni, iko kule vijijini, tunashindwa sisi kwenda kuiangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanakuja wana-*manipulate* tu zile *figures* wanasema hivi sawa sawa na vile, hivi sawa sawa na vile, mradi hujauona, na tupokuja huku kutoa ripoti na tunavyosema kwamba kitu hiki hakijakaa vizuri, ile *value for money,* lakini ni mambo ya kusikitisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa kuishauri Serikali, najua Bunge lilikuwa lina mfuko sasa sijui ule mfuko uko wapi? Kwamba watuwezeshe basi twendeni tukafanye kazi, tuko tayari kufanya kazi. Lakini sasa tunavyoshindwa kwenda kufanya kazi kule na tunakaa tu kama ni Dodoma au kama ni Dar es Salaam haisaidii. Twende kule tukafanye kazi tukaangalie miradi, fedha ambazo Serikali ilipeleka tukaangalie kwamba huu mradi upo au haupo. Sasa utaambaiwa kuna mradi umepelekwa kule umekamilika una milioni 300; milioni 500, lakini ukienda kule ule mradi haupo, mnazungushwa tu kwenye magari kule mpaka unachoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba niishie hapo, lakini ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mgimwa, Mheshimiwa Abdallah Chikota atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu na ni-*declare interest* na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC),* nikiwa kama Makamu Mwenyekiti wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kabla sijaanza kutoa michango yangu nilitaka tuweke *record* sawa na hasa kuhusu taarifa yetu. Kilichosisitizwa kwenye taarifa yetu ni mafunzo kwa Wakurugenzi wapya. Taarifa yetu imeweka wazi kabisa kwamba hatuna maswali, hatuhoji uteuzi wa watu mbalimbali kutoka kwenye kada mbalimbali kwenda kwenye Ukurugenzi lakini watu hawa sasa wanatakiwa wapate mafunzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, alivyofanya Mheshimiwa Rais kuchukua *breed* nyingine kutoka nje kupeleka kwenye utumishi wa umma na hasa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni kitu ambacho ni kizuri na kinaweza kuleta matunda ambayo tunayatarajia. Kuna watu ambao wametoka kwenye *private sector* wakaenda kwenye mashirika yetu, kwa mfano Mkurugenzi wa Shirika letu la Nyumba, Ndugu Mchechu, anafanya vizuri, lakini ametoka kwenye *private sector. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakurugenzi waliokuja mbele yetu wakati tunafanya mahojiano, wapo Wakurugenzi ambao wamefanya vizuri kabisa niwataje baadhi tu, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kiteto alifanya vizuri na alikuwa na miezi miwili tu ofisini; Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ileje, Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Mkurugenzi wa Tandahimba, lakini na Mheshimiwa Heche pale atakuwa shahidi, Mkurugenzi wa Tarime na yeye ni kijana mdogo, lakini ni mchapakazi vizuri na alionesha uwezo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii haikwepi jukumu la TAMISEMI kuwapeleka vyuoni hawa Wakurugenzi. Ukurugenzi ni kazi kubwa, kwenye *council* kuna idara na vitengo visivyopungua 15. Mkurugenzi huyu inabidi awe mganga, Mkurugenzi huyu ajue masuala ya elimu, Mkurugenzi huyu anatakiwa ajue masuala ya manunuzi, Mkurugenzi huyu anatakiwa ajue masuala ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vema Wakurugenzi hawa pamoja na kubana matumizi, tuwaandalie programu maalum ili tuwapeleke kwenye Chuo chetu cha Hombolo wakapitishwe kwenye taratibu za kawaida tu. Kwanza waifahamu sheria ambayo imeanzisha Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ile Sura ya 288, Sura ya 289, lakini na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura ya 290, ili zikawasaidie katika kutekeleza majukumu yao, hicho ni kitu cha msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna kitu hapa kimezungumzwa kuhusu mahusiano ya Wakurugenzi na Wakuu wa Wilaya. Kwenye mafunzo hayo wapitishwe kwenye Sheria ile ya *Regional Administration Act* ambayo wataona mahusiano kati ya Serikali Kuu na Serikali ya Mitaa. Kwa hiyo, naomba sana TAMISEMI pamoja na kubana matumizi mafunzo haya ni muhimu kwa Wakurugenzi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ambayo napenda nichangie ni kuhusu udhaifu wa mfumo wa udhibiti wa ndani. Haya yote ambayo tumeyaongea hapa yangeweza kudhibitiwa kama tungekuwa na mifumo imara ya udhibiti wa ndani na hapa naomba niseme tu kwamba Ofisi ya *Internal Auditor General* ilifanya kazi sana miaka mitatu, minne iliyopita chini ya uongozi wa Ndugu Mtonga. Aliandaa mafunzo kwa Wakaguzi wa Ndani ili wakasimike mifumo ya udhibiti wa ndani kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme tu kwamba, mafunzo yale hayakuleta tija ambayo tulitarajia kwa sababu mafunzo yale yalilenga kwamba Wakaguzi wa Ndani wakirudi kwanza watengeneze kitu ambacho kinaitwa *Risk Management Policy* kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa, watengeneze *Risk Framework,* lakini vilevile watengeneze *Risk Register* ambazo watakuwa wanazi-*update* kila mwaka kuangalia ni maeneo gani yana vihatarishi katika Mamlaka

ya Serikali za Mitaa na haya yanaweza yakafanyika vizuri chini ya *Internal Auditor*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitofautiane na wale ambao wanasema kwamba *Internal Auditor* anatakiwa ahamishwe, hapana. *Internal Auditor* ni jicho la karibu la Mkurugenzi Mtendaji. Ndugu zangu mimi nilikuwa mtumishi wa umma nilifanya kazi hiyo ya Ukurugenzi, Mkurugenzi ambaye anataka aone matokeo katika *council* yake mtu wake wa karibu ni *Internal Auditor*. Kuna Idara 15 kwa hiyo, atamsaidia Mkurugenzi katika Idara zake 15, *Risk Department* ni hi hapa kwa hiyo, *Internal Auditor* ni mtu wa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkurugenzi ambaye anataka matokeo atamuwezesha huyu *Internal Auditor,* atampa usafiri *Internal Auditor* kwa sababu hata Mkurugenzi akisafiri anajua kwamba kuna jicho lake la karibu ambalo ni Mkaguzi wa Ndani, lakini si vinginevyo kwa sababu watu wanafikiri kwamba kuwepo kwake huyu basi anaweza aka-*collude* na Mkurugenzi, hapana, Mkurugenzi ambaye anataka matokeo katika Halmashauri yake atamtumia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba, TAMISEMI mlikuwa na utaratibu wa kuwezesha hivi vietengo, mlinunua magari, lakini magari yale yameenda kwenye Halmashauri chache. Kuna Mamlaka ya Serikali za Mitaa tumeongeza Halmashauri mpya, hawana yale magari hebu wezesheni kwenye zile Halmashauri mpya wapate magari kwenye vitengo hivi ili viweze kuwasaidia hawa Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu la pili ambalo nataka nichangie ni kuhusu udhaifu katika mikataba. Sehemu nyingine ambayo ina udhaifu katika Mamlaka yetu ya Serikali za Mitaa na CAG ameonesha wazi ni udhaifu wa kwanza uingiaji wa mikataba yenyewe katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, lakini pili na usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana ulifanyika ukaguzi na *CAG* ametuonesha kwenye taarifa yake kwamba kwenye mikataba ya kukusanya fedha, kwanza Halmashauri hazifanyi *assessment* ya vyanzo vya mapato, yaani wanaingia mikataba na Mawakala wa Kukusanya Mapato bila kuangalia chanzo hiki kitapata Shilingi ngapi, na Halmashauri inategemea takwimu kutoka kwa Wakala. Hiyo ni taarifa mbaya sana kwa sababu Wakala anatafuta faida lazima atadanganya kwa hiyo, ni vizuri Halmashauri zifanye *assessment* ya chanzo cha mapato kabla ya kuingia mkataba na Wakala.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo kwenye Taarifa ya *CAG* inaonesha kabisa kwamba kwenye Halmashauri 76 kuna fedha bilioni 5.3 Mawakala hawakuwasilisha, waliingia mikataba, lakini kwa sababu ya usimamizi mbovu

wa mikataba fedha hizo wameondoka nazo Mawakala, Halmashauri hawakuzipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ambayo nilitaka nichangie kwenye hiyo hiyo mikataba, mimi naona TAMISEMI sasa mikataba kama hii ambayo inaonekana kwamba Halmashauri sasa imezidiwa hebu tuingilie kati mapema. Kwa mfano mkataba ule wa *Oysterbay Villa* na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, mkataba ambao hauna tija. Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ina *apartments* 17 wamepewa, lakini hadi leo hawajapangisha na hawapati zile fedha. TAMISEMI mnatakiwa muingilie kati ili chanzo kile kisaidie kupata mapato ya Kinondoni kwa sababu, Kinondoni kama mmiliki amezuiliwa kuingia kwenye ule mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mkataba mwingine ambao tuliona kwamba nao una mashaka ambao wenzangu mmeshasema ni ule wa UDA ambapo Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ilipeleka barua kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Sasa tunaomba ule ushauri ambao ameutoa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ufanyiwe kazi ili zile fedha ambazo ziko benki zaidi ya bilioni tano zitumike kwa maendeleo ya wananchi wa Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni usimamizi wa matumizi ya fedha. Hapa naomba TAMISEMI ilivalie njuga suala hili kwa sababu Mamlaka ya Serikali za Mitaa imeonekana tena kuanza udhaifu wa kuanza hoja ambazo huko nyuma zilikuwa zimeshafutwa. Kuna hoja hapa kwenye taarifa ya mwaka 2014/2015 kwamba Halmashauri za Wilaya zimefanya malipo ya bilioni 10 na milioni 31 bila kuwa na viambatisho muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi hoja ni za kizembe, hizi hoja sasa tuna Mfumo wa *EPICOR* kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kwa nini hoja kama hizi ziendelee kuwepo? Kwa hiyo, naomba TAMISEMI muingilie kati ili uzembe kama huu usiendelee kutokea na watumishi ambao wanafanya uzembe huu wachukuliwe hatua mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile naomba sasa ule Mfumo wa *EPICOR* usimikwe katika halmashauri zote. Kuna halmashauri mpya ambazo mfumo wa *EPICOR* haujasimikwa bado. Kwa hiyo naomba TAMISEMI ihakikishe kwamba, inatenga fungu la kutosha, ili halmashauri zote sasa ziweze kufunga mifumo hii ya *EPICOR* ili na wao waweze kufanya hesabu zao kupitia mfumo huu badala ya kutumia mifumo ya kizamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kuhusu uteuzi wa Wakuu wa Idara. Wakuu wa Idara kwa sheria iliyopo wanateuliwa na Mkurugenzi wa Halmashauri, lakini kuna mchakato, lazima waende kwenye *vetting.* Kwa hiyo,

naomba mamlaka zinazohusika ziongeze uharaka katika mchakato huu, ili tusiwe na makaimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na ninashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdallah Chikota kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa michango kwa leo, tutaendelea kesho, lakini niwakumbushe kwa sababu, majina yameshaletwa na vyama husika. Sasa majina ni mengi kuliko muda tutakaokuwanao kesho na hoja hii inahitimishwa kesho. Sasa niwakumbushe kwa wale ambao watataka kugawiana muda walete taarifa mapema tutakapokutana asubuhi kwa sababu la sivyo ni watu wachache watakaopata hiyo nafasi kwa sababu, kila mmoja ana dakika 15.

Lakini tangazo lingine, kesho hatutakuwa na Kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu, Waziri Mkuu amepata dharura na hayupo, kwa mujibu wa kanuni zetu zinavyosema.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho, siku ya Alhamisi, Tarehe 10, Saa 3:00 asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 10 Novemba, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*